# HATIMAYE NIMEONGOKA

*Kimeandikwa na:*
**Muhammad Tijani Samawi**

*Kimetarjumiwa na:*
**Musabah Shaban Mapinda**

*Kimetolewa na Kuchapishwa na:*
**Bilal Muslim Mission of Tanzania**
**P.O. Box 20033,**
**Dar es Salaam - Tanzania**
**Tel: 2120111 / 2112419**
**Email: bilaltz@africafederation.org**
**Website: www.bilaltz.org**

**Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
**Bilal Muslim Mission of Tanzania**

**ISBN: 9987 620 13 2**

**Chapa ya kwanza Nakala 5,000**
***January 2000/Ramadhan 1420***
**Chapa ya pili Nakala 2,500**
***Mei 2002/Rabbi ul Awwal 1423***
**Chapa ya tatu Nakala 2000**
***November 2011 / Dhil Hijja 1432***
**Chapa ya Nne Nakala 5000**
***Desemba 2014 / Safar 1436***
**Chapa ya Tano: Nakala 5000**
**Aprili 2015 / Jamaad' Thani 1436**

## YALIYOMO

1. Utangulizi........................................................................ 5
2. Zawadi........................................................................ 7
3. Dibaji........................................................................ 8
4. Hali ya Maisha yangu kwa ufupi...................................... 10
5. Safari ya kwenda kuhiji Nyumba Tukufu ya MwenyeziMungu................................................................ 13

**Safari yenye mafanikio ............................................................... 23**
6. Nikiwa Misri.................................................................. 24
7. Mkutano ndani ya Boti...................................................... 28
8. Ziyara ya lraq kwa mara ya Kwanza................................ 34
9. Abdul-Qadir Al-Jaylani na Musa Al-Kadhim .................. 36
10. Mashaka na Kujiuliza ........................................................ 44
11. Safari ya kwenda Najaf.................................................... 49
12. Kukutana na Wanachuoni.................................................. 52
13. Kukutana na Sayyid Muhammad Baqir as-Sadri............. 60
14. Mashaka na Mkanganyiko ............................................... 70
15. Safari ya kwenda Hijaz ..................................................... 77
16. KuanzaUtafiti.................................................................... 88

17. **Mwanzo wa Utafiti wa Kina:**
Mtazamo wa Shia na Sunni juu ya Masahaba.................. 91
(i) Masahaba siku ya Sulhu ya Hudaibiya.......................... 95
(ii) Masahaba na Msiba wa siku ya Alkhamisi................... 99
(iii) Masahaba ndani ya Jeshi la Usamah............................ 105

18. (1) Maoni ya Qur’an kuhusu Masahaba.............................. 119
(i) Muhammad Mjumbe wa Mwenyezi Mungu................... 120
(ii) Aya ya kugeuka nyuma................................................... 122
(iii) Aya ya Jihad ................................................................... 124

19. (2) Maoni ya Mtume kuhusu Masahaba............................... 127
(i) Hadithi ya Haudhi (Birika).................... ...................... 127
(ii) Hadithi ya kuwafuata Mayahudi na Wakristo................. 128

(iii) Hadithi ya Bitanatain ................................................ 131
(iv) Hadithi ya kushindania Ulimwengu .......................... 133

20. (3) Maoni ya baadhi ya Masahaba kuhusu wenzao ............ 134
(i) Ushahidi wao wenyewe juu ya kuibadilisha Sunna ya Mtume ........................................................................ 134
(ii) Masahaba hata Sala walibadilisha ................................ 138
(iii) Masahaba wanashuhudia wenyewe ............................. 141
(iv) Ushahidi wa Masheikh wawili (Abubakr na Umar) juu ya Nafsi zao wenyewe................................................. 141

21. Mwanzo wa kubadilika ..................................................... 158
22. Majadiliano na Mwanachuoni: ......................................... 160

23. Sababu za Utambuzi.......................................................... 174
(i) Maandiko yanayokhusu Ukhalifah ............................. 174
(ii) Kukhitilafiana Bibi Fatmah (a.s’) na Abubakr............ 177
(iii) Ali ndiye anayestahiki kufuatwa .................................. 180
(iv) Hadithi zilizokuja kukhusiana na Imam Ali zinawajibisha kumfuata.................................................... 186

24. Hadithi sahihi zinazolazimisha kuwafuata Ahlul-Bait........ 193
(i) Hadithi ya vizito viwili................................................. 193
(ii) Hadithi ya Safinah ....................................................... 205
(iii) Hadithi isemayo atakayefurahishwa kuishi maisha niliyoishi mimi................................................................ 207

25. Msiba uliotufika umetokana na kufanya ‘Ijtihad’ dhidi ya ‘Nnassi’.................................................. 215
*Ni nani aliyeanzisha Istilahi ya *Ahlus-Sunnah Wal-Jamaa?!* .............................................. 223

26. Mwito kwa Marafiki kuja kufanya utafiti............................ 225
27. Uongofu wa Haki.............................................................. 231
28. Rejea zilizotumika............................................................. 243

# UTANGULIZI

**Na:**

***Allamah Sayyid Saeed Akhtar Rizvi***

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيمِ

الْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعَالَمِيْنَ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى

خَيْرِ خَلْقِهٖ مُحَمَّدٍ وَّاٰلِهِ الطَّاهِرِيْنَ

Kitabu kilichopo mikononi mwako ni tarjuma ya Kitabu cha Kiarabu, kiitwacho ***Thummah-tadaytu,*** kilichoandikwa na Shaikh Muhammad Tijani Samawi wa Tunisia. Katika Kitabu hiki ameelezea kuhusu safari yake kuelekea kwenye Imani ya Kishi‘a. Kitabu hiki kimekuwa maarufu katika ulimwengu wa Kiislamu na tayari kimetafsiriwa katika lugha za Kiingereza, Urdu na Kiajemi. Wanachuoni wengi katika Afrika ya Mashariki wametuomba tukitafsiri kitabu hiki katika lugha ya Kiswahili pia.

Nilimuomba Shaikh Musabbah Sha’ban Mapinda kukitarjumi kitabu hiki katika lugha ya Kiswahili kutoka kwenye asili yake ya lugha ya Kiarabu. Namshukuru kwa kukubali ombi langu na kuifanya kazi hii kwa moyo mkunjufu. Nimeiangalia pamoja naye tarjuma hii kwa makini kuhakikisha kuwa maudhui yake ya asili hayakupotoshwa katika lugha ya Kiswahili.

Tunamshukuru Allah Subhanahu wa Ta‘ala na wale wote wanaotuunga mkono kwa njia moja au nyingine kwa kufanikisha kuchapishwa kitabu hiki. Tunamuomba Mwenyezi Mungu (s.w.t.) awalipe malipo mema hapa Duniani na baadaye huko Akhera. Amin.

Shaikh Tijani Samawi ameandika vitabu vitatu zaidi baada ya kitabu hiki; na Shaikh wetu Shaikh Musabbah Sha'ban pia ametrjumi vitabu viwili vifuatavyo kwa lugha ya Kiswahili:

*1. Li Akuna Ma'as-Sadiqin (Niwe pamoja na Wakweli)*
*2. Fas'alu Ahladhdhikr (Waulizeni Wanaofahamu)*

Mission inatoa shukurani zake za dhati kwa Mtarjumi na kwa wale wote waliosaidia kwa njia moja au nyingine katika uchapishaji wa kitabu hiki.

Dar-es-Salaam
15 Shaban 1420
24 November 1999

Sayyid Saeed Akhtar Rizvi
Mhubiri Mkuu

# ZAWADI

Kitabu changu ni kidogo hakina mikogo ndani yake, nacho kinakhusu kisa cha safari, kisa ambacho ni cha uvumbuzi mpya, siyo uvumbuzi unaohusu ulimwengu wa kiufundi na mazingira, lakini kinahusu uvumbuzi wa Dunia ya kiitikadi katika wingi wa madhehebu na falsafa za kidini.

Kwa ujumla uvumbuzi unategemea kwanza, akili iliyosalimika na fahamu madhubuti ambayo ndio iliomtenganisha mtu na viumbe wengine.

Kwa hiyo basi, mimi ninakitoa zawadi kitabu changu kwa kila mwenye akili iliyosalimika ambayo itachambua na kuifahamu haki kutokana na wingi wa batili, na atayapima maneno kwa mizani ya uadilifu na kuunga mkono kile kinachokubalika kiakili, na kulinganisha maneno na mazungumzo, kisha atabaini hoja inayokubalika kiakili kutokana na ile isiyokubalika kiakili na hoja yenye nguvu kutokana na hoja dhaifu.

Mwenyezi Mungu anasema:- *"Wabashirie waja wangu ambao wanasikiliza maneno na kufuata yale yaliyo mazuri mno, hao ndiyo ambao Mwenyezi Mungu amewaongoza, na wao ndiyo wenye akili."* Basi kwa wote hawa natoa zawadi ya kitabu changu hiki, hali ya kuwa nikitaraji kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu azifungue fahamu zetu kabla ya macho yetu, atuongoe na azitie nuru nyoyo zetu na atuoneshe haki kuwa ni haki waziwazi nasi tuifuate, na atuoneshe upotofu kuwa ni upotofu bila kificho na tujiepushe nao. Pia atuingize katika waja wake wema, kwa hakika yeye ni mwenye kusikia, mwenye kujibu maombi.

***MUHAMMAD AL-TIJANI AL-SAMAWI***

*KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU*

# DIBAJI

Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu, ambaye amemuumba mtu kutokana na udongo akamuweka katika umbo bora, na akamfadhilisha juu ya viumbe wengine kisha akawaamuru Malaika wake watakatifu wamsujudie. Akamtukuza kwa kumpa akili ambayo hubadilisha shaka yake na kuwa yakini, halafu akamjaalia macho mawili na ulimi na midomo miwili na akamuonesha njia mbili. Kisha akamtumia Mitume wenye kubashiria mema na wenye kuonya maovu ili wamzindue na wamlinde kutokana na upotovu wa ibilisi aliyelaaniwa, na akamuagiza kuwa asimuabudu shetani kwani shetani ni adui aliyedhahiri kwake na (akamuagiza) amuabudu yeye Mwenyezi Mungu peke yake na afuate njia iliyonyooka, hali ya kuwa ni mwenye kutambua uongofu, imani na Elimu ya yakini. Hatimaye akamuagiza awe katika itikadi ya kumuamini Mwenyezi Mungu, asifuate (tu itikadi za) jamaa na ndugu na wazazi waliotangulia, ambao waliwafuata waliokuwa kabla yao bila ya dalili iliyowazi wala hoja. Sasa basi, Ni nani mwenye kauli njema kuliko yule anayewalingania (watu) kwa Mwenyezi Mungu na akatenda mema na akasema, bila shaka mimi ni miongoni mwa waliojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu).

Kisha (naziomba) rehma za Mola wangu, salamu zake na baraka zake zimshukie Mtume aliyetumwa kuwa ni rehma kwa walimwengu, mtetezi wa wenye kudhulumiwa na wenye kudhalilishwa. Muokozi wa Wanaadamu kutoka kwenye upotovu wa wajinga na kumuelekeza kwenye uongofu wa waumini. Yeye ni Bwana wetu na msimamizi wetu Mwana wa Abdillahi, ambaye ndiye Mtume wa Waislamu.

Na ziwashukie Āli (Jamaa) zake wema waliotakasika, ambao Mwenyezi

Mungu amewateua juu ya viumbe wengine ili wawe ni kigezo cha waumini, na mnara wa wenye kutambua na ni alama ya wakweli na wenye utakaso wa moyo. Mwenyezi Mungu amewajibisha ndani ya Qur'an tukufu kuwapenda, baada ya kuwatakasa na akawajaalia kuwa miongoni mwa waliohifadhika, na akamuahidi uokovu mwenye kupanda safina yao, na yeyote mwenye kuwapa mgongo atakuwa miongoni mwa wenye kuangamia. Vile vile rehema na amani ziwashukie Masahaba wake Mtume wenye baraka, ambao walimtetea, wakamsaidia, wakamtukuza na wakajitolea nafsi zao kwa ajili ya kuinusuru dini, na wakaifahamu haki kisha wakampa ahadi ya utii kwa yakini. Na walisimama imara baada yake katika njia ya haki na wala hawakugeuza wala kubadilisha na walikuwa miongoni mwa wenye kushukuru. Basi Mwenyezi Mungu awalipe mema kwa kuutumikia Uislamu na Waislamu na (pia rehma na amani) ziwashukie waliowafuatia na wapitao njia ya uongofu wao mpaka siku ya Qiyama.

Mola wangu nikubalie (kazi yangu), kwa hakika wewe ni Mwenye kusikia Mwenye kujua, na uukunjue moyo wangu kwani wewe ndiyo mwenye kuongoa kwenye yakini ya kweli. Na ninakuomba uufungue mfundo wa ulimi wangu, kwani wewe ndiye Mwenye kutoa hekima kwa yule umtakaye miongoni mwa waja wako wenye kuamini. Mola wangu nizidishie Elimu na unikutanishe na watu wema.

# HALI YA MAISHA YANGU KWA UFUPI

Bado nakumbuka namna baba yangu mzazi alivyonichukua kwenda naye kwenye Msikiti ulioko mtaani, ambamo husaliwa sala ya Tarawehe katika Mwezi wa Ramadhani, na umri wangu ulikuwa miaka kumi, na akanitanguliza kwa watu wanaosali ambao kunifurahia kwao ni jambo ambalo halikufichikana.

Tangu hapo kabla nilikuwa nafahamu kwamba, Mwalimu alikuwa amepanga nisalishe sala ya Tarawehe siku mbili au tatu. Kwa kawaida ilikuwa nikiswali nyuma katika sala ya jamaa pamoja na kundi la watoto wa mtaani na nilikuwa nikisubiri Imam (wa msikiti ule) afikie kwenye nusu ya Qur'an inayofuatia yaani katika *Surat-Mar-yam*. Baba yangu mzazi alikuwa anahima tujifunze Qur'an katika Madrasa, na pia nyumbani katika vipindi vya usiku vilivyokuwa vikisimamiwa na Imam wa Msikiti mkuu ambaye ni jamaa yetu aliyekuwa kipofu na amehifadhi Qur'an tukufu. Kwa hiyo mimi nilikuwa nimehifadhi nusu ya Qur'an katika umri huo mdogo, na kwa ajili hiyo Mwalimu alitaka kudhihirisha uhodari wake na juhudi yake kupitia kwangu. Akanifundisha vituo vya kusimama katika kusoma na akanikaririsha mara nyingi ili athibitishe kuwa nimeifahamu.....

Baada ya kufaulu kwangu Mtihani na kuikamilisha na kisomo katika sala ya jamaa tena vizuri kama alivyokuwa akitarajia Mzazi wangu pamoja na Mwalimu, watu wote walinifuata wakanibusu na kufurahiwa na kumshukuru Mwalimu aliyenifunza na kumpongeza mzazi wangu, na wote walikuwa wakimshukuru Mwenyezi Mungu juu ya neema ya Uislamu na baraka za Sheikh.

Huenda kumbukumbu ya mambo niliyoyapata baada ya tukio hilo haitafutika katika maisha yangu kutokana kufurahiwa kwa watu na mimi na umashuhuri ambao ulivuka mtaa wetu na kuenea mji wote. Siku hizo

za Mwezi wa Ramadhani ziliweka athari ya kiitikadi katika maisha yangu, athari ambayo imebakia mpaka leo. Kutokana na hali hiyo kila nilipokuwa nikiteleza, nilihisi nguvu ya ajabu inanisukuma na kunirejesha kwenye umadhubuti, na kila nilipohisi unyonge na uzembe wa kibinafsi, basi kumbukumbu hizo huninyanyua na kuniweka kwenye daraja za juu kiroho na huwasha miali ya imani katika dhamira yangu ili niweze kuyabeba majukumu.

Na ni kama kwamba jukumu hilo alilonibebesha Mzazi wangu na (tuseme) zaidi Mwalimu wangu, juu ya kuongoza sala ya jamaa katika umri ule mdogo, lilinifanya siku zote nione kuwa mimi sijaweza kufikia kiwango ninachokikusudia, au niko chini ya kiwango kitakiwacho kwangu.

Kwa hiyo niliutumia muda wa utoto wangu na ujana wangu katika muongozo kwa kiwango fulani bila ya kuepukana na mchezo na utashi unaotawaliwa wakati mwingi na utoto na kupenda kujuwa na kuiga, hali ya kuwa uangalizi wa ki-Ungu ukinizunguka ili niwe mwenye kutambulikana baina ya ndugu zangu kwa umakini na utulivu na kutokuteleza katika maasi na maovu.

Sitaacha kueleza kwamba mama yangu *(Mwenyezi Mungu amrehemu)* alikuwa na athari kubwa katika maisha yangu. Kwa hakika yeye ndiye aliyeyafungua macho yangu kwa kunifundisha sura fupi fupi za Qur'an Tukufu kama ambavyo alinifunza Sala na Tahara, na alinisimamia kwa uangalizi wa pekee kwani mimi nilikuwa ndiye mwanawe wa kwanza.

Na alikuwa akiishi na mke mwenzie ndani ya nyumba hiyo hiyo ambaye alimtangulia kwa miaka mingi na ana watoto wengi ambao kuna waliokuwa wakimkaribia (Mama yangu) kwa umri. Hivyo basi alikuwa akisimamia malezi yangu na mafunzo yangu kama kwamba anafanya ushindani na mke mwenzie na watoto wa mumewe.

Jina hili la Tijani alilonipa Mama yangu lina ubora wa kipekee kwa familia zote za *Wasamawi* ambao wameikubali Tarika ya *Tijaniyah* na wamedumu nayo tangu mmoja wa watoto wa Sheikh Sayed Ahmad Tijani alipozuru mji wa Qafsah akitokea Algeria na akafikia katika nyumba ya Msamawi mmoja. Kwa hiyo wengi miongoni mwa watu wa mjini hasa familia za watu wenye elimu na matajiri wakaikubali Tarika hii ya

Kisufi na wakaipupia. Kutokana na jina langu hili, nimekuwa ni mwenye kupendwa mno katika mji wa Wasamawi ambao unakaliwa na zaidi ya familia Ishirini na pia nje yake wako watu miongoni mwao ambao wanayo maungamano na Tarika ya Tijaniyah. Kwa ajili hiyo wengi wa wazee waliokuwa wakisali ambao walikuwepo katika zile siku za Ramadhani nilizozitaja, walikuwa wakibusu kichwa changu na mikono yangu hali ya kuwa wakimpongeza Mzazi wangu na wakimuambia: *"Hizi ni miongoni mwa baraka za Bwana wetu Sheikh Ahmad Tijani."* Kwa kweli inafaa kusema kwamba, Tarika ya Tijaniyah imeenea kwa wingi huko Morocco, Algeria, Tunisia, Libya, Sudan na Misri, na kwamba wanaokubali Tarika hii wanayo namna fulani ya kuishikilia itikadi yao kwani hawazuru Makaburi ya Mawalii wengine kwa kuwa (wanaamini kwamba) Mawalii wote wamesoma kutoka kwa baadhi yao kwa kuachiziana isipokuwa Sheikh Ahmad Tijani yeye amechukua elimu yake moja kwa moja toka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) japokuwa amekuja baada ya zama za Utume kwa karne kumi na tatu. Na wanasimulia kwamba, yeye Sheikh Ahmad Tijani alikuwa akieleza kuwa, "Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) alimjia akiwa macho siyo usingizini." Kama ambavyo wanasema kwamba, "Dua kamili aliyoitunga Sheikh wao ni bora kuliko khitimisho la Qur'an tukufu mara arobaini."

Ili tusije tukatoka nje ya wigo wa kufupisha maelezo, tunaishia hapa kuhusu taarifa ya Tijaniyah tutawarudia tena Mwenyezi Mungu apendapo katika sehemu nyingine ya kitabu hiki.

Kwa hiyo basi nililelewa na kukulia katika itikadi hii kama ilivyo kwa vijana wengine wa mjini kwetu, sisi sote Al-hamdulilah tukiwa ni Waislamu wa Ahli Sunnah wal-Jamaah ndani ya Madh-hebu ya Maliki ibn Anas ambaye ni Imam wa mji wa Hijra (Madina), isipokuwa tumegawanyika katika Tarika za kisufi ambazo ni nyingi mno huko kaskazini mwa Afrika, kwani katika mji wa Qafsah peke yake kuna Tarika za *Tijaniyyah, Qadiriyah, Rahmaniyah, Salamiyah na Aisawiyah.* Na kila Tarika inao wafuasi wanaohifadhi qasida, dhikri, na nyiradi zake ambazo hufanywa katika hafla na mikesha ndani ya minasaba ya ndoa, jando, mafanikio fulani au nadhiri. Japokuwa yako baadhi ya mambo yasiyokubalika (katika sheria), lakini tarika hizi zimefanya kazi kubwa kuhifadhi mambo matukufu ya dini na kuwaheshimu Mawalii na watu wema.

# SAFARI YA KWENDA KUHIJI NYUMBA TUKUFU YA MWENYEZI MUNGU

Umri wangu ulikuwa miaka kumi na minane wakati Jumuiya ya Taifa ya maskauti wa Tunisia iliponiita kwa ajili ya kwenda kushiriki kwenye mkutano wa Maskauti wa nchi za Kiarabu na Kiislamu, (mkutano) ambao ulifanyika katika mji Makatifu wa Makkah nami nikiwa ndani ya ujumbe wa watu sita mashuhuri wa Jamhuri ya Tunisia.

Mimi nilijikuta kuwa ndiye mdogo kwa umri miongoni mwa wajumbe waliotumwa na pia mwenye elimu ndogo kuliko wote, kwani wawili kati yao walikuwa ni miongoni mwa walimu wakuu wa shule na mtu wa tatu alikuwa ni mwalimu katika mji mkuu (wa nchi yetu) na mtu wa nne alikuwa mwandishi wa habari na mtu wa tano sikufahamu cheo chake, bali nilifahamu tu kuwa yeye ni mmoja wa jamaa za Waziri wa Elimu katika zama hizo.

Safari yetu haikuwa ya moja kwa moja, tulishuka Athens ambao ni mji mkuu wa nchi ya Ugiriki mahali ambapo tulimaliza siku tatu na kutoka hapo tulikwenda Aman mji mkuu wa Jordan, na tulikaa hapo siku nne, na baada ya hapo tulifika Saudia, ambapo tulishiriki mkutanoni na tukafanya ibada za Hijja na Umra.

Hisia zangu zilikuwa hazielezeki wakati nilipokuwa naingia katika nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu kwa mara ya kwanza na moyo wangu ulikuwa kama unataka kuzivunja mbavu ambazo zinauzunguka kutokana na kudunda kwa nguvu hali ya kuwa unataka kutoka ili wenyewe uione nyumba hii kongwe ambayo umekuwa ukiiota kwa muda mrefu. Machozi yalinitiririka mpaka nikadhania hayatakatika, na nilijiona kama kuwa Malaika wananibeba juu ya Mahujaji wote ili nifikie kwenye paa la Kaaba tukufu na ninaitikia wito wa Mwenyezi Mungu nikiwa huko *''Labbaika-Allahumma labbaik''* ewe Mwenyezi Mungu huyu mja wako amekuja kwako.

Nilibaini hali ya kuwa nasikia *Tal-biyah* za Mahujaji ya kuwa, watu hawa wamemaliza umri wao hali ya kuwa wakijiandaa na wakifanya matayarisho na kukusanya mali ili waje hapa. Ama mimi kuja kwangu kulikuwa ni kwa ghafla bila ya maandalizi yatokanayo nami. Ninakumbuka kwamba Mzazi wangu alipoiona tiketi ya ndege na akayakinisha kuwa nitasafiri kwenda Hijja, alilia hali ya kuwa ananibusu na kuniaga huku anasema: "Hongera ewe mwanangu kwa hakika Mwenyezi Mungu ametaka uhiji kabla yangu nawe ukiwa katika umri huu, basi wewe ni mtoto wa Sayyid Ahmad Tijani, niombee kwa Mwenyezi Mungu katika nyumba yake anikubalie toba yangu na aniruzuku kuhiji nyumba yake tukufu."

Kwa ajili hiyo nilidhania kwamba Mwenyezi Mungu ndiye aliyeniita na akaniweka katika himaya yake na kunifikisha mahala hapo ambapo watu wanakufa bila kupafikia hali ya kuwa ni wenye simanzi na masikitiko, kwa hiyo inanistahikia mno mimi kufanya Talbiyah. Nilikuwa nikitufu mno na kusali sana na kufanya *Saa'yi (Baina ya Safa na Mar-wa)*.

Hata maji ya *Zamzam* nikiyanywa kwa wingi, na kupanda katika mlima mahala ambapo watu hushindana kufika kwenye pango la Hiraa na juu ya mlima uitwao *Jabal-Nnur,* hakuna aliyenishinda isipokuwa kijana mmoja wa Kisudani. Hivyo basi nilikuwa wa pili katika wawili *(Thaniyath-nain)* na niligaagaa ndani yake kama kwamba ninagaagaa ndani ya mapaja ya Mtume Mtukufu (s.a.w.) na ninaivuta pumzi zake, Aah.... kumbukumbu zilizoje ambazo zimeacha ndani ya nafsi yangu athari kubwa ambayo kamwe haitafutika!!

Majaaliwa mengine ya Mwenyezi Mungu, yalimfanya kila anionaye miongoni mwa wajumbe anipende na kutaka anuani yangu ili tuwasiliane. Hapana shaka kwamba, wenzangu ambao walinidharau tulipokutana nao kwa mara ya kwanza tukiandaa safari katika mji mkuu wa Tunis hatiamaye walinipenda, na nilihisi hivyo na nikavumilia kutokana na kujua kwangu toka mwanzo kwamba watu wa kaskazini (ya nchi yetu) wanawadharau watu wa kusini na wanawaona kuwa hawajaendelea. Lakini ghafla mtazamo wao ulibadilika wakati wa safari na mkutanoni na katika Hijja. Nilizing'arisha nyuso zao kwa mambo niliyokuwa nimeyahifadhi miongoni mwa Qasida na Mashairi na zawadi nilizopata katika mashindano ambayo yalifanyika katika mnasaba ule, na nilirejea

nchini kwangu nikiwa na zaidi ya anuani ishirini za marafiki wa mataifa mbali mbali.

Tulikaa Saudia kwa muda wa siku ishirini na tano na tulikuwa tukikutana na wanachuoni na kuwasikiliza katika mihadhara yao, na kwa hakika niliathirika kwa baadhi ya itikadi za Kiwahabi ambazo nilizipenda na nikatamani Waislamu wawe katika itikadi hizo. Kwa wakati huo nilidhani kuwa Mwenyezi Mungu amewachagua kutoka miongoni mwa waja wake kwa ajili ya kulinda nyumba yake tukufu, hivyo basi wao ni watakatifu na wanajua kuliko kiumbe mwengine wa Mwenyezi Mungu duniani, na Mwenyezi Mungu amewatajirisha kwa (kuwapa) petroli ili waweze kuwahudumia mahujaji ambao ni wageni wa Mwenyezi Mungu na pia kulinda usalama wao.

Wakati wa kurudi nchini kwangu kutoka Hijja nilikuwa nimevaa vazi la Kisaudia, na nilishtukizwa na mapokezi aliyokuwa ameyaandaa Mzazi wangu, kwani kulikuwa na watu wengi waliokusanyika kituoni wakiongozwa na Masheikh wa Tarika za Aisawiyah, Tijaniyah na Tarika ya Qadiriyah wakiwa na ngoma na dufu.

Walinizungusha katika mitaa ya mji wakifanya Tahlil na Takbira na kila tukipita kwenye Msikiti baadhi ya wakati walinisimamisha kwenye kizingiti chake na watu wakiwa pembeni yangu wakishindana kutaka kunibusu na hasa wazee wenye umri mkubwa walikuwa wakinibusu hali ya kuwa wanalia kwa shauku ya kutaka kuiona nyumba ya Mwenyezi Mungu na kusimama kwenye kaburi la Mjumbe Wake. Kwa hakika walikuwa hawajazoea kumuona Haji mwenye umri kama wangu, kama ambavyo jambo hili walikuwa hawajaliona katika Qafsah kabla yangu.

Niliishi maisha ya furaha katika wakati wote huo, na nyumbani kwetu walikuja watu wakubwa mashuhuri wa mjini kunisalimia na kunipongeza na wakiniombea. Mara nyingi walikuwa wakinitaka niwasomee fatiha na dua mbele ya Mzazi wangu, basi wakati mwingine nilikuwa naona haya na nikijipa moyo, naye Mama yangu kila mara alikuwa akiingia baada ya wageni waliokuja kuniona wanapotoka ili awashe ubani na kunifanyia kago kwa lengo la kunikinga kutokana na shari za mahasidi na kuniepusha na vitimbi vya mashetani.

Baba yangu alifanya karamu kwa muda wa siku tatu mfululizo kwa ajili ya wana Tarika wa Tijaniyah. Kila siku akichinja Kondoo na watu walikuwa wakiniuliza kila mambo makubwa na madogo na majibu yangu yote, aghlabu yalikuwa yakishikamana na kuwapenda na kuwasifu Wasaudia na kazi wanayoisimamia katika kueneza Uislamu na kutetea Waislamu.

Wakazi wa mjini wakanipa jina la "*Haji*," basi ikawa litajwapo jina hili haliendi kwingine isipokuwa kwangu, na baada ya hapo nikawa maarufu mno hasa hasa ndani ya makundi ya watu wa dini kama vile *"Jamaatu Ikh-wanil-Musli-mina".*

Nilikuwa nikizunguka katika Misikiti na kuwakataza watu kubusu makaburi na kujipangusia kwenye mbao, na nikijaribu juhudi zangu zote kuwakinaisha kwamba kufanya hivyo ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu. Utendaji wangu wa kazi ulizidi kupanuka, kwani nilikuwa nikitoa mafunzo ya kidini ndani ya Misikiti siku ya Ijumaa kabla ya khutba ya Imam na nikihama kutoka Msikiti wa Abu Yaa'qub kwenda Msikiti Mkuu, kwani sala ya Ijumaa katika Misikiti hiyo husaliwa kwa nyakati tofauti wakati ambapo ya kwanza husaliwa wakati wa adhuhuri, ya pili husaliwa wakati wa Alasiri.

Na ni mara nyingi wengi wa watu waliokuwa wakihudhuria masomo hayo niliyokuwa nikiyatoa siku ya Jumapili ni wanafunzi wa shule ya Sekondari ambayo nilikuwa nikisomesha somo la Teknolojia na ufundi, na walikuwa wakishangazwa na jambo hili na wakizidi kunipenda na kunihishimu kwani nilikuwa nawapa wakati mwingi kuwaondolea ndani ya fikra zao utando (wa fikra mbaya) zilizogandamizwa na baadhi ya waalimu wa falsafa za kikafiri na wasioamini Mungu na Wakomunisti na wengine wengi zaidi ya hao.

Hivyo basi walikuwa wakingojea kwa shauku wakati wa mafunzo hayo ya kidini, na miongoni mwao wakija nyumbani, na nilinunua vitabu vya dini na nikavisoma kwa bidii ili niwe katika kiwango cha kuweza kujibu maswali mbali mbali.

Katika mwaka huo niliohiji vile vile nilikamilisha nusu ya dini yangu, kwani mama yangu (Mwenyezi Mungu amrehemu) alipendekeza aniozeshe kabla ya kufa kwake, naye ndiye aliyewalea watoto wote wa mumewe na akahudhuria harusi zao. Kwa hiyo shauku yake ilikuwa anataka kuniona nimeoa, na Mwenyezi Mungu alimkubalia kile alichokitamania nami nilitii amri yake kwa kumuoa msichana mmoja ambaye nilikuwa sijamuona hapo kabla, na mama yangu alihudhuria kuzaliwa kwa mwanangu wa kiume wa kwanza na wa pili, na alifariki hali ya kuwa ameniridhia kama ambavyo Baba (Mwenyezi Mungu amrehemu) alikuwa amemtangulia mama kabla ya miaka miwili na alihiji Nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu na akatubia toba ya kweli kabla ya kufariki kwake kwa miaka miwili.

Katika kipindi ambacho Waislamu na Waarabu walikuwa wakinyanyasika kutokana na kushindwa katika vita vyao dhidi ya Israel, Mapinduzi ya Libya yalifaulu na akatuchomozea yule kijana ambaye ndiye Kiongozi wa Mapinduzi hali ya kuwa akizungumza kwa niaba ya Waislamu, na akisalisha watu Msikitini na kutoa mwito kuikomboa Quds. Kwa hakika alinivutia kama ambavyo aliwavutia vijana wengi Waislamu katika nchi za Kiarabu na za Kiislamu na alitulazimisha kupenda kuangalia (uwezekano) wa kuandaa safari ya mafunzo kwenda Libya. Tulikusanya watu arubaini miongoni mwa watu wasomi na tulifanya ziyara ya nchi hiyo ndugu mwanzoni kabisa mwa mapinduzi.

Tulirejea toka huko hali ya kuwa ni wenye kufurahishwa na mambo tuliyoyaona tukitazamia mustaqbali ambao tulitarajia kuwa utakuwa ndiyo suluhisho la Umma wa Kiarabu na Kiislamu ulimwenguni kote.

Muda wote huu uliopita mawasiliano ya barua na baadhi ya marafiki yalikuwa yakiendelea na mapenzi pia yakizidi, na mahusiano yangu na baadhi yao yaliimarika na walisisitiza niwatembelee. Nilijiandaa na nikayapanga mambo kwa ajili ya safari ndefu itakayomaliza likizo ya kiangazi ambayo hudumu miezi mitatu, na njia ilikuwa inapitia Libya kwa barabara kisha Misri na kutoka hapo hadi Lebanon kupitia Baharini hadi Syria na Jordan na hatimaye Saudia, napo ndipo penye makusudio ya kufanya *Umra* na kuimarisha mafungamano na Mawahabi ambao nimewatangaza mno miongoni mwa vijana wasomi na ndani ya Misikiti ambayo ndani yake *Ikhwanul-Muslimina* ni wengi.

Umaarufu wangu ulivuka mipaka ya mji wangu ukafika mpaka kwenye miji mingine ya jirani, basi huenda akapita msafiri akasali sala ya Ijumaa na kuhudhuria darasa zile na kwenda kulizungumzia katika jamii yake, na habari zikamfikia Sheikh Ismail Al-Hadifi, kiongozi wa Tarika mashuhuri ya kisufi katika mji wa Tuzer ambao ni mji mkuu wa Al-Jarid.

Sheikh huyu ana wafuasi na Murid wengi, katika Jamhuri nzima ya Tunisia na nje ya nchi yake miongoni mwa watu wanaofanya kazi huko Ufaransa na Ujerumani.

Wito wa kumzuru Sheikh huyo ulinifikia kupitia kwa watumishi wake walioko Qafsah, ambao waliniandikia barua ndefu wakinishukuru katika barua hiyo kutokana na kuhudumia kwangu Uislamu na Waislamu na wakadai kwamba jambo hilo haliwezi kunikurubisha kwa Mwenyezi Mungu japokuwa kidogo madamu siko katika Tarika ya Sheikh mwenye utambuzi, na pia kwa mujibu wa hadithi ambayo ni mashuhuri kwao (isemayo): “Asiyekuwa na Sheikh basi Sheikh wake ni shetani.” Vile vile wanasema kwamba “Ni lazima uwe na Sheikh atakayekuonesha njia, vinginevyo elimu yako uliyonayo ina upungufu.”

Walinibashiria kwamba *Sahibuz-Zaman* wakimlenga Sheikh Ismail ameniteua kutoka miongoni mwa watu ili niwe msiri wake.

Nilifurahi sana kutokana na khabari hizi na nililia kwa kuathirika na majaaliwa haya ya Mola ambayo yanaendelea kuninyanyua kutoka daraja ya juu hadi ya juu zaidi, na kutoka (mahali) pazuri hadi pazuri zaidi, kwani mimi hapo zamani maishani mwangu nilikuwa nikimfuata Sayyid yangu Al-Hadi Al-Haf-Yan ambaye ni Sheikh wa Tasawwuf. Yeye anasimuliwa kuwa na karama na mambo yasiyo ya kawaida, na nilikuwa katika vipenzi wake wakubwa, kama ambavyo nilifuatana na Sayyid yangu Saleh Bas-saih, na Sayyid yangu Jailani na wengineo miongoni mwa watu wa Tariqa wa miaka ya hivi karibuni, kwa hiyo niliungojea mkutano huo (na Sheikh Ismail) kwa shauku.

Nilipoingia nyumbani kwa Sheikh nilikuwa nikiziangalia nyuso za watu kwa hamu kubwa, na ukumbi ulikuwa umejaa wanamuridi. Miongoni mwao wamo Masheikh waliovaa mavazi meupe sana, na

baada ya kusalimiana, Sheikh Ismail alitutokea na wote wakasimama wakambusu mkono wake kwa hishima kubwa na yule wakili akanikonyeza kunijulisha kuwa huyu ndiye Sheikh mwenyewe. Mimi sikuonesha hamasa yoyote, kwani nilikuwa nikimsubiri asiyekuwa huyu niliyemuona kwa kuwa nilikuwa nimeunda picha ya kimawazo kufuatia karama na miujiza ambayo wakili wa Sheikh na wafuasi wake waliingiza katika akili zangu. Nilimuona ni Sheikh wa kawaida tu, hana haiba wala utukufu. Katikati ya kikao yule wakili alinitambulisha kwake naye akanikaribisha na kunikalisha kuliani kwake na nikapewa chakula.

Baada ya kula na kunywa, hadhara ile ilianza na akanitambulisha upya yule wakili ili nichukue ahadi na nyiradi kutoka kwa Sheikh.

Baada ya hapo wote walinipongeza, kunikumbatia na kuniombea baraka, na nilitambua kutokana na mazungumzo yao kwamba wao wanasikia mambo mengi juu yangu, na huu upendo wao kwangu ulinifanya nijione na kunisukuma nipinge baadhi ya majibu ya Sheikh aliyokuwa akiyatoa kwa waulizaji na nikitetea maoni yangu kwa kutumia Qur'an na Sunna.

Baadhi ya waliohudhuria hapo walichukizwa na huu uingiliaji kati na wakauzingatia kuwa ni utovu wa adabu mbele ya Sheikh na wao wamezoea kutozungumza mbele yake isipokuwa kwa idhini yake.

Sheikh aligundua chuki ya watu waliokuwepo hapo, basi akaiondosha kwa uerevu hali ya kuwa akisema: "Yeyote ambaye mwanzo wake ulikuwa wenye kuungua basi mwisho wake ni wenye kung'ara". Na wote waliohudhuria hapo walielewa kuwa ni dalili kutoka kwa Sheikh ya kuthibitisha ufanisi wa mustakbali wangu.

Lakini Sheikh yule wa Tarika alikuwa mwerevu na mzoefu, hivyo hakunipa nafasi ya kuendeleza ufidhuli unaokera. Alitusimulia kisa cha mtu mmoja Mcha Mungu ambaye katika darasa lake walikaa baadhi ya watu wenye Ilimu, basi alimwambia mmoja wao kuwa "Simama uende ukaoge." Yule mtu mwenye Ilimu alikwenda akaoga na akaja kukaa kwenye darasa, yule Mcha Mungu akamwambia tena mara ya pili "Simama ukaoge." Yule mwenye Ilimu alisimama akarudia kuoga vizuri kwa kadri inavyowezekana, akidhania kuwa kuoga alikooga mara ya kwanza

kulikuwa siyo sahihi na akaja ili akae. Basi yule Sheikh Mcha Mungu akamkemea na akamwamuru akaoge upya, yule mwenye Ilimu akapiga kelele akasema, "Ewe Bwana wangu hakika nimeoga kwa mujibu wa Ilimu yangu na juhudi yangu, na hapa kilichobakia ni vile atavyonijaalia Mwenyezi Mungu kupitia mikononi mwako." Basi hapo ndipo yule Sheikh Mcha Mungu akamwambia "Sasa kaa."

Mimi nilitambua kuwa anayekusudiwa katika kisa hicho ni mimi kama ambavyo ndivyo walivyofahamu watu waliokuwepo hapo. Walinilaumu baada ya Sheikh Ismail kutoka kwa ajili ya mapumziko na wakanitaka ninyamaze na niwe na hishima mbele ya Sheikh ambaye ndiye "Sahibuz-Zaman" ili matendo yangu mema yasije yakaharibika. Walitoa ushahidi wa aya tukufu ya Qur'an isemayo" *"Enyi mlioamini musipaze sauti zenu kuliko sauti ya Mtume, wala musiseme naye kwa sauti ya nguvu kama munavyosemezana ninyi kwa ninyi ili vitendo vyenu visije kukosa thawabu na hali ya kuwa hamtambui." (Qur'an, 49:2)*

Niliitambua hishima yangu na nikafuata maelekezo na nasaha nilizopewa. Sheikh alinikurubisha zaidi na nilikaa kwake siku tatu, na muda wote huo nilikuwa nikimuuliza maswali mengi, baadhi ya maswali hayo nilimuuliza kumjaribu na Sheikh huyo alikuwa akilitambua hilo, basi hunijibu kwa kusema: "Bila shaka Qur'an ina maana za dhahiri na zingine za ndani zaidi hadi daraja saba." Pia alinifungulia kabati lake ambalo alinionyesha daftari lake maalum ambalo ndani yake umo mfululizo wa majina ya watu wema na wachamungu, (mfululizo ambao) unafikia kwa Abul-Hasan As-Shadhiliy unaopitia kwa mawalii wengi waliotajwa hadi kufikia kwenye sanad ya Imam Ali ibn Abitalib, *Mwenyezi Mungu ametukuza uso wake na amemuwia radhi.*

Hapa sitaacha kueleza kwamba darasa walizokuwa wakizifanya ni za kiroho, kwani Sheikh alikuwa akizifungua kwa kusoma aya chache za kitabu cha Mwenyezi Mungu kwa Taj-wid, kisha baada ya kumaliza huanza kusoma Qasida na humfuata wale Muridi ambao wamehifadhi Mad-hi na Dhikri ambazo nyingi miongoni mwa hizo ni za kuishutumu Dunia na kupendelea Akhera, na ndani yake zina mafunzo ya uchamungu. Baada ya hapo Murid wa kwanza aliyekaa kuliani mwa Sheikh, hurudia kusoma aya chache za Qur'an, na anaposema, *"Sadaqallahu-Adhim,"*

Sheikh huanzisha upya Qasida na wote hushiriki kuisoma. Basi hivyo hivyo hupokea waliohudhuria kusoma japo aya moja, na hushirikiana hivyo mpaka wote waenee. Wakati wote huo, huwa wanayumbayumba kulia na kushoto kwa kufuata sauti ya Mad-hi hizo na khatimaye Sheikh hunyanyuka na Muridi nao hunyanyuka pamoja naye na hufanywa duara. Yeye Sheikh huwa katikati yake na huanza kufanya dhikri kwa kusema *"Aah aah aah"* na huku akizunguka katikati yao hali ya kumuelekea kila mara mmoja miongoni mwao mpaka panakuwa mtikisiko mkubwa kiasi cha kuufananisha na ngoma. Baadhi yao huruka huku na huko kama wamepatwa na kichaa, na sauti za kuimba huwa kubwa zilizopangika, lakini zinakera. Mwisho utulivu hurejea baada ya shida na taabu, na Sheikh husoma Qasida ya mwisho, kisha wote hukaa baada ya kukibusu kichwa cha Sheikh na mabega yake mmoja baada ya mwingine.

Mimi nilishirikiana nao katika harakati hizi, nikiwafuatisha tu lakini bila ya ridhaa yangu, na kwa kufanya hivyo nilijikuta nikipingana na itikadi yangu niliyokuwa nimeichagua, ambayo ni kutokumshirikisha Mwenyezi Mungu, kutokufanya *tawassul* kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu. Kutokana na hali hiyo niliangukа chini nikawa karibu kulia hali ya kuwa nimechanganyikiwa. Mawazo yakawa yamegawanyika baina ya fikra mbili zinazopingana, fikra ya kisufi ambayo ni undani wa kiroho anaoishi nao mtu na humjaza undani wake hisiya za kitawa na kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa njia ya mawalii wake wema na waja wake wenye uchamungu, na fikra (nyengine) ya Kiwahabi ambayo ilinifundisha kuwa yote hayo ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu hawezi kusamehe ushirikina.

Na iwapo Muhammad Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) hanufaishi kitu wala hapafanywi *Tawasul* kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwake, basi wana daraja gani mawalii hawa na watu wema waliokuja baada yake?

Japokuwa (nilikuwa na) cheo kipya alichonipa Sheikh, kwani nilikwishakuwa wakili wake katika mji wa Qafsah, lakini ndani ya nafsi yangu sikukubaliana moja kwa moja ingawa wakati mwingine nilikuwa nikielekea kwenye Tarika za kisufi na siku zote nikihisi kuwa ndani ya nafsi yangu kumejificha heshima kubwa kwa hii Tarika kwa ajili ya Mawalii wa Mungu na watu wema miongoni mwa waja wa Mungu, lakini

nikipinga na kujadili kwa kutumia kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo; *“Wala usimuombe pamoja na Mwenyezi Mungu mwingine” (28:88).*

Na ikiwa mtu ataniambia kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: *“Enyi mulioamini mcheni Mwenyezi Mungu na tafuteni wasila wa kumfikia.” (5:35)* Mimi nitamjibu kwa haraka kama walivyonifunza wanachuoni wa Kisaudi. *“Wasila ni matendo mema.”*

Jambo la muhimu ni kwamba katika kipindi hicho niliishi hali ya kuwa nimechanganyikiwa, fikra yangu ikiwa ni yenye kutatizwa, na wakati mwingine baadhi ya Murid (Wafuasi wa Tariqa) wakija nyumbani kwangu na tunakesha na tukifanya dhikri *(ile ya Aah......Aah……)!!*

Majirani walianza kunung’unika kutokana na sauti zinazokera ambazo zinatokea kooni kwa kufanya dhikri ya *“Aaah”,* lakini walikuwa hawanidhihirishii mimi jambo hilo bali wao humlalamikia mke wangu kupitia kwa wanawake zao. Nilipotambua hilo niliwaomba watu hawa wafanye hafla hizo katika moja ya nyumba zao, na nikawaomba radhi kwa kuwaambia kwamba mimi huenda nikasafiri nje ya nchi kwa muda wa miezi mitatu na niliwaaga ndugu na jamaa nikaazimia (safari) hali ya kuwa nimetegemea kwa Mwenyezi Mungu bila ya kumshirikisha na chochote.

# SAFARI YENYE MAFANIKIO

# NIKIWA MISRI

Sikukaa sana Tripoli ambao ni Mji mkuu wa Libya isipokuwa kiasi cha kupata Visa kutoka kwa Balozi wa Misri ili niweze kuingia katika ardhi ya *Kinanah*.

Huko nilikutana na baadhi ya marafiki zangu wakanisaidia kupata Visa, Mwenyezi Mungu awalipe mema kwa juhudi zao hizo. Wakati nikiwa njiani kuelekea Cairo, safari ambayo ni ndefu inayochukua muda wa siku tatu mchana na usiku, nilipanda ndani ya gari ya kukodi ambayo nilishirikiana na Wamisri wanne wanaofanya kazi Libya na walikuwa wakirudi nchini kwao.

Tukiwa safarini nilikuwa nikiwazungumzisha na kuwasomea Qur'an, basi walinipenda mno na kila mmoja wao akanitaka nifikie nyumbani kwake, nami nilimchagua mmoja wao ambaye nafsi yangu iliridhika naye kutokana na uchamungu wake na jina lake akiitwa Ahmad; alinikaribisha na kunipokea ipasavyo, Mwenyezi Mungu amlipe mema.

Nilikaa muda wa siku ishirini mjini Cairo, na katika kipindi hicho nilimtembelea mwanamuziki aitwaye *Farid Al-Atrash* katika jumba lake lililoko kando kando ya mto Nile. Tangu hapo mwanzo nilikuwa nikimpenda kutokana na maelezo niliyokuwa nimeyasoma ndani ya magazeti ya Misri yanayouzwa huko kwetu Tunisia kuhusu tabia yake na unyenyekevu wake. Sikuwa na bahati ya kukaa naye muda mrefu isipokuwa dakika ishirini tu, kwani alikuwa akitoka kuelekea uwanja wa ndege ili asafiri kwenda Lebanon. Pia nilimtembelea *Sheikh Abdul-Basit Muhamad Abdus-Samad* ambaye ni msomaji mashuhuri wa Taj-wid, nami nilikuwa nikimpenda mno, na nilikaa naye kwa muda wa siku tatu.

Wakati tukiwa naye nilikuwa nikifanya majadiliano na nduguze na marafiki zake kuhusu maudhui mbali mbali, nao walikuwa wakifurahiwa na hamasa yangu, ukunjufu wangu na maarifa yangu mengi. Hivyo basi

wakizungumzia juu ya mambo ya sanaa kwangu ilikuwa ni kama nyimbo, na wakizungumza juu ya uchamungu na Tasawuf, niliwaeleza kuwa mimi ni mwana Tarika ya Tijaniyah na pia Madaniyyah. Na wakizungumza kuhusu ulimwengu wa Magharibi, mimi huwasimulia habari za Paris, Londoni, Ubelgiji, Holland, Italia na Hispania ambazo nilizitembelea wakati wa likizo ya kiangazi. Na wakiongea habari za Hijja, basi mimi huwajibu kwamba mimi nilikwisha hiji na sasa nakwenda Umrah, na niliwasimulia sehemu ambazo hawazifahamu hata watu waliokwisha Hijji mara saba, kama vile pango la Hiraa na pango la Thaur na *madhabahu* ya Nabii Ismail (a.s.).

Na iwapo watazungumza habari za Sayansi na Teknolojia mimi nitawatosheleza shauku yao kwa kuwapa mifano na istilahi mbalimbali, na wakiongea juu ya siasa basi mimi huwakatiza kwa mtazamo nilionao hali ya kusema: "Mwenyezi Mungu amrehemu *Nasir Salahud-Din Al-Ayyūb* ambaye alijiharamishia kutabasamu sembuse kucheka, na pindi watu wa karibu yake walipomlaumu na wakamwambia, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa ni mwenye tabasamu wakati wote aliwajibu, "Vipi mimi munanitaka nitabasamu wakati Msikiti wa Aqsa unakaliwa na maadui wa Mwenyezi Mungu, hapana bali namuapa Mwenyezi Mungu sintatabasamu mpaka niukomboe au nife kwa ajili yake."

Na katika kipindi hicho hicho, Masheikh wa Azhar walikuwa wakihudhuria vikao hivyo na wakifurahiwa na mambo niliyoyahifadhi miongoni mwa Hadithi na Aya (za Qur'an) na hoja zenye nguvu nilizokuwa nazo. Basi walikuwa wakiniuliza kuhusu chuo nilichosoma, hivyo mimi hujifaharisha kwa kuwaambia kwamba nimemaliza masomo yangu katika chuo kikuu cha *Zaituniyah* ambacho kimeasisiwa kabla ya Azhar tukufu, na nikiongeza kwamba hao watawala wa dola ya *Fatimiyyah* walioiasisi Azhar walitokea katika mji wa *Mah-diyyah* nchini Tunisia.

Pia nilifahamiana na wanachuoni wengi wakubwa katika chuo kikuu cha Az-har ambao walinizawadia baadhi ya vitabu. Na siku moja nilipokuwa ndani ya ofisi ya mmoja wa wasimamizi wa mambo yanayohusu chuo cha Az-har, alikuja mjumbe fulani wa Baraza la Mapinduzi la Misri na akamtaka ahudhurie mkutano wa Waislamu na wakuu wengine kwenye shirika kubwa mno miongoni mwa mashirika ya Reli ya Cairo kutokana

na uharibifu uliyofanyika baada ya vita vya mwezi June vya Waarabu na Waisraeli. Bwana huyo akakataa kwenda isipokuwa nifuatane naye. Huko kwenye kikao nilikaa katika meza ya wageni waheshimiwa kati ya wanachuoni wa Misri na *Abu Shanadah.* Walinitaka nihutubie mbele ya wageni waalikwa nami nililifanya hilo kwa wepesi kwa kuwa nimezowea kutoa mihadhara Misikitini na katika kamati za Utamaduni nchini mwangu.

Jambo muhimu kuliko yote niliyoyasimulia katika mlango huu ni zile hisia zangu zilianza kutakabari na nikapandwa na baadhi ya majivuno na nikadhani kabisa kwamba mimi nimekwisha kuwa Mwanachuoni, na ni kwa nini nisihisi hivyo hali ya kuwa Wanachuoni wa Chuo cha Az-hari walinishuhudia kwa hilo na wako miongoni mwao waliosema: "Inapasa mahala pako pawe ni hapa katika chuo cha Azhar."

Miongoni mwa mambo yaliyoniongezea fahari na majivuno ni kwamba, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ameniruhusu kuingia na kuona vitu alivyoviacha kama alivyodai muangalizi wa Msikiti wa Sayyidina Hussein ulioko Cairo, na aliniingiza peke yangu kwenye chumba ambacho hakifunguliwi na mwingine isipokuwa yeye na aliufunga mlango kisha akanifungulia sanduku na akatoa kanzu ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) nami nikaibusu, pia alinionesha baadhi ya mabaki mengineyo. Nilitoka humo huku nikilia nikiwa nimeathirika juu ya upendeleo wa Mtume (s.a.w.w) alionifanyia mimi binafsi na khasa huyu mwangalizi hakunidai pesa yoyote, bali alikataa na akachukua kidogo tu baada ya kumsisitiza achukue, na alinipongeza na kunibashiria kwamba mimi ni miongoni mwa waliokubaliwa mbele ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w).

Huenda tukio hili lilileta athari katika nafsi yangu na likanifanya niwe ninafikiri mno kwa siku kadhaa yale mambo wayasemayo Mawahabi kwamba Mtume (s.a.w.w) amekwisha kufa basi na mambo yake yamekwisha kama ilivyo kwa watu wengine. Kwa kweli sikuiafiki fikra hii, bali niliyakinisha upotofu wa itikadi hii kwani ikiwa Shahidi aliyeuawa katika njia ya Mwenyezi Mungu si maiti bali yu hai na anaruzukiwa mbele ya Mola wake, basi vipi isiwe kwa Bwana wa mwanzo na wa mwisho (Mtume Muhammad s.a.w.w)? Jambo hili liliongeza hisiya na nguvu na mwanga wa mafunzo niliyoyapata hapo nyuma katika uhai

wangu miongoni mwa mafunzo ya masufi ambao huwapa Mawalii wao na Masheikh zao uwezo na athari katika kutenda mambo, na wanakiri kwamba Mwenyezi Mungu peke Yake ndiye ambaye aliyewapatia uwezo huu kwa kuwa wao walimtii na wakayapenda mema yaliyoko Kwake.

Je? siye Mwenyezi Mungu (s.w.t.) aliyesema ndani ya Hadithil-Qud'si kwamba, *"Ewe Mja wangu nitii utakuwa kama mimi, utakiambia kitu kuwa kitakuwa."*

Ushindani wa ndani kwa ndani ulianza kunivuta, na muda wa kubakia kwangu Misri ulimalizika baada ya kuwa nilikuwa nikizuru Misikiti mingi katika kipindi hicho na nilisali katika Misikiti yote katika Misri kutoka ile ya Madh-hebu ya Malik hadi ile ya Abuhanifah na ile ya Shafii na Ahmad ibn Hanbal. Kisha nilikwenda kwa Bibi Zainab na Sayyidina Husein kama ambavyo nilitembelea zawiya ya Tijani. Na kuhusu hilo ninayo mengi ya kusimulia ambayo itachukua muda mrefu kuyafafanua nami nimeona ni bora kufanya mukhtasari.

# MKUTANO NDANI YA BOTI

Nilisafiri kwenda Alexandria katika siku maalum, mahali ambapo huegesha boti za Misri zinazosafiri kwenda Beirut, na nilijikuta mwili na fikra zangu vimechoka. Nilijilaza juu ya kitanda changu, basi nikalala kidogo, na boti ilikuwa imeng'oa nanga kiasi cha saa mbili au tatu zilizopita. Niliamshwa na sauti ya jirani yangu aliyesema, "Yaonesha huyu ndugu amechoka." Nilimjibu nikasema: "Ndiyo, safari ya kutoka Cairo kwenda Alexandria imenichokesha, kwani niliamka mapema ili niweze kufika kwa wakati uliopangwa, hivyo basi jana sikulala isipokuwa kidogo."

Kutokana na *Lahaja* yake nilitambua kuwa siyo Mmisri, na udadisi wangu kama ilivyo kawaida yangu ulinishawishi nitake kumfahamu. Kwanza nikajitambulisha mimi ndipo nilipofahamu kwamba yeye ni Muiraq na ni Mwalimu katika Chuo Kikuu cha Baghdad na jina lake ni *Mun-i'm* na alikuja Cairo kuwasilisha maandiko yake ya shahada ya udaktari katika Chuo cha Azhar.

Basi tulianza mazungumzo yanayohusu Misri na ulimwengu wa Kiarabu wa Kiislamu na kuhusu kushindwa kwa Waarabu na ushindi wa Wayahudi na mazungumzo mengine yenye kuhuzunisha. Mimi nilisema katika msingi wa maneno yangu kuwa, "Sababu ya kushindwa huku ni kugawanyika kwa Waarabu na Waislamu kwenye dola ndogo ndogo na vikundi, na madh-habi mengi licha ya wingi wao kwa idadi, basi hawana tena uzito wala mazingatio kuhusu mtazamo wa maadui zao."

Tulizungumza sana kuhusu Misri na Wamisri, na tulikuwa tukiafikiana juu ya sababu za kushindwa, nami niliongezea kwamba mimi ninapinga mgawanyiko huu ambao wakoloni wanautilia mkazo miongoni mwetu ili iwe rahisi kwao kututawala na kutudhalilisha, nasi bado tunatofautisha baina ya Madh-hebu ya Malik na Mahanafi. Nilisimulia kisa cha kuhuzunisha kilichonipata wakati nilipoingia katika Msikiti wa Mahanafi mjini Cairo na nikasali nao sala ya Alasiri kwa jamaa, mara ghafla baada

ya sala, mtu aliyekuwa kasimama pembeni yangu akaniambia kwa hasira "Kwa nini hufungi mikono katika Sala"? Mimi nikamjibu kwa hishima na adabu kwamba, "Wafuasi wa Malik hawafungi mikono nami ni Malik." akaniambia "Nenda kwenye Msikiti wa Malik na ukaswali huko." Basi nilitoka hali ya kuwa nimechukia; tena mwenye uchungu kutokana na tendo hili lililoniongezea tatizo juu ya tatizo.

Basi mara yule Mwalimu wa Kiiraq akatabasamu na kuniambia kuwa yeye ni Shia. Kutokana na khabari hii nilichanganyikiwa na nikasema bila kujali kwamba, "Lau ningejua kuwa wewe ni Shia basi nisingezungumza nawe." Akasema, "Kwa nini?" Mimi nikasema, "Ninyi siyo Waislamu; kwani ninyi mnamuabudu Ali ibn Abitalib, na walioafadhali miongoni mwenu wanamuabudu Mwenyezi Mungu lakini nao hawaamini Utume wa Mtume Muhammad (s.a.w.w) na wanaomshutumu Jibril na wanasema kuwa, yeye alifanya khiyana badala ya kupeleka Utume kwa Ali akaupeleka kwa Muhammad." Niliendelea kuzungumza mambo kama haya wakati ambapo rafiki yangu alikuwa akitabasamu na wakati mwingine alikuwa akisema, *"La haula Wala quwwata Illa Billah,"* ishara ya kuonesha kushangazwa. Nilipomaliza maneno yangu aliniuliza tena, "Wewe ni mwalimu unayesomesha wanafunzi?" Nikasema, "Ndiyo." akasema "Basi ikiwa fikra za Waalimu ziko katika hali hii, hapana lawama kwa watu wengine wa kawaida ambao hawana ilimu." Nikasema, "Unakusudia nini?" Alijibu, "Samahani, lakini ni wapi ulikoyapata madai haya ya urongo?" Nikasema, "Katika vitabu vya historia ambavyo ni mashuhuri kwa watu wote." Akasema, "Tuachane na watu wote lakini ni kitabu gani cha historia ulichokisoma?"

Nilianza kuorodhesha baadhi ya vitabu kama vile *Faj-rul-Islam*, *Dhuhal-Islam* na *Dhuhril-Islam* vya Ahmad Amin na vyenginevyo. Akasema, "Tangu lini Ahmad Amin amekuwa ndiyo hoja dhidi ya Mashia?" Akaongeza kusema, "Hakika uadilifu na ukinzani ulio sawa ni kuyabainisha mambo kutoka katika rejea zao asilia zilizo mashuhuri." Mimi nikasema, "Basi nitawajibika vipi kubainisha jambo ambalo linaeleweka kwa watu wote?"

Yeye akasema, "Huyu Ahmad Amin yeye mwenyewe alizuru Iraq, nami nilikuwa miongoni mwa walimu waliokutana naye huko Najaf, na tulipomlaumu kuhusu maandiko yake juu ya Shia, aliomba radhi kwa

kusema kuwa, mimi sina chochote ninachokijua juu yenu, na kwa hakika sijawahi kukutana na Shia hapo kabla na hii ndiyo mara yangu ya kwanza kukutana na Shia."

Sisi tulimwambia, "Huenda udhuru ulioutowa ni jambo baya zaidi kuliko kosa ulilolitenda, kwani ni vipi ulikuwa hujui chochote kutuhusu siye nawe ukaandika kila kitu kibaya dhidi yetu?"

Kisha aliendelea akasema, "Ewe ndugu yangu sisi tutakapoyahukumu makosa ya Wayahudi na Wakristo kwa kutumia Qur'an Tukufu ambayo kwetu sisi ni hoja madhubuti, basi mtazamo wetu huu utakuwa dhaifu kwa sababu wao hawaikubali Qur'an, na hoja yetu itakuwa madhubuti yenye nguvu tu ikiwa tutayabainisha makosa yao kwa mujibu wa vitabu vyao wanavyoviamini na hili litakuwa katika mizani ya *"Ameshuhudia shahidi kutoka kwao wenyewe." (12:26)*

Maneno yake yalitua ndani ya moyo wangu kama yanavyoshuka maji katika moyo wa mtu mwenye kiu, na nilijikuta ninabadilika kutoka katika hali ya mpinzani na kuelekea kwenye hali ya mtu mwenye kutafuta na kuchunguza. Kwani (maneno yake) niliyahisi kuwa ni yenye mantiki iliyosalimika na ni hoja yenye nguvu, basi sikuwa na budi isipokuwa lau nitatulia kidogo na kumsikiliza, na ndipo nilipomwambia, "Kwa hiyo nawe ni miongoni mwa wanaoitakidi ujumbe wa Mtume wetu Muhammad (s.a.w.w)?"

Akanijibu, "Na Mashia wote ni kama mimi; wanaitakidi hivyo na ni juu yako wewe ndugu yangu kulithibitisha hilo wewe mwenyewe ili usiwe na shaka na jambo hili na usiwadhanie nduguzo Mashia dhana mbali mbali, kwani baadhi ya dhana ni makosa." Aliendelea kusema, "Na ikiwa kweli unataka kujua ukweli na kuyaona hayo kwa macho yako na moyo wako uyakinishe; basi mimi nakualika utembelee Iraq na ukutane na wanachuoni wa Kishia na watu wa kawaida na ndipo utakapoufahamu uongo wa watu wenye dhamira mbaya."

Nikasema, "Hakika matumaini yangu yalikuwa kwamba siku moja niitembelee nchi ya Iraq ili nione kumbukumbu zake mashuhuri za Kiislamu, ambazo ziliachwa na watawala wa Banu-Abbas hasa hasa Harun Rashid lakini, kwanza uwezo wangu wa mali hautoshi kwani nimeupanga

kuniwezesha kufanya Umra, pili paspoti yangu niliyonayo hainiruhusu kuingia Iraq." Yeye akasema. "Kwanza nilipokuwa nimekualika kutembelea Iraq hiyo ilikuwa na maana kwamba mimi nitabeba jukumu la matumizi ya safari yako kutoka Beirut hadi Baghdad kwenda na kurudi; na makazi yako huko Iraq utakuwa pamoja nami nyumbani kwangu wewe ni mgeni wangu. Pili kuhusu paspoti ambayo haikuruhusu kuingia Iraq, hilo tumwachie Mwenyezi Mungu Mtukufu, kama amekukadiria kuizuru Iraq basi hilo litawezekana hata bila ya pasipoti na tutajitahidi kupata Viza ya kuingia Iraq tutakapofika Beirut."

Nilifurahi sana kupata bahati hii na nikamwahidi rafiki yangu kwamba, apendapo Mwenyezi Mungu kesho nitampa jibu.

Nilitoka katika chumba cha kulala na nikapanda juu ya boti ili nivute hewa mpya hali ya kuwa nafikiria kwa makini fikra mpya hali ya kuwa akili yangu imetekwa na mandhari ya bahari ambayo imetandaa upeo wangu wa macho; na huku namhimidi na kumtakasa Mola wangu aliyeumba ulimwengu na nikimshukuru kwa kunifikisha mahala hapa. Pia nilikuwa nikimuomba Mwenyezi Mungu anilinde kutokana na shari na watu wenye shari na anihifadhi kutokana na kupotoka na kukosea.

Mawazo yangu yalifika mbali wakati nilipokuwa nikiyakumbuka mbele ya macho yangu matukio niliyokutana nayo, na nilikumbuka hali ya mafanikio tangu utotoni mwangu mpaka siku hiyo. Isitoshe nilikuwa nikiota mustaqbali bora na nikihisi kama kwamba Mwenyezi Mungu na Mtume wake wamenizunguka kwa ulinzi makhususi. Niligeuka upande wa Misri ambayo sehemu ya pwani yake ilikuwa bado ikionekana katika wakati wote hali ya kuwa naiaga nchi hiyo ambayo ndani yake nimeibusu kanzu ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) nacho ni kitu pekee cha thamani kubwa kilichobakia katika kumbukumbu nilizokutana nazo nchini Misri.

Khatimaye nilianza kuyakumbuka maneno mageni ya yule Shia ambaye aliniingizia furaha kubwa itakayoithibitisha ndoto yangu iliyokuwa ikinipitia tangu nilipokuwa mdogo, nayo si nyingine bali ni kuizuru nchi ya Iraq, nchi ambayo inanikumbusha mahakama ya *Al-Rashid* na *Maamuni* ambaye ndiye muanzilishi wa *Darul-Hikmah* ambayo wasomi wa ilimu mbali mbali wakienda huko kutoka nchi za magharibi zama za maendeleo makubwa ya Kiislamu.

Zaidi ya hayo Iraq ni nchi ya yule kiongozi wa kiroho Bwana wangu *Sheikh Abdul-Qadir Jailani* ambaye sifa zake zimeenea ulimwengu wote na Tariqa yake imeingia katika kila mji na nguvu ya Tariqa yake imeshinda kila Tariqa. Basi kwa mara nyingine haya hapa tena mapenzi yatokayo kwa Mwenyezi Mungu ili kuithibitisha ndoto hii. Hivyo nilianza kuwaza na kuogelea katika bahari ya mawazo na matumaini mpaka kiliponizindua kipaza sauti cha boti ambacho kinawatangazia wasafiri waende kwenye mgahawa ili wakajipatie chakula cha jioni, nami nilikwenda mahali palipotajwa. Watu walikuwa wakisongamana kama kawaida yao wanapokuwa katika kila mkusanyiko, na kila mmoja anataka kuingia kabla ya mwenziwe na makelele yakawa mengi na pia fujo.

Mara ghafla yule Shia aliishika nguo yangu na kunivuta taratibu nyuma hali ya kuwa anasema, “Njoo ndugu yangu usijisumbue sisi tutakula baadaye bila ya kusukumana na kwa hakika nilikuwa nakutafuta kila mahali.”

Kisha aliniuliza, “Je umekwisha Swali?” Nikasema “Bado sijaswali.” Akaniambia njoo basi tuswali kisha tuje kula wakati hawa jamaa watakuwa wamemaliza fujo na makelele yao.

Niliipenda rai yake na nikafuatana naye mpaka mahali ambapo hapakuwa na watu, nikatawadha na kumtanguliza yeye awe Imamu. Kwa hakika nilikuwa nimekusudia kumchunguza namna anavyoswali, nami baadaye nitarudia kuiswali swala yangu.  Mara alipoqimu sala ili kutekeleza faradhi ya Magharibi na akaanza kusoma visomo vya sala na kuomba dua,  mtazamo wangu ulibadilika. Na kwa hakika niliwaza kwamba mimi ninaswali nyuma ya mmoja wa Masahaba Watukufu ambao ninasoma habari zao kuhusu uchamungu wao.

Baada ya kuwa (yule Shia) amemaliza kuswali aliomba dua ndefu ambayo nilikuwa sijasikia dua kama hiyo nchini kwetu wala katika nchi ninazozifahamu, na nilikwa nikituliza moyo na kufurahi kila alipomswalia Mtume na Āli zake na kumsifu vile anavyostahiki kusifiwa.

Baada ya sala niliona machoni mwake kuna athari za machozi kama ambavyo nilimsikia akimuomba Mwenyezi Mungu anifungulie maono yangu na aniongoe.

Tulielekea kwenye mgahawa ambao ulikwisha anza kuwa hauna watu wanaokula nasi tukaingia. Yule Shia hakukaa mpaka alipokwisha kunikalisha mimi na tukaletewa sahani mbili za chakula. Nilimuona anabadilisha sahani yake kwa sahani yangu, kwani sehemu yangu ilikuwa na nyama chache kuliko sehemu yake na akaanza kunihimiza kula kama kwamba mimi ni mgeni wake na akinifanyia wema na kunisimulia masimulizi yanayohusu kula na kunywa na adabu za kukaa kwenye meza ya chakula, (masimulizi) ambayo hapo kabla sijawahi kuyasikia.

Nilifurahishwa na tabia yake; na alitusalisha sala ya Isha na kuomba dua ndefu mpaka aliniliza kwa dua hiyo. Nami nikamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu aibadilishe dhana yangu juu yake kwani baadhi ya dhana ni makosa, lakini ni nani ajuaye?

Nililala hali ya kuwa naota Iraq na *Al-fulela-ulela*, na niliamka kwa mwito wake alipokuwa akiniamsha kwa ajili ya Sala ya Alfajiri. Tulisali na tukaketi tukizungumzia neema za Mwenyezi Mungu juu ya Waislamu.

Tulirudi tena kulala, na nilipoamka nilimkuta amekaa kitandani kwake na mkononi mwake ameshika tasbihi anamdhukuru Mwenyezi Mungu. Nafsi yangu iliburudika kwa ajili yake na moyo wangu ukatulizana kwa ajili yake, nikamuomba Mola wangu anisamehe.

Tulikuwa tukila ndani ya mgahawa wakati tuliposikia kipaza sauti kinatangaza kwamba boti inakurubia kuingia pwani ya Lebanon, na huenda tukawa katika bandari ya Beirut baada ya saa mbili kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu. Aliniuliza, “Je umefikiria kwa undani na umeamua nini?”

Nikasema, “Mwenyezi Mungu atakaponiwepesishia kupata Viza ya kuingia Iraq mimi sina kipingamizi, kisha nikamshukuru kwa mwaliko wake.” Tuliteremka Beirut ambapo tuliumaliza usiku ule na kutoka Beirut tulisafiri hadi Damascus ambapo tulipofika tu tulielekea Ubalozi wa Iraq na nikapata Viza kwa haraka mno kiasi ambacho sikutegemea. Tulitoka huko na hali ya kuwa ananipongeza na kumuhimidi Mwenyezi Mungu kwa msaada Wake.

# ZIYARA YA IRAQ KWA MARA YA KWANZA

Tulisafiri kutoka Damascus hadi Baghdad katika gari moja kubwa lenye kipoza hewa linalomilikiwa na shirika kubwa la kimataifa la Al-Najaf na hali ya joto ilikuwa digrii 40% ya hapo Baghdad. Tulipofika tu, mara moja tulielekea nyumbani kwake katika mtaa wa *Jamillah*, na niliingia ndani ya nyumba iliyokuwa na kipoza hewa na nikapumzika kisha alinileteа kanzu ambayo wao wanaiita Dishdāshah.

Alileta matunda na chakula na watu wa nyumbani mwake waliingia na kunisalimia kwa adabu na hishima. Baba yake alikuwa akinikumbatia kama kwamba ananifahamu tangu hapo mwanzo, ama mama yake alisimama mlangoni akiwa amevaa baibui nyeusi akanisalimia na kunikaribisha.

Rafiki yangu aliniomba radhi kuhusu mama yake kwa kutonipa mkono, kwani wao Mashia kupeana mkono na mwanamke asiye *Mahram* kwao ni haramu. Nilistaajabu mno na nikajisemesha mwenyewe moyoni, “Hawa ndiyo tunaowatuhumu kwamba wametoka nje ya dini, lakini mbona wao ndiyo wanaoihifadhi dini zaidi kuliko sisi.”

Katika masiku ya safari nilipokuwa pamoja naye nimejionea tabia bora na utukufu wa nafsi, utu na unyenyekevu na ucha Mungu ambao sikuufahamu hapo kabla.

Nilijihisi kuwa mimi siyo mgeni bali ni kama kwamba niko nyumbani mwangu.

Usiku tulipanda juu ya paa la nyumba ambapo palikuwa pametandikwa kwa ajili yetu ili tulale na sikupata usingizi hadi usiku wa manane naweweseka, je naota au niko macho? Ni kweli kwamba mimi niko Baghdad karibu ya Sayyid yangu *Abdul-Qadir Al-Jailan?* Rafiki yangu

alicheka hali ya kuwa anauliza wanasema nini Watunisia juu ya huyu *Abdul-Qadir Al-Jailani?*

Nilianza kumsimulia kuhusu karama ambazo twasimuliwa na kwamba yeye ni *Qutbud-Dairah,* kama ambavyo Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na ni Bwana wa Mitume, basi *Abdul-Qadir* ni bwana wa mawalii na unyayo wake uko juu ya kila walii naye anasema: "Watu wote wanaitufu nyumba (Al-kaaba) mara saba nami nitaitufu pamoja na mahema yangu."

Kwa hiyo nilijaribu kumkinaisha kwamba Sheikh *Abdul-Qadir* huwa anawajia baadhi ya muridi wake na wapenzi wake wazi wazi na kuwaponya maradhi yao na kuwafariji kutokana na matatizo yao. Niliisahau au tuseme nilijisahaulisha ile itikadi ya Kiwahabi ambayo niliathirika nayo, ya kwamba yote hayo (niyasemayo) ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu. Na nilipohisi kuwa rafiki yangu hahamasiki, nilijaribu kuikinaisha nafsi yangu kwamba, niliyoyasema siyo sahihi na nikamuuliza nini maoni yake.

Rafiki yangu alisema hali ya kuwa anacheka "Usiku huu lala na pumzika kutokana na machofu yaliyokupata safarini, na kesho apendapo Mwenyezi Mungu tutamzuru Sheikh *Abdul-Qadir."* Nilifurahi kutokana na habari hii, na nikatamani alfajiri ingechomoza wakati huo huo lakini machovu yalikuwa yamenizidi, basi hatimaye nililala usingizi mzito kiasi cha kuwa Sala ya asubuhi ilinipita, kwani niliamka baada ya kuchomoza jua. Yule rafiki yangu alinijulisha kuwa alijaribu mara kadhaa kuniamsha bila mafanikio akaniacha ili nipumzike.

# ABDUL-QADIR AL-JAILAN NA MUSA AL-KADHIM

Baada ya kifungua kinywa tulikwenda kwa Sheikh na niliiona *Maqaam* ambayo muda mrefu nimekuwa nikitamani kuizuru. Nilitembea kwa haraka kama kwamba mimi nina hamu ya kumuona, na niliingia kwa pupa na majonzi kama kwamba nitajitupa miguuni pake na rafiki yangu alikuwa akinifuata kila nilipokwenda. Nilichanganyikana na watu waliokuwa wakizuru (mahala hapo) ambao walifurika kwenye *Maqaam* hiyo kama wanavyofurika Mahujaji kwenye nyumba ya Mwenyezi Mungu tukufu. Miongoni mwa watu hao, walikuwemo waliokuwa wakirusha pipi, na wenye kuzuru sehemu hiyo huzigombea kuziokota, nami nikakimbilia kuchukua mbili kati ya hizo nikala moja kwa haraka ili nipate baraka na nyingine nikaificha mfukoni mwangu kwa ajili ya kumbu kumbu.

Niliswali huko na kuomba dua chache kisha nikanywa maji na nilijiona kama nakunywa maji ya *Zamzam*, kisha nilimuomba rafiki yangu anisubiri kidogo ili niandike postakadi chache nilizozinunua huko kuwapelekea marafiki zangu wa Tunisia. Postakadi zote zilikuwa na picha ya Quba la kijani la Sheikh *Abdul-Qadir Al-Jailan,* na kwa kufanya hivyo nilikuwa nataka kuwaonesha marafiki zangu na ndugu zangu walioko Tunisia juu ya juhudi zangu kubwa zilizonifikisha kwenye Maqam hiyo ambayo wao hawajafika.

Baada ya hapo tulikula chakula cha mchana katika mgahawa uitwao Mat-a'mus-Shaa'bi ulioko katikati ya mji, kisha rafiki yangu alinichukua katika taxi mpaka *Kadhimiyyah*. Jina hili nililitambua pindi rafiki yangu alipotaja kumwambia dereva wa Gari, na tulifika huko.

Tuliposhuka kwenye gari tukitembea tulichanganyika na idadi kubwa ya watu wakielekea tuendako, wake kwa waume na watoto, hali ya kuwa wamebeba baadhi ya mizigo. Hali hii ilinikumbusha msimu wa Hijja, na

nilikuwa sijaelewa ni upande gani unaokusudiwa mpaka yalipojitokeza *Maqubah* na minara ya dhahabu inayong'ara na hapo nilitambua kwamba huo ni msikiti miongoni mwa misikiti ya Mashia kwa kuwa hapo kabla nilikuwa nikifahamu kwamba wao huipamba misikiti yao kwa dhahabu na fedha jambo ambalo Uislamu umeliharamisha. Nilijihisi vibaya kuingia ndani ya msikiti huo isipokuwa tu kwa kuchunga hisia ya rafiki yangu nilimfuata bila kupenda.

Tuliingia kupitia mlango wa kwanza na hapo nilianza kuona Wazee wakiishika na kuibusu milango nami nilijiliwaza kwa kusoma ubao mkubwa ulioandikwa *"Ni marufuku kuingia wanawake wasiokuwa na Hijab."* Maandishi hayo yaliambatana na hadith ya Imam Ali isemayo, "Kuna wakati utawafikia watu, wanawake watatoka nje hali ya kuwa wamevaa nguo zinazoonyesha (miili yao)...." mpaka mwisho wa hadithi.

Tulifika kwenye *Maqam*, na wakati rafiki yangu anasoma idhini ya kuingia, mimi nilikuwa nauangalia mlango na nilikuwa nastaajabia dhahabu na nakshi ambazo zimeenea mlango wote na zote zilikuwa ni (nakshi za) aya za Qur'an.

Rafiki yangu aliingia nami nikaingia baada yake hali ya kuwa ni mwenye tahadhari, akilini mwangu nafikiria namna mbali mbali ya uzushi niliousoma ndani ya baadhi ya vitabu vinavyowakufurisha Mashia. Ndani ya Maqam hiyo niliona nakshi na mapambo ambayo sikuwahi kuyaona hapo kabla, nilishangazwa na mambo niliyoyaona na nikajihisi kwamba niko katika ulimwengu usiyo wa kawaida na usiyofahamika. Kila wakati nilikuwa nikiwaangalia kwa chuki watu hawa waliokuwa wakitufu na wakizunguka pembeni ya kaburi huku wakilia na kubusu nguzo zake na kona zake, na wengine wanasali karibu na kaburi. Basi hapo niliikumbuka hadithi ya Mtume (s.a.w.) isemayo "Mwenyezi Mungu amewalaani Mayahudi na Wakristo walioyafanya makaburi ya Mawalii wao kuwa misikiti."

Nilijitenga na rafiki yangu ambaye alipoingia tu alianza kulia kisha nilimwacha anaswali na nikausogelea ubao ulioandikwa na kutundikwa kwenye kaburi kwa ajili ya ziyara.

Nikausoma na sikuyafahamu mambo mengi yaliyomo kutokana na kuwa na majina mengi ambayo kwangu ni mageni na siyajui.

Nilielekea kwenye kona na nikasoma *Suratul-fatiha* kwa ajili ya kumrehemu mwenye kaburi hilo nikasema, "Ewe Mwenyezi Mungu ikiwa maiti huyu ni miongni mwa Waislam basi umrehemu kwani wewe ni mjuzi mno kuliko mimi." Rafiki yangu alinisogelea na akaninong'oneza sikioni akasema: "Kama una haja yoyote ile muombe Mwenyezi Mungu mahala hapa kwani sisi tunapaita kuwa ni mlango wa maombi." Mimi sikuyajali maneno yake *(Mwenyezi Mungu anisamehe)*, bali nilikuwa nikiwaangalia wazee wenye umri mkubwa na vichwani mwao wamevaa vilemba vyeupe na vyeusi na katika nyuso zao kuna alama ya sijida. Haiba yao ilikuwa ikiongezewa na ndevu zilizokuwa zikinukia uzuri na wanao mvuto unaopendeza.

Hapana yeyote aliyeingia mahala hapo miongoni mwao isipokuwa alikuwa akilia nami nikajiuliza moyoni, "Je inawezekana machozi haya yakawa ni ya uongo? Hivi inawezekana wazee hawa wenye umri mkubwa wakawa wanakosea?"

Nilitoka hali ya kuwa nimechanganyikiwa na kushangaa kutokana na mambo niliyoyaona. Wakati wote huo rafiki yangu alikuwa akirudi kinyume nyume kwa heshima ili asije akaipa mgongo Maqām ile.

Nilimuuliza ni nani huyu mwenye Maqām hii?

Akasema, "Ni Imam Musa Al-Kadhim".

Nikasema, "Huyu Imam Musa Al-Kadhim ni nani?"

Akasema, "Subhanallah! ninyi ndugu zetu Masunni mumewacha kiini na mumeshikamana na maganda".

Nilisema kwa hasira, "Vipi tumeshikamana na maganda na tumeacha kiini?" Basi alinituliza na akasema: "Ndugu yangu, wewe tangu ulipoingia Iraq huachi kumkumbuka Abdul-Qadir Jailani, huyu aliyewajibisha uuone umuhimu wote huu ni nani? Nikajibu kwa haraka tena kwa fahari kubwa,

“Yeye ni katika watu wa kizazi cha Mtume, na lau kungekuwa na Nabii baada ya Muhammad basi angekuwa Abdul-Qadir Jailan (r.a.)”.

Akasema, “Ewe ndugu yangu Al-Samawi unaifahamu historia ya Uislamu?” Nilijibu bila kusita kwamba, “Ndiyo.” Lakini kwa kweli sikuwa nafahamu chochote katika historia ya Uislamu isipokuwa sehemu chache tu na siyo nyingi, kwani waalimu wetu walikuwa wakitukataza jambo hili *(la kujifunza historia ya Uislamu)* wakidai kwamba hiyo ni historia iliyochafuliwa hakuna faida kuisoma.

Kwa mfano nakumbuka kwamba Mwalimu aliyekuwa akihusika kutusomesha somo la Balaghah, siku moja alikuwa akitusomesha khutba ya Shaqshaqiyyah iliyoko ndani ya *Nahjul-Balaghah* ya Imam Ali (a.s.). Mimi nilishangaa kama walivyoshangaa wanafunzi wengi wakati wa kuisoma khutba hiyo, pale nilipofanya ujasiri wa kumuuliza Mwalimu kama kweli haya ni miongoni mwa maneno ya Imam Ali (a.s.). Mwalimu alinijibu kwa kusema; “Bila shaka nani mwingine mwenye lugha fasaha kama hii; hakuna ila yeye, na kama yasingekuwa ni maneno ya Ali *Karrama Llahu Waj-hahu,* basi wanachuoni wa Kiislamu mfano wa Sheikh Muhammad Abdou ambaye ni Mufti wa Misri wasingejishughulisha kuyasherehesha.”

Hapo mimi nilisema: “Kwa hakika Imam Ali (a.s.) katika hotuba hii anawatuhumu Abubakar na Omar kwamba wao wamempokonya haki yake ya Ukhalifa.”

Basi Mwalimu yule alifura na kunikemea kwa ukali na kunionya kwamba atanifukuza iwapo nitarudia kuuliza swali kama hili, na akaongeza kusema; “Sisi tunasoma Balaghah wala hatusomi historia, hakuna umuhimu wowote wa historia ambayo matukio yake yamejaa fitna na vita vya kumwaga damu baina ya Waislamu. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu amezitakasa panga zetu kwa damu zao, nasi tuzitakase ndimi zetu tusiwashutumu.”

Sikutosheka na sababu hii (aliyoitoa Mwalimu), bali nilibakia nimemkasirikia Mwalimu yule ambaye alikuwa akitufundisha Balaghah bila ya kutufafaulia maana zinazojitokeza (ndani ya somo hilo).

Nilijaribu mara nyingi kusoma historia ya Uislamu lakini sikupata rejea za kutosha, na pia uwezo wa kununua vitabu ulikuwa mdogo, istoshe sikumpata Sheikh yeyote miongoni mwa masheikh wetu na wanachuoni wetu anayeipa kipaumbele historia, kama kwamba wao wamekubaliana kuisahau na kutoichunguza. Zaidi ya hapo huwezi kumpata (Sheikh) yeyote anayemiliki kitabu kamili cha historia.

Basi rafiki yangu aliponiuliza kuhusu kuifahamu historia nilitaka kumpinga tu ndipo nilipojibu kuwa "Ndiyo," wakati hali halisi inasema kwamba "Nikijuacho ni kuwa, hiyo ni historia iliyovurugwa hakuna faida ndani yake isipokuwa kuna fitna na chuki na mambo yanayopingana.

(Rafiki yangu) alisema: "Je unafahamu ni lini na ni zama zipi Abdul-Qadir alizaliwa?" Mimi nilisema, "Kiasi amezaliwa katika karne ya sita au ya saba."

Basi kuna miaka mingapi (iliyopita) kati yake na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu? Nikasema, "Karne sita." Yeye akasema, "Basi karne moja kuna vizazi viwili kwa makadirio madogo, itakuwa nasaba ya Abdul-Qadir Al-Jailani kwa Mtume iko baada ya mababu kumi na mbili." Nikasema, "Ndiyo."

Akasema huyu Musa ibn Jaa'far ibn Muhammad ibn Ali ibn Hussein ibn Fatmah Az-Zahra, nasaba yake inafika kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu baada ya mababu wanne tu au yafaa kusema kuwa yeye ni kizazi cha karne ya pili ya Hijriyah. Sasa basi, ni yupi kati ya wawili hawa, Musa na Abdul-Qadir ambaye yuko karibu zaidi kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu,? Bila ya kufikiria nilisema; "Bila shaka huyu yuko karibu, lakini ni kwanini basi sisi hatumfahamu na wala hatusikii kutajwa kwake?" Akasema, "Hapa ndipo kwenye lengo na ndiyo maana nilisema kwamba, *samahani niruhusu nirudie,* mumeacha kiini na mumeng'ang'ania maganda, na usinielewe vibaya natarajia utaniwia radhi."

Tulikuwa tukizungumza huku tunakwenda na mara nyingine tunasimama mpaka tukafika mahala panaposomeshwa elimu, na hapo wanafunzi na waalimu walikuwa wamekaa wakibadilishana maoni na nadharia za kielimu. Tulikaa huko, na rafiki yangu alikuwa akimtafuta mtu maalum

miongoni mwa walioketi kama kwamba anayo ahadi na mmoja wao.

Hatimaye alikuja mtu akatusalimia na nilifahamu kuwa ni mwenziwe chuoni hapo, na alimuuliza kuhusu mtu fulani. Kutokana na majibizano nilifahamu kuwa mtu huyo ni Daktari na atafika hivi karibuni. Katika kipindi hicho rafiki yangu aliniambia kuwa, nimekuleta mahala hapa ili nikutambulishe kwa msomi anayehusika na uchambuzi wa mambo ya historia, naye ni Profesa wa historia katika chuo kikuu cha Baghadad na alipata shahada ya uprofesa kutokana na utafiti wake aliouandika kuhusu Abdul-Qadir Jailani, na kwa msaada wa Mwenyezi Mungu atakunufaisha, kwani mimi si bingwa wa somo la historia.

Tulikunywa juice ya baridi mpaka alipokuja yule Profesa, na rafiki yangu alinyanyuka kumsalimia na akanitambulisha kwake na akamtaka anidokezee kwa ufupi historia ya Abdul-Qadir Jailani, na aliniomba tumruhusu aende kwa ajili ya baadhi ya shughuli zake.

Yule profesa aliniagizia kinywaji baridi na akaanza kuniuliza jina langu, nchi yangu na kazi yangu kama ambavyo alinitaka nimsimulie umaarufu wa Abdul-Qadir Jailani ulivyo huko Tunisia.

Nilimsimulia mengi juu ya jambo hili kiasi kwamba kwetu sisi watu wanaitakidi kwamba Sheikh Abdul-Qadir alikuwa akimbeba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu mabegani kwake katika usiku wa Miiraj wakati Jibril alipochelea kuungua, na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akamwambia, “Unyayo wangu uko juu ya mabega yako na unyayo wako uko juu ya bega la kila walii mpaka siku ya Qiyamah.”

Yule Profesa akacheka sana alipoyasikia maneno yangu, lakini mimi sikufahamu je kucheka kwake kulitokana na riwaya nilizomsimulia au alikuwa akimcheka mwalimu wa Kitunisia aliyeko mbele yake? Baada ya majadiliano mafupi kuhusu mawalii na watu wachamungu alisema kwamba, “Ametafiti kwa muda wa miaka saba, na katika kipindi hicho alisafiri hadi Lahorre nchini Pakistani na alikwenda Uturuki, Misri na Uingereza na kila mahali yaliko maandiko (au kumbu kumbu zinazonasibishwa kwa Abdul-Qadir Al-Jailan. Yote hayo aliyachunguza na kuyapiga picha, na hakuna ndani ya kumbukumbu hizo kitu chochote

kinachothibitisha kwamba Abdul-Qadir Jailani anatokana na kizazi cha Mtume, bali kilichopo ni ubeti wa shairi unaonasibishwa kwa mmoja wa wajukuu zake anasema katika beti hiyo, *Na babu yangu ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.* Na hilo laweza likachukuliwa kuwa ni tafsiri ya hadithi ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa "Mimi ni babu wa kila Mchamungu."

Aliongeza kunieleza kwamba, "Historia sahihi inathibitisha kuwa Abdul-Qadir asili yake ni Muirani, na siyo Muarabu kamwe, na amezaliwa katika mji mmoja huko Iran uitwao Giilani na ndiyo anaonasibishwa kwao, na alihama kutoka huko na kwenda Baghdad, akasoma na kuishi huko huko na kufundisha katika kipindi ambacho maadili yalikuwa yameharibika."

Mtu huyu alikuwa Mchamungu na watu walimpenda, na baada ya kufa kwake waliasisi *Tariqa ya Qadiriyah* kwa munasaba wake kama wanavyofanya siku zote wafuasi wa kila mwana Tasawafi. Aliendelea akasema; Kwa kweli hali ya Waarabu kwa upande huu inahuzunisha."

Hamasa ya Kiwahabi ilifura kichwani mwangu nikamwambia yule mtaalam wa historia, "Kwa hiyo Muheshimiwa Profesa, wewe fikra zako ni za Kiwahabi, kwani wao wanasema kama usemavyo wewe kwamba hakuna Mawalii".

Akasema; "Hapana mimi siko katika misingi ya mtazamo wa Kiwahabi, jambo la kuhuzunisha kwa Waislamu ni kwamba, imma watamsifu mtu zaidi ya anavyostahiki kusifiwa, au kukebehi kila kitu, na au huamini na kusadiki kila aina ya uzushi ambao hautegemei dalili na haukubaliki kiakili wala kisheria. Na kuna wakati mwingine watapinga kila kitu hata miujiza ya Mtume wetu Muhammad (s.a.w.) na hadithi zake kwa kuwa tu havikubaliani na matamanio na itikadi yao wanayoitakidi. Na kwa ajili hiyo, kundi fulani (la Waislamu) limeelekea Mashariki na jingine Magharibi. Masufi kwa mfano wanasema kuwa kuna uwezekano wa Sheikh Abdul-Qadir Jailani kuwepo Baghdad na wakati huo huo akawa Tunisia, na huenda akamponya mgonjwa huko Tunisia na pia kumuokoa mtu anayezama katika mto Tigris kwa wakati huo huo. Basi huku ni kuvuka mipaka ya kumsifia mtu. Nao Mawahabi kwa kuwapinga Masufi wanakanusha kila kitu mpaka wamesema kuwa, ni shirki kutawassal kwa Mtume (s.a.w.) na hii ni kupuuza haki inayomstahiki mtu. Sivyo hivyo

ndugu yangu bali sisi ni kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani ya kitabu chake kitukufu; *"Namna hivyo, tumekufanyeni kuwa ni ummati wa kati na kati ili muwe mashahidi juu ya watu". 2:143.*

Maneno yake yalinipendeza sana, na kimsingi nilimshukuru na nikaonesha kukinaika kwangu kwa maneno aliyoyasema. Alifungua mkoba wake na akatoa kitabu kinachohusu Abdul Qadir Jailani na akanizawadia, vile vile alinialika nyumbani kwake lakini nilitoa udhuru na tukabakia tunazungumzia juu ya Tunisia, na Afrika kaskazini mpaka alipokuja rafiki yangu na tulirudi nyumbani usiku baada ya kuwa siku nzima tumeimaliza katika ziyara na majadiliano. Nilihisi kuchoka basi nikaenda kulala.

Niliamka mapema nikaswali na nikakaa nikisoma kile kitabu chenye utafiti wa maisha ya Abdul-Qadir. Rafiki yangu alipoamka nilikuwa nimekwisha kimaliza nusu yake na alikuwa akija mara kwa mara kuniita kwa ajili ya kifungua kinywa lakini sikukubali mpaka nilipokimaliza kitabu chote. Kilinivutia na kunitia mashaka ambayo hayakudumu bali yalitoweka kabla sijaondoka nchini Iraq.

# MASHAKA NA KUJIULIZA

Nilibakia nyumbani kwa rafiki yangu kwa muda wa siku tatu, na nilipumzika katika siku hizo huku nikiyafikiria kwa makini mambo yote niliyoyasikia toka kwa watu hawa ambao nimewagunduwa na ni kama kwamba wao walikuwa wanaishi juu ya mwezi, basi ni kwa nini hakutusimulia mtu yeyote kuhusu habari zao isipokuwa zile ambazo ni za kudharaulika na mbaya? Na ni kwa nini mimi nawachukia bila ya kuwafahamu? Huenda jambo hilo ni matokeo ya uvumi tunaousikia dhidi yao kwamba wao wanamuabudu Ali na kwamba wao wanawaweka Maimamu wao katika daraja ya Mungu, na kwamba wao wanaitakidi kuwa Mungu huingia ndani ya mwili wa kiumbe. Si hivyo tu bali wao wanasujudia jiwe kinyume cha Mwenyezi Mungu na wao (kama alivyotusimulia) baba yangu baada ya kurejea toka hija (akasema kuwa wao huwa wanakwenda kwenye kaburi la Mtume (s.a.w.) na kutia uchafu na najisi, na polisi wa Saudia waliwakamata na kuwahukumu wauliwe, na mengine mengi ya uzushi dhidi yao.....!! Basi sema lolote kuwahusu watu hawa si vibaya!!

Itakuwaje Waislamu wayasikie haya wasiwachukie watu hawa na kuwabughudhi? Bali vipi wataacha kuwaua, lakini pia ni vipi nitaamini uvumi huu hali ya kuwa nimeona kwa macho yangu mambo niliyoyaona, na nimesikia kwa masikio yangu niliyoyasikia na hapo sasa nimemaliza zaidi ya wiki moja nikiwa miongoni mwao na sikuona wala kusikia toka kwao isipokuwa maneno yanayokubalika akilini, maneno ambayo yanaingia akilini bila kupingwa bali nilivutiwa na ibada zao, dua zao, tabia yao na heshima yao kwa wanachuoni wao mpaka nilitamani niwe kama walivyo wao.

Nilibakia najiuliza, "Je, hivi ni kweli kwamba wao wanamchukia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kila nikimtaja (Mtume) na mara nyingi nilikuwa namtaja ili kuwajaribu nijue msimamo wao, basi wao husema kwa viungo vyao vyote, Allahumma Salli Alā Muhammadin Waāli Muhammadin.

Nilidhani kwamba wanafanya unafiki lakini dhana yangu hii iliondoka baada ya kuangalia vitabu vyao ambavyo nilisoma sehemu fulani ya vitabu hivyo nikakuta jinsi wanavyoiheshimu na kuitukuza na kuitakasa dhati ya Mtume (s.a.w.), jambo ambalo sikulizoea katika vitabu vyetu, kwani wao wanasema kuwa, "Mtume ni *Maa'sum* katika kila hali, kabla ya kupewa Utume na baada ya kupewa Utume." Wakati sisi Masunni tunasema kuwa, "Yeye ni *Maa'sum* katika kufikisha Qur'an tu, na lisilokuwa hilo yeye anakosea kama wengine." Mara nyingi tunatolea ushahidi jambo hilo kwa kumkosoa Mtume (s.a.w.) na kuziona kuwa rai za baadhi ya masahaba ni sahihi ukilinganisha na rai ya Mtume, na tunayo mifano mingi kuhusiana na jambo hilo, wakati ambapo Mashia wanapinga(usemi usemao) kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu hukosea na watu wengine kupatia hivyo basi baada ya yote haya ni vipi nitaamini kwamba wao wanamchukia Mtume wa Mwenyezi Mungu? Vipi itakuwa hali hii?

Siku moja nilipokuwa nazungumza na rafiki yangu nilimtaka anijibu wazi wazi, na mazungumzo yetu yalikuwa kama ifuatavyo: "Ninyi Mashia munamuweka Ali (r.a.) katika daraja ya Manabii kwani mimi mara nyingi kila nimsikiapo mtu miongoni mwenu anamtaja Ali basi husema *"Alaihi-Salaam."*

Alinijibu na akasema, "Bila shaka sisi tunapomtaja Amirul-Muuminina (Ali) au mmoja wa Maimamu huwa tunasema *"Alaihi Salam."* Hali hii haimaanishi kwamba wao ni Manabii, bali wao ni familia ya Mtume na ni watu wa kizazi chake ambao Mwenyezi Mungu ametuamrisha kuwatakia rehma katika kitabu chake kitukufu na kwa msingi huu inajuzu pia kusema *Alaihimus-salatu Was-salaam."*

Hapana ndugu yangu, sisi hatutambui kuziomba *Sala na Salaamu* isipokuwa kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na Manabii waliomtangulia na wala Ali na wanawe hawahusiki katika jambo hilo.

Yeye akasema; "Nakuomba na ninakutarajia usome zaidi mpaka ufahamu ukweli."

Nikasema, "Nitasoma vitabu gani ewe ndugu yangu, je siyo wewe uliyeniambia kuwa vitabu vya Ahmad Amin siyo hoja dhidi ya Shia? Vile

vile vitabu vya Shia siyo hoja dhidi yetu na wala hatuvitegemei, huoni ya kwamba vitabu vya Wakristo wanavyovitegemea vinasema kuwa Isa (a.s.) amesema kwamba "Mimi ni mtoto wa Mungu" wakati ambapo Qur'an tukufu ambayo ndiyo msema kweli inasema ikimnukuu Issa mwana wa Mariam kwamba, "Sikuwaambia ila yale uliyoniamrisha, mwabuduni Mwenyezi Mungu Mola wangu na ni Mola wenu".

Akasema, "Vema kwa hakika hivyo ndivyo nilivyosema, nikitakacho kwako ni hiki, yaani utumie akili, mantiki na dalili kwa kutumia Qur'an tukufu na Sunnah sahihi kwa kuwa sisi ni Waislamu, na lau mazungumzo hayo yangekuwa yanawahusu Wayahudi na Wakristo basi (tungetumia) dalili zisizokuwa hizi.

Mimi nikasema, "Kwa hiyo ukweli nitaufahamu kutoka katika kitabu gani kwani kila mwandishi, kila kundi na kila madh-hebu yanadai kuwa yako katika haki."

Akaniambia, "Sasa hivi nitakupa dalili thabiti ambayo Waislamu pamoja na Madh-hebu zao na vikundi vyao mbali mbali hawatofautiani japokuwa wewe huitambui (nayo ni hii ifuatayo) Waambie, Ewe Mola wangu nizidishie Elimu.

Akasema, "Je umepata kusoma tafsiri ya aya tukufu isemayo *"Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Mtume, Enyi mulioamini msalieni na mumpe salamu bila kusita." (Qur'an, 33:52)*

Wanachuoni wote wa tafsiri wameafikiana, Masunni na Mashia ya kwamba, Masahaba ambao aya hii ilishuka kwao walikuja kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wakasema "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, sisi tumekwisha fahamu ni vipi tutakusalimia na hatujafahamu ni vipi tutakusalia" Mtume akasema; "Semeni Ewe Mwenyezi Mungu mrehemu Muhammad na Aali zake Muhammad kama ulivyomrehemu Ibrahim na aali zake Ibrahimu katika walimwengu kwa hakika wewe ni mwenye sifa njema tena mtukufu na wala musinisalie sala iliyokatika". Wakasema, "Ni ipi hiyo sala iliyokatika ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?" Akasema, "Mtasema, Ewe Mwenyezi Mungu Msalie Muhammad na kisha mtanyamaza, na fahamuni kwamba Mwenyezi Mungu ni mkamilifu hakubali ila kitu kilichokamilika."

Masahaba waliyafahamu yote hayo na pia waliokuja baada yao walifuata amri ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, basi walikuwa wakimsalia sala iliyokamilika, kiasi kwamba Imam Shafii alisema kuhusu haki yao yaani (kizazi cha Muhammad) kama ifuatavyo:

“Enyi kizazi cha nyumba ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, mapenzi yenu ni faradhi (wajibu) kutoka kwa Mwenyezi Mungu ameyateremsha ndani ya Qur’an, yakutosheni ninyi heshima tukufu ya kwamba yeyote asiyekusalieni hana sala.”

Maneno yake yalikuwa yakitwanga masikio yangu na kupenya hadi moyoni na kuikuta nafsi yangu inakubali, na kwa kweli hapo kabla nilipata kusoma maneno kama haya ndani ya baadhi ya vitabu, lakini sikumbuki vema ni rejea gani.

Nilikiri kwamba sisi tunapomsalia Mtume tunawasalia na kizazi chake na Masahaba wake wote, lakini hatumpwekeshi Ali (r.a.) kwa salamu kama wasemavyo Mashia, *“Ali alaihis-salam.”*

Akasema: “Nini mtazamo wako kuhusu Bukhari, je yeye ni Shia?”

Nikasema “Ni Imam mtukufu miongoni mwa Maimamu wa Kisunni, na kitabu chake ni sahih mno baada ya kitabu cha Mwenyezi Mungu”.

Basi pale pale alisimama akatoa *Sahih Bukhari* ndani ya maktaba yake, akaifungua na kuutafuta ukurasa aliokuwa akiutaka kisha akanipa nisome. Nikasoma maneno yafuatayo; “Ametusimulia fulani toka kwa fulani naye toka kwa Ali *Alaihis-Salaam*. Sikuyaamini macho yangu na nilishangaa mpaka nikaikitilia mashaka kuwa hivi kweli hiyo ni sahihi Bukhari yenyewe?

Nilichanganyikiwa nikarudia kuangalia ndani ya kurasa na juu ya jalada, rafiki yangu alipohisi shaka yangu alikichukua kitabu na kunionyesha ukurasa mwingine ambao ndani yake kuna (riwaya) isemayo “Ametusimulia Ali ibn Hussein *Alaihis-salāmu.* Sikuwa na jibu baada ya hapo isipokuwa nilisema “Subhanallah.” Kutokana na jibu hili rafiki yangu alitosheka aliniacha na akatoka. Nilibaki nafikiri na kurudia kuzisoma zile kurasa na kuthibitisha chapa ya kitabu nikaikuta ni miongoni mwa chapa za shirika la Al-Halabi na wanawe lililoko Misri.

Ewe Mungu wangu ni kwa nini ninampinga na kumkanusha (mtu huyu), kwa hakika amenipa hoja thabiti kutoka ndani ya kitabu sahihi mno kwetu sisi, na huyu Bukhari siyo Shia kamwe, naye ni miongoni mwa Maimamu wa Kisunni na ni mwanachuoni wao wa hadithi. Basi je, niukubali ukweli huu ambao ni hii kauli yao ya kusema Ali *Alaihis-Salaam?* Lakini nachelea juu ya ukweli huu kwamba huenda ukafuatiwa na ukweli mwingine ambao sipendi kuukubali, nami nimeshindwa mara mbili mbele ya rafiki yangu, kwani nimekwisha kiporomosha cheo cha Abdul-Qadir Jailani, na nimekubali kwamba Musa Al-Kadhim ni bora kuliko yeye, na nimekubali pia kwamba Ali *Alaihis-Salaam* anastahiki hivyo. Pamoja na hayo sitaki kushindwa kwa mara nyingine, nami ndiye yule ambaye kabla ya siku kadhaa nilikuwa mwanachuoni (mkubwa) nchini Misri na nikaionea fahari nafsi yangu, bali Wanachuoni wa Azhar walinitukuza, na leo najikuta mwenye kushindwa na kuhemewa, ni nani hasa anishindaye? Je, ni wale watu ambao nilikuwa bado naamini kwamba wao wako katika upotofu? Kwa hakika nimelizowea tamko la *Shia* kuwa ni tusi.

Bila shaka hiki ni kiburi na majivuno, na hapana shaka kuwa huu ni ubinafsi, ubishi na chuki tu. Basi ewe Mungu wangu niongoze na unisaidie kuukubali ukweli japokuwa una machungu.

Ewe Mwenyezi Mungu nifungue macho yangu na moyo wangu na uniongoze kwenye njia yako iliyonyooka, unijaalie kuwa miongoni mwa wanaosikiliza kauli na kufuata iliyo njema mno. Ewe Mwenyezi Mungu tuoneshe haki kuwa ni haki na uturuzuku kuifuata na utuoneshe batili kuwa ni batili na uturuzuku kuiepuka.

Rafiki yangu alirudi nyumbani nami nikiwa katika hali ya kurudia rudia maombi haya akasema hali ya kuwa anatabasamu "Mwenyezi Mungu atuongoe sisi na ninyi na Waislamu wote, naye amesema ndani ya kitabu chake kitukufu: *Na wale wanaopigana Jihadi katika njia yetu, tutawaongoa (tuwaoneshe) njia yetu na Mwenyezi Mungu yu pamoja na watu wema." (Qur'an, 29:69)*

Na hili tamko la jihadi ndani ya aya hii linafasiriwa kwa maana ya utafiti wa kielimu ili kuufikia ukweli, na Mwenyezi Mungu anamuongoza kwenye ukweli kila anaye utaufuta ukweli.

# SAFARI YA KWENDA NAJAF

Katika usiku mmoja rafiki yangu alinijulisha kwamba kesho Mwenyezi Mungu apendapo tutasafiri kwenda Najaf, nami nikamuuliza, “Hii Najaf ni nini?” akasema: “Huo ni mji wa kielimu na katika mji huo ndimo yalimo malazi ya Imam Ali Ibn Abitalib (a.s.).” Nilistaajabu, itakuwaje Imam Ali awe na kaburi linalofahamika? Kwa sababu Masheikh wetu wanasema kwamba hakuna kaburi la Sayyidna Ali linalofahamika.

Tulisafiri ndani ya Gari la abiria mpaka tukafika *Al-Kufah*, na huko tuliteremka ili kuuzuru Msikiti wa *Al-Kufah,* ambao ni miongoni mwa kumbukumbu za kale za Kiislam. Rafiki yangu alikuwa akinionesha maeneo ya kumbukumbu na akanitembeza kwenye Msikiti wa Muslim ibn Aqil na Hani ibn Ur-wah. Alinisimulia namna walivyouawa, na vile vile aliniingiza kwenye Mihrab ambayo ni mahala alipouawa Imam Ali (a.s.).

Baada ya hapo tuliitembelea nyumba aliyokuwa akiishi Imam Ali na wanawe Hasan na Husein. Ndani ya nyumba hiyo kuna kisima ambacho walikitumia kwa maji ya kunywa na kutawadha. Katika kipindi hiki nilijikuta nikiishi maisha ya kiroho na kuisahau dunia na yaliyomo ili niogelee ndani ya bahari ya utawa wa Imamu Ali na maisha yake yasiopenda makuu, hali akiwa mtawala wa waumini na ni katika makhalifa waongofu. Sitaacha kueleza ukarimu na unyenyekevu ambao niliuona huko *Al-Kufah,* kwani hatukupita kwenye kundi la watu isipokuwa walisimama kwa heshima yetu na kutusalimia na ni kama kwamba rafiki yangu alikuwa akiwafahamu wengi miongoni mwao.Mmoja wao ambaye alikuwa ni Mkuu wa Chuo cha *Al-Kufah* alitualika nyumbani kwake ambako tulikutana na wanawe na tukalala kwao usiku mtulivu. Mimi nilijihisi kama kwamba niko miongoni mwa ndugu zangu na jamaa zangu. Walikuwa kila wanapozungumza kuhusu Massunni husema *Ndugu zetu Masunni,* hivyo niliyapenda mazungumzo yao na nikawauliza baadhi ya maswali ya kuwajaribu ili niyakinishe ukweli wa maneno yao.

Tulielekea *Najafu* ambako kuna umbali wa kilomita kama kumi kutoka *Al-Kufah*, na mara tulipofika niliukumbuka Msikiti wa *Al-Kadhmiyyah* ulioko Baghdad. Minara ya dhahabu ilijitokeza hali ya kuwa imelizunguka Quba la dhahabu tupu, na tukaingia kwenye Haram ya Imam Ali baada ya kusoma idhini ya kuingia kama kawaida ya Mashia wanaozuru. Niliona mambo ya ajabu kuliko yale niliyoyaona kule kwenye Msikiti wa Musa Al-Kadhim, na kama kawaida nilisimama nikasoma fatha hali ya kuwa nina mashaka kwamba hili ndilo kaburi ambalo limehifadhi mwili wa Imam Ali. Kwa kiasi fulani nilikuwa nimekinaika na ile nyumba ndogo ya kawaida aliyokuwa akiishi Imam huko *Al-Kufah,* na nikasema moyoni, "Haiwezekani kwa Imam Ali kuridhia mapambo haya ya dhahabu na fedha wakati ambapo kuna Waislamu wanaokufa njaa sehemu mbali mbali duniani, na hasa kwa kuwa niliwaona masikini njiani wakinyoosha mikono yao kwa wapita njia wakiomba sadaka, kwa hiyo moyoni nilikuwa nasema:- Enyi Mashia ninyi ni wenye makosa, kubalini angalau kidogo kosa hili, Imam Ali ndiye ambaye Mtume wa Mwenyezi Mungu alimtuma kwenda kuyasawazisha makaburi, ni ya nini basi makaburi yaliyojengwa kwa dhahabu na fedha? Kwa hakika kama siyo kumshirikisha Mwenyezi Mungu, basi kwa namna fulani ni kosa kubwa ambalo Uislamu hauwezi kulisamehe.

Rafiki yangu aliniuliza hali ya kuwa akinipa kipande cha udongo mkavu akaniuliza, "Je unataka kuswali?" Nilimjibu kwa ukali, "Sisi hatusali pembeni ya makaburi." Akasema, "Basi nisubiri kidogo niswali rakaa mbili." Wakati namsubiri nilikuwa nasoma ubao uliotundikwa kwenye kaburi, na nilikuwa natazama ndani yake kupitia nguzo za dhahabu, mara nikaona kuwa (ndani ya kaburi kumejaa sarafu na noti za kila rangi, kuanzia Dir-ham, Riyal mpaka Dinar na Lira (zimo humo), na zote hizo zikitupwa (humo) na watu wanaouzuru ili kupata baraka kwa ajili ya kuchangia kazi za kheri zinazohusika na *Maqam* hiyo. Mimi nilidhani kwamba kutokana na wingi wake labda zina miezi kadhaa (tangu zilipowekwa humo), lakini rafiki yangu alinijulisha kuwa wahusika wa kusafisha Maqām ile huzichukua kila siku usiku baada ya sala ya Isha.

Nilitoka nikimfuata hali ya kuwa nimeshangazwa, nikitamani wanipe mimi sehemu yake au wazigawe kwa mafakiri na masikini ambao huko ni wengi mno.

Nilikuwa nikiangalia kila upande ndani ya ukuta mkubwa unaozunguka Maqām, watu wengi walikuwa wakisali huku na huko na wengine wakiwasikiliza Makhatibu waliokuwa juu ya Mimbar, pia nilisikia vilio vya baadhi yao wakiomboleza kwa sauti za huzuni.

Niliona kundi la watu wakilia na kupiga vifua vyao na nikataka kumuuliza rafiki yangu kuwa, "Wana nini watu hawa mbona wanalia na kujipiga? Mara lilipita jeneza karibu yetu na nikawaona baadhi yao wanaondoa *marumaru* (kifuniko cha kaburi) katikati ya ukumbi unaozunguka Maqām na kumteremsha maiti humo, basi nilidhania kuwa kilio chao hawa jamaa ni kwa ajili ya maiti huyu ambaye ni mtu muhimu kwao.

# KUKUTANA NA WANACHUONI

Rafiki yangu aliniingiza ndani ya msikiti ulioko *pembeni* ya Haram umetandikwa wote kwa miswala, na kwenye Mihrab yake kuna aya nyingi za Qur'an zilizonakshiwa kwa hati nzuri. Niliwaona vijana wadogo wadogo wenye vilemba wamekaa karibu ya Mihrab wakisoma, na kila mmoja wao mkononi mwake anacho kitabu. Mandhari hii nzuri ilinistajaabisha mno, kwani hapo kabla sijawahi kuwaona Masheikh wenye umri huu. Umri wao ulikuwa kati ya miaka kumi na tatu na kumi na sita, na kilichowazidisha uzuri ni hilo vazi kwa kuwa wamekuwa kama miezi kutokana na kung'ara wanakong'ra.

Rafiki yangu aliwauliza juu ya *Sayyid* wakamwambia kwamba; "Anasalisha watu sala ya jamaa." Mimi sikutambua huyo *Sayyid* ambaye aliwauliza ni nani isipokuwa niliamini kuwa ni mmoja wa wanachuoni.

Baadaye nilitambua kwamba ni Sayyid Al-Khui ambaye ni kiongozi wa Chuo cha Elimu cha Kishia, pia nilifahamu kwamba *Laqabu ya Sayyid* kwa Mashia ni jina la kila yule ambaye anatokana na kizazi cha Mtume (s.a.w.). Na *Sayyid* ambaye ni mwanachuoni au mwanafunzi huvaa kilemba cheusi, amma wanachuoni wengine huvaa kilemba cheupe na *Laqabu* yao ni ya *Sheikh*. Na kuna watu wengine mashuhuri ambao siyo wanchuoni wao wanavilemba vya kijani.

Rafiki yangu aliwaomba nikae nao wakati atakapokwenda kukutana na Sayyid, nao walinikaribisha na kunizunguka nusu duara hali ya kuwa nami naziangalia nyuso zao na nikahisi hawana dhambi na ni wasafi wa tabia zao. Akilini mwangu nikawa naikumbuka hadithi ya Mtume (s.a.w.) isemayo; "Mtu huzaliwa katika mila ya Kiislamu, bali wazazi wake humfanya awe na mila ya Kiyahudi au Kikristo au Majusi." Moyoni nikasema, *"Au humfanya awe Shia."*

Waliniuliza kuwa mimi ninatoka nchi gani nikasema "Tunisia."

Wakasema; “Je kwenu kuna vyuo vya elimu?” Nikawajibu, “Kwetu tunavyo vyuo vikuu na shule.” Basi yalinimimiminikia maswali toka kila upande na yote ni maswali makali na yenye kutatiza. Sasa niwaambie nini maskini hawa ambao wanaamini kwamba katika ulimwengu wa Kiislamu wote kuna vyuo vya elimu ambavyo ndani yake munasomeshwa *Fiqhi Usulud-din, Sheria* na *Tafsiri*, na hawafahamu kwamba sisi katika ulimwengu wetu wa Kiislamu na katika nchi zetu ambazo zimeendelea na zimebadilika, tumezigeuza madrasa za Qur’an na kuwa shule za malezi ya watoto zinazosimamiwa na watawa wa Kikristo. Je niwaambie kwamba, “Wao bado wako nyuma kimaendeleo ukilinganisha nasisi?”

Mmoja wao aliniuliza, “Ni madh-hebu gani yanayofuatwa huko Tunisia?” Nilisema, “Madh-hebu ya Malik.” Nikawaona baadhi yao wanacheka lakini sikujali. Akauliza tena, “Je, madh-hebu ya *Jaafariyyah* munayafahamu?” Nikasema: “Vema *Insha-allah*, jina hili jipya ni kitu gani? Hapana sisi hatufahamu isipokuwa madh-hebu manne na yasiyokuwa hayo siyo Uislamu.”

Alitabasamu hali ya kuwa anasema “Samahani madh-hebu ya *Jaafariyah* ndiyo Uislamu halisi, hivi hufahamu kwamba Abu Hanifa amesoma kwa Imam Jaafar As-Sadiq? Na kwa ajili hiyo Abu Hanifa anasema; Lau si miaka miwili, basi Nuu’man angeangamia.”

Nilinyamaza na sikuwa na jawabu. Kwa hakika amenifahamisha jina jipya ambalo kabla ya leo nilikuwa sijalisikia, lakini nilimshukuru Mwenyezi Mungu kwamba huyu Imam wao *Jaafar As-Saadiq* hakuwa mwalimu wa Imam Malik, nami nikasema “Sisi ni Malik na siyo Mahanafi.” Akasema “Bila shaka madh-hebu hizi nne baadhi yao wamesoma kwa wenzao, (yaani wamesomeshana), kwani Ahmad ibn Hanbal amesoma kwa Shafii na Shafii kasoma kwa Malik na Malik amesoma kwa Abuhanifa, na Abuhanifah naye kasoma kwa Jaafar As-Sadiq, kwa ajili hii basi, wote ni wanafunzi wa Jaafar ibn Muhammad, naye ndiye mtu wa kwanza kufungua Chuo Kikuu cha Kiislamu ndani ya Msikiti wa babu yake ambaye ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) na kwake (huyu Jaafar ibn Muhammad) wamesoma zaidi ya wanachuoni wa hadithi na Fiqhi wapatao elfu nne.” Nilimshangaa mvulana huyu hodari ambaye ameyahifadhi maneno ayasemayo kama vile mmoja wetu anavyohifadhi sura fulani ya Qur’an,

pia alinishangaza zaidi wakati alipokuwa akinitiririshia baadhi ya vitabu vya rejea za historia ambazo amehifadhi idadi ya juzuu na milango yake. Aliendelea nami mfululizo kama kwamba yeye ni Mwalimu anamsomesha mwanafunzi wake, kwa kweli nilihisi kuwa mimi ni dhaifu mbele yake na nikatamani lau ningetoka pamoja na rafiki yangu badala ya kubakia na wavulana hao. Hapana yeyote miongoni mwao aliyeniuliza kitu kuhusu Fiqhi au Historia isipokuwa nilishindwa kujibu. Aliniuliza "Ni nani ninayemqalid miongoni mwa Maimamu?" nikasema "Imam Malik." Akasema; "Ni vipi unamfuata mtu ambaye amekwisha kufa? Na baina yako na yeye kuna karne kumi na nne, ikiwa utataka kumuuliza kuhusu mas-ala mapya hivi kweli atakujibu?"

Nilifikiri kwa kitambo na kisha nikasema "Na wewe pia Jaafari wako amekwisha kufa tangu karne kumi na nne, hivyo unamqalid nani?" Yule mvulana alijibu kwa haraka yeye na wenzake "Sisi tunamqalid Sayyid Al-Khui, yeye ndiye Imam wetu." Mimi sikuelewa Je, Khui ndiye aliyekuwa mjuzi mno au Jaafari? Nilibakia pamoja nao hali ya kuwa najaribu kubadilisha maudhui, basi nikawa nawauliza kuhusu kitu chochote kitakacho wasahaulisha wao kuniuliza mimi, hivyo basi nikawauliza kuwa Najaf ina wakazi wangapi, na ni masafa kiasi gani kutoka Najaf hadi Baghdad na je kuna nchi zingine wazijuazo zaidi ya Iraq? Ikawa kila wakinijibu mimi huwauliza swali jingine ili tu niwashughulishe wasiniulize kwani nilishindwa (kuwajibu) na nilihisi kuwa nilikuwa na upungufu, lakini sikukiri (hilo mbele yao) japokuwa moyoni nilikuwa nimekiri kwani utukufu, heshima na elimu waliyonipachika huko Misri hapo imekuwa kama mvuke na imeyeyuka, hasa baada ya kukutana na hawa wavulana nilitambua ile hekima isemayo: "Mwambie yule anayedai kuwa yeye ni mwanafalsafa kwamba, wewe umefahamu kitu kidogo na mambo mengi hujayafahamu."

Niliona kwamba akili za wavulana hawa ni kubwa kuliko akili za hao Masheikh niliokutana nao (huko Misri) katika chuo cha Az-har, na pia ni kubwa kuliko akili za wanachuoni wetu ninaowafahamu huko Tunisia.

Sayyid Al-Khui aliingia akiwa amezungukwa na wanachuoni wenye haiba na utulivu, na wavulana hawa walisimama na wakamfuata Sayyid na kuubusu mkono wake. Mimi nilibakia nimesimama mahali pangu, na

Sayyid alipoketi wote wakaketi na akawa anawasalimu kwa kusema *"Massaakumullahu Bil-kheir"* akimuambia kila mmoja miongoni mwao na hujibu hivyo hivyo hata alipofika kwangu nikamjibu kama nilivyosikia.

Baada ya hapo rafiki yangu aliniashiria nimkurubie Sayyid baada ya kumnongoneza naye akanikalisha kuliani kwake kisha baada ya kusalimiana rafiki yangu aliniambia "Msimulie Sayyid ni mambo gani mnayoyasikia kuhusu Shia huko Tunisia?

Nikasema, "Ndugu yangu zinatosha hizo hekaya tunazozisikia huku na kule, jambo la muhimu ni mimi mwenyewe kufahamu nini wanachokisema Mashia nami ninayo baadhi ya maswali ambayo nataka majibu yake wazi wazi."

Rafiki yangu akanisisitiza na kutilia mkazo nimsimulie Sayyid ni itikadi gani tuliyo nayo juu ya Mashia nikasema: "Mashia kwetu sisi ni waovu mno dhidi ya Uislamu kuliko Mayahudi na Wakristo, kwa sababu hawa (Wayahudi) wana muabudu Mwenyezi Mungu na wanaamini Utume wa Nabii Musa (a.s.), wakati ambapo tunayoyasikia kuhusu Mashia ni kwamba, wao wanamuabudu Ali na kumtukuza, na miongoni mwao kuna kundi linalomuabudu Mwenyezi Mungu lakini wao humpa Ali daraja ya Utume wa Mwenyezi Mungu". Pia nilikisimulia kisa cha Jibril ni namna gani alivyofanya khiyana ya uaminifu kama wasemavyo kwamba, "Badala ya kupeleka Utume kwa Ali yeye aliupeleka kwa Muhammad (s.a.w.)."

Sayyid aliinamisha kichwa chake kidogo kisha akanitazama na akasema, "Sisi tunashuhudia kwamba hapana Mola apasiwaye kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. (Na tunamuomba Mwenyezi Mungu amteremshie sala na salamu yeye na kizazi chake chema kilichotakasika) na (tunashuhudia kuwa) Ali ni mja miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu."

Aliwageukia waliokuwepo hapo hali ya kuwa akisema na kuniashiria; "Tazameni masikini hawa, ni namna gani unavyowapotosha uvumi wa uongo, na jambo hili siyo geni nimekwisha sikia zaidi ya hayo kutoka kwa watu wengine, *Lahaula Walaquwwata Illa Billahil-Aliyyil-a'dhim"*.

Kisha akasema: “Je umesoma Qur’an?” Nikasema, “Nimehifadhi nusu yake kabla sijafika miaka kumi ya umri wangu.” Akasema, “Je unafahamu kwamba vikundi vyote vya Kiislamu pamoja na hitilafu ya madh-hebu yao, wanaafikiana kuhusu Qur’an, na hii Qur’an tuliyonayo sisi ndiyo ile ile muliyonayo ninyi.”

Nikasema, “Ndiyo jambo hili nalifahamu.” Akasema; “Kwa hiyo basi hujaisoma kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo, Muhammad hakuwa isipokuwa ni Mtume kwa hakika wamepita kabla yake Mitume” (3:144), pia kauli yake isemayo “Muhammad ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu na wale walio pamoja naye ni wenye nguvu dhidi ya makafiri. (48:29) kadhalika kauli nyingine isemayo: “Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, lakini ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu naye ndiye mwisho wa Manabii.” *(35:40)*

Nikasema, “Bila shaka ninazifahamu aya hizi.” Yeye akasema; “Basi yu wapi Ali? Ikiwa Qur’an yetu inasema kwamba, Muhammad ndiye Mjumbe wa Mwenyezi Mungu basi uongo huu unatokea wapi?”

Nilinyamaza na sikuwa na jawabu, naye aliongeza kusema; “Amma khiyana ya Jibril, namuomba Mwenyezi Mungu amlinde kutokana na hilo; hili ni jambo baya zaidi kuliko lile la mwanzo kwa sababu Muhammad umri wake ulikuwa ni miaka arobaini wakati Mwenyezi Mungu alipomtuma Jibril (a.s.) kwa Muhamad, na Ali alikuwa ni mvulana mwenye umri wa miaka sita au saba, basi ewe Bwana ni vipi Jibril atakosea na asiweze kupambanua baina ya Muhammad ambaye ni mtu mzima na Ali ambaye ni mvulana?”

Kisha nilinyamaza kwa muda mrefu, nikiyafikiria maneno yake hali ya kuwa nawaza na kuchambua, na nimeyapenda mazungumzo yenye mantiki ambayo yameniingia moyoni na kuondoa kizibo machoni mwangu. Isitoshe nikajiuliza ndani kwa ndani, “Ni vipi sisi hatukuweza kutatua mambo haya kwa kutumia mantiki hii?” Sayyid Al-Khui aliendelea kusema: “Nakuongezea zaidi ya kwamba Mashia ndiyo kundi pekee kati ya makundi ya Kiislamu linalosema kuwa Mitume na Maimamu ni *Maasum*, kwa hiyo iwapo Maimamu wetu (a.s.) wamelindwa wasikosee nao ni watu kama sisi, basi itakuwaje kwa Jibril ambaye ni Malaika mwema na

Mola Mtukufu amemwita kuwa ni *Roho Mwaminifu?"* Mimi nilisema, "Basi uzushi huu umetokea wapi?" Akasema Unatoka kwa maadui wa Uislamu ambao wanataka kuwatenganisha Waislamu, kuwagawanya na kuwachonganisha wao kwa wao, kinyume cha hivyo ni kwamba Waislamu ni ndugu sawa sawa wakiwa ni Mashia au Masunni, kwani wao wanamuabudu Mwenyezi Mungu peke yake na hawamshirikishi na chochote na Qur'an yao ni moja na Mtume wao ni mmoja na kibla yao ni moja na wala Shia na Sunni hawatofautiani isipokuwa katika mambo ya Kifiqhi kama ambavyo Maimam wa Madh-hebu za Kisunni wenyewe wanatofautiana kati yao. Malik anamkhalifu Abu Hanifa na huyu naye anamkalifu Shafii na kadhalika.

Nikasema: "Kwa hiyo yote yanayosemwa juu yenu ni uzushi mtupu?" Akasema, *Al-hamdulilah* wewe ni mtu mwenye akili na unafahamu mambo na umekwishaiona miji ya Kishia na umetembea miongoni mwao, je, hivi umeona au kusikia chochote katika uzushi huo?" Nikasema, "Sikusikia wala kuona isipokuwa mambo mazuri, nami kwa hakika namshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyenitambulisha kwa Ustadh Mun-i'm ndani ya boti, kwani yeye ndiye sababu ya kuja kwangu Iraq na kwa hakika nimefahamu mambo mengi ambayo nilikuwa siyajui." Rafiki yangu Mun-i'm alicheka huku akisema, "Na miongoni mwa hayo usiyoyajua ni kuwepo kwa kaburi la Imam Ali....." Mimi nikamkatiza na kumuwahi hali ya kuwa ninasema "Bali nimejifunza mambo mapya hasa kutoka kwa wavulana hawa, na nimetamani lau kama ningepewa fursa ili nijifunze kama wao katika Chuo cha Elimu hapa."

Sayyid akasema' "Karibu, nafasi ni yako, ikiwa wewe unataka kusoma, Chuo kitakudhamini nasi tupo kwa ajili ya kukuhudumia." Rai hii ilipokelewa na wote waliohudhuria hapo na hasa rafiki yangu Mun-i'm ambaye uso wake ulionesha furaha.

Nikasema, "Mimi nimeoa na nina watoto wawili." Akasema, "Sisi tutabeba jukumu la kila mambo yako yanayokulazimu kuanzia makazi, chakula na kila utakachohitajia, jambo muhimu ni kusoma."

Nilifikiri kidogo na nikajisemeza moyoni "Siyo busara mimi kuwa mwanafunzi baada ya kumaliza miaka mitano nikiwa mwalimu

ninayefundisha na ni mlezi, na siyo jambo rahisi kulichukulia uamuzi jambo kama hili kwa haraka."

Nilimshukuru mno Sayyid Al-Khui kwa ahadi hii (ya kukubali kubeba jukumu) na nikasema; "Nitafikiria kuhusu maudhui hii kwa undani baada ya kurejea kwangu toka Umra kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, lakini nina haja ya baadhi ya vitabu."

Sayyid akasema, "Mpeni vitabu." Basi kilinyanyuka kikundi cha Wanachuoni na wakafungua makabati na punde nilijikuta mbele yangu kuna mijalladi (volumes) sabini na kila mmoja aliniletea aina ya vitabu na akasema, "Hii hapa zawadi yangu." Niliona kwamba siwezi kubeba idadi hii kubwa ya vitabu hasa kwa kuwa ninaelekea Saudi Arabia ambako hawaruhusu kuingia kitabu chochote katika nchi yao, kutokana na hofu yao ya kuenea kwa itikadi ambazo zinakwenda kinyume na Madh-hebu yao. Lakini sikupenda kuikosa bahati ya vitabu hivi ambavyo sijawahi kuipata hapo kabla maishani mwangu.

Basi nikamwambia rafiki yangu na wote waliokuwepo hapo kwamba, "Safari yangu ni ndefu, inapitia Damascus, Jordan hadi Saudi Arabia, na wakati wa kurudi itakuwa ndefu zaidi kwani nitapita Misri, Libya hadi Tunisia na licha ya kuwa ni mzigo mzito nchi nyingi zinazuia kuingiza vitabu."

Sayyid akasema; "Tuachie anuani yako nasi tutabeba jukumu la kukutumia." Rai hii niliiona ni nzuri na niliipenda, nikachukua kadi yangu binafsi yenye anuani yangu ya Tunisia nikampa nikamshukuru kwa wema wake.

Nilipomuaga nikasimama ili nitoke, alisimama pamoja nami hali ya kuwa anasema, "Nakuombea Mwenyezi Mungu akupe salama na utakapofika kwenye kaburi la babu yangu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu mfikishie salamu zangu."

Watu wote waliathirika, nami niliathirika mno hali ya kuwa nayaona macho yake yanatiririka machozi na nikasema moyoni, "Haiwezekani mtu huyu kuwa miongoni mwa watu wanaokosea, na haiwezekani mtu

huyu kuwa miongoni mwa watu waongo, bila shaka haiba yake, heshima na unyenyekevu wake vinaonesha kweli kwamba yeye anatokana na kizazi kitakatifu. Sikuwa na lakufanya isipokuwa niliushika mkono wake nikaubusu bila kujali kwamba alikuwa akiuzuwiya.

Watu wote walinyanyuka niliposimama na wakaniombea salama, na baadhi ya wale wavulana waliokuwa wakijadiliana nami walinifuata na kunitaka anuani yangu ili tuwasiliane nikawapa.

Kwa mara nyingine tena tulielekea mji wa *Kufah* kwa mwaliko wa mmoja wa watu waliokuwa pale kwenye kikao na Sayyid Khui, naye ni rafiki wa yule rafiki yangu Mun-i'm jina lake ni Abu Shubbar.

Tulifika kwake na tulikesha usiku kucha pamoja na jumla ya vijana wenye taaluma wakiwemo wanafunzi wa Sayyid Muhammad Bāqir Sadir. Hawa walinishauri niende nikamzuru Sayyid Bāqir Sadir, na waliniahidi kuwa wao watapanga utaratibu wote wa kukutana naye siku ilinayofuata.

Rafiki yangu Mun-i'm aliona ni wazo zuri, isipokuwa alisikitishwa na kutoweza kwake kuhudhuria kwa kuwa alikuwa na kazi mjini Bughdad iliyomlazimu aende huko. Tulikubaliana nibakie nyumbani kwa Sayyid Abū-Shubbar siku tatu au nne mpaka atakaporudi Mun-im ambaye alituacha baada ya sala ya asubuhi, nasi tulilala alipoondoka. Kwa hakika nilifaidika sana na wanafunzi wale niliokesha nao. Nilistaajabishwa na aina tofauti ya elimu wazisomazo ndani ya *Hauzah*, kwani wao kando na elimu za dini ya Kiislamu kama vile Fiq'hi, Sharia, Tauheed, wanasoma na elimu ya uchumi pia elimu ya kijamii siasa, historia, lugha tofauti na elimu ya Sayari na nyinginezo.

# KUKUTANA NA SAYYID MUHAMMAD BAQIR AS-SADR

Nilifuatana na Sayyid Abu-Shubbar kwenda kwa Sayyid Muhammad Bāqir As-Sadri, na wakati tukiwa njiani alikuwa akinienzi na kunipa maelezo yanayohusu wanachuoni mashuhuri pia juu ya Taqlid na mengineyo. Tuliingia nyumbani kwa Sayyid Muhammad Bāqir As-Sadri na palikuwa pamejaa wanafunzi, wengi wao wakiwa ni vijana wenye vilemba. Sayyid alisimama na kutusalimia kisha walinitambulisha kwake naye akanikaribisha na kunikalisha pembeni yake halafu akaanza kuniuliza habari za Tunisia na Algeria, pia kuhusu wanachuoni mashuhuri kama vile Al-Khidhri Hussein na Tahir ibn Asfur na wengineo.

Nilinufaika kwa mazungumzo yake licha ya ile haiba aliyonayo na heshima wampayo watu wanaoketi pamoja naye. Nilijikuta sina uzito wowote na ni kama kwamba nilifahamiana naye toka hapo kabla. Nilifaidika kutokana na kikao hicho kwani nilikuwa nikisikiliza maswali ya wanafunzi na majibu ya Sayyid.

Katika kipindi hicho, nilifahamu faida ya kuwafuata wanachuoni walio hai ambao hujibu utata wowote pale pale na kwa uwazi na nikayakinisha vile vile kwamba Mashia ni Waislamu wanaomuabudu Mwenyezi Mungu na wanauamini Utume wa Mtume wetu Muhammad (s.a.w.). Yote haya ni kwa sababu baadhi ya shaka zilikuwa zikinihadaa, shetani naye akinitia wasiwasi ya kwamba niliyoyaona hapo kabla ilikuwa ni kuigiza tu na huenda ni kile kitu wakiitacho *Taqiyyah* (ndicho wanachonionesha) yaani wao hudhihirisha kile wasichokiamini. Kwa haraka mno shaka hii inaondoka na ule wasiwasi nao unadhoofika kwa kuwa haiwezekani kwa hali yoyote ile wote niliowaona na niliowasikia ambao ni mamia ya watu waafikiane juu ya kuigiza na ni kwa nini waigize na mimi ni nani hata (wafanye wasiyoyaamini)? Isitoshe nina umuhimu gani

kwao hata niwafanye watumie Taqiyyah hii? Kisha hivi vitabu vyao vya zamani ambavyo vimeandikwa tangu karne nyingi, na vitabu vipya ambavyo vimechapishwa kwa miezi michache tu iliyopita pia vipo, na vyote vinampwekesha Mwenyezi Mungu na kumtukuza Mtume wake Muhammad (s.a.w.) kama nilivyolisoma jambo hilo katika utangulizi wake. Sasa hivi niko ndani ya nyumba ya Sayyid Muhammad Baqir-As-Sadri ambaye ni *Mar-jaa* mashuhuri nchini Iraq na nje ya Iraq. Pia kila litajwapo jina la Mtume Muhammad wote kwa sauti moja wanasema "*Allahumma salli allā* Muhammad waāli Muhammad."

Ulifika wakati wa sala na tulitoka kwenda Msikitini na ulikuwa karibu ya nyumba ya Sayyid, na yeye Sayyid Muhammad Baqir As-Sadri akatusalisha sala ya Adhuhuri na Alasiri. Nilijihisi kama kwamba mimi ninaishi miongoni mwa Masahaba Watukufu. Sala hizo mbili zilikuwa zikifuatwa na dua nzito iliyosomwa na mmoja wa watu waliokuwa wakiswali humo na alikuwa na sauti ya huzuni.

Na kila akimaliza kusoma dua wote husema kwa sauti za juu: "Allahumma salli Alā Muhammad waāli Muhammad" Du'a yote ilikuwa imejaa sifa na Utukufu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kisha sifa za Mtume Muhammad na Kizazi chake chema kilichotakasika.

Baada ya sala Sayyid alikaa kwenye *Mihrab*, baadhi yao walianza kumsalimia na kumuuliza kwa siri na wengine wazi wazi, naye alikuwa akiwajibu kwa siri baadhi ya Mas-ala ambayo nilitambua kwamba yanahitajia kujibiwa kwa siri kwani yanahusiana na mambo binafsi naye muulizaji anapopata jawabu alikuwa akiubusu mkono wa Sayyid kisha huondoka. Na hii ni dalili ya kumpongeza (kumshukuru) Mwanachuoni huyu ambaye anatatua matatizo yao na anashirikiana nao katika taabu zao. Tulikuwa pamoja na Sayyid na kwa mara nyingine ambapo alinitendea wema na alinipa mapokezi mazuri ambayo yanisahaulisha watu wangu na jamaa zangu na nikahisi kwamba lau ningebakia pamoja naye kwa mwezi mmoja ningekuwa Shia kutokana na tabia yake na unyenyekevu wake na ushirikiano wake mzuri, kwani kila nikimwangalia yeye hutabasamu na kuanza kunisemesha na kuniuliza, "Je, kuna kitu fulani kimenipungukia?" Kwa hali hiyo nilikuwa simwachi kwa muda wote wa siku nne isipokuwa wakati wa kulala, licha ya kuwa na Wanachuoni na wageni wengi

waliokuwa wakifika kwake toka nchi mbali mbali.

Niliwaona Wasaudia huko, na sikudhania kabisa kwamba katika nchi ya Hijaz wako Mashia, pia wanachuoni wa Bahrain na wengine toka Qatar, Imārāt na kutoka Lebanon, Syria, Iran, Afghanistan na Uturuki na pia toka Afrika nyeusi. Naye Sayyid alikuwa akizungumza nao na kuwakidhia haja zao na walikuwa wakitoka hali ya kuwa ni wenye furaha.

Hapo sitaacha kueleza tukio nililoliona, na nilishangaa namna lilivyotatuliwa, nami nalitaja kwa ajili ya kumbukumbu ya kihistoria kutokana na umuhimu wake mkubwa ili Waislamu wapate kufahamu ni kwa kiasi gani wamepata hasara kwa kuacha hukumu ya Mwenyezi Mungu.

Kuna watu wanne walikuja kwa Sayyid Muhammad Baqir As-Sadr na nadhani walikuwa Wairaq nililifahamu hilo kutokana na lahaja yao. Mmoja wao alirithi makazi fulani toka kwa babu yake aliyefariki miaka mingi iliyopita, na huyu Bwana akapauza mahali hapo kwa mtu mwingine ambaye alikuwepo (siku hiyo). Baada ya kupita mwaka tangu kuuzwa mahala hapo, kuna ndugu wawili walikuja kuthibitisha kwamba wao ni warithi wa Kisheria wa Mar-hum yule, na wote wanne walikaa mbele ya Sayyid na kila mmoja wao akatoa nyaraka zake na ushahidi alionao.

Baada ya Sayyid kusoma nyaraka zao na akazungumza nao kwa muda wa dakika chache, aliwatatulia tatizo lao kwa uadilifu, akampa yule mnunuzi haki ya kutumia mahala pale na akamtaka yule muuzaji awape wale ndugu wawili fungu lao kutoka kwenye thamani aliyoichukua kisha wote walisimama na kuubusu mkono wa Sayyid na wakakumbatiana.

Nilishangazwa na hali hii na sikuamini, ndipo nilipomuuliza Abu Shubbar, “Je tatizo hili ndiyo limemalizika?” Akasema, “Limekwisha na kila mmoja amechukua haki yake.” *Subhanallah!!* kiurahisi namna hii na kwa muda mchache kama huu, dakika chache zinatosha kusuluhisha ugomvi? Kwa hakika tatizo kama hili nchini kwetu linachukua muda wa miaka kumi kwa uchache na baadhi yao hufariki na watoto wao kuendelea kulifuatilia tatizo hilo, na gharama za mahakama na watu wa kuwatetea huweza wakati mwingine kugharimu ile thamani ya makazi yenyewe. Si

hivyo tu bali huanzia mahakama ya mwanzo kisha mahakama ya Hakimu Mkazi na hatimaye kwenda mahakama ya rufaa na mwisho wote huwa hawaridhiki baada ya kuwa wamesumbuka, kutaabika, kupoteza pesa na rushwa, hatimaye uadui na chuki (hujitokeza) miongoni mwa ndugu na jamaa."

Abu Shubbar alinijibu "Hata sisi hali ni ile ile au zaidi." Mimi nikasema, "Vipi?" Akasema, "Watu wanapopeleka mashitaka yao kwenye mahakama za kiserikali basi hali inakuwa kama hiyo uliyoisimulia, ama wakiwa ni watu wanaomqalid Mar-jaa wa kidini na wanafuata hukumu za Kiislamu, basi hawapeleki mashitaka yao isipokuwa kwa Mwanachuoni huyo, naye huwatatulia kwa dakika chache kama ulivyoona. *Na ni nani mwenye hukumu nzuri kuliko Mwenyezi Mungu kwa watu wenye akili?* Sayyid Sadr hakuchukua kwao japo senti moja, na lau wangekwenda kwenye Mahakama za Serikali wangenyanyasika. Nilicheka kutokana na maelezo haya ambayo kwetu pia inatendeka na kisha nikasema, *"Subhanallah!!* Mimi bado siamini haya niliyoyaona na lau nisingeshuhudia kwa macho yangu kamwe nisingesadiki." Abu Shubbar akasema, "Usipinge ndugu yangu hili ulililiona ni dogo ukilinganisha na matukio mengine ambayo yana utata mkubwa na husababisha damu kumwagika, lakini pamoja na hali hiyo Mar-jaa huweza kuyasuluhisha kwa muda mchache."

Nilisema hali ya kuwa nastaajabu, "Kwa hiyo ninyi hapa Iraq munazo serikali mbili, serikali ya Dola na Serikali ya watu wa dini." Akasema, "Sivyo tuliyonayo ni Serikali ya Dola peke yake, lakini Waislamu wa Kishia ambao wanawaqalid Mar-jaa wa kidini hawajishughulishi na Serikali isiyo ya Kiislamu. Wao wanaitii katika mambo ya uraia, kodi, haki za nchi na mazingira binafsi, na lau Muislamu mwenye kushika dini atagombana na mmoja wa Waislamu wasioshika dini basi atalazimika kupeleka tatizo lake kwenye Mahakama za Serikali kwani huyu mwingine hawezi kuridhia kuamuliwa na Wanachuoni wa kidini. Ama waliohitilafiana wakiwa ni watu wenye kushika dini, basi hapo hakuna tatizo, na kile atakachokiamua Mar-jaa wote watakikubali. Na kwa msingi huu matatizo ambayo huhukumiwa na Mar-jaa hutatuliwa siku hiyo hiyo, wakati ambapo matatizo mengine (yanayohukumiwa kwingine) huendelea kwa miaka mingi."

Kwa hakika hili ni tukio lililoitingisha nafsi yangu, zile hisia za kuiridhia hukumu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na nikaifahamu ile maana ya kauli ya Mwenyezi Mungu iliyoko katika kitabu chake kitukufu aliposema: *"Na asiye hukumu kwa mujibu wa hukumu aliyoiteremsha Mwenyezi Mungu watu hao ni makafiri, na asiye hukumu kwa mujibu wa hukumu aliyoiteremsha Mwenyezi Mungu watu hao ni madhalimu, na asiye hukumu kwa mujibu wa hukumu aliyoiteremsha Mwenyezi Mungu watu hao ni mafasiki." (5:44, 45, 47).* Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kweli.

Kama ambavyo pia liliamsha hisia katika nafsi yangu za kuchukia na kuwapinga madhalimu hawa ambao wanazibadilisha hukumu adilifu za Mwenyezi Mungu kwa kuleta hukumu na kanuni za wanadamu ambazo ni za kijeuri na wala yote hayo hayawatoshi, bali wanazikosoa bila aibu na kuzikebehi hukumu za Mwenyezi Mungu, na wanasema kuwa ni za kikatili na kishenzi kwa kuwa zinaweka adhabu ya kumkata mkono mwizi na kumpiga mawe mzinifu na kumuuwa muuwaji.

Sasa basi nadharia hii ya kigeni imetujia kutoka wapi (mpaka ikawa) dhidi ya urithi wetu? Hapana shaka hiyo ni nadharia toka nchi za Magharibi ambao ni maadui wa Uislamu, wameona kuwa kuzitumikisha hukumu za Mwenyezi Mungu kuwaangamiza wao moja kwa moja kwa kuwa wao ni wezi, mahaini wazinifu na ni waovu na wauaji. Na lau hukumu za Mwenyezi Mungu zingetekelezwa dhidi yao basi tungeepukana na watu wote wa aina hii.

Katika kipindi hicho cha kuwepo Najaf, yalikuwa yakifanyika mazungumzo kati yangu na Sayyid Muhammad Al-Baqir na nilikuwa nikimuuliza kila jambo dogo na kubwa kufuatia mambo niliyokuwa nimeyafahamu kupitia kwa marafiki zangu ambao walinisimulia mengi juu ya itikadi yao na kile wakisemacho juu ya Masahaba (r.a.) na kile wanachokiamini kuhusu Maimamu kumi na mbili yaani Ali na wanawe na mambo mengine ambayo sisi tunahitilafiana nao.

Nilimuuliza Sayyid juu ya Imam Ali na ni kwa nini wanamshuhudia kwenye adhana kwamba yeye ni walii wa Mwenyezi Mungu? Alinijibu akasema "Kwa hakika Amirul-muuminina Ali amani ya Mwenyezi

Mungu imshukie, yeye ni mja miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu ambao amewachagua na kuwatukuza ili waendeleze jukumu zito la ujumbe baada ya Mitume. Watu wa namna hii ni Mawasii wa Mitume, kwani kila Nabii anayewasii wake na Ali ibn Abitalib ni wasii wa Muhammad, nasi tunamboresha juu ya masahaba wengine kwa vile Mwenyezi Mungu na Mtume wake wamemboresha. Na kuhusu hali hii sisi tunazo dalili za kiakili na zingine ni zile za Qur'an na Sunna. Dalili zote hizi haiwezekani kuingiwa na shaka kwani ni mutawatir kwa njia zetu na hata kwa njia za Ahlu-Sunnah wal-Jamaa, pia wanachuoni wetu wametunga vitabu vingi juu ya jambo hilo lakini ilipokuwa utawala wa Banu-Umaiyyah umesimama kidete kufuta ukweli huu na kumpiga vita Amirul-Muuminina Ali na wanawe na kuwaua, na mambo yakafikia kumtukana na kumlaani juu ya mimbari za Waislamu na kuwalazimisha watu kwa nguvu wamtukane na kumlaani, hapo ndipo Mashia wake na wafuasi wake (r.a.) wanashuhudia kwamba Ali ni Walii wa Mwenyezi Mungu na haifai kwa Muislamu kumtukana Walii wa Mwenyezi Mungu. Walifanya hivyo ili kuonesha upinzani wao kwa Tawala dhalimu. Ili utukufu uwe ni wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na waumini na ili (kushuhudia huko) kuwe ni msukumo wa kihistoria kwa Waislamu wote katika vizazi vyote wapate kufahamu ukweli juu ya Ali (a.s.) na uovu wa maadui zake. Wanachuoni wetu wameendelea kushuhudia kwamba Ali (a.s.) ni Walii wa Mwenyezi Mungu katika adhana kwa kupendekeza kuwa ni jambo jema na wala siyo kuwa ni sehemu ya adhana au Iqamah. Iwapo muadhini au mwenye kuqim atanuwia kuwa ni sehemu ya Adhana, Adhana na Iqamah yake vitabatilika. Mambo mustahabu ndani ya Ibada na matendo ni mengi mno, na Muislamu hupata thawabu kwa kuyatenda wala haadhibiwi kwa kuyaacha. Kwa mfano imekuja kwamba ni mustahabbu baada ya kushuhudia kwamba hapana Mola apasiwaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na kwamba Muhammad ni mjumbe wake, Muislamu aseme nashuhudia kwamba pepo ni kweli na moto ni kweli (upo) na kwamba Mwenyezi Mungu atawafufua waliomo makaburini."

Mimi nikasema "Wanachuoni wetu wametufundisha kwamba, ukweli halisi ni kuwa khalifa bora mno ni Sayyidna Abubakar As-Sidiq, kisha Sayyidna Umar *Al-Faruq* kisha Sayyidna Uthman na kisha Sayyidna Ali Mwenyezi Mungu awe radhi nao wote." Sayyid alinyamaza kisha akanijibu, "Wanao uhuru wa kusema wapendavyo, lakini hawawezi

kulithibitisha hilo kwa dalili za kisheria, kisha kauli hii inakwenda kinyume na maelezo yaliyomo ndani ya vitabu vyao sahihi vya kutegemewa. Ndani ya vitabu hivyo imeelezwa kwamba mtu mbora mno kuliko watu wote ni Abubakr kisha Omar kisha Othman na wala Ali hayumo bali wamemfanya kuwa ni mtu wa kawaida tu, isipokuwa ametajwa na wanachuoni wa baadaye kwamba ni mustahabbu kumtaja miongoni mwa *Ma-Khalafaur-Rashiduna.”*

Baada ya hilo nilimuuliza juu ya udongo wanaoutumia kusujudu juu yake ambao wanauita *“Tur-batul-Husaniniyyah.”* Alinijibu akasema; “Kabla ya yote inakupasa ufahamu kwamba sisi tunasujudu juu ya udongo na wala hatusujudii udongo kama baadhi ya watu wanavyodhani na hatimaye kuwazushia uongo Mashia. Sijda ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake, na kilichothibiti kwetu sisi na kwa Masunni ni kwamba, kilichobora ni kusujudu juu ya ardhi au kitu kilichoota ardhini kisicholiwa, na wala haisihi kusujudu juu ya kitu kinginecho na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa akitandika udongo na akitumia jamvi lililotengenezwa kwa udongo na makuti na husujudu juu yake. Aliwafundisha Masahaba wake (r.a.) wakawa wanasujudu juu ya ardhi na changarawe, na akawakataza yeyote kati yao asisujudu kwenye ncha ya nguo yake, na mambo haya kwetu sisi yanajulikana bila haja ya dalili. Imam Ali ibn Husein ambaye ni mashuhuri kwa jina la Zainul Abidina (a.s.) naye ni Bwana wa wenye kusujudu alichukua udongo wa kaburi la Baba yake Abu Abdillah (Imam Husein a.s.) kwa kujua kwamba huo ni udongo uliotakasika na ambao damu za mashahidi zimemwagika juu yake. Mashia wake nao wakaendelea kufanya hivyo mpaka leo. Sisi hatusemi kwamba kusujudu hakusihi isipokuwa juu ya udongo huo, bali tukisemacho ni kwamba, Sijda inasihi juu ya udongo wowote na jiwe lolote lenye tahara kama inavyosihi kusujudu juu ya jamvi na kilichotengenezwa kwa makuti ya mtende na mfano wa hicho.”

Nikamuuliza Sayyid kuhusu kumbukumbu ya Saydna Husein (r.a.), “Je, ni kwa nini Mashia wanalia na kujipiga wenyewe mpaka damu inawatoka hali ya kuwa jambo hili katika Uislamu ni haramu, kwani Mtume (s.a.w.) amesema: Si miongoni mwetu atakayejipiga mashavu na kuchana mifuko na akalingania mwito wa kijahiliya.”

Sayyid akajibu, “Hadithi hii ni sahihi lakini haiendani na maombolezo ya Abu Abdillah (Husein ibn Ali a.s.) kwani mtu anaelingania kisasi kwa ajili ya Husein huyo yuko katika njia ya Husein, na katika mwito wa Husein na wala siyo mwito wa kijahiliya. Kisha ieleweke kuwa Mashia ni watu, miongoni mwao kuna mwanachuoni na mjinga, na wanahisia za kimaumbile ya kibinadamu, hivyo basi endapo miongoni mwao kuna ambaye hisia zake za kimaumbile zimechemka na kumshinda kwa ajili ya kukumbuka jinsi alivyokufa kishahidi Abu Abdilahi na yale aliyotendewa yeye na watu wa nyumba yake na waliyotendewa masahaba wake kwa kuuwawa kikatili, kuwavunjia hadhi yao ya kibinadamu na kuchukuliwa mateka, bila shaka wenye kufanya hayo watalipwa mema kwa nia zao, kwa kuwa (wamefanya kwa) ajili ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu humlipa mtu ujira kulingana na nia yake.

Sayyid aliendelea kusema; “Wiki iliyopita nimesoma ripoti rasmi ya serikali ya Misri ikielezea kifo cha aliyekuwa rais wa nchi hiyo Jamal Abdun-Nasir, kwamba: Watu wanane wamejiuwa mara tu waliposikia habari za kifo chake, kuna aliyejitupa kutoka juu ya nyumba na kuna aliyejiingiza mwenyewe chini ya gari moshi n.k. na wako wengi mno waliojeruhiwa na kupagawa kwa ajili ya huzuni hii. Mifano hii niitajayo ni ya hisia za kimaumbile ya kibinadamu ambayo kuna wakati huwazidi wenye nayo, na watu hao ni Waislamu bila shaka wamejiua kwa ajili ya kufa Jamal Abdun-Nasir hali ya kuwa amekufa kifo cha kawaida.Kwa msingi wa tukio hili hatuna haki kuwahukumu Masunni kuwa ni wenye makosa. Hivyo basi sio haki wala uadilifu kwa ndugu zetu Masunni kuwahukumu ndugu zao Mashia kuwa wanamakosa kwa kumuhuzunikia Bwana wa Mashahidi, nao Mashia wameishi na wanaendelea kuishi katika hali ya mateso mpaka leo. Hapana shaka kwamba, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu Mwenyewe alimlilia Husein kiasi kwamba Jibril naye alilia kutokana na kilio cha Mtume Mtukufu (s.a.w.).”

Nikasema, “Ni kwa nini Mashia wanayapamba makaburi ya mawalii wao kwa dhahabu na fedha jambo ambalo ni haramu katika Uislamu?” Sayyid As-Sadri alijibu: “Tendo hilo siyo kwa Mashia peke yao na wala siyo haramu, bali iko Misikiti ya ndugu zetu Masunni sawa iwe Iraq au Misri au Uturuki au penginepo katika nchi za Kiislamu imepambwa kwa dhahabu na fedha na pia Msikiti wa mjumbe wa Mwenyezi Mungu huko

Madina tukufu na nyumba ya Mwenyezi Mungu tukufu huko Makkah ambayo kila mwaka huvalishwa vazi la dhahabu jipya linalogharimu mamilioni ya fedha, kwa hiyo hili siyo la Mashia peke yao.

Nikasema “Wanachuoni wa Kisaudia wanasema kuwa, kujipangusa (kugusa) kwenye makaburi na kuwaomba watu wema na kutabaruku kwao ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu basi nini maoni yenu?”

Sayyid Muhammad Baqir As-Sadri alijibu: “Kuyagusa makaburi na kuwaomba wenye makaburi hayo kwa nia ya kwamba wanadhuru na kunufaisha hii bila shaka ni shirki, na hapana shaka kwamba Waislamu wanampwekesha Mwenyezi Mungu na wanafahamu kwamba ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiye mwenye kudhuru na kunufaisha na wao wanawaomba mawalii na maimamu ili wawe ni wasila kwake na hii siyo shriki. Vilevile Masunni na Mashia wanakubaliana juu ya hilo tangu zama za Mtume mpaka leo, isipokuwa Mawahabi ambao ni wanachuoni wa Saudia uliowataja na ndiyo ambao wameikhalifu Ijmai ya Waislamu kwa madh-hebu yao mapya yaliyojitokeza mno katika karne hii. Kwa hakika hawa wamewafitini Waislamu kutokana na itikadi yao hii na wamewakufurisha na kuhalalisha kumwaga damu zao, kwani wao huwapiga wazee miongoni mwa Mahujaji wa nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu kwa kadiri ya mmoja wao kusema: *“Assalaamu Alaika ya Rasulallah* na hawamruhusu yeyote kugusa kaburi lake tukufu.”

Sayyid akaendelea kueleza, “Yalipata kutokea majadiliano kati yao (wanachuoni wa Kiwahabi) na wanachuoni wetu lakini hata baada ya kuoneshwa ukweli waliendelea na ubishi na wakatakabari mno. Sayyid Sharafud-din ambaye ni miongoni mwa wanachuoni wetu wa Kishia alipokwenda kuhiji kwenye nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu zama za mfalme Abdul-Aziz Al-Saud alikuwa miongoni mwa wanachuoni walioalikwa kwenda kwenye jumba la mfalme ili kumpa mkono wa sikukuu ya *“Idd Al-Udh-ha.”* Kama ilivyokuwa kawaida ya huko, ilipofika zamu yake kupeana mkono na mfalme, (Sayyid) alimpa (mfalme huyo) zawadi ambayo ilikuwa ni msahafu uliofungwa ndani ya ngozi, naye akaubusu na kuuweka kwenye paji lake la uso kwa kuuheshimu na kuutukuza. Hapo ndipo Sayyid Sharafud-din alipomwambia mfalme “Ewe mfalme, kwa nini unaibusu ngozi na kuitukuza wakati hiyo ni ngozi ya mbuzi?”

Mfalme akajibu “Mimi nimeikusudia Qur’an Tukufu ambayo imo ndani ya ngozi na sikukusudia kuitukuza ngozi.” Basi Sayyid Sharafud-din akasema, “Vema ewe mfalme, basi ni hivyo hivyo tufanyavyo sisi tunapoyabusu madirisha ya chumba cha Mtume au milango yake. Sisi pia tunafahamu kabisa kwamba hivyo ni vyuma havidhuru na wala havinufaishi, lakini huwa tunakikusudia kilichopo nyuma ya vyuma hivyo na mbao hizo, kwa hiyo sisi hukusudia kumtukuza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) kama wewe ulivyoikusudia Qur’an kwa kuibusu ngozi ya mbuzi ambayo imefunika Qur’an.”

Basi waalikwa walitoa takbira *“Allahu Akbar”* kwa kumfurahiya Sayyid na wakasema umesema kweli na jambo hilo lilimlazimisha mfalme huyo katika zama zake awaachie Mahujaji watabaruku kwa athari za Mtume (s.a.w.) mpaka alipokuja (mfalme) ambaye alifuatia baada yake akarudia katika uamuzi ule wa zamani. Basi hapa tatizo lao siyo kwamba, khofu yao ni kuwa watu watamshirikisha Mwenyezi Mungu, kwa kiwango fulani tatizo lao ni la kisiasa limewekwa ili kuwapinga Waislamu na kuwaua ili kuimarisha ufalme wao na utawala wao dhidi ya Waislamu, na historia ni shahidi mkubwa kwa mambo waliyowatendea ummati Muhammad (s.a.w.).

Na nilimuuliza kuhusu Tarika za masufi, akanijibu kwa ufupi kwamba, “Ndani ya Tariqa hizo kuna mambo ambayo ni mema na mengine si mema.  Ama yaliyomema ni kuilea na kuizowesha nafsi taabu ya maisha na kujitenga na mambo ya starehe za dunia yenye kupita na kuipandisha kwenye daraja za ulimwengu wa kiroho. Amma yasiyokuwa mema ni kujitenga na kuacha hali halisi ya maisha na kuifanya dhikiri ya Mwenyezi Mungu iishiye kwenye idadi ya matamshi n.k.”

Na inastahiki kusema kwamba, Uislamu na mafunzo yake yote ni mema.

# MASHAKA NA MKANGANYIKO

Majibu ya Sayyid Muhammad Baqir As-Sadr yalikuwa na ufafanuzi na yenye kutosheleza, lakini itawezekanaje kupenya haraka ndani ya nafsi ya mtu kama mimi ambaye katika umri wake wa miaka ishirini na tano ameishi juu ya msingi wa kuwatukuza masahaba na kuwaheshimu na hasa wale *Khulafaur-Rashiduna* ambao mjumbe wa Mwenyezi Mungu ametuamuru tushikamane n a sunna yao na kufuata uongozi wao wakitunguliwa na Sayyidna Abubakr As-Sidiq, kisha Sayidna Umar Al-Faruq. Mimi sikuwahi kusikia watu hawa wakitajwa toka nilipofika Iraq bali nimekuwa nikiyasikia yakitajwa majina mengine mapya nisiyoyajua kabisa, na nimekuwa nikisikia Maimamu kumi na wawili kwa idadi na pia madai kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kabla hajafariki alitamka kuwa, Imam Ali awe Khalifa wake basi ni vipi nitayaamini mambo hayo?

Hivi kweli Waislamu tena masahaba watukufu ambao ni viumbe bora baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wanaweza kukubaliana dhidi ya Imam Ali *Karramallah Waj-hahu?* Masheikh wetu wametufundisha tangu utotoni kwamba Masahaba walikuwa wakimuheshimu Imam Ali na wakiitambua haki yake, kwani yeye ndiye mume wa Fatmah Az-Zahra naye ndiye mzazi wa Hasan na Husein na ndiye mlango wa mji wa Elimu.

Hali ni ile ile kwa upande wa pili, kwani Sayyidna Ali anaitambua haki ya Abubakr As-Sidiq ambaye alisilimu kabla ya watu wote, naye ndiye mwenza wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika pango. Mwenyezi Mungu Mtukufu amemtaja ndani ya Qur'an, na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimtawalisha Uimamu katika sala wakati alipokuwa mgonjwa na isitoshe Mtume (s.a.w.) alisema, "Lau ningelikuwa mwenye kumfanya mtu fulani kuwa mwandani wangu, basi ningemfanya Abubakr awe mwandani wangu."

Juu ya yote hayo Waislamu walimchagua (Abubakr) awe khalifa wao na vivyo hivyo, Imam Ali anaitambua haki ya Sayyidna Omar ambaye

Mwenyezi Mungu aliutukuza Uislamu kupitia kwake. Pia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akamwita kuwa ni "Farouq" ambaye anatenganisha baina ya haki na batili, na ni kama ambavyo anaitambua pia haki ya Sayyidna Uthman ibn Affan ambaye Malaika wa Mwenyezi Mungu walimstahi na ni yeye aliyeliandaa jeshi la Usrah, na ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliyempa jina la *Dhun-Nurain.*

Ni kwa nini basi ndugu zetu Mashia hawayajui yote haya au wanajifanya hawayajui na kisha wanawafanya watukufu hawa kuwa ni watu wa kawaida ambao wanaoweza kupotoshwa na tamaa za kidunia na wakaacha kufuata haki, kisha wakaiasi amri ya Mtume baada ya kufariki kwake wakati hawa ndiyo ambao walikuwa wakishindana kutekeleza amri zake? Wakiwaua watoto wao na baba zao na jamaa zao katika njia ya kuutukuza Uislamu na kuutetea. Kwa hiyo mtu anayemuuwa baba yake na mwanawe kwa ajili ya kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawezi kabisa kudanganywa na tamaa za kidunia kwa lengo la kupata madaraka ya ukhalifa na kisha wapuuze na kuipa mgongo amri ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

Naam, kwa ajili ya yote hayo sikuyaamini maneno yote wayasemayo Mashia, licha ya kwamba nilikuwa nimekubaliana nao katika mambo mengi na nilibakia katika mkanganyiko na mashaka ambayo Wanachuoni wa Kishia waliyaingiza ndani ya akili yangu. Hapana shaka maneno yao yanaingia akilini na ni yenye mantiki inayokubalika. Kutokana na kukanganyikiwa kulikonipata, sikuamini kabisa kwamba Masahaba (r.a.) wamewekwa katika daraja hii na wakawa ni watu wa kawaida tu kama sisi ambao Nuru ya Utume haikuwakosha na wala uongofu wa Muhammad haukuwabadilisha tabia. Ewe Mola wangu itakuwaje hali hii, hivi kweli inawezekana Masahaba wakawa katika hali hii waisemayo Mashia?

Jambo la muhimu ni kwamba mashaka haya na mkanganyiko huu ndicho chanzo cha unyonge na ndiyo mwanzo wa kuthibitisha kwamba kuna mambo ambayo yamefichwa na hapana budi kuyachunguza ili kuweza kuufikia ukweli.

Rafiki yangu Mun-im alikuja na tukasafiri hadi Kar-bala. Huko niliishi katika mazingira ya tukio la masaibu ya Sayyidna Husein kama wanavyoishi Mashia wake. Mahala hapo ndipo nilipotambua kwamba Sayyidna Husein

hajafa bado, kwani watu wanasongamana na kuzunguka kwenye kaburi lake kama vipepeo huku wakilia kwa huzuni na majonzi. Sijapata kuona mfano wake na ni kama kwamba Hussein ameuawa sasa hivi. Niliwasikia Wahadhiri wanaziamsha hisia za watu kwa kusimulia tukio la Karbala kwa kulia na kuomboleza, kiasi kwamba msikilizaji hawezi kuizuia nafsi yake ila atalia.Basi kwa hakika nililia, nikalia nikaiacha huru nafsi yangu kama kwamba ilikuwa imefungwa, na nilihisi raha kubwa katika nafsi ambayo sikuifahamu kabla ya siku hiyo. Pia nilijiona kama kwamba nilikuwa kwenye safu ya maadui wa Husein na ghafla nimegeuka na kuwa upande wa wafuasi wake na Masahaba wake ambao wanajitolea roho zao. Kuna mzungumzaji mmoja alikuwa akieleza kisa cha Bwana Hurru ambaye ni mmoja wa viongozi waliopewa jukumu la kumpiga vita Husein, lakini alisimama katika uwanja wa vita akitetemeka kama kuti, na baadhi ya wenziwe walipomuuliza kuwa, “Je wewe unaogopa kufa?”

Hurru alijibu, “Wallahi hapana, lakini ninaihiyarisha nafsi yangu baina ya pepo na moto.” Kisha hapo hapo akampiga farasi wake akaenda kwa Husein akamwambia: “Ewe Mwana wa Mtume wa Mwenyezi Mungu naweza kutubia?” Basi baada ya kusikia hayo sikuweza kujizuwia bali nilianguka chini hali ya kuwa ninalia kama kwamba ninachukuwa nafasi ya tendo la Hurru na ninamuomba Husein kwa kusema, “Ewe Mwana wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu naweza kutubia? Nisamehe Ewe mtoto wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.” Sauti ya mzungumzaji yule ilikuwa inaathiri, hivyo basi sauti za watu zilipaa kwa kulia sana na wakati huo rafiki yangu alisikia kilio changu akanikumbatia hali ya kuwa analia na kunipakata kifuani kama mama anavyompakata mwanawe huku akirudia rudia kusema “Ewe Husein! Ewe Husein!”

Kipindi hicho kilikuwa ni wakati na muda niliokifahamu kilio cha kweli na nikahisi machozi yangu kuwa yameukosha moyo wangu na mwili wote toka ndani na hapo pia ndipo nilipoifahamu hadithi ya Mtume isemayo, “Lau mungelifahamu mambo niyajuwayo mimi, basi mungecheka kidogo na mungelia sana.” Kutwa nzima ya siku hiyo nilikuwa mwenye huzuni, na rafiki yangu alijaribu kuniliwaza na kunipa baadhi ya viburudisho, lakini nilikuwa sina hamu navyo kabisa. Nilichokifanya ilikuwa ni kumuomba anieleze tena kisa cha mauaji ya Sayyidna Husein, kwani sikupata kukisikia japo kidogo zaidi ya kuwa masheikh wetu wanapotusimulia

kisa hicho husema kwamba wanafiki na maadui wa Uislamu waliomuuwa Sayyidna Omar na Sayyidna Uthuman na Sayyidna Ali ndiyo waliomuua Sayyidna Husein, na hakuna tukijuacho isipokuwa muhtasari huu tu, bali tulikuwa tunasherehekea siku ya Ashura kwa kufahamu kwamba ni moja ya sikukuu za Kiislamu. Na katika Sikukuu hiyo hutolewa Zaka za mali na kupikwa vyakula vinono vya aina mbali mbali pia watoto nao hupita wakiwaomba pesa watu wazima ili waweze kununua *Hal-wa* na vifaa vya kuchezea.

Naam katika baadhi ya miji kuna aina ya desturi ambazo miongoni mwazo ni wakazi wa maeneo hayo huwasha moto na siku hiyo hawafanyi kazi wala hawaowi na wala hawasherehekei. Lakini desturi hizo tunaziita kuwa ni desturi ambazo hazina maelezo wala tafsiri yake, na wanachuoni wetu husimulia hadithi mbali mbali zinazoelezea ubora wa siku ya Ashura na baraka zilizomo na rehma nyingi za ajabu!

Baada ya kuzuru kaburi ya Imam Husein (a.s.) tulizuru kaburi ya Abbas ambaye ni ndugu wa Husein, nami nilikuwa simfahamu Abbas kuwa ni nani. Rafiki yangu alinisimulia kisa cha ushujaa na uhodari wa Abbas. Hapo pia tulikutana na Wanachuoni wengi ambao siwakumbuki majina yao kikamilifu, isipokuwa baadhi ya Laqabu zao kama vile, Bah-rul-ulum na Sayyid Al-hakim, Kashiful-ghitaa na Āli-Yasin, Tabatabai, Fairuz Abaad, Asad Haidar na wengineo ambao nilibahatika kuonana nao.

Ukweli na usemwe, "Kwa hakika ni Wanachuoni wachamungu ambao wamefunikwa na haiba na heshima. Mashia wanawaheshimu sana na huwa wanatoa *Khums* ya mali zao kwa Wanachuoni hao ambao huzitumia *Khums* hizo kuendeshea Vyuo vya elimu na kuasisi Madrasah na viwanda vya uchapishaji. Vile vile huzitumia kuwapa wanafunzi wanaokuja hapo kusoma kutoka nchi mbali mbali za Kiislamu. Wanachuoni hao wanajitegemea wenyewe wala hawana uhusiano na watawala wa Serikali kwa namna yoyote ile, kinyume na walivyo wanachuoni wetu ambao hawatoi Fatwa wala kusema kitu isipokuwa kwa mujibu wa maoni ya watawala wanaodhamini maisha yao na kumstaafisha wamtakaye na kumpa cheo wamtakaye.

Kusema kweli ni ulimwengu mpya niliouvumbua au alionionesha

Mwenyezi Mungu na nimeliwazika nao baada ya kuwa nilikuwa nikiuchukia na niko pamoja nao baada ya kuwa nilikuwa naupinga. Kwa hakika ulimwengu huu umenipatia fikra mpya na umenipa hali ya kupenda kuchunguza, kutafiti na kusoma mpaka niupate ukweli unaohitajika, ukweli ambao siku zote umekuwa ukinipitia akilini nilipoisoma hadithi tukufu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu aliposema, "Wana wa Israil walifarakana wakawa makundi sabini na moja, na Wakristo wamefarakana mpaka wakafikia makundi sabini na mbili, na Umati wangu watafarakana na kuwa makundi sabini na tatu na yote yataingia motoni isipokuwa kundi moja."

Hatuna la kusema juu ya dini yingine nyingi ambazo kila moja inadai kuwa ndiyo ya kweli na nyingine si za kweli, lakini nashangaa na kustajaabu na kuchanganyikiwa ninapoisoma hadithi hii, na huku kustaajabu kwangu na kushangaa kwangu na kuchanganyikiwa si kwa sababu ya hadithi yenyewe, lakini (ninaowashangaa na kuwastaajabu na kunichanganya mawazo) ni Waislamu wenyewe ambao huisoma hadithi hii na kuirudia rudia katika hotuba zao na kuiacha bila kuchanganua wala kutafiti maana yake ili walibainishe lile kundi lenye kuokoka kutokana na makundi yaliyopotoka.

Cha ajabu ni kuwa kila kundi linadai kuwa wenyewe ndiyo pekee wenye kuokoka wakati ambapo mwisho wa hadithi imekuja kama ifuatavyo: "(Masahaba) wakasema ni kina nani hao watakaookoka ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?" Mtume akasema, "Ni wale ambao watakuwa kama nilivyo mimi na Sahaba wangu." Hapana kundi ila (linadai kuwa) limeshikamana na Kitabu na Sunna, na hakuna kundi la Kiislamu ambalo linadai kinyume na hivyo. Kwa hiyo lau Imamu Malik ataulizwa au Abu Hanifa au Imamu Shafii au Ahmad ibn Hanbal, kila mmoja wao atadai kwamba yeye anashikamana na Qur'an na Sunna sahihi.

Madh-hebu haya ya Kisunni na tukiongeza na kundi la Mashia ambao nilikuwa nikiamini kuwa ni waovu na wamepotoka, nao ni kundi jingine linalodai pia kwamba limeshikamana na Qur-an na Sunnah sahihi iliyonakiliwa toka kwa Watu wa nyumba ya Mtume waliotakasikia, na wenye nyumba ndio wanaofahamu kilichomo ndani mwao kama wasemavyo (Mashia).

Basi je inawezekana wote hawa wawe kwenye haki kama wanavyodai? Jambo hili haliwezekani kwani hadithi tukufu inamaanisha kinyume cha hivyo isipokuwa kama hadithi hiyo itakuwa ni ya uongo, na hili haliwezekani kwa sababu hadithi yenyewe ni mutawatiri kwa Masunni na Mashia. Au basi hadithi hii iwe haina maana yoyote na haijulishi lolote? Na haiwezekani kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kusema kitu kisichokuwa na maana na hakijulishi chochote, kwani Mtume hasemi kwa matamanio ya nafsi yake na hadithi zake zote zimejaa hekima na mazingatio.

Kilichobakia kwetu ni kukiri lipo kundi moja lililoko kwenye haki, na yaliyobakia ni upotofu. Basi hadithi hii inaniletea mkanganyiko kama ambavyo inavyoniletea (hali ya kumfanya mtu) atafiti na kufuatilia kwa yule atakaye kuiokoa nafsi yake.

Kwa ajili hii basi, iliniingia shaka na utata baada ya mimi kukutana na Mashia, kwani ni nani ajuaye, huenda wao wako kwenye haki na wanasema kweli! Na ni kwa nini nisifanye utafiti na kufuatilia?

Nao Uislamu umenilazimisha kupitia Qur-an yake na Sunna yake nifanye utafiti, nilinganishe na nizingatie. Mwenyezi Mungu anasema, *"Na wale wanaojitahidi kwa ajili yetu tutawaongoza kwenye njia zetu" 29:69 Na amesema tena kwamba, "Wale ambao husikiliza kauli (zisemwazo) wakafuata zile zilizo njema hao ndiyo aliowaongoa Mwenyezi Mungu na hao ndiyo wenye akili "39:18* Na bila shaka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amesema, "Fanya utafiti kuhusu dini yako mpaka isemwe kuwa wewe ni maj-nuni"

Kwa hiyo kufanya utafiti na kulinganisha ni wajibu wa kisheria juu ya kila *mukallaf*. Kwa ajili ya uthibitisho huu na kutokana na azma ya kweli niliahidi mwenyewe nafsi yangu kufanya utafiti na kulinganisha, na niliwaahidi hivyo marafiki zangu Mashia huko Iraq wakati nilipokuwa nawaaga kwa kuwakumbatia tena mwenye huzuni kwa kutengana nao. Kusema kweli niliwapenda na wao walinipenda, niliwaacha wapendwa hao Watukufu wenye moyo safi waliojitolea wakati wao kwa ajili yangu si kwa ajili nyingine kama walivyosema siyo kwa khofu fulani wala tamaa fulani, bali kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Imekuja *(riwaya)* katika hadithi tukufu kwamba, "Mwenyezi Mungu akimuongoa

mtu mmoja kupitia kwako ni bora kwako kuliko kila kitu kinachoangaziwa na jua.”

Niliondoka Iraq baada ya kukaa huko siku ishirini nikiwa ndani ya mazingira ya Maimamu na Mashia wao, siku hizo zilipita mfano wa ndoto tamu ambayo aliyelala hutamani asiamke mpaka aikamilishe.

Niliondoka Iraq nikiwa ni mwenye huzuni kutokana na uchache wa muda, nilihuzunika kwa kutengana na nyoyo nilizozipenda ambazo zinasafika kwa kuwapenda Ahlul-bait. Nilielekea Hijaz hali ya kuwa naikusudia Nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu na Kaburi la Bwana wetu Mtukufu wa daraja kwa wale wa mwanzo na wa mwisho. Sala na salamu za Mwenyezi Mungu zimshukie yeye na Āli zake wema walotakasika.

# SAFARI YA KWENDA HIJAZ

Niliwasili Jeddah na nikakutana na rafiki yangu Bashir ambaye alifurahi kwa kufika kwangu, akanikaribisha nyumbani kwake, akanikirimu kwa takrima kubwa na alikuwa akitumia wakati wa mapumziko yake katika matembezi pamoja nami kwa gari lake.

Tulikwenda sote Umra na tukakaa huko siku kadhaa katika ibada na Uchamungu, na nilimuomba radhi kwa kuchelewa kwangu kwani nilikuwa Iraq. Nilimsimulia juu ya uvumbuzi wangu mpya au ushindi mpya naye alikuwa ni mtu aliyefungukiwa, pia ni mtambuzi akasema: "Bila shaka mimi nasikia kwamba miongoni mwao wamo Wanachuoni wakubwa na wana mambo wayasemayo, lakini wanavyo vikundi vingi vyenye kufru vilivyopotoka vinavyotusababishia matatizo mengi wakati wa msimu wa Hijja."

Nilimuuliza; "Ni yepi matatizo ambayo wanayasababisha?" Alijibu: "Wao wanasali kwenye makaburi, huingia Baqii kwa wingi na wanalia na kuomboleza, na mifukoni mwao huchukua vipande vya mawe na kuvisujudia, na wanapokwenda kwenye kaburi la Sayidna Hamzah lililoko Uhud, basi huko huweka jeneza na kujipiga na kulia kama kwamba Hamza amekufa katika muda huo na kwa ajili hiyo basi serikali imezuwiya kuingia sehemu zenye makaburi."

Nilitabasamu na nikasema; "Kwa sababu hii unawahukumu kwamba wamekwenda kinyume cha Uislamu?"

Akasema: "Na mengineyo, kwani wao huja kumzuru Mtume lakini wakati huo huo husimama kwenye kaburi la Abubakar na Umar na kuwatukana na kuwalaani, na miongoni mwao wako ambao hutupia uchafu na najisi kwenye kaburi la Abubakar na Umar."

Kauli hii ilinikumbusha kisa nilichokisikia toka kwa mzazi wangu

baada tu ya yeye kurejea kutoka Hija, lakini yeye alisema kwamba wao hutupia uchafu kwenye kaburi la Mtume. Hapana shaka mzazi wangu hakulishuhudia jambo hilo kwa macho yake kwani yeye alisema: "Tuliwaona askari wa jeshi la Saudia wakiwapiga baadhi ya Mahujaji kwa fimbo, na tulipowakemea kwa tendo hilo la kuwadhalilisha Mahujaji wa nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu, walitujibu kuwa hawa siyo Waislamu wao ni Mashia wamekuja na uchafu ili wautupie kwenye kaburi la Mtume". Mzazi wangu aliongezea kwa kusema, "Hapo tuliwalaani na kuwatemea mate hao Mashia."

Na sasa na mimi nayasikia toka kwa rafiki yangu ambaye ni Msaudia mzaliwa wa mjini Madina kwamba wao huja kuzuru kaburi la Mtume lakini hutupia najisi juu ya kaburi la Abubakr na Umar. Nilizitilia mashaka riwaya zote mbili kwani mimi nimehiji na nimeona kwamba chumba kitukufu ambacho ndani yake limo kaburi la Mtume, Abubakr na Umar kimefungwa na haiwezekani kwa mtu yeyote kukisogelea ili kugusa mlango wake au dirisha licha ya kutupia vitu ndani yake.

Kwanza hakuna upenyo, na pili wapo walinzi imara miongoni mwa askari washupavu ambao hupokezana kulinda na kuchunga mbele ya kila mlango, na mikononi mwao wanafimbo ambazo humpiga kila anayesogelea na au kujaribu kuchungulia ndani ya chumba. Ninadhani kwamba, miongoni mwa baadhi ya askari hao wako wanao wakufurisha Mashia na ndiyo waliowatupia tuhuma hii ili kuhalalisha tendo lao la kuwapiga ili kuwachochea Waislamu nao wawapige, na au kwa uchache wanyamaze dhidi ya kuwanyanyasa (Mahujaji) hao na waeneze uvumi warudipo katika nchi zao kwamba Mashia wanambughudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu na wanatupia najisi kwenye kaburi lake na kwa njia hiyo wanapiga ndege wawili kwa jiwe moja.

Na hali hii inafanana na ile aliyoisimulia mheshimiwa mmoja miongoni mwa watu ninaowaamini alisema kwamba, "Tulikuwa tunatufu Al-Kaaba, basi mara kijana mmoja alishikwa na maumivu makali ya tumbo kutokana na msongamano akatapika, askari waliokuwa wakilinda Hajarul-As-wad walimpiga na wakamtoa akiwa katika hali ya kuhuzunisha wakamtuhumu kwamba alikuja na najisi ili kuichafua Al-Kaaba na wakatoa ushahidi dhidi yake akauawa siku ile ile."

Maelezo haya yakawa yanazunguka kichwani mwangu na nilibakia naifikiria kwa kitambo hoja ya yule rafiki yangu Msaudia inayowakufurisha Mashia hawa. Kwa kweli mimi sikusikia lolote isipokuwa wanalia, kujipiga vifua, wanasujudu juu ya jiwe, wanaswali kwenye makaburi, na ndipo nikajiuliza je katika matendo haya liko la kumkufurisha mtu anayeshuhudia kwamba hapana Mola apasiwaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad ni Mja wake na ni Mjumbe wake? Isitoshe anasali sala (tano), anatoa zaka, anafunga Ramadhani, anahiji Makka na anaamrisha mema na kukataza maovu.

Sikutaka kumpinga rafiki yangu na kuingia naye katika majadiliano ambayo hayana faida, basi nikatosheka kwa kusema "Mwenyezi Mungu atuongoe kwenye njia yake iliyonyooka sisi na wao na awalaani maadui wa dini ambao wanaufanyia vitimbi Uislamu na Waislamu."

Nilikuwa kila ninapoitufu nyumba kongwe *(Al-Kaaba)* katika Umra na kila wakati wa kuzuru Makka tukufu, na inapotokezea kukawa hakuna watu wengi wanaotufu miongoni mwa wenye kufanya Umra, niliswali na kumuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu kutoka katika kila kiungo changu anifungulie moyo wangu na aniongoze kwenye ukweli.

Nilisimama kwenye Maqam Ibrahim (a.s.) na nikasoma aya tukufu ya Qur'an isemayo *"Na ipiganieni dini ya Mwenyezi Mungu kama inavyostahiki, yeye ndiye aliyekuumbeni wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika dini, nayo ni mila ya baba yenu Ibrahim yeye ndiye aliyekuiteni kuwa ni Waislamu tangu mwanzo na katika hili Mtume awe shahidi juu yenu na ninyi muwe mashahidi juu ya watu (waliotangulia), basi salini sala na toeni zaka na shikamaneni pamoja kwa ajili ya Mwenyezi Mungu yeye ndiye Mola wenu Mola mwema mno na ni msaidizi mwema mno" (22:78).*

Kisha nikaanza kumsemesha bwana wetu Ibrahim au baba yetu Ibrahim kama ilivyomuita Qur'an nikasema, "Ewe Baba yangu! ewe uliyetuita Waislamu angalia! Watoto wako wamekhitilafiana baada yako, wamekuwa Mayahudi, Wakristo, na Waislamu. Ama Wayahudi wamekhitilafiana baina yao wakawa makundi sabini na moja nao Wakristo wamekhitilafiana makundi sabini na mbili, Waislamu nao wamekhitilafiana makundi sabini na tatu, na

yote yako katika upotofu kama alivyoeleza mwanao Muhammad (s.a.w.), na kwamba kundi moja limebakia kwenye ahadi yako ewe Baba yangu!!"

(Niliendelea kusema), "Je, huo ndio utaratibu wa Mwenyezi Mungu kwa waja wake kama wasemavyo Qadariyyah, kwamba:- Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye yeye alieiandikia kila nafsi iwe Yahudi au Mkristo au Muislamu au Mlahidi au Mshirikina au kuipenda dunia na kujitenga na mafundisho ya Mwenyezi Mungu? Yote hayo ni kwa sababu wamemsahau Mwenyezi Mungu basi naye akawasahaulisha nafsi zao. Kwa hakika akili yangu hainikubalii kusadiki kwamba Qadhaa na Qadar ndiyo iliyoamua hatima ya mtu, bali karibu nikate shauri kwamba Mwenyezi Mungu ndiye aliyetuumba na akatuongoza na akatufahamisha mabaya na mema, na akawatuma kwetu Mitume wake ili watubainishie yanayotutatiza na watujulishe haki kutokana na batili lakini mtu mwenyewe ndiye ambaye amezugwa na maisha ya dunia na mapambo yake.

Mtu kwa ubinafsi na ujeuri wake, kwa ujinga wake na kujitosa kwake katika mambo yasiyo na faida, na kwa inadi yake na uhasama wake na kwa dhulma yake na kuvuka kwake mipaka ameiacha haki na amemfuata shetani na akajitenga na Mwenyezi Mungu, amepotea njia na kula kisicholiwa. Bila ya shaka Qur'an tukufu imekwishalieleza hilo vyema na kulieleza kwa mukhtasari kama ifuatavyo: *"Kwa hakika Mwenyezi Mungu hawadhulumu watu kitu chochote lakini watu wanajidhulumu wenyewe." (10:44).* Ewe baba yetu Ibrahim hawana lawama Mayahudi ambao waliipinga haki kwa kufanya dhulma baina yao pindi ukweli ulipowafikia, basi umma huu aliouokoa Mwenyezi Mungu kupitia kwa mwanao Muhammad, na akautoa kwenye giza na kuupeleka kwenye nuru na kuufanya kuwa ni Umma bora uliotolewa kwa watu, Umma huu nao vile vile umehitilafiana na kufarakana na kukufurishana wao kwa wao na hali ya kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliwatahadharisha na kuwatanabahisha juu ya hilo na akawasisitiza mno mpaka akasema "Siyo halali kwa Muislamu kumnunia nduguye Muislamu zaidi ya siku tatu." Umma huu umegawanyika na kufarakana na umekuwa vijidola vidogo vidogo vinavyofanyiana uadui vyenyewe kwa vyenyewe na kupigana wao kwa wao na huyu hamjui yule na kumnunia maisha yake yote.

Umma huu una nini Ewe baba yetu Ibrahim, baada ya kuwa ulikuwa ni umma bora kuliko nyumati zingine na ulitawala dunia yote na ukawafikishia

watu uongofu, elimu, maarifa na maendeleo, leo hii ghafla umekuwa ni umma mdogo na dhaifu mno, ardhi yao imeporwa na wananchi wake wametawanyika, Msikiti wao Mtakatifu umekaliwa na kupokonywa na Wazayoni na wala hawawezi kuukomboa. Utakapozitembelea nchi zao hakuna utakachokiona isipokuwa umasikini uliopea, njaa inayoua, ardhi kame, maradhi mabaya, na tabia mbaya. Zaidi ya hayo wako nyuma kifikra na kiteknolojia, dhulma na ukandamizaji umejaa na kuna uchafu na wadudu.

Itakutosheleza tu (hali hii) iwapo utalinganisha vyoo vya umma viko namna gani huko Ulaya na kwetu sisi vikoje. Msafiri anapoingia kwenye vyoo vyote vya Ulaya atavikuta ni visafi vinanga'ara kama kioo na ndani yake muna harufu nzuri, wakati ambapo katika nchi za Kiislamu msafiri hawezi kuingia katika vyoo kutokana na mvundo wake na najisi na kunuka kwake, nasisi ndiyo ambao Uislamu umetufundisha kwamba "Hakika Usafi ni sehemu ya Imani na uchafu unatokana na shetani". Hivi je imani imehamia Ulaya na shetani anaishi kwetu? Kwa nini Waislamu wamekuwa wanahofu kudhihirisha itikadi yao hata katika miji yao? Ni kwa nini Muislamu hawi hata mwenye maamuzi ya mwili wake kiasi kwamba hawezi hata kufuga ndevu wala kuvaa mavazi ya Kiislamu, wakati ambapo watu waovu wanajidhihirisha kwa kunywa pombe na zinaa na kuvunja heshima za watu na Muislamu hawezi tena kuwazuia bali hata kuwaamrisha mema na kuwakataza mabaya. Kuna habari zilizonifikia kwamba katika baadhi ya nchi za Kiislamu kama vile Misri na Morocco, wapo wazazi ambao huwatuma mabinti zao wakafanye umalaya kutokana na umasikini uliokithiri na shida nying,i Lahaula wala Quwata Illa Bilahil-aliyyil-adhim. Ewe Mola wangu kwa nini umekuwa mbali na umma huu? Umeuacha (umma huu) unahangaika katika giza hapana! hapana! Nakuomba unisamehe Ewe Mola wangu na ninatubia kwako. Bali umma huu wenyewe umekaa mbali na utajo wako na umechagua njia ya shetani, nawe Ewe Mola ambaye hekima yako na Qudra yako vimetukuka umesema na kauli yako ni ya kweli. "Yeyote anayeacha utajo wa (Mola) Mwingi wa rehma tunamuwekea shetani kuwa ndiye rafiki yake". (43:36)

Vile vile umesema *"Na hakuwa Muhammad ila ni Mtume, wamepita kabla yake Mitume wengi, basi endapo akifa au akiuawa mtageuka mrudi nyuma? Na atakayegeuka akarudi nyuma, huyo hatamdhuru kitu Mwenyezi*

*Mungu, na Mwenyezi Mungu atawalipa wanaomshukuru."  (3:144)*

Hapana shaka hali waliyoifikia Umma wa Kiislamu katika kuporomoka, kubakia nyuma, unyonge na umasikini ni dalili isiyo na shaka kwamba wako mbali mno na njia iliyoonyooka. Na hapana shaka kwamba watu wachache au kundi la watu wachache miongoni mwa sabini na tatu haliathiri chochote katika mwendo mzima wa maisha ya Umma kwa jumla.

Bila shaka mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) alikwisha sema *"Amrisheni mema na mkataze maovu vinginevyo Mwenyezi Mungu atawapa uwezo watu waovu (wawe) juu yenu, wema wenu watakapoomba hawatajibiwa." Ewe Mola wetu tumeyaamini uliyoyateremsha na tumemfuata Mtume, basi utuandike pamoja na mashahidi. Ewe Mola wetu, usizipotoshe nyoyo zetu baada ya kutuongoa na utupe rehma kutoka kwako, hakika wewe ni mpaji. Ewe Mola wetu, sisi tumejidhulumu wenyewe na iwapo hutatusamehe na kutuhurumia, basi tutakuwa miongoni mwa watu wenye kupata hasara.*

Hatimaye nilisafiri kuelekea Madina nikiwa na barua kutoka kwa rafiki yangu Bashiri kwenda kwa mmoja wa ndugu zake ili nikafikie kwake kwa muda nitakaobakia huko, na kabla ya hapo alikwishazungumza naye kwa simu. Huyu bwana alinipokea na kunikaribisha  nyumbani kwake, baada ya kufika nilikwenda kumzuru Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hivyo basi nilikoga na kujitia manukato, nikavaa nguo zangu nzuri zilizo safi. Kulikuwa na watu wachache wanaouzuru hapo ukilinganisha na msimu wa Hijja, hivyo niliweza kusimama mbele ya kaburi la Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na lile la Abubakr na Omar jambo ambalo sikuweza kulifanya wakati wa msimu wa Hijja kutokana na msongamano. Pia nilijaribu kuugusa mlango mmoja wapo kwa ajili ya kutabaruku basi askari aliyekuwa kasimama hapo alinikemea, na kila mlango ulikuwa na askari analinda.

Niliposimama kwa muda mrefu hali ya kuwa ninaomba na kuzifikisha salamu walizonipa rafiki zangu, askari waliniamuru niondoke nami nilijaribu kuzungumza na mmoja wao lakini sikufaulu.

Nilirejea kwenye Uwanja mtukufu, nikaketi na kusoma Qur'an tena kwa vizuri nikarudia mara kadhaa, na ikawa nawaza kama kwamba Mjumbe

wa Mwenyezi Mungu ananisikiliza na nikajiambia moyoni mwangu, je yawezekana kuwa Mtume amekufa kama watu wengine? Basi kwa nini katika sala zetu tunasema, "Salamu zikushukie ewe Mtume na rehma za Mwenyezi Mungu na baraka zake?" Matamko ambayo yanayo ibara ya mwenye kusemeshwa? Na iwapo Waislamu wanaitakidi kuwa Sayyidna Khidhr (a.s.) hakufa na humrejeshea salamu kila anayemsalimia bali masheikh wa Tariqa za kisufi wanaamini kabisa kuwa Sheikh wao Ahmad Tijani au Abdul-Qadir Jailani huwajia wazi wazi wakiwa macho na wala siyo usingizini basi ni kwanini tunamnyima Mjumbe wa Mwenyezi Mungu utukufu kama huu wakati yeye ndiye mbora wa viumbe wote? Nafsi yangu ilijipunguzia uzito wa wazo hili na kusema: "Waislamu hawazuii uwezekano huo isipokuwa Mawahabi ambao nilikwishaanza kuwachukia kwa sababu ya jambo hili na sababu nyinginezo. Miongoni mwa sababu hizo ni ukatili walionao ambao nimeuona, na ukali dhidi ya Waumini wanaokwenda kinyume na itikadi zao.

Nilitembelea uwanja wa makaburi ya *Baqii*, na nilikuwa nimesimama huku nikiziombea roho za watu wa nyumba ya Mtume (s.a.w.). Karibu yangu alikuweko Mzee mmoja mwenye umri mkubwa sana analia nami nilitambua kuwa ni Shia kwa mujibu wa kilio chake. Mzee huyu alielekea Qibla na akaanza kuswali, mara ghafla askari alimjia kwa haraka kama kwamba alikuwa akimfuatilia nyendo zake akampiga teke hali ya kuwa yuko katika sijida akaanguka chali. Masikini Mzee huyu alizimia kwa dakika chache na yule askari akaanza kumpiga, kumtukana na kumshutumu.

Nilimhurumia Mzee yule na nikadhani kuwa amekufa, hasira zikanipanda. Basi huruma zangu zilinilazimisha niseme kumwambia yule askari, "Ni haramu kwa nini unampiga huku anasali?" Lakini alinikemea huku akisema "Nyamaza wala usiingilie nisije nikakufanya kama nilivyomfanya." Nilipoona macho yake kuwa yana sura ya uovu nilijiepusha naye hali ya kuwa nimeikasirikia nafsi yangu ambayo ilishindwa kumsaidia mtu aliyedhulumiwa, na pia nimewakasirikia Wasaudia ambao wanawatendea watu mambo wayatakayo wao bila ya kuwepo mtu wa kuwazuwia, kuwadhibiti wala kuwakemea.

Baadhi ya Mahujaji waliokuwepo hapo wengine walisema, *"Lahaula wala Quwata illa Billahi"* na wengine walisema "Anastahiki kufanyiwa

hivyo kwa sababu anaswali makaburini jambo ambalo ni haramu." Basi mimi sikuweza kuvumilia na nikamkemea huyu aliyesema hivi na kumwambia, "Nani alikwambia kuwa kusali makaburini ni haramu?" Alijibu akasema, "Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kakataza jambo hilo."

Nilisema bila kujali, "Mnamzulia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu." Lakini nikaogopa wasije wakanifanyia njama watu hawa wakamwita askari na akanipiga, basi nikasema kwa upole, "Ikiwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) amekataza jambo hilo, ni kwa nini mamilioni ya Mahujaji na wanaozuru wanakhalifu katazo lake na wanafanya haramu kwa kusali karibu na kaburi la Mtume, Abubakr na Umar ndani ya Msikiti Mtukufu wa Mtume na (kuna makaburi) ndani ya misikiti mingi ya Waislamu katika ulimwengu wa Kiislamu. Hebu tujaalie kuwa ni haramu kuswali karibu ya makaburi, basi ndiyo tutatatua tatizo hilo kwa ukali na ukatili namna hii? Au tutatatua kwa upole na huruma? Hebu nipeni nafasi nikusimulieni kisa cha yule Bedui aliyekojoa ndani ya Msikiti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, mbele yake na mbele ya Masahaba wake bila haya wala aibu, na baadhi ya Masahaba waliposimama hali ya kuwa wamezinyoosha panga zao wamuuwe, Mtume wa Mwenyezi Mungu aliwazuwia na akasema, "Mwacheni musimkatize bali mwagieni maji juu ya mkojo wake, kwa hakika mumetumwa ili murahisishe mambo na siyo mlete uzito, mubashirie wala msiwafukuze watu". Hapana walichokifanya Masahaba hao ila kutii amri yake na ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu alipomuita yule Bedui akamkalisha karibu yake, akaongea naye kwa upole na heshima na akamfahamisha kuwa mahali pale ni nyumba ya Mwenyezi Mungu haifai kuinajisisha. Yule bedui alisilimu baada ya hapo akawa anakuja Msikitini katika hali ya mavazi mazuri na safi mno. Mwenyezi Mungu amesema kweli pale alipomwambia Mtume wake, *"Lau ungekuwa mkali mwenye moyo mgumu wote wangelikukimbia." (3:159)*

Baadhi ya watu waliathirika walipokisikia kisa hiki, mmoja wao akaniita faragha pembeni akaniuliza, "Wewe unatoka wapi"? Nikamwambia: "Tunisia." Akanisalimia na kuniambia, "Ndugu yangu nakunasihi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ulinde ulimi wako wala usiseme namna hivi mahala hapa kabisa nakunasihi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu." Nilizidi kukasirika na kuwachukia watu hawa ambao wanadai kuwa wao ni walinzi wa Haram mbili takatifu kisha wanawatendea ubaya kiasi hiki

wageni wa Mwenyezi Mungu na wala hawezi mtu yeyote kutoa rai yake au kusimulia hadithi ambazo haziafikiani na riwaya zao au zenye itikadi isiyokuwa yao.

Nilirudi nyumbani kwa rafiki yangu mpya ambaye sikuwahi kulitambua jina lake, akaniletea chakula cha jioni na akakaa mbele yangu. Kabla hatujaanza kula aliniuliza kuwa "Nilikwenda wapi?" Nami nikamsimulia kisa changu mwanzo hadi mwisho na nilimwambia kuwa; "Ndugu yangu ni wazi kabisa nimeanza kuwachukia Mawahabi na kuwapenda Mashia." Uso wake ulibadilika na akaniambia, "Ole wako usizungumze tena maneno kama haya." Aliniacha na hakula pamoja nami, nilimsubiri sana mpaka usingizi ukanishika na nilizindukana mapema kutokana na adhana ya Msikiti wa Mtume nikakiona chakula bado kiko pale pale kama nilivyokiacha hivyo nikatambua kuwa mwenyeji wangu hakurudi tena.

Nilitia shaka kutokana na hali hiyo na nikaogopa huenda akawa ni miongoni mwa majasusi. Basi nikaamka kwa haraka na nikaondoka hapo nyumbani sikurudi tena na nikaimaliza kutwa nzima ndani ya Msikiti Mtukufu wa Mtume nikifanya ziyara na kuswali na nilikuwa nikitoka kwa ajili ya kukidhi haja na kutawadha.

Baada ya sala ya alasiri nilimsikia khatibu mmoja akisomesha katikati ya watu wenye kuswali, nikaenda hapo na nikatambua kupitia kwa mmoja wa watu waliokuwa wameketi hapo kwamba huyo alikuwa Qadhi wa Madina.

Nilimsikiliza akifasiri baadhi ya aya za Qur'an na alipomaliza darasa lake akataka kutoka nikamsimamisha nikamuuliza, "Bwana wangu, unaweza kunijulisha maana ya aya iliyoko katika kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: "Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondoleeni uchafu enyi watu wa nyumba ya Mtume na kukutakaseni sana sana (33:33), basi ni nani hawa Ahlul Bayt waliokusudiwa ndani ya aya hii?

Alinijibu kwa haraka akasema "Ni wakeze Mtume, na aya hiyo imeanza kwa kuwataja, Enyi wake wa Mtume ninyi si kama yeyote miongoni mwa wanawake iwapo mtakuwa wacha Mungu".

Mimi nikamwambia, “Kwa hakika wanachuoni wa Kishia wanasema kwamba aya hiyo inawahusu Ali, Fatmah, Hasan na Hussein, nami niliwapinga na nikawaambia kwamba mwanzo wa aya inasema: “Enyi wake wa Mtume.” Wao wakanijibu kwamba, “Ilipokuwa wanazungumziwa wao mfumo wa aya wote ulikuwa kwa kutumia nuni ambayo nidhamiri ya kike, na Mwenyezi Mungu akasema, *“Lastunna, initaqaitunna, falatakh-dhaa’na, waqar-na fi buyutikunna, wala Tabar-rajna, waaqimna, waatinaz-zakah, wa-ati-i’nallaha warasulahu.”* Lakini kipande hiki kilipokuwa kinawarejea watu wa nyumba ya Mtume mfumo wa aya ukabadilika Mwenyezi Mungu akasema: *“Liyudh-hiba an-kum, wayutah-hirakum.”* Alinitazama na hali ya kuwa anatoa miwani yake na akasema “Ole wako na fikra hizi zenye sumu, bila shaka Mashia hufasiri maneno ya Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa matamanio yao na wanazo aya zinazomuhusu Ali na wanawe ambazo sisi hatuzijuwi pia wanayo Qur’an maalum wanayoita kuwa ni msahafu wa Fatmah, mimi nakutahadharisha wasije kukuhadaa.”

Mimi nikamwambia “Usihofu Ewe Bwana wangu, mimi ninayo tahadhari na ninafahamu mambo yao mengi, lakini nilitaka tu kuthibitisha”. Akasema, “Wewe unatokea wapi? Nikamwambia “Tunisia.” Akasema; “Unaitwa nani?” Nikasema *“Al-Tijani”* Alicheka katika hali ya kujifakharisha na akasema “Hivi unamjua huyu Ahmad Al-Tijani ni nani?” Nikasema “Yeye ni Sheikh wa Tariqa”. Akasema “Huyu ni kibaraka wa wakoloni wa Kifaransa, na Wafaransa waliimarika huko Al-geria na Tunisia kwa msaada wake, na ukitembelea Paris nenda kwenye Maktaba ya Taifa na ukasome mwenyewe kamusi ya Kifaransa katika mlango wa herufi (A), utaona kwamba Wafaransa wamempa nishani ya Utumishi bora huyo Ahmad Tijani, ambaye aliwatumikia kwa utumishi usiyo na kipimo.”

Nilistaajabishwa mno na maneno yake nikamshukuru kisha nikamuaga na nikaondoka. Nilibakia Madina kwa wiki moja kamili, ambapo nilisali sala arobaini na nikayatembelea maziyara yote na nilikuwa mchunguzi mno wakati nilipokuwa huko na sikuzidisha kitu isipokuwa kuwa mbali na mawahabii na kuwachukia.

Niliondoka Madina yenye Nuru kuelekea Jordan mahala ambapo nilikutana na marafiki ambao nilijuana nao wakati wa Hija niliyokwisha ieleza hapo kabla.

Nilikaa nao kwa muda wa siku tatu, nikakuta kuwa wanachuki dhidi ya Shia zaidi kuliko ile iliyoko kwetu Tunisia. Masimulizi ni yale yale tu, na uvumi ni huo huo na hakuna yeyote niliyemuuliza dalili ila alisema kuwa yeye amesikia tu habari zao, na wala sikumpata hata mmoja miongoni mwao aliyekaa na Shia na kusoma kitabu cha Shia wala hajakutana na Shia maishani mwake.

Kutoka huko nilikwenda Syria, na nilipokuwa mjini Damascus niliutembelea Msikiti wa Banu Umayyah na pembezoni mwake kuna mahala kilipo kichwa cha Sayyidina Hussein, vile vile nilitembelea kaburi la Salahud-din Al-Ayubi na lile la Bibi Zainab.

Na kutokea Beirut nilikatisha moja kwa moja hadi Tripoli kwa safari iliyodumu muda wa siku nne baharini, na katika kipindi hicho nilipumzika kimwili na kimawazo, nikaleta kumbukumbu ya safari ambayo ilikuwa karibu kumalizika, nikajikuta ninapata natija ya kuwapenda na kuwaheshimu Mashia, na wakati huo huo kuzidi kujitenga na kuwachukia Mawahabi ambao nimekwishafahamu ubaya wao.

Nikamshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema aliyonineemesha na hali ya kuwa namuomba aniongoe kwenye njia ya haki.

Nikarudi nyumbani nikiwa na shauku na mapenzi kwa familia yangu, watu wangu, rafiki zangu na wote niliwakuta hawajambo, na nilikumbana na vitabu vingi nilipokuwa nikiingia nyumbani mwangu vitabu ambavyo viliwasili kabla yangu na nilitambua chanzo chake.

Nilipovifungua vitabu hivyo ambavyo vilikuwa vimejaa ndani ya nyumba nilizidi kuwapenda na kuwaheshimu watu hao ambao hawakwenda kinyume na ahadi yao na vilikuwa vingi mno kuliko vile nilivyozawadiwa huko.

# KUANZA UTAFITI

Nilifurahi sana na nikavipanga vitabu hivyo katika chumba maalum ambacho nilikiita kuwa ni maktaba. Nilipumzika kwa siku kadhaa, na nilipokea ratiba ya nyakati za kazi kwa kuanza mwaka mpya wa masomo nami kazi yangu ilikuwa ni siku tatu mfululizo za kusomesha na siku nne za mapumziko kwa wiki.

Nilianza kuvisoma vile vitabu nikasoma kitabu cha *Aqida ya Imamiyah,* na *As-lus-shiah wa Usuluha*. Nafsi yangu ilitua kutokana na itikadi hizo na fikra hizo ambazo ndiyo mtazamo wa Mashia, kisha nilisoma kitabu cha *Al-Murajaat* cha Sayyid Sharafud-din Al-Musawi. Sikusoma isipokuwa kurasa chache bali kitabu hiki kiliniteka na kikanipa mvuto nikawa sikiachi isipokuwa mara chache, na wakati mwingine nilikichukua hadi chuoni.

Kitabu hicho kilinishangaza mno kutokana na uchambuzi uliomo wa Mwanachuoni wa Kishia na pia kutatua mishkeli aliyokuwa nayo yule mwanachuoni wa Kisunni ambaye ni Sheikh wa chuo cha Az-har. Makusudio yangu niliyakuta ndani ya kitabu hicho kwani kitabu hicho si kama vitabu vingine ambavyo mwandishi huandika akitakacho pasi na kuwa na mpinzani wala mwenye kukijadili. Lakini *Al-Murajaat* ni majadiliano baina ya Wanachuoni wawili kutoka madh-hebu mawili yanayo tofautiana ambayo kila mmoja wao anamuona mwenziwe kuwa yuko ndani ya upotofu katika kila jambo dogo na kubwa. Katika swala hilo la majadiliano wanategemea rejea mbili za msingi kwa Waislamu wote ambazo ni Qur'an tukufu na Sunnah sahihi ambayo ni yenye kukubalika katika vitabu sahihi vya Kisunni.

Kwa kweli kitabu hicho kilikuwa kinawakilisha wajibu wangu kama mtafiti anayetafuta ukweli na kuukubali popote atakapoukuta, na kwa msingi huu basi kitabu hiki kilikuwa kinafaa mno; na kwangu mimi kina ubora mwingi.

Nilisimama nikaduwaa pindi kilipokuwa kikiwazungumzia masahaba pale walipokosa kuzitii amri za Mtume na kuleta mifano mingi juu ya jambo hilo, na miongoni mwake ni lile tukio la msiba wa siku ya Al-Khamisi, kwani nilikuwa sifikirii kabisa kwamba Sayyidna Omar ibn Khatab angeweza kupinga amri za Mtume wa Mwenyezi Mungu na kumtuhumu kuwa anaweweseka. Na hapo mwanzoni nilidhani kwamba riwaya hiyo inatoka katika vitabu vya Mashia, lakini nilizidi kushangazwa na kuchanganyikiwa nilipomuona yule mwanachuoni wa Kishia ameinakili kutoka ndani ya sahihi Bukhari na Sahihi Muslim na nikajisemeza mwenyewe, "Iwapo nitalikuta jambo hili ndani ya sahihi Bukhari, basi nitaangalia nini cha kufanya."

Nilisafiri hadi mji mkuu wa nchi yetu na huko nilinunua *Sahih Bukhari, Sahih Muslim, Musnad ya Imam Ahmad, Sahihut-Tirmidh* na *Muwatta ya Imam Malik* na vitabu vinginevyo mashuhuri, na sikusubiri kurudi nyumbani, bali njia nzima baina ya Tunis na Qafsah nikiwa ndani ya basi nilikuwa nikizifungua kurasa za Sahih Bukhar na kutafuta tukio la msiba wa siku ya Al-Khamisi hali ya kuwa natamani nisilione tukio hilo, bila kutarajia nikalikuta.

Nikalisoma mara nyingi lakini lilikuwa kama alivyolinakili Sayyid Sharafud-din, nikajaribu kulikanusha tukio hilo lote na (pia nikajaribu kukanusha) kuwa Sayyidna Omar ndiye aliyetenda tendo hilo la hatari, lakini itawezekana vipi kwangu mimi kupinga kitu ambacho kimetajwa ndani ya (vitabu vyetu) sahihi ambavyo ni zile Sihahi za *Ahlis-Sunnah Wal-Jamaah* na tumejilazimisha wenyewe na kushuhudia juu ya usahihi wake?

Hivyo basi kuvitilia mashaka au kuvipinga sehemu fulani tu, italazimu kuvitupilia mbali na kwa kufanya hivyo itatulazimu kuzitupilia mbali itikadi zetu zote. Na lau mwanachuoni huyo wa Kishia angekuwa ananukuu kutoka katika vitabu vyao basi kamwe nisingeamini, amma alivyonakili kutoka katika Sihahi za Kisunni jambo hilo halina nafasi ya kupingwa kwa kuwa sisi tumezilazimisha nafsi zetu wenyewe kuwa hivyo ni vitabu sahihi mno baada ya kitabu cha Mwenyezi Mungu. Jambo hilo limekuwa ni lazima, vinginevyo itabidi kuvitilia mashaka vitabu hivyo na hapo ndipo tutakapobakia bila ya hukumu yoyote ya Kiislamu tunayoitegemea

kwa sababu hukumu zilizokuja ndani ya kitabu cha Mwenyezi Mungu ni *Mujmal* na siyo *Mufassar* na kwa kuwa sisi tuko mbali na zile zama za Utume na tulirithi dini yetu kutoka kwa baba, naye kutoka kwa babu tena kwa njia hii hii ya sihahi hizi, basi kwa hali yoyote ile haiwezekani kuvitupa vitabu hivi.

Nilijilazimisha mwenyewe kwa kuweka ahadi wakati nikiingia katika utafiti huu mrefu na mgumu kwamba, nitegemee hadithi sahihi ambazo Masunni na Mashia wameafikiana, na nizitupilie mbali hadithi ambazo zimepokelewa na kundi moja kinyume na lile jingine. Kwa kutumia njia hii ya kati na kati nitakuwa nimejitenga na upendeleo, ung'ang'anizi wa kimadhehebu na chuki za kitaifa na kwa wakati huo huo naikata kamba ya mashaka ili niufikie mlima wa yakini nao ni njia ya Mwenyezi Mungu iliyonyooka.

# MWANZO WA UTAFITI WA KINA

# MTAZAMO WA SHIA NA SUNNI JUU YA MASAHABA

Miongoni mwa utafiti muhimu ambao mimi nauzingatia kuwa ndiyo jiwe la msingi katika utafiti wote unaoongoza kufikia kwenye ukweli, ni ule utafiti unaohusu Maisha ya Masahaba, mambo yao waliyoyafanya na waliyokuwa wakiyaitakidi, hiyo ni kwa sababu wao ndiyo nguzo ya kila kitu, na tumeipokea dini yetu kutoka kwao na kupitia kwao tutaondokana na kiza ili tuzifahamu hukumu za Mwenyezi Mungu.

Wanachuoni wa Kiislamu (wa zamani) wametangulia katika kuwachunguza Masahaba na mienendo yao, na kwa ajili ya jambo hili wametunga vitabu vingi kama vile *Usudul-Ghabah, Al-Isaabah Fimaarifatis-Sahabah, Miizannul-itidal,* na vingine (vyote hivyo ili) kupima na kuchanganua maisha ya Masahaba, lakini vitabu hivyo ni kwa mujibu wa mtazamo wa Kisunni.

Lipo tatizo ambalo linabainisha kwamba, Wanachuoni wa hapo mwanzo wengi wao walikuwa wakiandika na kusimulia kwa namna inayokubaliana na maoni ya watawala wa Kibani Umayyah na Bani Abbas, watawala ambao wao walikuwa wanatambulikana kwa uadui wao dhidi ya Watu wa nyumba ya Mtume (s.a.w.) bali na kila anayewafuata na kupita katika muongozo wao. Kwa ajili hii basi siyo uadilifu kutegemea kauli zao bila ya kauli za Wanachuoni wengine wa Kiislamu ambao tawala hizo ziliwakandamiza, kuwatawanya na kuwaua kwa sababu ya wao kuwa ni wafuasi wa Watu wa nyumba ya Mtume, na ndiyo waliokuwa chimbuko la mapinduzi dhidi ya tawala hizo za kidhalimu zilizopotoka.

Na tatizo la msingi katika yote hayo ni Masahaba, kwani wao ndiyo waliohitilafiana kuhusu lile suala la Mjumbe wa Mwenyezi Mungu

kuwaandikia yale maandiko ambayo yangewalinda wasipotee mpaka siku ya Qiyamah. Kuhitilafiana kwao huku ndiko kuliko unyima umma wa Kiislamu fadhila hii na kuutumbukiza ndani ya upotofu mpaka ukagawanyika, kufarakana, kugombana na kisha ukashindwa na nguvu zake zikatoweka.

Na ni hao hao Masahaba ambao walihitilafiana kuhusu ukhalifa na wakagawanyika baina ya kundi linalotawala na jingine pinzani, na hilo likasababisha Umma kubakia nyuma na kugawanyika (baadhi yao) kuwa wafuasi wa Muawiya na wengine kuwa wafuasi wa Ali (a.s.).

Ni masahaba hao hao waliohitilafiana katika tafsiri ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Hadithi za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na ndipo yalipotokea madhehebu, makundi vikundi vidogo vidogo hatimaye yakazuka mafunzo yaliyojulikana kwa jina la *Il-mul-Kalami* na fikra nyingine tofauti. Si hivyo tu, bali kukajitokeza falsafa aina kwa aina zilizochochewa na tamaa za kisiasa tu zenye kufungamana na tamaa za kuhodhi madaraka.

Waislamu wasingegawanyika wala kuhitilafiana katika jambo lolote lau siyo Masahaba, na tofauti yeyote iliyokwishaanza na inayoanza hivi sasa kwa hakika inarudi kwenye hitilafu yao juu ya Masahaba.

Mola wao ni mmoja, Qur'an moja, Mtume mmoja na Qibla moja. Waislamu wote wanaafikiana juu ya hayo na tofauti zaozimeanzia kwa Masahaba ndani ya *Saqifa bani Saidah* kuanzia siku ya kwanza baada ya Mtume kufariki na (tofauti baina yao) ikaendelea mpaka leo hii na itaendelea mpaka Mwenyezi Mungu mwenyewe atakapotaka.

Nami nimegundua wakati wa mazungumzo yangu pamoja na Wanachuoni wa Kishia kwamba, kwa mujibu wa mtazamo wao ni kuwa Masahaba wamegawanyika kwenye makundi matatu:

Kundi la kwanza: Ni la wale Masahaba wema ambao walimtambua Mwenyezi Mungu na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa maarifa ya kweli kabisa na wakamuunga mkono kwa dhati na kusuhubiana naye kwa ukweli katika kauli na utakaso wa moyo katika matendo, na wala

hawakugeuka baada yake, bali waliimarika juu ya ahadi waliyomuahidi. Hapana shaka Mwenyezi Mungu Mtukufu amewasifu ndani ya Kitabu chake Kitukufu mara nyingi na mahali pengi. Naye Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amewasifu mara nyingi na mahali pengi pia, na Mashia huwataja Masahaba hawa kwa heshima na kuwatukuza kama ambavyo Masunni nao huwataja kwa heshima na kuwatukuza pia.

Na kundi la pili: Ni la wale Masahaba ambao waliingia ndani ya Uislamu wakamfuata Mjumbe wa Mwenyezi Mungu imma kwa kupenda au kwa kuogopa. Hawa walikuwa wana msimbulia Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa kusilimu kwao na katika baadhi ya nyakati wao walikuwa wakimuudhi na hawafuati maamrisho yake na makatazo yake, bali waliyapa maoni yao nafasi (ya kwanza) dhidi ya hukumu zilizowazi mpaka Qur'an ilikuwa inashuka ili kuwakemea na mara nyingine ilishuka kuwatisha. Mwenyezi Mungu aliwafedhehesha katika aya nyingi, pia Mtume aliwahadharisha katika hadithi nyingi. Mashia hawawataji Masahaba hawa ila kwa mujibu wa matendo yao bila ya kuwaheshimu wala kuwatukuza kama wale wa mwanzo.

Amma kundi la tatu la Masahaba: Ni wanafiki ambao walimfuata Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ili kumfanyia vitimbi, wakadhihirisha Uislamu, wakaficha ukafiri, wakajisogeza ili wauvuruge Uislamu na Waislamu wote. Bila shaka Mwenyezi Mungu ameyateremsha sura kamili kwa ajili yao na akawataja mara nyingi mahali pengi na kuwaonya kuwa wataingia katika tabaka la chini kabisa ndani ya moto.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) amewataja na kuwahadharisha, na kuna baadhi ya Masahaba wake aliwafahamisha majina ya wanafiki hao na alama zao. Na Shia na Sunni wanaafikiana juu ya kuwalaani na kujitenga nao.

Na wapo aina maalum ya Masahaba ambao japokuwa walikuwa miongoni mwa Masahaba, lakini wao wanazo sifa pekee mbali na Masahaba wengine kwani wanayo Qaraba (udugu) kwa Mtume na ubora wa kimaumbile, kiroho na mambo mengine maalum aliyowahusisha nayo Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hapana yeyote mwenye kuwafikia katika daraja hiyo.

Hawa ndiyo wale Watu wa nyumba ya Mtume (s.a.w.) ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na kuwatakasa mno. *(Qur.33:33)* Na akawajibisha kuwasalia kama alivyowajibisha sala hiyo kwa Mtume wake, pia amewajibisha khumsi kwa ajili ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na wao. *(Qur. 8:41)* Vile vile akawajibisha kwa kila Muislamu awapende na (mapenzi hayo) ndiyo malipo ya Utume wa Muhammad (s.a.w.). *(Qur. 42:23)*

Wao ndiyo wenye mamlaka ambao Mwenyezi Mungu ameamuru kuwatii *(Qur. 4:59)*. Nao ndiyo waliobobea katika elimu, ambao wanafahamu taawili ya Qur'an na wanazijua aya Mutashabih na Muh-kam *(Qur.4:59)*. Hao pia ndiyo wale wenye kumbukumbu (Ahlud-Dhikr) ambao Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amewalinganisha na Qur'an katika ile hadithi ya vizito viwili na akawajibisha kushikamana navyo. Pia akawalinganisha na Safina ya Nabii Nuhu ambayo mwenye kuipanda ataokoka na mwenye kuikengeuka ataangamia.

Masahaba walikuwa wakifahamu Utukufu wa Watu wa nyumba ya Mtume (s.a.w.), (kwa hiyo) wakiwatukuza na kuwaheshimu, na Mashia wanafuata uongozi wao na kuwatanguliza juu ya kila sahaba, na wanazo dalili sahihi zilizo wazi.

Amma Ah-lus-Sunnah Wal-Jamaa, bila shaka wao pamoja na kuwaheshimu kwao Watu wa nyumba ya Mtume (s.a.w.) na kuwatukuza na kuwaboresha, wao hawakkubali kuwepo kwa mgawanyiko huu wa Masahaba, wala hawaamini kwamba kuna Masahaba wanafiki, bali kwa mtazamo wao Masahaba wote ni viumbe bora baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) na kama kutakuwa na mgawanyo, basi huo utakuwa ni katika mlango wa kuzidiana ubora kama kutangulia kusilimu na kujitolea ndani ya Uislamu, hivyo basi huwaboresha zaidi Khulafaur-Rashiduna kwa (kuwapa) daraja ya kwanza kisha wale sita miongoni mwa wale waliobashiriwa pepo na hii ni kwa mujibu wa maoni yao. Ndio maana utawaona pindi wamsaliapo Mtume na Āli zake huongezea na Masahaba wote bila kumtoa hata mmoja. Hiki ndicho nikijuacho toka kwa wanachuoni wa Kisunni na nilichokisema mwanzo ndicho nilichokisikia toka kwa Wanachuoni wa Kishia; yaani kuwagawa Masahaba mafungu manne na hili ndilo lililonipelekea niufanye utafiti wangu wa kina uanzie

na somo hili kuhusu Masahaba. Nilimuahidi Mwenyezi Mungu iwapo ataniongoa nijiepushe na jazba ili nisifungamane na upande wowote bila upinzani na nisikilize kauli toka pande zote mbili kisha nifuate iliyokuwa bora. Na rejea yangu ndani ya utafiti huo ni:

(1) Kanuni sahihi za kimantiki: Yaani nisitegemee isipokuwa lile jambo ambalo wote wameafikiana juu ya tafsiri ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna Sahihi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.).

(2) Akili: Ambayo ni neema kubwa miongoni mwa neema za Mwenyezi Mungu juu ya mwanadamu, kwani kwa akili hiyo Mwenyezi Mungu amemtukuza na kumboresha juu ya viumbe wengine. Je huoni kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu pindi anapotoa hoja dhidi ya waja wake huwataka watumie akili kwa kusema: "Je hawafikiri, je hawafahamu, je hawazingatii, je hawaoni n.k.?

Kimsingi, Uislamu wangu uwe ni kumuamini Mwenyezi Mungu, Malaika wake, Vitabu vyake, Mitume wake na kwamba Muhammad ni Mja wake na ni Mjumbe wake, na kwamba Uislamu ndiyo dini (sahihi) mbele ya Mwenyezi Mungu na wala nisimtegemee katika utafiti huo yeyote miongoni mwa Masahaba hata akiwa na ukaribu kiasi gani au ana daraja kubwa kiasi gani, kwani mimi siyo miongoni mwa Banu Umayyah wala Banu Abbas wala Banu Fatmah. Vile vile mimi siyo Sunni wala Shia na sina uadui wowote na Abubakar wala Umar wala Uthman wala Ali na hata yule Wah-shi aliyemuua Bwana wetu Hamza maadam alisilimu na Uislamu unafuta yaliyotendwa kabla yake, na bila shaka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) alimsamehe.

Kwa kuwa nafsi yangu nilikwisha kuiingiza ndani ya utafiti huu kwa lengo la kuufikia ukweli, na kwa kuwa nimejiepusha na fikra zote zilizotangulia kwa nia njema kabisa, basi sasa hivi naanza uchunguzi huu juu ya Masahaba nikitaraji baraka za Mwenyezi Mungu.

**1). Masahaba siku ya Sulhu ya Hudaibiyyah**

Kisa chenyewe kwa ujumla ni kwamba: Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) katika mwaka wa sita A.H. alitoka akikusudia kufanya Umra akiwa pamoja na Masahaba elfu moja na mia nne. Akawaamuru panga zao wazitie ndani ya ala, kisha akavaa *Ihram* yeye na Masahaba wake

mahala paitwapo *“Dhil-Halifah.”* Wakawatanguliza ngamia kwa ajili ya kuchinja ili kuwatambulisha Maquraishi kwamba yeye amekuja Makkah kufanya Umrah na siyo kwa ajili ya vita. Lakini Maquraish kwa kiburi chao waliogopa iwapo Waarabu watasikia kuwa Muhammad ameingia kwa nguvu mjini Makkah na kuvunja nguvu zao. Hivyo basi walimtumia ujumbe ulioongozwa na Suhailibn Amr ibn Abdi Wuddi Al-Āmiri, wakamtaka safari hii arudi alikotoka na kwamba mwaka ujao watamuachia Makkah kwa siku tatu.

Kwa hakika walimpa masharti magumu ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliyakubali kutegemeana na mas-lahi ambayo Mola wake Mtukufu alimfunulia.

Hata hivyo baadhi ya Masahaba jambo hili alilolifanya Mtume halikuwapendeza, wakampinga kwa nguvu mno, na Umar ibn Khatab akamjia Mtume na kumuambia; “Je, wewe siyo Mtume wa Mwenyezi Mungu wa haki?” Mtume akasema, “Bila shaka mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu wa haki.”

Umar akasema; “Je sisi hatuko kwenye haki na adui yetu yuko kwenye batili?” Mtume akasema, “Bila shaka ndivyo.” Umar akasema, “Basi ni kwa nini tunaonyesha udhaifu katika dini yetu?” Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akamwambia: “Bila shaka mimi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na siwezi kumuasi naye ndiye Mwenye kunilinda,” Umar akasema, “Je, si ulikuwa ukituambia kwamba tutaingia kwenye Nyumba Tukufu na tutaitufu?” Mtume akasema, “Bila shaka nilisema, lakini je nilikuambia tutaingia mwaka huu?” Umar akasema, “Hapana.” Mtume akasema, “Basi bila shaka utaingia na utaitufu.”

Hatimaye Umar ibn Al-Khatab akamuendea Abubakr akasema: “Huyu siye Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wa haki?” Abubakr akasema, “Bila shaka ni Mtume wa haki”. Kisha Umar alimuuliza Abubakr maswali yale yale aliyomuuliza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu naye Abubakr akamjibu majibu yale yale na akamwambia, “Ewe bwana bila shaka yeye ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na hawezi kumuasi Mola wake naye ndiye Mwenye kumlinda hivyo basi shikamana naye.”

Na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipomaliza kutia saini mkataba wa Sul-hu ya Hudabiyah aliwaambia masahaba wake: "Simameni mchinje na mnyoe." Basi Wallahi hakuna miongoni mwao aliyesimama mpaka akasema mara tatu na ilivyokuwa hapana yeyote miongoni mwao aliyetekeleza amri yake aliingia kwenye hema lake kisha akatoka na wala hakumsemesha yeyote kati yao akachinja mnyama wake na akamuita kinyozi wake akamnyoa.

Masahaba wake walipoiona hali hiyo, walisimama wakachinja na wakawa wananyoana wao kwa wao karibu wauane wao kwa wao. Kisa hiki wamekiandika waandishi wa sera na tarikh, kama ambavyo amekiandika Bukhari ndani ya sahih yake katika *Kitabus-shurūt, babus-shurūt fil-jihad juz.2 uk.122 (pia) Sahih Muslim katika babu Sul-hul-hudaibiyah Juz. 2.*

Kwa ujumla hiki ndicho kisa cha Sul-hu ya Hudaibiyyah nacho ni miongoni mwa matukio ambayo Mashia na Masunni wameafikiana na wamelitaja tukio hilo waandishi wa sera kama vile Tabari, Ibn Al-athir na Ibn Saa'd na wengineo kama vile Bukhari na Muslim.

Nami hapa ninao msimamo wangu; haiwezekani nisome maelezo kama haya yaliyopita hivi punde kisha nisiathirike wala kushangazwa na matendo ya Masahaba hawa kwa Mtume wao.

Hivi mtu mwenye akili atakubaliana na kauli ya wale wasemao kwamba; Masahaba (r.a.) walikuwa wakitii maamrisho ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kuyatekeleza, wakati tukio hili linawasuta na linapinga wanayoyakusudia.?

Hivi kweli mtu mwenye akili anaweza akafikiria kwamba, matendo haya dhidi ya Mtume (s.a.w.) ni jambo dogo linalokubalika au linalosameheka?

Mwenyezi Mungu anasema: *"Naapa kwa Mola wako, hawawi waumini mpaka wakufanye wewe uwe muamuzi katika yale wanayozozania baina yao. Kisha wasione uzito katika nafsi zao kwa yale uliyoyaamua na wasalimu amri mara moja. (Qur. 4:65)*

Basi je Umar ibn Al-Khatab alisalimu amri mara moja mahali hapo na hakuona uzito ndani ya nafsi yake kwa maamuzi aliyoyaamua Mtume (s.a.w.)? Au katika msimamo wake alikuwa na mashaka juu ya amri ya Mtume? Na hasa pale aliposema. "Je wewe siyo Mtume wa Mwenyezi Mungu wa haki? Na je siyo wewe uliyekuwa ukituambia ..." mpaka mwisho wa maneno yake.?

Na je hivi alisalimu amri mara moja baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kumjibu maswali hayo kwa majibu yanayokinaisha.? Sivyo kabisa, hakika hakutosheka na majibu ya Mtume (s.a.w.) na akaenda kumuuliza Abubakr (r.a.) maswali yale yale. Je, hivi alikubali hata baada ya Abubakr (r.a.) kumjibu na kumpa nasaha na akamtaka ashikamane na Mtume? Mimi sijui kama alikubali au alitosheka na majibu ya Mtume au majibu ya Abubakr (r.a.). Kinyume chake ni kwamba, ni kwa nini tena Umar anasema yeye mwenyewe kwamba "Nilifanya mambo mengi kwenye tukio hilo ..."? Na sijui ni sababu ipi iliyowafanya wengine waliobakia miongoni mwao wapinge baada ya hapo, pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipowaambia, "Chinjeni kisha mnyoe." Hakuna yeyote miongoni mwao aliyetii amri hiyo mpaka Mtume akakariri mara tatu bila mafanikio.

*Subhana-llah!!* Mimi nakurubia kutokuamini nikisomacho, hivi kweli inafikia hali hii kwa Masahaba kumfanyia Mtume? Kwa hakika lau kisa hiki kingelikuwa kimesimuliwa na Mashia peke yao, basi ningeyachukulia hayo waliyoyasema kuwa ni uzushi wao dhidi ya Masahaba watukufu, lakini kisa hiki kwa usahihi na umashuhuri wake kimenakiliwa pia na wanachuoni wote wa hadithi wa Kisunni.

Kwa kuwa mimi niliilazimisha nafsi yangu kukubali yale waliyoafikiana Mashia na Masunni, basi nilijikuta ninasalimu amri na kuchanganyikiwa ilikuwaje hali hii!! Niseme nini, na nitawatakasa vipi Masahaba hawa ambao waliishi na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu karibu miaka ishirini tangu kuanza Utume mpaka siku ya Hudaibiyyah, hali ya kuwa wanaona miujiza yake na Nuru ya Unabii, na Qur'an ikiwafundisha usiku na mchana, namna gani wataishi na Mtume na jinsi gani wazungumze naye. Ilifikia hali ambayo Mwenyezi Mungu aliwaonya kuwa matendo yao mema yataharibika iwapo watanyanyua sauti zao juu ya sauti ya Mtume.

Ninalazimika kufikiri kwamba Umar ibn Khatab ndiye aliyewachochea wengine na kuwafanya wapinge amri ya Mtume, na zaidi ya hapo ukiongeza kukiri kwake kwamba yeye siku hiyo alifanya mambo ambayo hakutaka kuyataja na ameyakariri mahala pengi akisema: "Nimekuwa nikifunga, kutoa sadaka, kusali na kuwaacha huru watumwa kwa kuchelea maneno yangu niliyoyasema ..." hadi mwisho kama ilivyovyosimuliwa toka kwake kuhusu tukio hili. *(Taz: Siratul-Halabiyyah Babu sul-hil-Hudaibiyyah Juz. 2 uk. 706.)*

Maelezo haya yanatujulisha kwamba Umar mwenyewe alikuwa akitambua upeo wa msimamo aliokuwa nao siku hiyo, kwa hakika ni kisa cha ajabu lakini cha kweli.

**2). Masahaba na msiba wa Siku ya Alhamisi**

Ujumla wa kisa chenyewe ni kwamba, Masahaba walikuwa wamekusanyika ndani ya nyumba ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu siku tatu kabla ya kufariki kwake. Mtume akawaamuru wamletee mfupa wa begani na wino ili awaandikie maandiko yatakayowalinda wasipotee, lakini Masahaba walihitilafiana miongoni mwao, wako walioiasi amri yake na wakamtuhumu kuwa anaweweseka. Jambo hilo lilimkasirisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na akawatoa nyumbani mwake bila ya kuwaandikia chochote.

Hebu soma sehemu kidogo ya kisa hiki kwa ufafanuzi. Ibn Abbas amesema; "Siku ya al-hamisi, hiyo siku ya al-hamisi ilikuwa na tukio gani? Mtume wa Mwenyezi Mungu yalimzidia maumivu yake akasema, Njooni nikuandikieni maandiko ambayo hamtapotea baada yake, Umar akasema, bila shaka Mtume kazidiwa na maumivu nanyi mnayo Qur'an, kinatutosha kitabu cha Mwenyezi Mungu. Basi watu waliokuwemo ndani ya nyumba ya Mtume wakahitilafiana na kuzozana miongoni mwao, wako wanaosema sogeeni ili Mtume akuandikieni maandiko ambayo hamtapotea baada yake na wengine wanasema alivyosema Umar. Walipozidisha zogo na kuhitilafiana mbele ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu; akawaambia niondokeeni." Kwa ajili hii Ibn Abbas alikuwa akisema "Msiba mkubwa kuliko yote ni yale majibizano yaliyotokea baina ya Mtume na kuwaandikia maandiko kwa sababu ya kuhitilafiana kwao na zogo lao." *Taz. Sahih Muslim Juz. 5 uk. 75 mwishoni mwa kitabul-Wassiyyah.*

Tukio hili ni sahihi na la kweli halina shaka ndani yake, wanachuoni na wanahadithi Wakishia wameliandika katika vitabu vyao, kama ambavyo wanachuoni, wanahadithi na wanahistoria wa Kisunni wameliandika ndani ya vitabu vyao nalo linanilazimisha mimi nitimize kile nilichojilazimisha nafsi yangu.

Mpaka hapa nasimama hali ya kuwa nimechanganyikiwa kuufasiri msimamo wa Umar ibn Al-Khatab dhidi ya amri ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Ni amri ipi hiyo? Ni ile ya kuulinda Umma huu usipotee, na hapana shaka maandiko haya ndani yake kulikuwa na kitu kipya kwa ajili ya Waislamu ambacho kingewaondoshea kila aina ya mashaka.

Hebu tuachane na kauli ya Mashia isemayo kwamba Mtume alitaka kuandika jina la Ali kuwa ni Khalifa wake, na Umar akalitambua jambo hilo kisha akamzuia Mtume asiandike.

Huenda (Mashia) wasitukinaishe kwa madai yao haya ambayo kimsingi hayaturidhishi, lakini je kunapatikana tafsiri nyingine inayoingia akilini kuhusu tukio hili lenye kutia uchungu ambalo lilimkasirisha Mtume mpaka akawafukuza Masahaba na likamfanya Ibn Abbas alie hadi machozi yake yakazilowanisha changarawe na akaliita kuwa ni msiba mkubwa? Masunni wanasema kwamba, "Umar alihisi ukali wa maradhi ya Mtume hivyo alimhurumia na alitaka ampumzishe". Lakini sababu hii haikubaliki kwa watu wa kawaida sembuse wanachuoni? Mimi nilijaribu mara nyingi kumtakia udhuru Umar, lakini uhakika wa tukio lenyewe unanizuia kufanya hivyo, hata kama neno anaweweseka litabadilishwa "Mwenyezi Mungu apishe mbali" liwe tamko la "Maradhi yamemzidia" bado hatutapata kitu kitakachoitakasa kauli ya Umar aliposema: "Munayo Qur'an na kinatutosha kitabu cha Mwenyezi Mungu."

Basi je, yeye alikuwa anaifahamu mno Qur'an kuliko Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ambaye ameteremshiwa au kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hazingatii akisemacho? Haiwezekani!! Au (tuseme) kwamba Mtume kwa amri yake hiyo alikuwa anataka kuleta hitilafu na kutokuelewana? "*Namuomba Mwenyezi Mungu anisamehe.*"

Lau sababu ya Masunni ingekuwa sahihi, basi hilo lisingefichikana kwa Mtume na asingekosa kuifahamu nia nzuri ya Umar, na Mjumbe wa

Mwenyezi Mungu angelimshukuru kwa ajili hiyo na angemkurubisha badala ya kumkasirikia na akasema *"Niondokeeni"!!*

Kwa hakika mimi najiuliza ni kwa nini wao waliitii amri yake alipowafukuza kutoka ndani ya chumba cha Mtume mbona hawakusema kuwa anaweweseka? Walipotambua ya kwamba bila shaka walikuwa wamefanikisha njama yao ya kumzuia Mtume kuandika maandiko yale, basi hawakuona tena sababu yoyote ya kuwafanya wabakie hapo, na dalili ya hilo ni kuwa wao walizidisha mzozo na kuhitilafiana mbele ya Mtume (s.a.w.) na wakagawika makundi mawili, wapo miongoni mwao wanaosema sogeeni kwa Mtume awaandikieni hayo maandiko, na miongoni mwao wako wanaosema alivyosema Umar yaani "Mtume anaweweseka."

Suala hili halikuwa jepesi kiasi cha kumuhusu Omar peke yake!! Lau mambo yangekuwa hivyo basi Mtume wa Mwenyezi Mungu angelimnyamazisha na kumkinaisha kwamba yeye Mtume hatamki jambo kwa matamanio yake na wala haiwezekani kuzidiwa na maumivu katika kuuongoa Umma usipotee, lakini jambo hili lilikuwa nyeti na likapata watetezi kama kwamba walikuwa wameafikiana mapema na ndiyo maana walizidisha zogo na kuhitilafiana wakasahau au wakajisahaulisha kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: *"Enyi mulioamini musipaze sauti zenu juu ya sauti ya Mtume, na wala msisemezane naye kwa sauti ya nguvu kama mnavyosemezana ninyi kwa ninyi, visije vitendo vyenu vikakosa thawabu na hali ya kuwa hamtambui." (Qur. 49:2)*

Katika tukio hili walivuka mipaka ya kupaza sauti na kumsemesha kwa nguvu hadi wakamtuhumu Mtume (s.a.w.) kuwa anaweweseka. Mwenyezi Mungu apishilie mbali. Kisha wakazidisha zogo na kuhitilafiana na kukawa na vita vya maneno mbele ya Mtume (s.a.w.), mimi nakurubia kuamini kwamba wengi wao waliunga mkono kauli ya Umar na ndiyo maana Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliona kuwa hakuna mafanikio katika kuandika maandiko hayo kwa sababu alifahamu kuwa wao hawakumuheshimu na wala hawakutii amri ya Mwenyezi Mungu kuhusiana naye yaani, kutokupaza sauti zao mbele yake. Na iwapo wao wanaiasi amri ya Mwenyezi Mungu basi hawawezi kutii amri ya Mtume wake.

Hekima ya Mtume ilikuwa ni kutokuwaandikia maandiko yake kwani alituhumiwa kuhusu maandiko hayo bado yuko hai, basi mambo yangekuwaje kuhusu maandiko hayo baada ya kufa kwake? Bila shaka wenye kumtuhumu wangesema, "*Ni maneno ya mwenye kuweweseka!!"*.

Huenda wangetilia shaka hata baadhi ya hukmu alizoweka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika kipindi cha maradhi aliyofia, kwani itikadi yao kuhusu kuweweseka kwake ilikuwa na nguvu. Namuomba Mwenyezi Mungu anisamehe, na ninatubia kwake kutokana na kauli hii mbele ya Mtume Mtukufu.

Basi ni vipi nitaikinaisha nafsi yangu na dhamira yangu iliyo huru kwamba, Umar ibn Khatab alifanya jambo la kusameheka wakati ambapo wenzake na waliokuwepo hapo walilia kwa ajili ya kilichotokea mpaka machozi yao yakalowesha mchanga na wakaiita siku hiyo kuwa ni msiba kwa Waislamu?

Kwa ajili hii niliamuwa kuzikataa sababu zote zilizotolewa ili kulitakasa tendo hilo, na nilijaribu kulipinga tukio hili na kulikanusha ili niepukane na maafa yake, lakini vitabu vimelinakili na kulithibitisha na kulifanya kuwa ni tukio sahihi na havikufaulu kufanya vyema katika utetezi wake.

Ninakurubia kukubaliana na mtazamo wa Mashia katika kulifasiri tukio hili kwani mtazamo huo unazo sababu za kimantiki na unadalili nyingi.

Bado nakumbuka jawabu la Sayyid Muhammad Baqir As-Sadr nilipomuuliza, "Ni jinsi gani alivyofahamu Sayyidna Umar miongoni mwa Masahaba kile ambacho Mtume anataka kukiandika, nacho ni kumpa Ali Ukhalifa kwa mujibu wa madai yenu (ninyi Mashia)?"

Sayyid As-Sadr akasema, "Umar hakuwa peke yake aliyetambua makusudio ya Mtume, lakini masahaba wengi walitambua kile alichokitambua Umar, kwani Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) alikwisha kuwaambia jambo kama hili pale aliposema, Hakika mimi ninaacha kwenu vizito viwili, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Kizazi changu Watu wa nyumba Yangu, vitu ambavyo mkishikamana navyo kamwe hamtapotea baada yangu." Na katika kipindi cha maradhi yake hayo akawaambia, "Njooni niwaandikieni maandiko ambayo

kamwe hamtapotea baada yake”. Waliokuwepo hapo akiwemo Umar walifahamu kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anataka kutilia nguvu kwa maandiko, kile alichokieleza ile siku ya Ghadir Khum, nacho ni kushikamana na kitabu cha Mwenyezi Mungu na Kizazi chake Mtume (s.a.w.) na Bwana wa kizazi hicho ni Ali, basi ni kama kwamba Mtume (s.a.w.) alitaka kusema “Shikamaneni na Qur’an na mshikamane na Ali.” Na hilo alikwishalisema katika matukio mengi kama walivyoyaeleza wanachuoni wa hadithi.

Maquraishi wengi walikuwa hawamridhii Ali kwa sababu eti ni mdogo kwao na kwamba yeye ndiye aliyewavunja wenye kibri (miongoni mwa Maquraishi) wao. Aliwakatisha tamaa na kuwaua mashujaa wao, lakini hawakuonesha jeuri mbele ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (kama Umar) kwa kiwango kilichotokea katika sulhu ya Hudaibiyyah, na pia upinzani mkali (aliouonesha) kwa Mtume pale alipomsalia Abdallah ibn Ubayyi yule mnafiki, na mahala pengine pengi ambapo historia imeandika. Tukio hili ni miongoni mwa hayo mengi, nawe utaona kwamba ule upinzani wa kuandika maandiko katika kipindi cha maradhi ya Mtume uliwachochea wengine kuthubutu kumpinga Mtume na hatimaye kuzidisha zogo mbele ya Mtume (s.a.w.).

Bila shaka kauli hii ilikuja ikiwa ni upinzani kamili wa makusudio ya hadithi, kwani kusema mnayo Qur’an, kinatutosha Kitabu cha Mwenyezi Mungu ni kinyume na madhumuni ya hadithi ambayo inawaamuru washikamane na Kitabu cha Mungu na Kizazi cha Mtume vyote kwa pamoja. Hivyo basi ni kama kwamba makusudio yao ni kuwa kinatutosha Kitabu cha Mwenyezi Mungu tu, hatuna haja na Kizazi cha Mtume.

Hapana tafsiri nyingine inayoingia akilini isiyokuwa hii kulingana na tukio hili, isipokuwa kama itakuwa makusudio ni kumtii Mwenyezi Mungu tu bila ya Mtume wake, na maana hii vile vile ni batili na haingii akilini.

Nami nikiweka kando kuegemea upande mmoja na ubinafsi uliovuka mpaka na kuipa maamuzi akili iliyosalimika na fikra iliyohuru, ninaegama kwenye ufumbuzi huu, na hili ni jepesi kuliko kumtuhumu Umar kwamba yeye ni wa mwanzo kuipinga Sunna ya Mtume kwa kusema kwake kuwa kinatutosha Kitabu cha Mwenyezi Mungu.

Pia iwapo kuna baadhi ya watawala walioikataa Sunna ya Mtume kwa madai kuwa inapingana, basi hali hiyo imefuatia mambo yaliyopita ndani ya historia ya Waislamu. Pamoja na kuwa mimi simbebeshi Umar peke yake lawama ya tukio hili na kule kuukosesha Ummah mwongozo na ili nibaki kuwa mwadilifu upande wa haki, nambebesha yeye na waliokuwa upande wa rai yake miongoni mwa Masahaba watukufu ambao walisema usemi kama wake na kuunga mkono msimamo wake ili kupinga amri ya Mjumbe wa Mungu.

Kwa hakika mimi nashangazwa na mtu anayesoma tukio hili na akapita tu kama kwamba hapakuwa kitu pamoja na kuwa tukio hili ni miongoni mwa misiba mikubwa kama alivyoliita Ibn Abbas. Nashangazwa mno na watu ambao wanajaribu kwa juhudi zao kulinda heshima ya sahaba na kulitakasa kosa lake hata kama heshima hiyo itakuwa iko dhidi ya heshima na utukufu wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na ni dhidi ya Uislamu na misingi yake!!

Ni kwa nini tunaukwepa ukweli na tunajaribu kuufuta pindi unapokwenda kinyume cha matakwa yetu? Ni kwa nini hatukubali kuwa Masahaba ni watu kama sisi nao wana matamanio na wanakosea na kufanya vizuri kama sisi.?

Siachi kushangaa, isipokuwa ninapokisoma kitabu cha Mwenyezi Mungu ambacho kinatusimulia visa vya Manabii (a.s.) na mambo waliyopambana nayo toka kwa watu wao licha ya kushuhudia miujiza ya Mtume wao:

*Ewe Mola wetu usizipotoshe nyoyo zetu baada ya kuwa umetuongoa na utupe rehma kutoka kwako, bila shaka wewe ni mpaji.*

Namna hivi nimekuwa nikifahamu rejea ya msimamo wa Mashia kwa Khalifa wa pili ambaye wao Mashia humbebesha sehemu kubwa ya jukumu la misiba iliyotokea katika maisha ya Waislamu tangu siku ya msiba ule wa siku ya Al-hamisi, msiba ambao uliunyima Umma yale maandiko ya uongofu ambayo Mtume (s.a.w.) alitaka kuwaandikia.

Haiwezekani kukwepa ukweli kwamba, mwenye akili ni yule aliyeijua haki kwanza kabla ya kuwajua watu anaowatakia udhuru. Ama wasioijuwa

haki isipokuwa kupitia kwa watu sisi hatuna cha kuzungumza juu yao.

**3). Masahaba katika Jeshi la Usamah:**

Kisa hiki kwa ujumla ni kwamba, Mtume (s.a.w.) aliandaa jeshi ili kulikabili jeshi la Warumi siku mbili kabla ya kufariki kwake na akampa uamirijeshi Usamah ibn Zaid ibn Harith aliyekuwa na umri wa miaka kumi na minane. Katika jeshi hili Mtume (s.a.w.) aliwatayarisha wakuu wa Kimuhajirina na Ansari kama vile Abubakr, Umar, Abu-Ubaidah na wengineo miongoni mwa Masahaba wakubwa mashuhuri. Miongoni mwao wapo waliopinga uamirijeshi wa Usamah na wakasema "Itakuwaje tuongozwe na kijana ambaye bado hajakomaa?"

Kabla ya hapo waliwahi kupinga uamirijeshi wa Baba yake (Usamah) na walisema mengi juu ya jambo hilo na walikosoa mno (hali hiyo) iliyomfanyaMtume (s.a.w.) akasirike sana  kuhusiana na upinzani wao na kukosoa kwao. Hivyo basi Mtume (s.a.w.) alitoka akiwa mgonjwa hali amefunga kitambaa kichwani akiyumba kati ya watu wawili huku miguu yake inakokota chini kutokana na taabu ya maradhi aliyonayo. Basi akapanda kwenye mimbari akamshukuru Mwenyezi Mungu na kumtukuza kisha akasema: "Enyi watu ni maneno gani yaliyonifikia kutoka kwa baadhi yenu kuhusu uamirijeshi wa Usamah? Basi ikiwa mutakebehi kwa kumpa kwangu Usamah uamiri, kwa hakika mulikwishakebehi kumpa kwangu uamiri baba yake kabla ya mwanawe basi namuapa Mwenyezi Mungu kwa hakika yeye Zaid anastahiki kuwa amiri na bila ya shaka mwanawe baada yake anastahiki uamiri huo.

*(1) Tabaqat cha ibn Saad Juz 2 uk.190*
*(2) Tarikh Ibn Al-athir Juz 2 uk.317*
*(3) Tarikh At-Tabari Juz 3 uk. 226*
*(4) As-Siratul-Halabiyyah Juz. 3 uk.207*

Kisha Mtume (s.a.w.) akawa anawahimiza wafanye haraka akawaambia, "Liandaeni jeshi la Usamah, nendeni na jeshi la Usamah, upelekeni ujumbe wa Usamah." Alikariri jambo hilo mbele ya masikio yao na hali ya kuwa ni wazito. Kwa hakika tendo kama hili linanilazimisha nijiulize: "Ni kwa nini wamethubutu kuwa dhidi ya amri ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake? Na ni uasi gani huu kuhusu haki ya Mtume Mtukufu ambaye siku

zote alikuwa na hamu kubwa juu yao ili waongoke na ni mpole na mwenye huruma kwa waaminio?"

Sikufikiria kama ambavyo mtu mwingine naye hawezi kufikiria tafsiri nyingine inayokubalika juu ya uasi huu na ushupavu huu. Kama ilivyo kawaida wakati wa kusoma matukio kama haya yanayogusa heshima ya Masahaba kwa karibu au kwa mbali, najaribu kukanusha na kupuuza matukio kama haya, lakini haiwezekani kupinga na kupuuza kitu ambacho wameafikiana wanahistoria na wanahadithi katika Wanachuoni wa Kisunni na Kishia.

Bila shaka nilikuwa nimemuahidi Mola wangu kwamba nitakuwa muadilifu, sitang'ang'ania madhehebu yangu na sitathamini kisichokuwa kweli, na ukweli hapa ni mchungu kama isemwavyo, na Mtume (s.a.w.) alikwishasema kuwa; "Sema kweli hata kama ni dhidi ya nafsi yako na sema kweli japokuwa ni chungu".

Ukweli uliopo ndani ya tukio hili ni kwamba, masahaba hawa waliopinga uamiri wa Usamah walikwenda kinyume na amri ya Mola wao na waliikhalifu amri iliyo wazi isiyokuwa na shaka wala tafsiri nyengine, na wala hawana udhuru wowote kwa tendo lao hilo na wala hawana udhuru isipokuwa udhuru baridi wanaoutafuta baadhi ya watu ili kulinda heshima ya masahaba na *Salafus-Salih.* Mtu mwenye akili iliyo huru kwa vyovyote vile hawezi kuzikubali nyudhuru hizi, isipokuwa kama atakuwa miongoni mwa wasiofahamu wala kutumia akili au akawa miongoni mwa wale ambao chuki imewapofua macho yao.Watu ambao hawatenganishi baina ya faradhi ambayo ni wajibu kuitii na katazo ambalo ni wajibu kuliacha. Kwa hakika nilifikiri kwa muda mrefu ili labda nitawapatia udhuru unaokubalika kwa watu hawa lakini sikupata ufumbuzi.

Nilizisoma nyudhuru za Masunni juu ya watu hawa, kwamba wao walikuwa ndiyo wazee wa Kiquraish na ndiyo wakubwa zao, na walikuwa wa mwanzo kusilimu wakati ambapo Usamah ni mdogo na wala hakushiriki katika vita ili kuutukuza Uislamu kama vile vita vya Badri, Uhud, na Hunayn na hakuwa wa mwanzo kusilimu. (Usamah) alikuwa mdogo kwa umri wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu alipompa uamirijeshi, na maumbile ya nafsi za watu wote yanapinga iwapo miongoni mwao kuna

wazee na watu wazima (iweje) waongozwe na vijana, na ndiyo maana walipinga uamirijeshi wake na walimtaka Mtume (s.a.w.) ambadilishe kwa kumpa (uamiri mtu) mwingine miongoni mwa Masahaba wakubwa.

Kwa hakika huo ni udhuru usiotegemea dalili ya kiakili wala kisheria na wala haiwezekani kwa Muislamu yeyote aliyeisoma Qur'an na akazifahamu hukumu zake isipokuwa ataukataa udhuru huu ,kwani Mwenyezi Mungu mtukufu anasema:

> *"Na kile anachokupeni Mtume kichukueni na kile anachokukatazeni komeni (msikifanye)". (Qur: 59:7)*

Na amesema tena: *"Haiwi kwa Muumini mwanaume wala Muumini mwanamke pindi Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na hiyari katika shauri hilo, na yeyote mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake hakika amepotea upotofu ulio wazi kabisa". (Qur: 33:36.)*

Basi je ni udhuru gani watakaoukubali watu wenye akili baada ya aya hizi zilizowazi? Niseme nini juu ya watu ambao walimkasirisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hali ya kuwa wanafahamu kuwa Mwenyezi Mungu hughadhibika pindi Mtume anapoghadhibika, na hayo ni baada ya wao (Masahaba) kumtuhumu Mtume kuwa anaweweseka, na bila woga wakasema waliyoyasema mbele yake na wakazidisha zogo na kuhitilafiana hali ya kuwa Mtume ni mgonjwa mpaka akalazimika kuwafukuza toka chumbani mwake. Je yote haya hayakuwatosha?

Badala ya wao kujikosoa na kutubia kwa Mwenyezi Mungu na kumtaka awasamehe kwa hayo waliyoyafanya na wamuombe Mtume awaombee msamaha kama ilivyowafundisha Qur'an, kinyume chake waliongeza maji ndani ya unga kama mithali isemwavyo huko kwetu. Hivyo basi wakawa watovu wa nidhamu kwa Mtume aliyekuwa mpole kwao na mwenye huruma. Hawakumpa haki yoyote wala kutambua heshima yake, wakamkebehi kwa kumpa uamiri Usamah baada ya siku mbili tu toka walipomtuhumu kuwa anaweweseka. Kabla jeraha halijapona, walimlazimisha atoke akiwa katika hali waliyoieleza wana historia kuwa, alikuwa hawezi kutembea kutokana na uchungu wa maradhi, tena

anayumba akiwa kati ya watu wawili. Kisha Mtume (s.a.w.) akawa anaapa kuwa Usamah anastahiki kuwa amiri, na vile vile Mtume anaongeza kutujulisha kwamba; ni hao hao Masahaba waliompinga alipompa uamiri Zaid ibn Harith hapo kabla. Mtume aliyasema hayo kwa lengo la kutujulisha kwamba wao Masahaba wanayo mambo mengi na ushuhuda mwingi kuwa wao hawakuwa miongoni mwa wale ambao huwa hawaoni uzito katika nafsi zao kwa yale aliyoyakatia shauri Mtume na wakasalimu amri mara moja, bali walikuwa miongoni mwa wabishi wanaomjadili na kujifanya wanayohadhi ya kukosoa na kupinga hata kama watakwenda kinyume na hukumu za Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Na miongoni mwa mambo yanayotujulisha juu ya upinzani uliyowazi ni kwamba, licha ya mambo waliyoyashuhudia ikiwemo kukasirika kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na kuikabidhi bendera ya uamiri yeye mwenyewe kwa Mkono wake Mtukufu, na kuwaamuru wafanye haraka kuondoka, lakini wao walikuwa wazito na hawakwenda mpaka Mtume akafariki hali ya kuwa ndani ya moyo wake kuna huzuni juu ya umma wake uliofikwa na msiba ambao utaufanya umma wake urudi nyuma kwa visigino vyake na kuingia motoni na hawataokoka na moto huo isipokuwa wachache ambao Mtume wa Mwenyezi Mungu amewafananisha na kikundi kidogo cha ngamia waliosahauliwa na mchungaji.

Ikiwa tutataka kukifanyia mazingatio kisa hiki, basi bila shaka tutamkuta Khalifa wa pili ndiye chimbuko halisi la tukio hilo, kwa sababu baada ya kifo cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu yeye ndiye aliyekwenda kwa Khalifa Abubakr na akamtaka amuuzulu Usamah na kumbadilisha kwa kuweka amiri mwingine. Khalfa Abubakr akamwambia, *“Mama yako amekula hasara ewe mwana wa Khatab waniamuru nimuuzulu na hali ya kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu alimtawalisha?”*

*Taz: (1) Tabaqat al-kubra cha Ibn Saad Juz. 2 uk. 190*
*(2) Tarikh At-Tabari juz 3 uk. 226*

Vipi Umar hakutambua ukweli huu ambao Abubakr aliutambua? Au tuseme ndani ya jambo hili kuna siri nyingine ambayo haikutambulikana kwa wanahistoria? Au tu ni kwamba wanahistoria ndiyo waliouficha ukweli kwa kulinda heshima ya Umar kama ilivyo kawaida yao na kama

walivyoibadilisha ibara ya *Anaweweseka* pakawekwa tamko *Maradhi yamemzidia?*

Kinachonishangaza kwa Masahaba hawa waliomkasirisha Mtume siku ya Al-hamisi na kumtuhumu kuweweseka na kuchanganyikiwa na wakasema, "Kinatutosha kitabu cha Mwenyezi Mungu." Na wakati huo huo kitabu cha Mwenyezi Mungu kinawaambia ndani ya aya zake kwamba: *"Waambie ikiwa ninyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni". (Qur. 3:31)*

Eti kama kwamba wao (wanajiona kuwa) wanakijua mno kitabu cha Mwenyezi Mungu na hukumu zake kuliko yule aliyeteremshiwa. Ndiyo maana baada ya siku mbili tu tangu ule msiba wenye machungu na ni kabla ya siku mbili tu Mtume afariki wanamkasirisha zaidi walipomkebehi kwa kumpa Usamah uamiri na wala hawakutii amri yake alipowataka watoke waungane na jeshi la Usamah. Katika ule msiba wa mwanzo (uliotokea siku ya Al-hamisi) Mtume alikuwa mgonjwa amelala kitandani, basi katika msiba huu wa pili, Mtume alilazimika atoke hali kafunga kitambaa kichwani, amejifunika shuka na anayumba kati ya watu wawili, miguu yake inakokota chini. (Mtume) akawahutubia hotuba kamili akiwa juu ya mimbari, hotuba ambayo alianza kwa kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kumtukuza ili awajulishe kwamba yeye hakuwa anaweweseka. Kisha akawatambulisha kufahamu kwake kebehi yao na hatimaye akawakumbusha tukio jingine walilomkebehi miaka minne iliyopita, basi je baada ya yote hayo bado tu wanaamini kuwa Mtume anaweweseka au kwamba maradhi yamemzidia kiasi kwamba hawezi kufahamu anachokisema?

Ewe Mwenyezi Mungu umetakasika na umetukuka, ni vipi watu hawa wanafanya ushupavu mbele ya Mtume wako na wala hawaridhii na maamuzi aliyoyapitisha, na wanampinga kwa nguvu zote bila kusita hata alipowaamuru kuchinja na kunyoa mara tatu hakuna yeyote aliyekubali miongoni mwao. Na katika tukio jingine walimvuta kanzu yake na kumzuia asimswalie Abdallah ibn Ubayyi wakamwambia, "Hakika Mola wako amekukataza kuwasalia wanafiki!!". Kama kwamba wao ndio wanaomfundisha kile alichoteremshiwa wakati ambapo (Ewe Mwenyezi Mungu) umesema ndani ya Qur'an yako kuwa:

*"Na tumekuteremshia ukumbusho ili uwabainishie mambo yaliyoteremshwa kwao." (Qur.16:44)*

Pia umesema:

*"Hakika sisi tumekuteremshia kitabu kwa haki ili uhukumu baina ya watu kwa yale aliyokuonesha Mwenyezi Mungu". (Qur. 4:105)*

Na umesema na kauli yako ni ya kweli:

*"Kama tulivyomtuma Mtume kwenu anayetokana nanyi anakusomeeni aya zetu na kuwatakaseni na kuwafundisheni kitabu na hekima na anawafundisheni mambo mliyokuwa hamyajui". (Qur. 2:151).*

Watu hawa wanashangaza, wanajiweka kwenye daraja ya juu kuliko ya Mtume, na wakati mwingine hawatii amri yake na mara nyingine wanamtuhumu kuwa anaweweseka na kuzidisha zogo mbele yake bila ya heshima wala adabu. Na kuna wakati mwingine wanampinga kwa kumpa uamiri Zaid ibn Harith na baada yake alimpa uamiri mwanae Usamah ibn Zaid. Ni mashaka gani yatakayobakia kwa wenye kutafiti baada ya yote haya kwamba Mashia wako kwenye haki wanapoidhibiti mienendo ya baadhi ya Masahaba kwa alama ya kuuliza na wakawa wakali kutokana na mienendo hiyo kwa ajili tu ya kumheshimu na kumpenda Mtume na watu wa nyumba yake?

Mimi sikutaja mengi ambayo (Masahaba) walikwenda kinyume, halifu isipokuwa mambo manne au matano na nimefanya hivyo kwa sababu ya kufupisha na hayo niliyoyataja yawe ni mfano tu. Lakini wanachuoni wa Kishia wamehifadhi mamia ya mambo ambayo Masahaba walikwenda kinyume na maelekezo ya wazi. Wanachuoni hawa Wakishia hawakutoa dalili isipokuwa zile zilizoandikwa na wanachuoni wa Kisunni ndani ya Sihahi zao na Musnad zao.

Kwa hakika ninapoeleza baadhi ya mambo waliyotenda baadhi ya Masahaba kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, nabakia ni mwenye kushangaa tena mwenye kuchanganyikiwa. Kinachonishangaza si tabia za Masahaba tu kumwelekea Mtume, lakini mtazamo wa wanachuoni wa

Kisunni ambao siku zote unatuonesha kuwa, Masahaba wote wako kwenye haki, na haiwezekani kuwakosoa kwa namna yoyote ile. Kwa ajili hiyo wanamzuia mwenye kutafiti kuufikia ukweli na anabakia anahangaika ndani ya fikra zinazopingana.

Zaidi ya hayo yaliyotangulia, ninaleta baadhi ya mifano ambayo itatupatia picha halisi juu ya Masahaba hawa na hapo tutaufahamu msimamo wa Mashia kuhusu Masahaba.

Bukhari ameandika ndani ya sahihi yake *Juz. 3 uk. 47* mlango wa subira juu ya maudhi, na kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemwayo *"Bila shaka wenye kusubiri watatekelezewa malipo yao"* kutoka katika kitabul-adabi amesema, "Ametusimulia Aa'mash amesema, Nimemsikia Shaqiq anasema, Abdallah amesema, Mtume (s.a.w.) aligawa mgao kama baadhi ya migao aliyokuwa akigawa, basi mtu mmoja miongoni mwa maansari akasema, Namuapa Mwenyezi Mungu, hakika mgao huu haukukusudiwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Mimi nikasema, Kwa hakika mimi nitamwambia jambo hili Mtume (s.a.w.), basi nikamfuata Mtume hali ya kuwa yuko kati ya Masahaba wake nikamkabili nikamwambia. Jambo hili lilimuumiza Mtume, uso wake ulibadilika na akakasirika mpaka nikatamani laiti nisingemwambia, kisha Mtume akasema kwa hakika Musa aliudhiwa zaidi kuliko hivyo lakini alisubiri."

Vile vile Bukhari ameandika katika kitabu hicho hicho yaani *Kitabul-Adab katika Babut-Tabassum Wad-dhahak,* amesema, "Ametusimulia Anas ibn Malik amesema, nilikuwa natembea pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) hali yakuwa amejifunika shuka ya Kinajirani yenye pindo nene, basi bedui mmoja akakutana na Mtume akamvuta shuka yake kwa nguvu sana, Anas akasema: Niliangalia kwenye bega la Mtume (s.a.w.) nikaliona limeathirika kutokana na pindo la shuka kwa sababu ya kuvutwa kwa nguvu sana alikofanya yule Bedui, kisha bedui yule akasema, Ewe Muhammad toa amri nipewe mali ya Mwenyezi Mungu uliyonayo, basi Mtume alimgeukia (kumtazama) kisha akacheka halafu akaamuru apewe."

Kama ambavyo Bukhari ameandika ndani ya *Kitabul-Adab* katika mlango uitwao, *Asiyewakabili watu kwa lawama* Amesema: "Bibi Aisha

amesema, Mtume (s.a.w.) alifanya jambo fulani na akaliruhusu (lifanywe), baadhi ya watu hawakulifanya. Habari hiyo ikamfikia Mtume (s.a.w.), basi akatoa hotuba akamtukuza Mwenyezi Mungu kisha akasema, Wana nini watu walioacha kufanya kitu ninachokifanya mimi, namuapa Mwenyezi Mungu kwa hakika mimi namfahamu zaidi Mwenyezi Mungu kuliko wao nami namcha zaidi kuliko wao!...”

Mimi naamini kwamba wanaoitakidi kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) matamanio yanampindisha na kumpotosha njia ya haki, akagawa mgao ambao hakusudii radhi ya Mwenyezi Mungu bali anafuata matamanio yake na vile apendavyo, na wale ambao wanaacha kufanya mambo aliyoyafanya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hali yakuwa wanaitakidi kuwa wao ni wacha Mungu mno na wanamfahamu zaidi Mwenyezi Mungu kuliko Mjumbe wake, kuna baadhi ya watu wamewaweka (Masahaba) katika daraja la Malaika na kuhukumu kwamba wao ni viumbe bora baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kwamba Waislamu wanatakiwa kuwafuata na kuziandama sera zao, si kwa lolote isipokuwa tu kwa kuwa ni Masahaba wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Lakini watu hawa hawastahiki kabisa utukufu huo.

Na hali hii (kwa kweli) inapingana na Masunni ambao hawamsalii Mtume (s.a.w.) na kizazi chake isipokuwa huongeza juu yao Masahaba wote, wakati ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu amekwisha kukitambulisha cheo cha Mtume na kizazi chake, na akawapa daraja yao kisha akawaamuru (Masahaba) wamsalie Mtume wake na Watu wa nyumba yake waliotakasika ili kuwafanya wawe watiifu na wanyenyekevu na waitambue daraja ya Watu hawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Basi (kama ni hivyo) ni kwa nini sisi tunawaweka (Masahaba) juu kuliko daraja yao na tunawalinganisha na watu ambao Mwenyezi Mungu amewatukuza na kuwaboresha juu ya walimwengu wote?

Hebu niwache nihitimishe (kwa kueleza) kwamba, Banu Ummayyah na Banu Abbas ambao waliwafanyia uadui Watu wa Nyumba ya Mtume, wakakawatenga, wakawatawanisha na kuwauwa wao na wafuasi wao, waliitambua maana halisi ya daraja na ubora mkubwa wa Ahlul-Bait. Basi ikiwa Mwenyezi Mungu haikubali sala ya Muislamu ila kwa kuwasalia wao, ni kwa nini basi wanautetea uadui wao na kupotoka kwao

dhidi ya Ahlul-Bait? Na kwa ajili hiyo utawaona wamewalinganisha Masahaba kwa Ahlul-Bait (katika kuwasalia) ili kuwapotosha watu waone kuwa Masahaba na Ahlul-Bait ni sawa tu katika daraja. Na hasa iwapo tutafahamu ya kwamba mabwana wao na wakubwa wao ni baadhi ya Masahaba ambao waliwaajiri watu wanyonge wa akili miongoni mwa Masahaba wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu au miongoni mwa Tabiina ili tu wasimulie hadithi za uongo zinazohusu fadhila za Masahaba na hasa wale waliofaulu kukalia kiti cha Ukhalifa na wakawa moja kwa moja ndiyo sababu ya wao Banu Umayyah na Banu Abbas kuufikia utawala na kufanya wapendavyo dhidi ya Waislamu. Historia ni shahidi mwema juu ya haya niyasemayo, kwani Umar ibn Al-Khatab ambaye ni mashuhuri kwa kuwaadhibu magavana wake kwa kiasi cha dhana tu, tunamuona ni mpole mno kwa Muawiyyah ibn Abi Sufiyan wala hamuadhibu kabisa. Na huyu Muawiyyah alitawalishwa na Abu Bakr, na Umar alipokuja akamkubali kwa muda wote wa uhai wake na wala hakuthubutu hata kumkemea au kumlaumu licha ya mashitaka ya watu wengi waliokuwa wakienda kumshitakia kuhusu Muawiyah na wakimwambia, “Kwa hakika Muawiyah anavaa dhahabu na hariri vitu ambavyo Mtume wa Mwenyezi Mungu ameviharamisha kwa wanaume.” Basi Umar alikuwa akiwajibu, “Mwacheni kwa kuwa yeye ni Kisra wa Waarabu.” Hivyo basi Muawiyah aliendelea kutawala zaidi ya miaka ishirini na hakuna yeyote aliyethubutu kumkosoa wala kumuuzulu. Na alipotawalia Uthman Ukhalifa wa Waislamu, alimuongezea (Muawiyah) madaraka mengine yaliyomuwezesha kuupora utajiri wa Waislamu, na kuchukua uongozi kwa nguvu, kisha kufanya apendavyo na kuwalazimisha Waislamu wale kiapo cha utii kwa mwanawe Yazid aliyekuwa muovu na mlevi. Hiki ni kisa kingine kirefu ambacho sikukikusudia kukieleza kwa urefu ndani ya kitabu hiki, lakini jambo muhimu ni kutambulisha mwenendo wa masahaba hawa ambao walikalia Ukhalifa na moja kwa moja wakaandaa kusimama kwa dola ya Bani Umayyah ili kuwaridhisha Maquraish ambao hawakutaka Utume na Ukhalifa uwe ndani ya (nyumba ya) Bani Hashim.

Kwa maelezo zaidi soma:

*(1) Al-Khilafatu Wal-Mulk; Abul Aala-al-Maududi.*
*(2) Yaumul-Islam: Ahmad Amin.*

Kwa hakika dola ya Banu Umayyah ina haki bali ni wajibu wake iwashukuru wale wote ambao waliiandalia utawala, na shukurani ya chini kabisa ni kuajiri wapokezi wa hadithi wa kulipwa watakaosimulia fadhila za mabwana zao na wakati huo huo kuwakweza zaidi kuliko Makhasimu wao ambao ni Ahlul-Bait kwa sifa na ubora wa aina mbali mbali ambao Mwenyezi Mungu anashuhudia kuwa, (sifa hizo na ubora huo waliopewa hao Masahaba) iwapo utaufanyia utafiti kwa mujibu wa dalili za kisheria, kiakili na kimantiki, hapana chochote cha kutajwa kitakachobakia, isipokuwa tu kama akili zetu zitakapokuwa na kasoro tukaamini mambo yanayopingana.

Kwa mfano, tunasikia mengi juu ya uadilifu wa Umar ambao umevuka mpaka hadi ikasemwa "Umekuwa muadilifu mno mpaka umelala". Na imesemwa pia kuwa, "Umar amezikwa wima ili uadilifu wake usijekufa pamoja naye". Basi yalivyo ya Umar kuhusu uadilifu unaweza kusimulia, ukasimulia-ukasimulia.....hulaumiwi.

Historia sahihi inatueleza kwamba, katika mwaka wa ishirini Hijiriyah ilipomlazimu kutoa (kugawa), yeye hakufuata Sunna ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, wala hakufuata mipaka yake kwani Mtume (s.a.w.) aliweka usawa baina ya Waislamu wote katika mgawo huo hakumboresha yeyote juu ya mwingine, na Abubakr alimfuata Mtume kwa jambo hilo muda wote wa Ukhalifa wake. Lakini Umar ibn Al-Khatab alianzisha njia mpya akawaboresha Waliosilimu mwanzo juu ya wengine, na akawaboresha Muhajirina miongoni mwa Maquraishi juu ya Muhajirina wengine. Akawatanguliza Muhajirina wote juu ya Maansari wote, na aliwafadhilisha Waarabu juu ya wasiokuwa Waarabu na alimboresha mtu huru juu ya mtumwa  Si hivyo tu bali akaliboresha kabila la Mudhar juu ya kabila la Rabiah, akafaradhisha kabila la Mudhar wapewe mia tatu na Rabia mia mbili  na aliwaboresha kabila la Ausi juu ya Khazraj.

*Futubul-Bul-Dan uk. 437.*

Basi uko wapi usawa na uadilifu Ewe mwenye akili? Na tunasikia juu ya elimu ya Umar ibn Al-Khatab mambo mengi yasiyo na idadi mpaka imesemwa kwamba yeye ndiye mjuzi mno kuliko Masahaba (wengine) na imesemwa kuwa yeye alimuwafiki Mola wake katika mengi miongoni

mwa maoni yake ambayo Qur'an ikishuka kuyaunga mkono katika aya nyingi ambazo Umar na Mtume (s.a.w.) walitofautiana.

Lakini historia sahihi inatujulisha kwamba Umar hakuiafiki Qur'an hata baada ya kushuka kwake, pale alipoulizwa na Sahaba mmoja katika zama za Ukhalifa wake akasema: "Ewe Amirul-Muuminina mimi nimepatwa na janaba lakini sikupata maji", Umar akamwambia, "Usisali". Hapo Ammar ibn Yasir alilazimika kumkumbusha kutayamam, lakini Umar hakukinaika kwa hilo na akamwambia Ammar, "Tutakubebesha jukumu kwa yale uliyojibebesha."

Basi yu wapi Umar yeye na aya ya kutayamam iliyoteremshwa ndani ya kitabu cha Mwenyezi Mungu, na iwapi elimu yake na Sunna ya Mtume (s.a.w.) ambaye amewafundisha namna ya kutayammam kama ambavyo amewafundisha (namna ya) kutawadha. Na Umar yeye mwenyewe mara nyingi anakiri katika matukio kadhaa kwamba yeye si mjuzi, bali watu wote ni wajuzi kuliko yeye hata yule mwanamke mwenye mimba, na akisema mara nyingi, "Lau si Ali, basi Umar angeliangamia". Na alifikwa na mauti akafa na hakuwahi kutambua hukumu ya "Al-Kalalah" ambayo alihukumu kwa hukumu nyingi tofauti tofauti kama inavyoshuhudia historia.

Vile vile tunasikia mambo mengi juu ya uhodari wa Umar na ushujaa wake na nguvu zake mpaka imesemwa kwamba Maquraishi waliogopa pindi Umar aliposilimu, na nguvu ya Waislamu iliimarika kwa kusilimu kwake. Na imesemwa kwamba Mwenyezi Mungu aliupa nguvu Uislamu kupitia kwa Umar ibn Al-Kataab, na imesemwa kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hakudhihirisha wazi wito wake isipokuwa baada ya kusilimu Umar.

Lakini historia thabiti na sahihi haituoneshi chochote juu ya uhodari huu na ushujaa, wala hakuna mtu yeyote miongoni mwa watu mashuhuri au hata watu wa kawaida ambao Umar ibn Khataab aliwauwa katika makabiliano ya ana kwa ana au katika vita kama vile Badr au Uhud au Khandaq na vinginevyo, bali kinyume chake ndiyo sahihi, na historia inatusimulia kwamba, yeye alikimbia pamoja na wengine waliokimbia katika vita ya Uhud na vile vile alikimbia siku ya (vita ya) Hunain. Pia

Mtume (s.a.w.) alimtuma ili akalete ushindi katika mji wa Khaibar lakini alirudi bila ushindi na hata katika vikosi vidogo vidogo ambavyo alishiriki hakuwa kiongozi bali aliongozwa na cha mwisho ni kile cha Usamah ambacho yeye alikuwa mwenye kuamrishwa chini ya uongozi wa kijana Usamah ibn Zaid.

Basi yako wapi madai ya uhodari na ushujaa wa Umar (ukilinganisha) na ukweli huu unaoonekana wazi? Tunasikia mambo mengi juu ya ucha Mungu wa Umar na namna alivyokuwa akilia kwa kumuogopa Mwenyezi Mungu, mpaka imesemwa kwamba yeye alikuwa anakhofu kuwa Mwenyezi Mungu atamuadhibu japo itatokea nyumbu akaanguka njiani kutokana na (Umar) kutomtengenezea nyumbu huyo njia nzuri ya kupita huko Iraq.

Lakini masimulizi ya historia yaliyothibiti yanatueleza kwamba, Umar alikuwa mkali tena mgumu (wa tabia) hahisi ubaya na haogopi. Alikuwa akimpiga yeyote aliyemuuliza suali juu ya aya moja tu ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu mpaka humtoa damu pasina kosa lolote alilolifanya mtu huyo. Bali zaidi ya hapo mwanamke akiharibu ujauzito wake kwa kiasi tu cha kumuona Umar kutokana na woga na tisho alilokuwa nalo Umar.

Na ni kwa nini Umar hakuona vibaya pale alipounyoosha upanga wake kumuonya kila yule atakayesema kuwa (Mtume) Muhammad amekufa, na akaapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa Mtume hakufa bali kaenda kuzungumza na Mola wake kama alivyofanya Musa ibn Imran, na akaonya kuwa yeyote atakayesema kuwa Mtume amekufa ataikata shingo yake. Basi ni kwanini asimukhofu Mwenyezi Mungu (kutokana na tendo hili)?

Na ni kwanini asione kuwa ni vibaya wala asimukhofu Mwenyezi Mungu juu ya onyo lake la kutaka kuiunguza kwa moto nyumba ya Fatmah Az-Zahra iwapo tu watu waliopinga *Baia* ya Abu Bakr, hawatatoka ndani ya nyumba hiyo kwenda kufanya *Baia*. (Umar hakujali) haliyakuwa alikwisha ambiwa kuwa ndani ya nyumba hiyo yumo Fatmah, basi yeye alijibu akasema, “Hata kama yumo Fatmah”.

Umar alithubutu kuwa dhidi ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna

ya Mtume wake, akahukumu katika zama za Ukhalifa wake hukumu zinazokwenda kinyume na Qur'an na Sunnah Tukufu ya Mtume.

Ukowapi huo uchamungu wake ukiulinganisha na matukio ya kweli tena yanayoumiza moyo Enyi! waja wema wa Mwenyezi Mungu?

Kwa hakika nimemtaja Sahaba huyo mkubwa tena mashuhuri kama mfano tu, na nimeacha mambo mengi kusudi nisirefushe maelezo, lakini lau ningetaka kufanya kwa upana ningejaza vitabu vingi, bali kama nilivyosema ninataja hivi kama mfano na siyo yote.

Maelezo niliyoyataja ni sehemu ndogo tu inayotupatia dalili iliyowazi juu ya hali halisi ya Masahaba (namna walivyo) na pia msimamo unaopingana wa wanachuoni wa Kisunni, kwani wao wanawazuia watu kuwakosoa na kuwatilia mashaka na wakati huo huo ndani ya vitabu vyao wanasimulia mambo yanoyoleta shaka na tuhuma kwa Masahaba. Na lau wanachuoni wa Kisunni wasingetaja mfano wa mambo kama haya wazi wazi, yanayochafua na kutia doa heshima ya Masahaba katika uadilifu (usemwao) kuwa wanao, hakika wangetupumzisha na taabu hii ya mkanganyiko.

Kwa hakika mimi naukumbuka mkutano wangu pamoja na mwanachuoni mmoja katika mji Mtukufu wa Najaf aitwaye Sayyid Asad Haidar ambaye ndiye mtunzi wa kitabu kiitwacho, *"Al-ImamuS-Sadiq Wal-Madhahibul-Arbaa"*. Katika mkutano huo tulikuwa tukizungumzia juu ya Usunni na Ushia, basi akanisimulia kisa cha mzazi wake ambaye alipokuwa Hijja alikutana na mwanachuoni wa Kitunisia miongoni mwa wanachuoni wa Zaitunah. Tukio hili lilitokea miaka hamsini iliyopita. Baina yao kulifanyika majadiliano kumuhusu Amirul-Muuminina Ali ibn Abi Talib, ambapo yule mwanachuoni wa Kitunisia alikuwa akimsikiliza mzazi wangu akitaja dalili za Uimamu wa Imamu Ali (a.s.) na kustahiki kwake Ukhalifa, akataja dalili nne au tano. Na alipokwisha zitaja yule mwanachuoni wa Zaitunah alimuuliza mzazi wangu, "Je, unazo dalili zingine zisizokuwa hizi?" Akasema: "Hapana." Basi yule Mtunisia akasema, "Hebu toa *'tasbihi'* yako na uanze kuhesabu." Basi yule mwanachuoni wa Kitunisia akaanza kuzitaja dalili zinazohusu Ukhalifa wa Imam Ali (a.s.) mpaka zikafikia mia moja, ambazo mzazi wangu alikuwa hazifahamu. Naye

Sheikh Asad Haidar aliongeza akasema, *"Lau Ahlul-Sunnah Wal-Jamaa* watasoma ndani ya vitabu vyao, basi wasingekuwa na usemi isipokuwa ule tuusemao sisi na tofauti hii ingemalizika tangu siku nyingi."

Naapa kwamba huu ni ukweli usiokwepeka iwapo tu mtu atakuwa huru kutokana na chuki yenye kupotosha na kibri chake na kisha akazirejea dalili zilizowazi.

# 1). MAONI YA QUR'AN KUHUSU MASAHABA.

Kabla ya yote sina budi nieleze kwamba bila shaka Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani ya kitabu chake Kitukufu mahala pengi amewasifu Masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ambao walimpenda Mtume, wakamfuata na kumtii bila ya tamaa na hawakupinga wala kujikweza, wala kufanya majivuno, bali walimfuata kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi hao Mwenyezi Mungu amewaridhia nao wamemridhia na sifa hii hapati isipokuwa yule anayemuogopa Mola wake.

Kundi hili la Masahaba ndilo lile ambalo Waislamu wanatambua heshima yao kutokana na msimamo wao na matendo yao walipokuwa na Mtume (s.a.w.). Waislamu wanawapenda, wanawaheshimu na kukitukuza cheo chao na kuwaombea radhi kila wanapowataja.

Utafiti wangu (nilioufanya) hauhusiani na kundi hili la Masahaba ambao wao ndiyo kitovu cha heshima na utukufu kwa Masunni na Mashia, kama ambavyo utafiti wangu hauhusu kundi la Masahaba ambao ni Mashuhuri kwa unafiki na ambao wanalaaniwa na Waislamu wote Sunni na Shia.

Lakini uchunguzi wangu unalihusu kundi hili la Masahaba ambao Waislamu wamekhitilafiana juu yao, na Qur'an ilishuka kuwakemea na kuwaonya katika baadhi ya matukio, na ndiyo wale ambao Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliwahadharisha katika minasaba mingi au alionywa kutokana nao.

Naam, ikhtilafu iliyopo baina ya Shia na Sunni iko katika kundi hili la Masahaba, kwani Mashia wanayakosoa maneno yao na vitendo vyao na wanautilia mashaka uadilifu wao, wakati ambapo *Ahlus-Sunna Wal-Jamaa* wanawatukuza bila kujali mambo yaliyo kinyume (cha sheria ya dini) yaliyothibiti kuwa waliyatenda.

Kwa hiyo basi utafiti wangu unahusika na kundi hili la Masahaba, ili kwa kupitia utafiti huu niweze kuufikia ukweli ulivyo au sehemu ya ukweli huo.

Nimeyasema haya ili mtu yeyote asijedhani kuwa mimi nimezipuuza zile aya ambazo zimewasifu Masahaba wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na nikazionesha zile tu zinazowapinga, bali mimi kwa hakika katika utafiti wangu nimegundua kwamba ziko aya zinazowasifu, ndani yake kuna maana ya lawama au kinyume chake.

Na huenda sitaikalifisha nafsi yangu kwa juhudi kubwa kama nilivyofanya katika kipindi cha miaka mitatu ya uchunguzi huu, bali nitatosheka kwa kutaja baadhi ya Aya tu ziwe mfano kama ilivyo kawaida, na hivi ni kwa ajili ya (kutaka) kufanya mukhtasari, na ni juu yao wale watakao upana zaidi kufanya juhudi ya utafiti, na kulinganisha kama nilivyofanya mimi ili kuongoka kwao kuwe kumetokana na juhudi na mchujo wa fikra, kitu ambacho Mwenyezi Mungu anakitaka kipatikane kwa kila mtu na ndivyo hali halisi inavyotaka ili mtu apate kukinaika barabara na asije akababaishwa na upepo mkali. Inaeleweka moja kwa moja kwamba uongofu unaopatikana kwa kukinai nafsi ni bora mno kuliko ule unaopatikana kutokana na athari za nje.

Mwenyezi Mungu amesema alipokuwa akimsifu Mtume wake: *"Na Mola wako amekukuta ukiwa unahangaika akakuongoza." (Qur. 93:7)* Yaani: Amekukuta unaitafuta haki akakuongoza kwenye haki. Na amesema tena: *"Na wale waliofanya juhudi kwa ajili yetu basi tutawaongoza kwenye njia zetu" (Qur. 29:69).*

### i). Muhammad Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

Mfano wa kwanza juu ya jambo hilo ni ile aya isemayo: *"Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu."*

Mwenyezi Mungu Amesema:

> *"Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na walio pamoja naye wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao. Utawaona wanarukuu na kusujudu wakitafuta fadhila na radhi*

*za Mwenyezi Mungu. Alama zao ziko katika nyuso zao kwa athari ya kusujudu. Huu ndio mfano wao katika Torati. Na mfano wao katika Injili ni kama mmea uliotoa chipukizi lake, kisha ukalitia nguvu ukawa mnene, ukasimama sawa juu ya ubuwa wake, ukawafurahisha wakulima, ili kuwakasirisha kwa ajili yao makafiri. Mwenyezi Mungu amewaahidi walioamini na wakatenda mema miongoni mwao msamaha na ujira mkubwa." (Qur. 48:29)*

Aya hii tukufu yote inamsifu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na Masahaba walio pamoja naye, ambao wamesifika kwa sifa alizozitaja Mwenyezi Mungu kuwa wao ni wakali mbele ya makafiri na ni wenye huruma wao kwa wao. Aya hii Tukufu inaendelea katika kuwasifu watu hawa na kutaja sifa zao mpaka inamalizika kwa kueleza ahadi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa, atatoa msamaha na malipo makubwa siyo kwa masahaba wote waliotajwa lakini kwa baadhi yao ambao wameamini na kutenda mema. Basi lile tamko lisemalo: *"Miongoni mwao"* alilolitaja Mwenyezi Mungu Mtukufu linajulisha kuwa ni, *Baadhi* na limeweka wazi kwamba miongoni mwao Masahaba msamaha wa Mwenyezi Mungu na radhi zake hawatavipata. Pia limejulisha kuwa baadhi ya Masahaba hawakuwa na sifa ya imani na matendo mema. Hivyo basi aya hii ni miongoni mwa zile aya zinazowasifu na kuwakosoa kwa wakati mmoja, kwani imekisifu kikundi fulani cha Masahaba na kuwakosoa wengine.

Jambo la kusikitisha na kuhuzunisha ni kwamba watu wengi wanaitolea ushahidi aya hii Tukufu juu ya kuhifadhika kwa Masahaba kutokana na makosa na kwamba ni waadilifu na kwanaifanya aya hii ni hoja dhidi ya Shia, wakati ambapo aya hii ni hoja iliyo wazi dhidi yao na inawaunga mkono Mashia katika kuwagawa Masahaba kuwa kuna Sahaba aliyeamini kisawasawa na akawa mkamilifu wa imani na matendo mema, basi Mwenyezi Mungu akamuahidi msamaha na radhi yake na malipo makubwa. Na kuna Sahaba mwingine aliyesilimu na imani ikawa haijaingia kisawasawa katika moyo wake, au aliamini na kutenda mema katika zama za uhai wa Mtume s.a.w, lakini huyo huyo aligeuka kinyume nyume, basi huyu hawezi kumdhuru Mwenyezi Mungu kwa lolote lile, na Mwenyezi Mungu amemuonya kuwa matendo yake yataporomoka kwa kiasi tu cha kupaza sauti yake juu ya sauti ya Mtume. Basi je, unadhani ana hali gani yule aliyemuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake na akapotea

upotovu ulio wazi? Kisha unamfikiriaje yule ambaye hakuhukumu kwa hukumu aliyoteremshiwa au alibadilisha hukumu ya Mwenyezi Mungu akahalalisha kile alicho kiharamisha Mwenyezi Mungu na akaharamisha kile alichokihalalisha Mwenyezi Mungu na akafuata maoni yake na matamanio yake katika yote hayo?

**ii). Aya ya kugeuka nyuma:**

Mwenyezi Mungu anasema:

*"Na Muhammad hakuwa ila ni Mtume tu. Wamekwishapita kabla yake Mitume. Je, akifa au akiuawa ndiyo mtageuka kurudi nyuma? Na atakayegeuka na akarudi nyuma huyo hatamdhuru kitu Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu atawalipa wanaomshukuru. (Qur. 3:144)*

Aya hii tukufu iko wazi mno kwamba Masahaba watageuka nyuma baada tu ya kufariki Mtume, na hawatabakia ila wachache. Kama ilivyotambulisha aya katika maelezo ya Mwenyezi Mungu juu yao yaani: Wenye kubakia ambao hawatageuka ndiyo wale wenye kushukuru, kwani wenye kushukuru hawawi ila ni wachache kama inavyotujulisha kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo:

*"Ni wachache katika waja wangu wanaoshukuru". Qur. 34:13*

Vile vile ni kama zilivyotambulisha hadithi Tukufu za Mtume ambazo zinafasiri maana ya kugeuka na ambazo tutazitaja baadhi yake. Na iwapo Mwenyezi Mungu Mtukufu katika aya hii hakubainisha adhabu ya wale watakaogeuka nyuma akatosheka kwa kuwasifu wenye kushukuru ambao watastahiki malipo yake, lakini kinachofahamika moja kwa moja ni kwamba wenye kugeuka hawastahiki malipo mema ya Mwenyezi Mungu na msamaha wake, ni kama alivyotilia mkazo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) katika hadithi nyingi, hapo baadaye tutazichambua baadhi yake ndani ya kitabu hiki apendapo Mwenyezi Mungu.

Na haiwezekani kufasiri aya hii tukufu kuwa inawahusu Tulaiha, Sajah na As-wad-Al-ansa, eti tu kwa kutaka kulinda heshima ya Masahaba, kwani watu hawa waligeuka wakaritadi kutoka kwenye Uislamu na wakadai

Utume katika uhai wa Mtume (s.a.w.) naye aliwapiga vita akawashinda. Kama ambavyo haiwezekanani kuifasiri aya tukufu kuhusu tukio la Malik ibn Nuwairah na wafuasi wake ambao walizuia kutoa zaka katika zama za Abu Bakr kutokana na sababu nyingi tu na miongoni mwa hizo ni hizi zifuatazo:

Kwanza, walizuia zaka na hawakumpa Abu Bakr ili kufanya subira mpaka wafahamu ukweli wa mambo kwani wao walikuwa wamehiji na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika Hija ya kuaga na walimpa Baia yao Imam Ali ibn Abi Talib kule Ghadir Khum baada tu ya Mjumbe wa Mwenyezi kumsimika Ukhalifa, ambapo Abu Bakr mwenyewe alikuwa amempa Imam Ali baia yake. Mara ghafla (Malik na watu wake) wakashitukizwa na Mjumbe wa Khalifa Abu bakr aliyewapasha habari ya kifo cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na wakati huo huo akawataka watoe zaka kwa niaba ya Khalifa mpya ambaye ni Abu bakr. Kisa hiki ni kirefu na historia haikielezi kwa undani kwa kulinda heshima ya masahaba, lakini sehemu tu ya kisa hicho ni kwamba: Malik na wafuasi wake walikuwa Waislamu hilo lilishuhudiwa na Umar na Abu Bakr mwenyewe, vile vile idadi kadhaa miongoni mwa Masahaba ambao wote walimkemea Khalid ibn Walid kwa tendo lake la kumuua Malik ibn Nuwairah. Historia nayo inashuhudia kwamba Abu Bakar alimlipa Mutamim ambaye ni ndugu wa Malik fidia kutoka katika Baitul-mali ya Waislamu na akamwomba radhi kutokana na mauaji yale. Na inafahamika kwamba, mwenye kuritadi akatoka katika Uislamu ni wajibu kumuuwa na wala halipwi fidia kutoka katika Baitul-mali na wala haombwi radhi kutokana na kuuawa kwake.

Jambo la muhumu ni kwamba ile aya ya kugeuka, inawakusudia Masahaba waliokuwa wakiishi na Mtume (s.a.w.) hapo mjini Madina, na inawaashiria kugeuka kwao mara tu baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.) bila kutoa mwanya. Nazo hadithi za Mtume (s.a.w.) zinabainisha wazi juu ya jambo hilo kitu ambacho kinaondoa shaka na tutaliangalia suala hili hivi punde Mwenyezi Mungu apendapo na historia ni shahidi bora juu ya kugeuka kulikotokea baada ya kifo cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.). Mwenye kuyasoma matukio yaliyotokea baina ya Masahaba wakati wa kifo cha Mtume basi haitabakia kwake shaka yoyote juu ya kugeuka huko kulikotokea miongoni mwao na hakuna aliyesalimika isipokuwa wachache.

**iii). Aya ya Jihadi:**

Mwenyezi Mungu anasema:

> *"Enyi mlioamini mna nini mnapoambiwa: Nendeni katika njia ya Mwenyezi Mungu, mnajitia uzito katika ardhi? Je, mmeridhia maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kulinganisha na ya akhera ni chache. Kama hamuendi atakuadhibuni adhabu chungu na atawaleta watu wengine wala ninyi hamtamdhuru chochote, na Mwenyezi Mungu ni muweza wa kila kitu." (Qur. 9:38-39)*

Pia aya hii iko wazi kwamba, Masahaba walikuwa wazito kwenda kwenye Jihad na walichagua maisha ya dunia licha ya wao kufahamu kuwa ni starehe ya muda mfupi mpaka wakalazimisha Mwenyezi Mungu Mtukufu awakemee na awaonye kwa adhabu kali na kubadilishwa mahali pao waje waumini wenye kusadiki.

Onyo hili la kubadilishwa (na kuletwa) wasiokuwa wao limekuja mara nyingi ndani ya aya nyingi, jambo ambalo linafahamisha dalili iliyo wazi kwamba wao walifanya uzito kwenda kwenye Jihad mara nyingi kwani imekuja katika kauli ya Mwenyezi Mungu kwamba:

> "Na mkirudi nyuma, (Mwenyezi Mungu) atabadilisha (alete) watu wengine wasiokuwa ninyi kisha hawatakuwa kama ninyi" (Qur. 47:38)

Ni kama ilivyokauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: *"Enyi mlioamini, atakayeiacha miongoni mwenu Dini yake, basi hivi karibuni Mwenyezi Mungu ataleta watu ambao atawapenda, nao watampenda, wanyenyekevu kwa Waislamu (wenzao), wenye nguvu juu ya makafiri. Wataipigania Dini ya Mwenyezi Mungu na wala hawataogopa lawama ya anayewalaumu, hiyo ndiyo fadhila ya Mwenyezi Mungu, humpa amtakaye na Mwenyezi Mungu ni mwenye wasaa, mwenye kujua." (Qur. 5:54)*

Na lau tungetaka kuzieleza aya tukufu zilizopo, ambazo zinaitia nguvu maana hii na kuweka wazi uhakika wa mgawanyo wausemao Mashia kuhusu aina hii ya Masahaba, basi ingelazimu kuandika kitabu maalum,

na bila shaka Qur'an Tukfu imeeleza juu ya jambo hilo kwa kutumia maelezo mafupi yenye ufahamisho wa kina pale iliposema:

*"Na wawepo miongoni mwenu watu wanaolingania wema na kukataza maovu, na hao ndio watakaotengenekewa. Na wala musiwe kama wale waliofarikiana na kukhitilafiana baada ya kuwafikia dalili zilizo wazi, na hao ndio watakaokuwa na adhabu kubwa. Siku ambayo nyuso zitanawiri na nyuso zingine zitasawijika wataambiwa: Je, mlikufuru baada ya kuamini kwenu? Basi onjeni adhabu kwa vile mlivyokuwa mnakufuru. Ama wale ambao nyuso zao zitanawiri watakuwa katika Rehema ya Mwenyezi Mungu. Wao humo watakaa milele." (Qur. 3:104, 105, na 106)*

Aya hizi kama ambavyo haifichikani kwa kila mwenye kuchunguza kwa undani, zinawaambia Masahaba na kuwahadharisha wasifarakane na kuhitilafiana baada ya kuwafikia ubainisho, na zinawaonya juu ya adhabu kubwa na kuwagawa mafungu mawili. Fungu moja litafufuliwa siku ya Qiyama likiwa na nyuso zenye kunawiri na hao ndiyo wenye kushukuru ambao wamestahiki huruma ya Mwenyezi Mungu, na fungu jingine watafufuliwa wakiwa na nyuso zilizosawijika na hawa ndiyo ambao waliritadi baada ya kuamini, na Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaonya kwa adhabu kubwa.

Bila shaka inaeleweka kwamba, Masahaba walifarakana baada ya Mtume, wakahitilafiana na wakawasha moto wa fitna mpaka jambo hili likawafikisha kwenye mauaji na vita zilizomwaga damu, kitu kilichosababisha Waislamu wageuke na kubakia nyuma na hatimaye maadui zao kuwa na tamaa (ya kuwavuruga).

Na aya hiyo iliyotajwa haiwezekani kuifanyia *Taawili* na kuigeuza kutoka kwenye *Maf-Hum* yake inayotangulia kueleweka akilini.

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

*"Je, wakati haujafika kwa wale walioamini kwamba, nyoyo zao zinyenyekee kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kwa mambo ya haki yaliyoteremka, na wala wasiwe kama wale waliopewa kitabu hapo*

*kabla na muda wao (wa kuondokewa na Mitume) ukawa mrefu, kwa hivyo nyoyo zao zikawa ngumu na wengi wao wakawa waasi. (Qur. 57:16)*

Ndani ya kitabu kiitwacho *Ad-Durul-Ma-nthoor* kilichoandikwa na Jalalud-Dini Suyut amesema: "Pindi Masahaba wa Mtume (s.a.w.) walipofika Madina, wakapata maisha mazuri ambayo hawakuwa nayo baada ya kuwa walikuwa katika shida, walizembea (kutenda) baadhi ya wajibu uliokuwa juu yao, hivyo wakakemewa na ikashuka kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: "*Je, wakati haujafika kwa wale walioamini"?* Na katika riwaya nyingine itokayo kwa Mtume (s.a.w.) inasema kwamba, "Mwenyezi Mungu aliziona nyoyo za Muhajirina kuwa ni nzito (hata) baada ya miaka kumi na saba tangu kushuka Qur'an, basi akateremsha kauli yake isemayo, *"Je, wakati haujafika kwa wale walioamini.....?"*

Ikiwa hawa ndiyo Masahaba ambao ndiyo wabora mno kuliko watu wengine (kama wasemavyo *Ahlul-Sunnah wal-Jamaa*) nyoyo zao hazikuwa na unyenyekevu katika kumtaja Mwenyezi Mungu na kile alichokiteremsha katika haki kwa muda wote wa miaka kumi na saba mpaka Mwenyezi Mungu akawaona wana nyoyo nzito, akawakemea na kuwaonya kutokana na ugumu wa nyoyo zao zinazowakokota kuwapeleka kwenye uovu, basi hapana lawama yoyote kwa vigogo wa Kiquraishi waliochelewa halafu wakasilimu katika mwaka wa saba Hijriyah na baada ya Makkah kuingia mikononi mwa Waislamu.

Basi hii ni baadhi ya mifano niliyoileta kutoka ndani ya Kitabu kitukufu cha Mwenyezi Mungu, inatosha kuwa ni dalili kwamba siyo kweli kuwa Masahaba wote ni waadilifu kama wasemavyo *Ahlis-Sunna Wal-Jamaa.*

Na tukifanya uchunguzi katika hadithi za Mtume (s.a.w.), basi bila shaka tutakuta mifano mingi lakini kwa mukhtasari nitaleta baadhi tu ya mifano, na itakuwa ni juu ya mwenye kutaka kufanya utafiti achunguze zaidi kama analitaka jambo hilo.

# MAONI YA MTUME KUHUSU MASAHABA.

**i). Hadithi ya Haudh (Birika):**

Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: "Nitakuwa nimesimama (siku ya Qiyama) halafu watanijia watu, na nitakapowafahamu, atatokea mtu kati yangu na wao atasema: (kuwaambia), twendeni, mimi nitasema waende wapi? Atasema motoni, nitasema wamefanya nini hawa? Atasema, hakika wao walirudi baada yako kinyumenyume. Basi sintawaona wenye kuokoka miongoni mwao isipokuwa kikundi kidogo."

Na amesema Mtume (s.a.w.): "Mimi nitawatangulia kwenye hodhi, yeyote atakayepitia kwangu atakunywa na atakayekunywa, milele hatahisi kiu, bila shaka watanifikia watu mbali mbali ambao mimi nawafahamu na wao wananifahamu kisha patawekwa kizuizi baina yangu na wao, mimi nitasema, hao ni Sahaba wangu, patasemwa, hakika wewe hujui mambo waliyoyazusha baada yako, basi mimi nitasema: Aangamie aliye badilisha (dini) baada yangu."

Yeyote mwenye kufanya mazingatiao ndani ya hadithi hizi nyingi walizoziandika wanachuoni wa Kisunni katika vitabu vyao, hawezi kuwa na shaka kwamba Masahaba wengi kwa hakika walibadilisha na kugeuza (dini), bali waliritadi na kurudi nyuma kwa visigino vyao baada ya Mtume (s.a.w.) isipokuwa wachache ambao Mtume (s.a.w.) amewaeleza kuwa ni kikundi kidogo. Haiwezekani kwa hali yoyote ile kuziweka hadithi hizi kwenye kundi la tatu ambalo ni la wanafiki kwani maandiko yanasema: "Nitasema Masahaba wangu". Hii ni kwa sababu wanafiki hawakubadilika baada ya Mtume (s.a.w.) vinginevyo basi (kama wangebadilika) mnafiki angelikuwa muumini baada ya kufariki Mtume (s.a.w.) kama ambavyo hadithi hizi ni kielelezo na ni tafsiri ya kile tulichokisajili hapo kabla miongoni mwa aya tukufu ambazo zimezungumzia juu ya kugeuka kwao na kuritadi na kuonywa kwao kutokana na adhabu kali.

**ii). Hadithi inayohusu kuwafuata Wayahudi na Wakristo:**

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) amesema:

"Bila shaka mtafuata nyendo za waliokutangulieni *shubiri* kwa *shubiri* na *dhiraa* kwa *dhiraa* hata kama wataingia ndani ya shimo la kenge mutawafuata", tukasema, "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ni Wayahudi na Wakristo"? Mtume akasema, "Ni nani basi kama siyo hao"?

Basi kwa yeyote anayefanya utafiti anawajibika kujiuliza pindi anapoisoma hadithi hii ambayo usahihi wake unakubalika kwa Waislamu wote ya kwamba, Masahaba ambao ndiyo waliokusudiwa katika hadithi hii walifanya mambo gani miongoni mwa matendo ya Wayahudi na Wakristo kiasi kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) akawataja kwa sifa ya kuwa watawafuata *Shubiri* kwa *Shubiri* na *dhiraa* kwa *dhiraa* hata kama wataingia ndani ya shimo la kenge nao wataingia.

Ndani ya Qur'an na katika historia sahihi inaeleweka wazi kuwa Wayahudi walimuasi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu Nabii Musa (a.s.), wakaiasi amri yake, wakamuudhi na wakaabudia ndama alipokuwa hayupo, kisha walifanya njama dhidi ya Harun nduguye Musa (a.s.) na walikaribia kumuua, na kwa ajili hiyo walipewa adhabu ya unyonge na umaskini na wakastahiki adhabu ya Mwenyezi Mungu, hayo yakiwa ni malipo yao kwa matendo waliyokuwa wakiyafanya. Waliritadi baada ya kuamini kwao na wakafanya njama dhidi ya Mitume wa Mwenyezi Mungu, na kila alipowafikia Mtume kwa jambo ambalo nafsi zao hazipendi, basi baadhi yao walimpinga na wengine walimuua. Mambo yalifikia kiasi cha Mayahudi kupanga njama dhidi ya Bwana wetu Isa (a.s.) na walimsononesha mama yake Mtukufu (Bibi Mariam) na hawakutulia mpaka waliopomuua na kumsulubu kama wanavyodai wao. Kisha wakahitilafiana baada ya hayo na wakafarakana kuhusu Nabii Isa, kwani miongoni mwao wako wasemao kuwa yeye alikuwa ni muongo na ni mzushi, na wengine walivuka mipaka na kumpa daraja ya uungu, wakasema kuwa ni mtoto wa Mungu.

Na ili kuipa uthibitisho hadithi hii, ninayo haki ya kuwaona Masahaba kwamba wao vile vile waliasi amri ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu

(s.a.w.) katika mambo mengi, na miongoni mwa hayo, ni pale walipomzuia asiwaandikie maandiko ambayo yatawalinda wasipotee, na katika hayo ni pale walipomshutumu kwa kumpa uamiri wa jeshi Usamah ibn Zaid, na wakakataa kutoka pamoja naye hata baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.) na bila shaka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimlaani kila aliyegoma (kutii amri hiyo) miongoni mwa watu aliowateua (wafuatane na Usamah).

Na katika mambo waliyoasi ni pale walipohitilafiana na kuzozana ndani ya *Saqifa Bani Saidah* juu ya suala la kumtawalisha Khalifa, na hawakumkubali Khalifa aliyetangazwa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika siku ya Ghadir Khum ambaye ni Ali ibn Abi Talib kama wanavyodai Mashia, na wanao ushahidi kutoka ndani ya vitabu vya hadithi vya Kisunni na vile vya historia, (ushahidi ambao) hauwezekani kubadilishwa. Si hivyo tu, bali walimuonya Binti ya Mtume Bibi Fatmah Zahra ambaye ni mwanamke bora kuliko wanawake wote kwamba, wangeliichoma moto nyumba yake kama watu wanaopinga Baia (ya Abubakr) wasingetoka (ndani ya nyumba hiyo) kwa nguvu. Kwa hakika inaingia akilini mno kwa mtafiti muadilifu kuyakubali maandiko yaliyo wazi juu ya Ukhalifa wa Ali ibn Abi Talib, kwa kuwa haingii akilini kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu afariki bila ya kumbainisha mtu yeyote (atakayechukua mahali pake), Mtume ambaye hakutoka nje ya Madina kwenda vitani au safarini isipokuwa huacha Khalifa. Na inaingia akilini pia kwamba, mtafiti muadilifu aikubali kauli ya Imam *Sharafud-Din* iliyomo ndani ya Kitabu chake kiitwacho *Al-Murajaat* pale alipomwambia Sheikh wa Az-har Sheikh Salim Al-Bishri: “Mmekubali, (Mwenyezi Mungu akupeni amani), ya kwamba Masahaba walichelewa kwenda kwenye jeshi la Usamah na wakawa wazito wakati huo pamoja na kuwa waliamuriwa wafanye upesi tena haraka, na mumekubali kwamba Masahaba walimshutumu Mtume s.a.w. kwa kumpa uamirijeshi Usamah, licha ya wao kusikia na kuyafahamu maelekezo ya Mtume kwa kauli na vitendo vya kumpa Usamah uamirijeshi, na mumekubali juu ya kumtaka kwao Abu Bakr amuuzulu Usamah hata baada ya Mtume (s.a.w.) kuwa alichukizwa na shutma yao juu ya kumpa kwake uamiri na kwa sababu hiyo akatoka hali ya kuwa ana homa kajiinamia na kajifunika nguo, kisha akawakemea katika hotuba yake akiwa juu ya mimbari, kitu ambacho mumesema lilikuwa ni miongoni mwa matukio ya kihistoria, na kwamba Mtume alitangaza wazi wazi kuwa Usamah alikuwa anastahiki uamiri

jeshi huo aliopewa na Mtume. Na mmekubali kuwa Masahaba walimtaka Khalifa (Abu Bakr) apuuze ujumbe huo (wa Kijeshi) alioutuma Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) na aitengue bendera aliyoifunga Mtume kwa mkono wake Mtukufu, hali ya kuwa waliona ni jinsi gani Mtume alivyosisitiza kupelekwa haraka jeshi hilo na maelekezo mengi juu ya wajibu huo. Pia mumekubali kuhusu baadhi ya Masahaba aliowateua Mtume (s.a.w.) ndani ya jeshi hilo na kuwaamuru waende chini ya uongozi wa Usamah, walivyogoma.

Na mmeyakubali haya yote kama walivyoyaeleza waandishi na wakaafikiana watu wa hadithi na wahifadhi wa kumbukumbu za Kiislamu na mmesema kwamba wao walikuwa na udhuru kwa hilo. Mukhtasari wa yote mliyoyataja katika udhuru wao ni kwamba, wao katika mambo haya walitanguliza mbele maslahi ya Uislamu kwa mujibu wa mtazamo wao na siyo kama yalivyowajibisha maagizo ya Mtume, nasi hakuna tulichokidai (mahala hapa) zaidi ya haya."

Kwa maelezo mengine iwapo tutajiuliza, basi tutakuwa katika mzunguko ufuatao: Je, wao katika ibada zao walikuwa wakizifanya kwa mujibu wa maagizo yote ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake au baadhi tu ya maagizo hayo? Ninyi mmechagua tamko la kwanza nasi tumechagua tamko la pili, basi kukiri kwenu sasa hivi kwamba hawakutii maamrisho hayo ya Mtume kunakithibitisha kile tulichokichagua sisi. Na kuwa kwao na udhuru au kutokuwa na udhuru ni jambo lililo nje ya maudhui inayochunguzwa kitu ambacho kiko wazi.

Na kwa kuwa imethibiti kwenu kwamba wao walitanguliza mbele maslahi ya Uislamu kuhusu jeshi la Usamah kama ulivyo mtazamo wao wa kutii maagizo ya Mtume, basi ni kwa nini hamsemi kwamba wao walitanguliza mbele maslahi ya Uislamu kuhusu Ukhalifa baada ya Mtume (s.a.w.) kama ulivyo mtazamo wao ili tu wayatii maagizo ya Ukhalifa yaliyoagizwa siku ya Ghadiri na mfano wa hayo?

Mmetoa udhuru kuhusu shutuma ya walioshutumu kupewa uamiri jeshi Bwana Usamah, kwamba watu hao hapana kilichowafanya washutumu isipokuwa ni ule umri mdogo aliokuwa nao (Usamah) wakati walikuwepo miongoni mwao watu wazima na wazee, na mkasema, hakika nafsi za

wazee na watu wazima hao hazikukubali kwa jumla na kwa maumbile yake kuongozwa na vijana, basi ni kwa nini msitoe sababu kama hii hii kuhusu wale waliokataa kutii maagizo ya Ghadiri yanayompa uongozi Ali juu ya watu wazima na wazee na hali yakuwa ni kijana. Kwa hukumu ya dharura katika maelezo yao ni kwamba siku aliyokufa Mtume waliuona umri wake (Ali) kuwa ni mdogo kama walivyouona umri wa Usamah kuwa ni mdogo siku Mtume (s.a.w.) alipomtawalisha juu yao katika umri ule, na kuna tofauti kubwa baina ya Ukhalifa na Uamiri jeshi wa kikosi.

Iwapo nafsi zao zote zilikataa kuongozwa (na Usamah) kwa sababu ya umri mdogo katika kikosi kimoja, basi nafsi hizo zilikuwa na haki ya kukataa kuongozwa na mtu mwenye umri mdogo katika muda wote maishani mwake katika mambo yake yote ya dunia na akhera. Kwa msingi wa yale mliyoyaelezea kwamba nafsi za wazee na watu wazima hao kwa tabia zake zinapinga kuongozwa na vijana wenye umri mdogo ni jambo lisilokubalika ikiwa makusudio yenu ni kutoipa mpaka hukumu hii, kwani nafsi za waumini wazee waliokamilika katika imani zao hazipingi kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake katika suala la kuongozwa na vijana wenye umri mdogo, wala katika mambo mengine, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

*"Naapa kwa Mola wako, kamwe hawawezi kuwa ni waumini mpaka wakufanye wewe kuwa ni muamuzi wao kwa yale wanayozozana baina yao, kisha wasiwe na uzito ndani ya nafsi zao katika yale uliyoyaamua na wasalimu amri mara moja".*

*"Na chochote anachokupeni Mtume basi kichukuweni na anachokukatazeni basi komeni."*

Maelezo haya tumeyanukuu kutoka ndani ya kitabu kiitwacho *Al-Murajaat (Barua Na.92).*

**iii). Hadithi ya Bitanataini (vikundi viwili):**

Amesema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.): "Mwenyezi Mungu hakumtuma Mtume yeyote wala hakumpa Ukhalifa Khalifa yeyote

isipokuwa anakuwa na makundi mawili, kundi moja linamuamrisha mema na kumhimiza, na kundi jingine linamuamrisha shari na kumsisitiza juu ya shari hiyo, basi *Maa'sum* ni yule aliyehifadhiwa na Mwenyezi Mungu.

Hadithi hii ndani yake kuna dalili iliyowazi ya kwamba Masahaba walikuwa wamegawika mafungu mawili. Na tukitaka kuipanua maudhui hii bila shaka tutayakinisha zaidi kwamba baadhi ya Masahaba walikuwa wakimuelekeza Mtume kufanya yasiyokuwa mema.

Na mfano wa hilo ni hadithi aliyoiandika Al-Khatib ndani ya *Tarikh Al-Baghadad* katika juzuu ya kwanza na Ibn Jariri amesema kuwa hadithi hiyo ni sahihi:-

Amesema: "Kuna watu miongoni mwa Maquraishi walikuja kwa Mtume (s.a.w.) wakasema, Ewe Muhammad bila shaka sisi ni jirani zako na tumewekeana nawe ahadi, na kwa hakika kuna watu katika vijana wetu wamekujia wewe wala hawana haja ya Uislamu wala kutaka kujifunza, bali hakuna lolote ila wamekimbia kutoka katika miliki zetu." Mtume akamwambia Abubakr, Wasemaje? Akasema, "Wasemavyo ni kweli wao ni jirani zako na umewekeana nao ahadi." Uso wa Mtume ukabadilika kwa maelekezo aliyoyatoa Abubakr kisha Mtume akamwambia Omar, "Wasemaje, "Akasema, "Wasemavyo ni kweli, hakika wao ni jirani zako na umewekeana nao ahadi." Basi uso wa Mtume ukabadilika kwa maelelekezo ya huyu Bwana mwingine.

Na kisa hiki ni uthibitisho wa hadithi ya Bitanatain, kwani walichokiashiria Abubakr na Omar siyo katika kheri wala mema vinginevyo uso wa Mtume (s.a.w.) usingebadilika.

Imam Ahmad ibn Hanbal ndani ya Musnad yake na Muslim ndani ya Sahih yake wameandika: "Nilimsikia Omar akisema, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) aligawa mgao fulani, basi mimi nikamwambia wako wanaostahiki mno kuliko hawa (*Ahlus-Suffah*). Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema, "Ninyi munanitaka nifanye uchafu na munanitaka niwe bakhili namimi siyo bakhili."

Hiki ni kisa kingine kilichowazi kwamba Umar ibn Khatab hakuwa katika kikundi cha wanaoamrisha mema, bali yeye ni miongoni mwa wale wanaotaka uovu na kuamrisha ubakhili kwa mujibu wa maelezo yaliyomo

ndani ya hadithi ya Mtume (s.a.w.).

**iv). Hadithi ya kushindania Ulimwengu:**

Amesema Mtume (s.a.w.); “Mimi ni Mwenye kuwatangulieni na ni shahidi juu yenu, na bila shaka mimi namuapa Mwenyezi Mungu, sasa hivi nakiangalia kidimbwi changu, na kwa hakika nimepewa funguo za hazina ya ardhi, namuapa Mwenyezi Mungu sihofii kwenu kwamba mtafanya ushirikina baada yangu lakini nawahofia kuwa mutashindania ulimwengu. Taz: Sahih Bukhari Juz.4 uk.100 -101.

Amesema kweli Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.), kwa hakika walishindania ulimwengu mpaka wakazichomoa panga zao kupigana na wakakufurishana wao kwa wao, na baadhi ya hawa masahaba walikuwa mashuhuri kwa kukusanya na kuhifadhi dhahabu na fedha wakati baadhi ya Waislamu wanakufa kwa njaa. Wanahistoria kama vile *Al-Mas-oodi* ndani ya *Muroojud-Dhahabi* na Tabari na wengineo wanatusimulia kwamba utajiri wa Zuberi peke yake ulifikia dinari alfu khamsini na farasi alfu moja na watumwa alfu moja na alikuwa na milki nyingi za ardhi katika mji wa Basra, Kufah, Misri na miji mingineyo. *Taz: Muroojud-Dhahabi cha Al-Mas-oodi Juz.2 uk.341.*

Naye Abdur-Rahman ibn Auf alikuwa na farasi mia moja , ngamia alfu moja, mbuzi elfu kumi na robo ya thamani ya mali yake iliyogawiwa kwa wakeze baada ya kifo chake ilifikia themanini na nne. Taz: Rejea iliyotangulia.

Naye Uthman ibn Affan siku aliyokufa aliacha dinari laki moja na alfu khamsini ukitoa mifugo, ardhi na mashamba yasiyokuwa na idadi. Ama Zaid ibn Thabiti yeye aliacha dhahabu na fedha ambazo zilikuwa zikivunjwa kwa mashoka mpaka mikono ya watu ikatoka malengelenge.

Hii ni baadhi ya mifano michache, na ndani ya historia kuna ushahidi mwingi ambao hatutaki kuingia katika uchunguzi wake sasa hivi bali tunatosheka na kiasi hiki cha dalili juu ya ukweli wa ile hadithi kwamba, wao Masahaba dunia iliwapambia machoni mwao na yakawafurahisha mapambo yake, wakajilimbikizia mali nyingi juu ya hesabu ya Waislamu wanyonge.

# MAONI YA BAADHI YA MASAHABA KUHUSU WENZAO

**i). Ushahidi wao wenyewe juu ya kuibadilisha Sunna ya Mtume**

Imesimuliwa toka kwa Said Al-Khudri amesema: "Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa akitoka siku ya *Idi Al-Fitri* na *Al-Adh-ha* kwenda kusali, basi kitu cha mwanzo alichokuwa akikianza ni sala kisha husimama mbele ya watu, na hali yakuwa wao wamekaa katika safu zao, huwapa mawaidha, kuwausia na kuwapa muongozo na endapo anataka kukatisha somo hulikatisha, au kuamrisha kitu huamrisha, kisha huondoka. Abu Said amesema, watu waliendelea kufanya hivyo mpaka nilipotoka pamoja na Mar-wan akiwa ndiyo Amiri wa Madina katika siku kuu ya *Al-Adh-ha* au *Al-Fitri*, basi pindi tulipofika mahali pa kusalia, hapo kulikuwa na mimbari aliyoijenga Kathir ibn As-Silt, Ghafla Mar-wan akataka kupanda kwenye mimbari hiyo kabla ya kuswali, mimi nikaivuta nguo yake naye akaivuta kisha akapanda akahutubia kabla ya kuswali. Mimi nikamwambia, "Wallah mumebadilisha", akasema, "Ewe, Baba Said yamekwishaondoka uyajuwayo." Akasema, "Kwa hakika watu walikuwa hawakai nasi baada ya kusali ndiyo maana tumeifanya khutba kabla ya kusali." *(Taz: Sahihi Bukhari Juz.1 uk.122 katika Kitabul-Idain Mlango wa Al-Khuruju Ilal-Musala Bighair Mimbar.*

Kwa hakika nimefanya uchunguzi juu ya sababu zilizokuwa zikiwafanya Masahaba hawa waigeuze Sunna ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.), nikagundua kuwa, Banu Umayyah na wengi wao wakiwa ni miongoni mwa Masahaba wa Mtume (s.a.w.), wakiongozwa na Muawiyah ibn Abi Sufiyan *mwandishi wa Wahyi* kama wanavyomwita wenyewe, huyu alikuwa akiwalazimisha watu wamtukane Imam Ali ibn Abi Talib, na wamlaani katika mimbari msikitini, kama walivyoeleza hayo wanahistoria.

Muslim ameandika ndani ya Sahih yake katika mlango wa *Fadhail Ali ibn Abi Talib* kama ifuatavyo: Muawiyah aliwaamuru wafanyakazi wake katika kila mji kuifanya laana hiyo ya (kumlaani Imam Ali a.s.) kuwa ni sunna inayosemwa na makhatibu juu ya mimbari, na pindi baadhi ya Masahaba walipoona uchungu kutokana na tendo hilo na wakamkemea, Muawiyah aliamuru wauawe na wachomwe moto. Miongoni mwa waliouawa ni sahaba mashuhuri Bwana Hujru ibn Adiyi Al-Kindi na jamaa zake na baadhi yao walizikwa hai kwa sababu tu ya wao kukataa kumlaani Imam Ali na kupinga jambo hilo.

Naye Abul-aa'la Al-Maududi ameandika ndani ya Kitabu chake kiitwacho, *Al-khilafatu Wal-Muluku - Ukhalifa na ufalme* Akimnukuu Al-Hasan Albasri amesema:-

"Mambo manne alikuwa nayo Muawiyah, lau asingekuwa nayo isipokuwa jambo moja, basi lingetosha kuwa ni lenye kumwangamiza.

1). Kuchukua Ukhalifa bila ushauri wakati wapo Masahaba bora zaidi kuliko yeye.

2). Kumrithisha Ukhalifa mwanawe (Yazid) aliyekuwa mlevi, anayevaa hariri na kupiga zumari.

3). Kumfanya Ziyad kuwa ni mtoto wake wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amesema, "Mtoto ni wa kitanda na yule mzinifu atapata jiwe."

4. Kumuua Hujru ibn Adiyyi Al-Kindi na jamaa zake Hujru, basi Ole wake kwa kumuua Hujru, Oh!! Ole wake kwa kumuua Hujru na jamaa wa Hujru. *Taz: Abul-Aala Al-Maudud, Kitabu Al-Khilafatu Wal-Mulku uk.106.*

Baadhi ya waumini miongoni mwa Masahaba walikuwa wakikimbia kutoka Misikitini baada ya kumaliza kusali ili tu wasijehudhuria Khutba ambayo itahitimishwa kwa kumlaani Ali (a.s.) na watu wa nyumba yake, na kwa ajili hii basi, Banu Umayyah waliibadilisha Sunna ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wakatanguliza khutba kabla ya Sala ili watu wote wahudhurie na walazimike kusikiliza japo hawapendi.

Ajabu kubwa kwa Masahaba hawa ambao walikuwa hawaoni vibaya kubadili Sunna ya Mtume (s.a.w.) na hata hukmu za Mwenyezi Mungu ilimradi tu watimize malengo yao machafu, chuki yao iliyojificha na tamaa zao mbaya, na wakamlaani mtu ambaye Mwenyezi Mungu amemuondolea amemtakasa mno na akawajibisha kumuombea Rehma kama anavyoombewa Mjumbe wake. Vile vile Mwenyezi Mungu na Mtume wake wamewajibisha kumpenda mpaka Mtume (s.a.w.) amesema, "Kumpenda Ali ni dalili ya imani na kumbughudhi ni dalili ya unafiki." *Taz: Sahih Muslim Juz.1 uk.61.*

Lakini Masahaba hawa walibadili na kugeuza na wakasema tumesikia na tumeasi, na badala ya wao kumuombea Rehma Ali (a.s.), kumpenda na kumtii, wao walimtukana na kumlaani kwa muda wa miaka sitini kama inavyoelezea ndani ya vitabu vya historia.

Basi kama watu wa Musa (a.s.) walifanya njama dhidi ya Harun (a.s.) na wakakaribia kumuua, hakika baadhi ya Masahaba wa Muhammad (s.a.w.) walimuua Harun wake Ali a.s. na wakawafuatilia wanawe na wafuasi wake kila upande na kila mji. Wakayafuta majina yao katika diwani na wakazuwia mtu yeyote asiitwe kwa jina lake. Hawakutosheka na hayo bali waliwalazimisha Masahaba wenye utakaso wa moyo wafanye hayo kwa nguvu na dhulma.

Nami Wallahi husimama hali yakuwa nimechanganyikiwa sijuwi la kufanya, pale ninaposoma Sihahi zetu (vitabu vyetu) na mambo yaliyoandikwa humo juu ya mapenzi ya Mtume kwa nduguye na mwana wa Ami yake Ali (a.s.), na jinsi alivyomtanguliza mbele kuliko Sahaba yeyote mpaka Mtume akasema; "Wewe (Ali) kwangu mimi unayo daraja ya Harun kwa Musa, isipokuwa hapana Nabii baada yangu." *Taz: Sahih Bukhari, Juz.2 uk.305, Muslim Juz.2 uk.360, Mus -Tadrak ya Al-Hakim Juz.3 uk.109.*

Pia alimwambia: "Wewe unatokana na mimi, nami natokana nawe" *Taz: Sahih Bukhari Juz.2 uk.76, Sahih Tirmidh Juz.5 uk.300, Sunan ibn Majah Juz.1 uk.44.*

Na alisema Mtume: "Kumpenda Ali ni dalili ya imani na kumbughudhi ni dalili ya unafiki." *Taz: Sahih Muslim Juz.1 uk.61, Sunan An-Nasai*

*Juz.6 uk.116, Sahih Tirmidh Juz.8 uk.306.* Pia alisema Mtume, "Mimi ni mji wa elimu na Ali ndiyo mlango wake." *Taz. Sahih Tirmidhi Juz.5 uk.201, Mus-Tadrak ya Al-Hakim Juz.3 uk.126.*

Na alisema: "Ali ni Walii wa kila Muumini baada yangu." *Taz: Musnad Imam Ahmad Juz.5 uk.25, Mus-Tadrak Al-Hakim Juz.3 uk.134, Sahih Tirmidh Juz.5 uk.296.*

Pia Mtume (s.a.w.) alisema: "Yeyote ambaye Mimi nilikuwa Mtawala wake, basi huyu hapa Ali ni Mtawala wake, Ewe Mwenyezi Mungu mtawalishe atakaye mtawalisha na umpinge atakayempinga." *Taz: Sahih Muslim Juz.2 uk.362 Mustadrak Al-Hakm Juz.3 uk.109, Musnad Ahmad Juz.4 uk.28.*

Lau tungetaka kusimulia fadhila ambazo Mtume (s.a.w.) amezitaja kumhusu Ali (a.s.), na ambazo wameziandika wanachuoni wetu hali yakuwa wamekiri juu ya usahihi wake, basi jambo hilo lingelazimu kuandika kitabu maalum. Lakini ni vipi Masahaba walijifanya kuwa hawayajui maagizo haya na wakamtukana Ali na kumfanyia uadui, wakamlaani juu ya mimbari na ni vipi wakampiga vita na kisha kumuua?

Hakika Mimi najribu kupata namna ya kuwatakasa watu hawa, lakini siipati isipokuwa nawaona ni watu walioipenda dunia na kuishindania, au ni unafiki na au waliritadi na kurudi nyuma kwa visigino. Ninajaribu kuwabebesha jukumu hili wale Masahaba wasio na hadhi yeyote na baadhi ya wanafiki, lakini inasikitisha sana kwamba hawa waliofanya haya wanatambulikana kuwa ni miongoni mwa masahaba wakubwa, wenye hadhi na ni watu mashuhuri, kwani wa kwanza kutoa onyo la kuiunguza nyumba ya Ali (a.s.) na waliomo ni Omar ibn Khatab, na wa tu wa mwanzo kumpiga vita (Ali a.s.) ni Zuberi, Ummul-Muuminin Aisha bint Abubakr, Muawiyah ibn Abi Sufiyan na Amr ibn Al-As na wengi mfano wa hawa.

Kwa hakika mimi nastaajabu sana na huenda kustaajabu kwangu kusifikie mwisho kama anavyoniunga mkono juu ya hili kila mwanafikra aliyehuru na mwenye akili (ya kuchambua mambo). Najiuliza ni vipi wanachuoni wa Kisunni wamekubaliana juu ya uadilifu wa Masahaba wote na kuwaombea radhi na pia kuwaombea Rehma wote, hawamtoi yeyote miongoni mwao

kiasi kwamba baadhi ya wanachuoni hao wamesema, “Mlaani Yazid wala usizidishe (chochote).” Basi ana nafasi gani Yazid kutokana na maafa hayo (aliyoyasababisha) ambayo hayakubaliwi na Dini wala akili?

Mimi siridhiki na Ahlus-Sunnah Wal-Jamaa, ikiwa kweli wao wanafuata Sunna ya Mtume, basi ni vipi wanamhukumu kuwa ni muadilifu mtu ambaye Qur’an na Sunna (ya Mtume) vimemhukumu juu ya uovu wake, kuritaddi kwake na kukufuru kwa mtu huyo? Hapana shaka kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) amesema, “Yeyote mwenye kumtukana Ali hakika amenitukana mimi, na yeyote atakayenitukana mimi bila shaka amemtukana Mwenyezi Mungu, na mwenye kumtukana Mwenyezi Mungu atamtupa kifudi fudi motoni.” *(Taz: Mus-Tadrak-Alhakim Juz.3 uk.121, Khasaisun-Nasai uk.24, Musnad Imam Ahmad Juz.6 uk. 33, Manaqib-Alkhawarzami uk.81, Ariyad¬¬-Dhu Anadhrah ya Tabari juz. 2 uk. 219, Tarikh-As-Suyut uk. 73.*

Haya ndiyo malipo ya mtu atakayemtukana Ali (a.s.). Sasa basi unamfikiriaje mtu atakayemlaani na kumpiga vita? Wana hali gani wanachuoni wetu kuhusu ukweli wote huu au kuna vifuniko kwenye nyoyo?

Na useme, “Ewe Mola! najikinga kwako uniepushe na wasiwasi wa mashetani, na ninajikinga kwako wasinifikie.”

**ii). Masahaba hata Sala waliibadilisha:**

Amesema Anas ibn Malik: “Hapana kitu nilichokifahamu vyema miongoni mwa mambo yaliyokuwepo katika zama za Mtume (s.a.w.) kuliko Sala, akasema, Je, siyo kwamba mumepoteza vitu fulani ndani yake.

Na Az-Zuhri amesema, niliingia kwa Anas ibn Malik huko Damscus nikamkuta analia, nikamwambia, “Ni jambo gani linalokuliza,?” Akasema, “Hapana kitu nikijuacho vyema miongoni mwa vitu nilivyovidiriki isipokuwa hii Sala ambayo imekwishapotezwa.” *(Taz: Sahih Bukhari Juz.1 uk.74)*.

Ili mtu yeyote asije dhani kwamba Tabiina (waliofuata baada ya Masahaba) ndiyo waliobadilisha mambo yaliyobadilishwa baada ya fitna hizo na vita, napenda nikumbushe kwamba mtu wa kwanza aliyeibadilisha Sunna ya Mtume ndani ya Sala ni Khalifa wa Waislamu Uthman ibn Affaan na vile vile Ummul-Muumina Aisha.

Wameandika Masheikh wawili Bukhari na Muslim ndani ya Sahih zao ya kwamba: Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alisali rakaa mbili Mina, na Abubakr baada ya Mtume, na Omar baada ya Abu Bakr na Uthman mwanzoni mwa Ukhalifa wake kisha baadaye alisali rakaa nne. *(Taz: Sahih Bukhari Juz.2 uk.154 Sahihi Muslim Juz.1 uk.260).*

Vile vile Muslim ameandika ndani ya Sahih yake: Amesema Az-Zuhri, "Nilimwambia Ur-wah, ana nini Aisha mbona anakamilisha Sala katika Safari?" Akasema, "Yeye (ameawili) amebadilisha kama alivyobadilisha Uthman." *(Taz. Sahih Muslim Juz.2 uk.143 Kitabu Salatil-Musafirina).*

Sub-hanallah!! Hivi kuna taawili yoyote inayofuta Sunna ya Mtume kuliko hii na mfano wa hii miongoni mwa Taawili? Je, kuna mtu yeyote atakayemlaumu Abu Hanifa, au kumlaumu mmoja wa Maimamu wa Madhehebu ya watu waliogeuza, wakahalalisha na kuharamisha kufuatana na Taawili zao na Ij-tihadi zao hali yakuwa katika kufanya hivyo wanafuata Sunna za Masahaba hawa?

Na Umar ibn Khatab alikuwa akifanya Ij-tihadi na Taawili mbele ya Nnass zilizowazi katika Sunna za Mtume bali mbele ya maandiko yaliyowazi ya Qur'an Tukufu, kisha yeye anahukumu kwa mujibu wa maoni yake kama ilivyo katika kauli yake, "Mut-a mbili zilikuweko katika zama za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, mimi nazizuwia na nitatoa adhabu kwa mwenye kuzitenda."

Na anasema (Umar) kumwambia mtu mwenye Janaba ambaye hakupata maji ya kuoga, "Usiswali." Ajabu!! licha ya kuwepo kauli ya Mwenyezi Mungu ndani ya Sura Al-Maidah isemayo; *"Na iwapo hamtapata maji, basi fanyeni Tayamam kwa udongo safi". (Qur., 5:6)*

Bukhari ameandika ndani ya Sahihi yake katika mlango usemao, pindi mtu mwenye Janaba akiichelea nafsi yake Amesema:- "Nilimsikia Shaqiq ibn Salamah akisema, nilikuwa mbele ya Abdullah na Abu Musa, basi

Abu Musa akamwambia Shaqiq, waonaje Ewe Abu Abdur-Rahman iwapo mtu akipatwa na Janaba na akakosa maji atafanya nini? Abdullah akasema, Hawezi kuswali mpaka apate maji. Abu Musa akasema, basi utaifanya nini kauli ya Ammar wakati Mtume (s.a.w.) alipomwambia ukiwa na Janaba na hukupata maji inakutosha upige mapigo mawili (juu ya udongo)? Mtume akamfunza kutayamam. Abdullah akasema, "Je, wewe huoni kwamba Umar hakutosheka na kauli hiyo? Abu Musa akasema, "Haya basi tuachane na kauli ya Ammar sasa utafanya nini kuhusu aya hii, *"Na iwapo hamtapata maji, basi fanyeni Tayamam kwa udongo safi". (Qur.5:6)?* Abdullah hakufahamu akisemacho (alichanganyikiwa) hatimaye akasema, "Bila shaka sisi tunaona lau tutawaruhusu kufanya hivyo kuna mashaka kwamba itakapokuwa kuna hali ya baridi kwa mmoja wao ataacha kutumia maji na atatayamamu." Mimi nikamwambia Shaqiq, "Kilichomchukiza Abdallah ni hiki." Akasema: "Ndiyo". *(Taz: Sahih Bukhar Juz.1 uk.54).*

Mashaallah; Huyu Abdullah alijifanya kuwa ni kiongozi wa Umma huu akatoa Fat-wa kwa matamanio yake na vile atakavyo, na siyo vile hukmu za Mwenyezi Mungu alizoziteremsha ndani ya Qur'an zinavyotaka, licha ya Abu Musa Al-Ash-ari kutoa ushahidi wa aya ya kutayamam, kwani Abdullah anasema, "Lau tutawaruhusu kufanya hivyo...."

Wewe ni kama nani (Ewe Abdullah)? Kiasi kwamba unahalalisha na kuharamisha, unaruhusu na kukataza kama upendavyo? Naapa kwa hakika kuhusu jambo hili wewe umefuata mwendo wa aliyekutangulia, na umezidi kuwa jeuri na kuyatia nguvu maoni yake ambayo alikuwa akitolea Fat-wa ya kuacha kuswali wakati maji yanapokosekana, na wala hakukinaishwa na hoja ya Ammar ibn Yasir aliyoitowa kupitia Sunna ya Mtume (s.a.w.) kama ambavyo Abu Musa Al-Ash-ari aliyoitoa kupitia aya ya Qur'an!! Je, Baada ya yote haya, hivi kweli wanachuoni wetu wanaweza kudai kwamba Masahaba ni kama nyota basi yeyote tutakayemfuata tutaongoka?

*(Je, Munastaajabu kwa hadithi hii na munacheka na wala hamlii, hali yakuwa mumeghafilika)!! (Qur'an, 53:59)*

**iii). Masahaba wanashuhudia wenyewe:**

Anas ibn Malik amesimulia kwamba, "Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliwaambia Ansar, Hakika ninyi baada yangu mutaona ubinafsi mkubwa, basi subirini mpaka mkutane na Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwenye Haudh." Anas akasema, Hatukusubiri." *(Taz: Sahih Bukhari Juz.2 uk. 135)*

Na imesimuliwa kutoka kwa Al-Alau ibn Al-Musayyab naye toka kwa baba yake Amesema: "Nilikutana na Al-Bar-raa ibn Azib (r.a.) nikamwambia, Hongera, wewe ulikuwa Sahaba wa Mtume na ulimpa Baia chini ya mti, akasema: Ewe mtoto wa ndugu yangu, wewe hutambui ni mambo gani tuliyoyazusha baada yake. *(Taz: Sahih Bukhari Juz.3 uk.32 mlango wa Ghazuwatul-Hudaibiyah).*

Basi ikiwa Sahaba huyu ni miongoni mwa waliotangulia (kusilimu) ambao walimpa Baia Mtume chini ya mti (siku ya Hudaibiyah) na Mwenyezi Mungu aliwaridhia na akayafahamu yaliyomo ndani ya nyoyo zao, akawapa ushindi kwa zama za karibu, anashuhudia juu ya nafsi yake na wenzake kwamba wao walizusha mambo baada ya Mtume. Ushahidi huu ndiyo uthibitisho wa yale aliyoyasema Mtume (s.a.w.) na kuyaeleza yakuwa Masahaba wake baada yake watazusha na watageuka nyuma. Je, inawezekana kwa mtu mwenye akili baada ya maelezo haya akausadiki uadilifu wa Masahaba wote kabisa kwa mujibu wa kauli ya *Ahlus-sunna Wal-Jamaa?* Na yeyote asemaye kauli kama hii bila shaka atakuwa anapingana na akili na maandiko, na wala hatabakia na kipimo chochote cha kufikiri akitegemeacho mtu anayefanya uchunguzi ili aweze kuufikia ukweli.

**iv). Ushahidi wa Masheikh wawili**
**(Abubakr na Umar) Juu ya nafsi zao wenyewe:**

Bukhari ameandika ndani ya Sahih yake katika mlango unaotaja sifa za Umar ibn al-Khatab amesema: "Pindi Umar alipopigwa upanga akawa anaugua, Ibn Abbas alimwambia: Ewe Amirul-Muuminin hata kama umefikwa na hayo bila shaka wewe ulishirikiana vema na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kisha ulitengana naye hali ya kuwa

amekuridhia, na ulishirikiana vema na Abubakr, halafu ulitengana naye hali yakuwa amekuridhia, kisha ulishirikiana vema na masahaba wao na iwapo utatengana nao, basi bila shaka utatengana nao hali yakuwa wamekuridhia."

Umar akasema, "Ama ulivyosema kuhusu usuhuba wangu kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kuwa kwake radhi hakika hayo ni neema ya Mwenyezi Mungu aliyonineemesha, na ama usuhuba wangu kwa Abubakr na radhi yake kwangu si kingine bali ni neema ya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyonieemesha, ama huzuni yangu uionayo, hiyo ni kwa sababu yako na jamaa zako. Namuapa Mwenyezi Mungu lau ningekuwa na kilima cha dhahabu ningejikomboa kwa kilima hicho kutokana na adhabu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kabla sijamuona". *(Taz: Bukhari Juz.2 uk.201).*

Pia historia imesajili kauli ya Umar isemayo; "Laiti mimi ningekuwa kondoo wa watu wangu, wakaninenepesha wapendavyo nikishanenepa vizuri, wakatembelewa na baadhi ya wanaowapenda, (wakanichinja) kisha sehemu yangu fulani wakaichoma na wakanikata vipande vipande kisha wakanila na wakanitoa nikiwa ni uchafu na nisingekuwa mtu."

*(Taz: Min-Hajus-Sunnah cha ibn Taimiyah Juz.3 uk.131, Hil-Yatul-Auliyai cha Abu Nuaim Juz.1 uk.52.*

Vile vile historia imesajili tukio kama hili kumhusu Abubakr. Kuna wakati Abubakr alimuangalia ndege aliyekuwa juu ya mti akasema: "Ni furaha kubwa uliyonayo Ewe ndege, unakula matunda na unatua juu ya mti na wala huna hesabu wala adhabu, hakika napenda ningelikuwa mti pembezoni mwa njia, ngamia akipita anile na anitoe nikiwa uchafu na wala nisingekuwa mtu.

*(Taz: Tarikh Tabari uk.41, Ar-ri Yadhun-Nadhrah Juz.1 uk.134, Kanzul Ummal uk.361 Min-Hajus-Sunnah cha ibn Taimiyyah Juz.3 uk.120).*

Na kuna mara nyingine tena alisema: "Laiti mama yangu asingenizaa, laiti ningekuwa pumba ndani ya tofali." Hayo ni baadhi ya maandiko niliyoyaleta kama mfano na siyo yote.

Na hiki hapa kitabu cha Mwenyezi Mungu kinawabashiria waja wake walioamini kwa kusema:-

*"Fahamuni ya kwamba, Mawalii wa Mwenyezi Mungu hawana khofu juu yao wala hawahuzuniki. (Hao) ni wale ambao wameamini na walikuwa wachaji Mungu wanayofuraha Duniani na Akhera. Hapana mabadiliko katika maneno ya Mwenyezi Mungu, hayo ndiyo mafanikio makubwa". (Qur. 10: 62, 63, 64.)*

Na kinasema tena:- *"Bila shaka wale ambao wamesema kuwa Mola wetu ni Allah kisha wakawa na msimamo, basi huteremka juu yao Malaika (na kuwaambia) msikhofu na wala msihuzunike, na jibashirieni kupata pepo ambayo mulikuwa mukiahidiwa, sisi ni wasimamizi wenu ndani ya maisha ya Dunia na Akhera, na humo mutapata chochote ambacho nafsi zenu zinakitamani, na humo mutapata mukitakacho, ni Tarkrima itokayo kwa (Mola) mwingi wa kusamehe, mwingi wa Rehma." (Qur. 41:30-32)*

Basi ni vipi Masheikh hawa wawili Abubakr na Umar wanatamani wasiwe miongoni mwa binaadamu ambaye Mwenyezi Mungu amemtukuza kuliko viumbe wake wengine?

Na iwapo Muumini wa kawaida ambaye anao msimamo wa (Dini) katika maisha yake huwa anateremkiwa na Malaika na kumbashiria daraja yake aliyonayo peponi, basi hawezi kuogopa adhabu ya Mwenyezi Mungu wala hahuzuniki kwa matendo aliyoyaacha nyuma yake duniani na anayo furaha maishani mwake hapa duniani kabla hajafika Akhera. Sasa inakuwaje kwa Masahaba hawa wakubwa ambao ni viumbe bora baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (kama tulivyofunzwa) ni vipi wanatamani wawe takataka na kapi za ngano?

Hivyo basi, lau Malaika wangekuwa wamewabashiria pepo kamwe wasingetamania kupata kilima chenye dhahabu ili wapate kujikomboa kutokana na adhabu ya Mwenyezi Mungu kabla ya kukutana naye.

Mwenyezi Mungu Anasema:

*"Na lau kila mtu aliyejidhulumu angekuwa amemiliki vyote vilivyoko ardhini, bila shaka angevitoa vyote ili ajikomboe, na pindi watakapoiona adhabu watajitahidi kuficha majuto yao lakini hawawezi,*

*na patahukumiwa baina yao kwa uadilifu na wala hawatadhulumiwa." (Qur. 10:54)*

Pia amesema Mwenyezi Mungu:

*"Na lau wale waliojidhulumu wangemiliki vyote vilivyoko ardhini na vingine mfano kama huo, wangevitoa kujikomboa kutokana na adhabu mbaya ya siku ya Qiyama, na yatawadhihirikia kwa Mwenyezi Mungu mambo ambayo hawakuyatazamia, na utawadhihirikia ubaya wa yale waliyoyachuma na yatawazunguka yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha."(Qur. 39:47-48).*

Mimi kwa hakika natamani kwa moyo wangu wote aya hizi zisiwakumbe masahaba wakubwa mfano wa Abubakr Siddiq na Umar Al-Farouq.....

Isipokuwa mara nyingi nimekuwa natulizana mbele ya maandiko kama haya ili nichunguze sehemu zinazoathiri uhusiano wao na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.w.t.), kutokana na wao kwenda kinyume na maamrisho yake na matakwa yake mwishoni mwa umri wake Mtukufu Mtume (s.a.w.) hali ambayo ilimkasirisha na kumfanya awaamuru wote watoke nje. Vile vile naweka mbele matukio yaliyopita baada ya kufariki Mtume na aliyofanyiwa Binti ya Mtume Bibi Fatmah miongoni mwa maudhi hali yakuwa Mtume (s.a.w.) amesema, "Fatmah ni sehemu ya mwili wangu, mwenye kumkasirisha hakika amenikasirisha mimi.

Naye Bibi Fatmah alisema kuwaambia Abu Bakr na Umar, "Nakuapieni Mwenyezi Mungu Mtukufu, Je, ninyi hamjamsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akisema, Ridhaa ya Fatmah ni katika riadhaa yangu, na kuchukia kwa Fatmah ndiyo kuchukizwa kwangu, basi yeyote mwenye kumpenda Binti yangu Fatmah hakika amenipenda mimi, na mwenye kumridhisha Fatmah basi ameniridhisha mimi, na mwenye kumkasirisha Fatmah amenikasirisha mimi." Wakasema, "Ndiyo tumeyasikia (hayo) kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi." Fatmah akasema, "Basi mimi ninamshuhudisha Mwenyezi Mungu na Malaika wake kwamba ninyi mumenichukiza Mimi na wala hamukuniridhisha. Na pindi nitakapokutana na Mtume Wallahi nitawashitaki."

*(Taz: Al-Imamah Was-Siyasa cha ibn Juz.1 uk.20, Fadakun Fit-Tarikh uk. 92).*

Hebu tuachane na riwaya hizi ambazo zinaumiza moyo, kwani huenda Ibn Qutaybah naye ni miongoni mwa wanachuoni wa Kisunni waliojitokeza katika fani nyingi na anazo tungo nyingi za tafsiri, hadithi, lugha, nahau na historia, basi huenda ameshakuwa Shia kama alivyoniambia mtu fulani miongoni mwa wapinzani pale nilipomuonesha kitabu cha (Ibn Qutaibah) kiitwacho, *"Tarikh Al-Khulafa"*.

Madai kama haya ndiyo wanayoyakimbilia baadhi ya wanachuoni wetu wanapokosa njia, basi Tabari huku kwetu ni Shia, na Imam Nasai ambaye alitunga kitabu kinachohusu sifa makhususi za Imam Ali ni Shia, Ibn Qutaibah naye ni Shia hadi Twaha Husein ambaye ni miongoni mwa wanachuoni wa zama zetu naye ni Shia, eti tu kwa kuwa ametunga kitabu chake kiitwacho, *"Al-Fitnatul-Kubra"*. (fitna kubwa) na humo akaeleza hadithi ya Ghadir, na akayakubali mambo mengi yenye ukweli basi naye kawa Shia!!!

Lakini ukweli ulivyo wote hawa hawakuwa Mashia, bali wanapozungumza kitu kuhusu Mashia, hawawataji Mashia isipokuwa kwa sifa mbaya, pia (wanachuoni hawa) wanatetea uadilifu wa Masahaba kwa kila njia inayowezekana. Lakini mtu yeyote anayeeleza ubora wa Imam Ali ibn Abi Talib na akakiri juu ya mambo yaliyofanywa na Masahaba wakubwa basi tunamtuhumu kuwa ni Shia. Na inatosha tu kusema mbele ya mmoja wao wakati unapomtaja Mtume, (ukasema), "*Sala Llahu Alaihi Waalihi Was-Salama"* au useme, *"Ali alaihis-Salaam" t*ayari utaambiwa wewe ni "Shia".

Na kwa msingi huu, siku moja nilimwambia mmoja wa wanachuouni wetu katika hali ya majadiliano, "Una maoni gani juu ya Bukhari"? Akasema, "Yeye ni miongoni mwa Maimamu wa hadithi, na kitabu chake ni sahihi mno kwetu sisi kuliko vitabu vingine baada ya kitabu cha Mwenyezi Mungu, na wanachuoni wetu wamekubaliana juu ya hilo."

Basi mimi nikamwambia, "Bila shaka Bukhari ni Shia" akacheka kwa kicheko cha dharau kisha akasema, "Haiwezekani Bukhari akawa Shia."

Mimi nikasema, “Je, siyo wewe uliyesema kwamba kila asemaye” Ali Alaihis-Salaam ni Shia?” Akasema, “Bila shaka nimesema.” Basi nikamuonesha yeye na waliokuwa pamoja naye Sahih Bukhari tena mahala pengi kila linapokuja jina la Ali yeye husema; Alaihis-Salaam, na Fatmah Alaihas-Salaam, na Husein ibn Ali Alaihimas-Salaam.  Basi alichanganyikiwa asijuwe alisemalo.

Narejea tena kwenye ile riwaya ya Ibn Qutaibah ambayo amedai kwamba, Bibi Fatmah (a.s.) aliwakasirikia Mabwana Abubakr na Umar, basi iwapo wewe utakuwa na mashaka nayo, mimi siwezi kuitilia shaka *Sahihi Bukhari* ambayo huku kwetu ni kitabu Sahihi mno baada ya kitabu cha Mwenyezi Mungu, nasi tumejilazimisha wenyewe kuwa ni kitabu sahihi. Hawa  Mashia wanawajibika kukitolea hoja dhidi yetu ili watulazimishe kukubali hoja zao kwa kutumia kitu ambacho sisi wenyewe tumejilazimisha (kuwa ni sahihi), na namna hii ndiyo uadilifu kwa watu wenye akili.

Basi huyu hapa Bukhari ameandika ndani ya mlango uitwao, “Ubora wa Qaraba (Jamaa) wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu” kwamba, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amesema, “Fatmah ni sehemu itokanayo na mimi, basi yeyote mwenye kumkasirisha, amenikasirisha mimi.”

Pia ameandika katika mlango wa Ghaz-watu Khaibar kutoka kwa Bibi Aisha amesema, “Fatmah (a.s.) Bint ya Mtume alipeleka ujumbe kwa Abubakr akimtaka ampe mirathi yake aliyoacha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Abubakr akakataa kumpa Fatmah chochote katika mirathi hiyo. Fatmah akamkasirikia Abubakr kuhusu jambo hilo, akamsusa na hakumsemesha tena hadi (Fatmah) alipofariki. *(Taz: Sahih Bukhari Juz.3 uk.39.)*

Matokeo ya mwisho kuhusu kisa hiki ni ya aina moja, Bukhari ameyataja kwa mukhtasari naye Ibn Qutaibah ameyataja kwa urefu, matokeo hayo ni haya: Kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) hukasirika Fatmah anapokasirika na huwa radhi pindi Fatmah anapokuwa radhi, na (hali iliyopo ni) kwamba Fatmah amefariki hali ya kuwa amemkasirikia Abubakr na Umar.

Sasa iwapo Bukhari amesema kwamba Fatmah alifariki hali yakuwa amemkasirikia Abubakr na hakumsemesha hadi alipofishwa, basi ni wazi maana (iliyopo) ni moja tu, na iwapo Fatmah ambaye ni mwanamke bora kuliko wote ulimwenguni kama alivyobainisha Bukhari ndani ya (Kitabul-Istiidhan) katika mlango wa (Man Naaja Baina Yadayn-Nas). Pia iwapo Fatmah ndiye mwanamke pekee katika umma huu ambaye Mwenyezi Mungu amemuondolea uchafu na kumtakasa kikamilifu, basi hawezi kukasirika kwa jambo lisilokuwa la haki, na ndiyo maana Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake wanachukia kwa kuchukia kwake Fatmah, na kwa ajili hiyo Abubakr alisema: “Mimi na jilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana na kuchukia kwake na kuchukia kwako Ewe Fatmah.” Kisha Abubakr alilia mno mpaka karibu nafsi yake itoke, na huku Fatmah akisema, “Wallahi nitamuomba Mwenyezi Mungu dhidi yako ndani ya kila sala nitakayoisali.” Abubakr alitoka hali yakuwa analia huku anasema, “Sina haja na Baia yenu tengueni Baia yangu.”

*(Taz: Tarekh Al-Khula-faa ambacho ni maarufu kwa Jina la Al-Imamah Was-Siyasah cha Ibn Qutaibah Ad-Dainūri Juz.1 uk.20).*

Lakini wengi wa wanahistoria na baadhi ya wanachuoni wetu wanakiri kwamba Fatmah (a.s.) alimkasirikia Abubakr kuhusu qadhia ya zawadi ya shamba alilopewa na Baba yake na mirathi na sehemu ya Qaraba wa Mtume (s.a.w.), kwani madai ya Fatmah yalikataliwa mpaka akafariki hali yakuwa amemkasirikia, isipokuwa (wanahistoria hao na wanachuoni wanapotaja) matukio haya hupita wima na wala hawataki kusema kitu kuhusiana nayo ili tu kulinda heshima ya Abubakr kama ilivyo kawaida yao kwa kila jambo linalomgusa kwa karibu au kwa mbali. Miongoni mwa maajabu niliyoyasoma kuhusiana na maudhui hii ni kauli ya baadhi yao baada ya kutaja sehemu ya tukio kwa urefu husema: “Haiwezekani Fatmah kudai kitu kisichokuwa haki yake na haiwezekani kwa Abubakr kumzuwilia Fatmah haki yake.”

Na kutokana na mizani hii ya ajabu, mwanachuoni huyu alidhani kwamba ametatua tatizo na amewakinaisha watafiti. Maneno yake haya ni sawa na kauli ya msemaji asemaye: “Haiwezekani Qur’an kusema jambo lisilo la kweli, pia haiwezekani kwa Banu Israil kuabudia ndama.”

Hakika tumepata mtihani kwa kuwa na wanachuoni wanaosema wasiyoyajua na wanaoamini vitu viwili vinavyopingana kwa wakati mmoja, (ajabu mwanachuoni) akasisitiza kwamba Fatmah alipeleka madai na Abu Bakr akayapinga madai yake, basi ima Fatmah awe ni muongo (Mwenyezi Mungu apishe mbali) hawezi kuwa hivyo, au basi Abu Bakr awe amemdhulumu Fatmah, na hakuna aina nyingine ya tatu ya ufumbuzi wa suala hili kama wanavyotaka baadhi ya wanachuoni wetu.

Na ilivyoshindikana kwa dalili za kiakili na za maandiko kuwa Fatmah ni muongo kutokana na maneno ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu yaliyothibiti aliposema: "Fatmah ni sehemu iliyotokana nami, yeyote mwenye kumuudhi, basi atakuwa kaniudhi mimi". Bila ubishi muongo yeyote hawezi kustahiki mfano wa kauli hii itokayo kwa Mtume (s.a.w.), kwani hadithi hii kwa dhati yake inajulisha juu ya Ismah kuhifadhika kwa Bibi Fatmah kutokana na kusema uongo na mambo mengine machafu. Kama ambavyo ile aya ya utakaso nayo inajulisha juu ya Ismah yake, na hapana shaka kwamba iliteremka kwa ajili ya Bibi Fatmah, Mumewe na Wanawe wawili Hasan na Husein (a.s.) na hili ni kwa ushahidi wa Bibi Aisha mwenyewe. (Taz: Tarekh Al-Khulafai Juz.1 uk. 20.

Kwa hiyo basi hakuna kinachobakia isipokuwa ni watu wenye akili wakubaliane kwamba, Bibi Fatmah (a.s.) alidhulumiwa. Kukanusha madai ya Bibi Fatmah ni jambo jepesi kwa mtu aliyeruhusu kumchoma moto iwapo wapinzani waliomo nyumbani mwake hawatotoka nje ya nyumba na kwenda kuwapa Baia mabwana hao. (Taz: Tarekh Al-Khulafai Juz.1 uk.20).

Na kutokana na (matatizo) yote haya ndiyo maana unamuona (Fatmah a.s.) hakuwaruhusu kuingia nyumbani mwake walipomuomba ruhusa, ama pale Imam Ali alipowaingiza ndani, yeye aligeuza uso wake kuelekea ukutani na hakuwa radhi kuwaangalia. (Taz: Rarekh Al-Khulafa, Juz.1 uk.20).

Kwa hakika Bibi Fatmah alifariki na akazikwa usiku kwa mujibu wa usia wake ili tu asijehudhuria yeyote miongoni mwao, na kaburi lake limebakia katika hali ya kutofahamika mahali lilipo hadi leo hii. Kwa hiyo mimi najiuliza ni kwanini wanachuoni wetu wanaunyamazia ukweli

huu wala hawataki kuufanyia utafiti, wala hata kuuelezea na wanatupatia picha ya Masahaba wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kama kwamba wao ni Malaika wasiokosea wala kutenda dhambi.

Na ikiwa utamuuliza mmoja wao ni vipi Khalifa wa Waislamu Sayyidna Uthman Dhun-Nurain aliuawa, atakujibu kwamba, Wamisri (ambao ni makafiri) walikuja na wakamuuwa. Maudhui hii hukamilika kwa sentensi mbili tu. Lakini nilipopata fursa ya kufanya uchunguzi na kuisoma historia nikakuta kwamba, walio mstari wa mbele katika wauaji wa Uthman ni hao hao Masahaba wakiongozwa na Ummul-Muuminina Aisha ambaye alikuwa akinadi auawe na kuihalalisha damu yake mbele ya watu na alikuwa akisema: "Muuweni mpumbavu amekufuru."

Pia tunamkuta Tal-ha, Zuberi na Muhammad ibn Abi Bakr na wengineo miongoni mwa Masahaba mashuhuri, walimzingira na wakamzuia asinywe maji ili tu wamlazimishe kujiuzulu.

Wanahistoria wanatusimulia kuwa ni hao hao Masahaba ndiyo waliomzuwilia Uthman asizikwe ndani ya eneo la makaburi ya Waislamu, na akazikwa (Hash Kaukab) bila ya kukoshwa wala kusaliwa, Subhanallah! Basi ni vipi tuambiwe kuwa aliuawa kwa kudhulumiwa na kwamba waliomuuwa siyo Waislamu?

Ni kisa kingine kinachofanana na qadhia ya Bibi Fatmah na Abubakr, kwa hiyo ima Sayidna Uthman atakuwa ndiye aliyedhulumiwa na ikiwa hivyo basi (itabidi) tuwahukumu Masahaba waliomuua au walioshiriki mauaji yake kwamba wao ni wauaji tena waovu kwa sababu wamemuua Khalifa wa Waislamu kwa dhulma na uadui na wakalifuatia jeneza lake wakalipiga kwa mawe, wakamdhalilisha akiwa hai na baada ya kufa. Au Masahaba hawa walihalalisha mauaji ya Uthman kutokana na mambo aliyoyatenda ambayo yanapingana na Uislamu kama ilivyoelezwa ndani ya vitabu vya historia. Hakuna namna nyingine ya kati na kati itakayosawazisha isipokuwa kama tutaikanusha historia na tukachukua upotofu (usemao) kwamba, "Wamisri ambao walikuwa makafiri ndiyo waliomuua." Na katika namna zote mbili kuna kanusho madhubuti kwa ile kauli inayohusu uadilifu wa Masahaba wote bila kubakisha, basi (kama ni hivyo) ima Uthman atakuwa siyo muadilifu au waliomuua siyo

waadilifu (kwani) wote hawa ni miongoni mwa Masahaba na kwa sababu hiyo yanabatilika madai yetu (ya uadilifu wa Masahaba wote).

Kinachobakia ni madai ya wafuasi wa nyumba ya Mtume wasemao kwamba, "Uadilifu uko kwa baadhi tu miongoni mwao na kwa wengine haupo."

Na tunajiuliza kuhusu vita ya Jamal ambayo moto wake uliwashwa na Ummul-Muuminin Aisha, kwani yeye mwenyewe ndiye aliyeiongoza. Ni vipi Umul-Muumina Aisha anatoka nje ya nyumba yake ambayo Mwenyezi Mungu ameamrisha kukaa ndani yake aliposema:

> *"Kaeni majumbani mwenu wala msioneshe mapambo yenu kama walivyokuwa wakionesha mapambo yao wanawake wa zama za Jahiliya: (Qur. 33:33)*

Sisi tunauliza, ni kwa haki gani iliyomfanya Ummul-Muuminina ahalalishe kumpiga vita Khalifa wa Waislamu Ali ibn Abi Talib ambaye ni walii wa kila Muumini mwanaume na mwanamke?

Kama ilivyo kawaida na kwa ufafanuzi wanachuoni wetu wanatupatia jawabu ya kwamba, Bibi Aisha alikuwa hampendi kwa sababu Ali alimuashiria Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ampe talaka katika lile tukio la *"Ifki"*, na wanachuoni wetu hawa wanataka kutukinaisha ya kwamba tukio hili (iwapo litasihi) ambalo ni ishara ya Ali kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amuache Bibi Aisha, linatosha kabisa kumfanya amuasi Mola wake na kubomoa stara aliyowekewa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) hatimaye akapanda ngamia ambaye Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimkataza kumpanda na alimhadharisha kwamba atabwekewa na mbwa wa Hauab.? Lakini Bibi Aisha alikata masafa marefu kutoka Madina hadi Maka na kutoka Maka akaenda hadi Basra, akahalalisha mauaji ya watu wasio na hatia na akampiga vita Jemedari wa waumini pamoja na Masahaba waliompa Baia na kusababisha mauaji ya maelfu ya Waislamu kama walivyoeleza wanahistoria. (Taz: Tabari, Ibn Al-Athir, Almadaini na wengineo miongoni mwa wanahistoria waliohadithia matukio ya mwaka wa thelathini na sita A.H.)

Yote haya ni kwa sababu Bibi Aisha alikuwa hampendi Imam Ali ambaye alimuashiria Mtume ampe talaka, lakini pamoja na hali hiyo Mtume hakumtaliki. Basi chuki yote hii ni ya nini na hapana shaka kwamba wanahistoria wameandika msimamo wa uadui usiyoweza kutafsirika aliokua nao Bibi Aisha kwa Imam Ali. Kuna kipindi Bibi Aisha alikuwa akirudi Madina kutoka Maka, akiwa njiani alijulishwa kuhusu kuuawa kwa Uthman, basi alifurahi sana. Lakini alipofahamu kwamba watu wamempa Baia Imam Ali, alikasirika na kusema, "Natamani mbingu ingeliifunika ardhi kabla mwana wa Abu Talib hajatawalia kiti cha Ukhalifa." Kisha akasema tena, "Nirudisheni". Hapo ndipo alipoanza kuwasha moto wa fitnah ili kumpindua Imam Ali ambaye hakutaka hata kumtaja jina lake kama walivyoandika wanahistoria kuhusu Bibi Aisha.

Basi Je, Umul-Muuminina Aisha hakusikia kauli ya Mtume (s.a.w.) kwamba, "Kumpenda Ali ni imani, na kumbughudhi ni unafiki? Kiasi kwamba baadhi ya Masahaba wamesema; "Tulikuwa hatuwatambui wanafiki isipokuwa kwa kumbughudhi kwao Ali."

Je, Ummul-Muuminina hakuisikia kauli ya Mtume (s.a.w.) aliposema, "Yule ambaye mimi nilikuwa nikitawalia mambo yake, basi Ali ni mtawala wa mambo yake." Hapana shaka alisikia yote hayo lakini hakumpenda Ali wala hakuweza kutaja hata jina lake, bali aliposikia kuwa Ali amefariki alisujudu sijda ya kumshukuru Mwenyezi Mungu. *(Taz: Tabari, ibn Al-Athir na wanahistoria wengine walioandika matukio ya mwaka wa arobaini A.H.)*

Na tuyaachilie mbali yote haya, mimi sitaki kuichambua historia ya Ummul-Muuminina Aisha, lakini nikitakacho nikuleta ushahidi unaohusu Masahaba kwenda kinyume na misingi ya Uislamu, kukhalifu kwao amri za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) na inanitosha fitna (aliyoizua) Ummul-Muuminina kuwa ni dalili moja ambayo wanahistoria wamekubaliana juu yake, wamesema kuwa, "Pindi Mama Aisha alipoyapita maji ya Hauab mbwa wa mahali hapo walimbwekea wakimkumbusha lile onyo na katazo la Mumewe ambaye ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu kupanda ngamia (wa fitna), basi Mama Aisha alilia na kusema, "Nirudisheni, nirudisheni."

Lakini Tal-ha na Zubair wakamletea watu khamsini waliowapa rushwa, wakamuapia Mama kwa Mwenyezi Mungu ya kwamba hapa sipo kwenye maji ya Hauab, basi Mama (akadanganyika) akaendelea na Safari yake mpaka Basra. Wanahistoria wanaeleza kwamba, huo ndio ulikuwa ushahidi wa kwanza wa uongo ndani ya Uislamu. *(Taz: Tabari, Ibn Al-Athir Al-Madain na wengineo walioyataja matukio ya mwaka wa thelathini na sita).*

Tuambieni Enyi Waislamu, Enyi wenye akili pevu inayoweza kufumbua fumbo hili, Je, hawa ndiyo Masahaba watukufu ambao sisi tunahukumu kuwa ni waadilifu na kuwafanya kuwa ndiyo viumbe bora baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.)? Wanaoshuhudia ushahidi wa uongo kitendo ambacho Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amekihesabu kuwa ni miongoni mwa madhambi makubwa yanayoangamiza, ambayo yanampeleka mtu motoni?

Suala hili siku zote linajirudia na kukaririka, Je, ni yupi yuko katika haki na ni yupi yuko katika upotofu? Basi imma Ali pamoja na wote aliokuwa nao ni madhalimu na hawako katika haki, na au Aisha na wale aliokuwa nao na Tal-ha na Zubairi na wale waliokuwa nao ni madhalimu na hawakuwa katika haki. Na imma Aisha na aliokuwanao na Twalha na Zubair na waliokuwa pamoja nao ni madhalimu na hawakuwa juu ya haki, hakuna mtazamo mwingine wa tatu. Mchunguzi muadilifu simuoni isipokuwa ataelekea kwenye haki ya Ali ambaye, Haki inazunguka pamoja naye popote azungukiapo, na kuiponda fitna ya "Umul-Muuminina Aisha na wafuasi wake ambao waliuwasha moto wa fitna na hawakuuzima mpaka ulipokuwa umeunguza vibichi na vikavu na athari zake zimebakia mpaka leo.

Ili kuongezea uchunguzi na ili moyo wangu utulie nasema, "Bukhari ameandika ndani ya Sahih yake katika *Kitabul-Fitnah*, ambayo inavuma kama yanavyovuma mawimbi amesema: "Pindi Tal-ha na Zubair na Aisha walipokwenda Basra, Ali alimtuma Ammar ibn Yasir na Hasan ibn Ali wakaenda Al-kufah, kisha wakapanda juu ya mimbar, Hasan ibn Ali alikuwa juu kabisa ya mimbar na Ammar ibn Yasir alisimama chini kidogo ya Hasan. Tulikusanyika kwa ajili yake, nami nilimsikia Ammar anasema: "Bila shaka Aisha amekwishakwenda Basra, Wallahi yeye ni mke wa

Mtume wenu hapa duniani na kesho Akhera, lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu amekupeni mtihani ili abainishe, Je, mtamtii yeye Mwenyezi Mungu au Aisha?" *(Taz: Sahih Bukhari Juz.4 uk.161).*

Pia Bukhari ameandika ndani ya Sahihi yake, Kitabus-Shurut Babu Majaa Fi Buyuut Az-Wajin-Nabi amesema: "Mtume (s.a.w.) alisimama akahutubia, hatimaye aliashiria yaliko makazi ya Aisha kisha akasema, hapa ndipo itapoanzia fitina, hapa ndipo itapoanzia fitna, hapa ndipo itapoanzia fitna, wakati itakapochomoza pembe ya shetani." *(Taz: Sahih Bukhar uk.128).*

Kadhalika Bukhari ameandika ndani ya Sahih yake mambo ya ajabu na ya kushangaza juu ya tabia isiyo nzuri ya Bibi Aisha (aliyokuwa) akimfanyia Mtume (s.a.w.) kiasi kwamba Baba yake alimpiga na kumvujisha damu.

Na baada ya yote haya, najiuliza ni vipi mama Aisha alistahiki heshima zote hizi (apewazo) kwa *Ahlus-Sunnah Wal-Jamaa?* Hapana kingine isipokuwa kwa kuwa ni mke wa Mtume, lakini wake wa Mtume ni wengi na miongoni mwao wako waliobora kuliko Aisha kwa mujibu wa utambulisho wa Mwenyewe Mtume. *(Taz: Sahih tir-midhi, Al-Istiiabu Tarjuma ya Safiyyah, Al-Isabah Tar-Juma ya Safiyyah Ummul-Muuminina).*

Labda kwa vile yeye ni Binti wa Abubakr na yeye ndiye aliyeisimamia kwa kiwango kikubwa kampeni ya kukanusha wasia wa Mtume kwa Ali kiasi kwamba pindi alipoambiwa kwamba Mtume aliuisia kwa Ali akasema, "Nani aliyesema hivyo, kwa hakika Mtume alikuwa kaegemea kifuani pangu, aliomba dishi la maji ghafla alidhoofika na kufa."

Au kwa sababu alimpiga Ali vita isiyo na huruma, na baada ya Ali akawafanyia hivyo hivyo wanawe mpaka alizuwia jeneza la Hasan Bwana wa vijana wa peponi na akakataza asizikwe pembezoni mwa Babu yake Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) akasema (Bibi Aisha), "Msimuingize nyumbani mwangu mtu nisiyempenda." Mama Aisha alisahu kauli ya Mtume kuhusu Hasan na nduguye, "Hasan na Husein ni Mabwana wa vijana wa peponi." Au kauli ya Mtume isemayo: "Mwenyezi Mungu ampende awapendaye (Hasan na Husein) na Mwenyezi Mungu amkasirikie anayewabughudhi wao." Au aliposema: "Mimi nampiga vita

anayekupigeni vita, na nitampa amani mwenye kukupeni amani." Na kauli nyinginezo nyingi ambazo sitozieleza - Ni kwanini (wasistahiki sifa hizi) hali ya kuwa wao ni pambo la Umma huu?

Haishangazi kwani amekwisha sikia mengi zaidi ya hayo kuhusu haki ya Ali, lakini licha ya maonyo ya Mtume (s.a.w.) kwa mama Aisha, hakukubali isipokuwa (akaendelea) kumpiga vita Imam Ali na kuwahimiza watu wampinge na kuzikanusha fadhila zake na ubora wake.

Na kwa ajili hiyo, Banu Umayyah walimpenda na kumuweka kwenye daraja hiyo kubwa na wakasimulia mengi juu ya fadhila za Mama Aisha, ambazo zimeenea kila pahali, mpaka wakamfanya kuwa ndiyo rejea kubwa ya (dini katika) Umma wa Kiislamu kwani eti yeye peke yake anayo nusu ya maarifa ya Dini.

Na huenda nusu ya pili ya dini wamemuhusisha nayo Abu Hurairah ambaye kapokea (na kusimulia) kwa (manufaa ya Banu Umayyah) mambo wayapendayo, ndipo nao walipomsogeza karibu yao na kumpa ugavana wa mji wa Madina na kumjengea jumba kubwa la Aqiqi, ambapo hapo kabla alikuwa mtu duni kisha wakampa Laqabu ya kuwa ni *Msimulizi wa Uislamu.*

Na kwa ajili hiyo ikawa ni jambo rahisi kwa Banu Umayyah kupata Dini yao iliyo kamilika ambayo ndani yake hakuna kitabu cha Mwenyezi Mungu wala Sunna ya Mtume wake, bali kilichomo ni yale mambo ambayo nafsi zao zinayataka na kuimarisha ufalme wao na nguvu zao. Na stahiki ya Dini hii (ya Banu Umayyah) ni kuwa imejaa mchezo na upuuzi na uzushi, na kutokana na hali hii ukweli halisi ukafutwa na pahali pake pakakaa kiza.

Bila shaka waliwalizimisha watu kufuata misingi ya dini yao na kuwadanganya mpaka dini ya Mwenyezi Mungu kwao wao ikawa ni kitu cha mzaha miongoni mwa mizaha, wakakosa kuithamini na wala watu hawakumuogopa Mwenyezi Mungu kama walivyokuwa wakimuogopa Muawiyah.

Pindi tuwaulizapo wanachuoni wetu kuhusu sababu za Muawiyah

kumpiga vita Imam Ali, vita kali iliyosababisha Waislamu wagawanyike kwenye Usunni na Ushia, na Uislamu nao ukabomoka na usiungike hadi leo, wakati ambapo Muhajirina na Ansari walikwisha kumpa Baia Ali, wao hujibu kama ilivyo kawaida yao tena kwa urahisi tu husema, "Hapana shaka Ali na Muawiyah ni Masahaba watukufu, wote walifanya ijtihadi, Ali alifanya jitihada na akapatia hivyo ana ujira mara mbili, na Muawiyah alijitahidi akakosea basi anao ujira mmoja, nasi hatuna haki kutoa hukumu dhidi yao, na Mwenyezi Mungu amesema. *"Hao ni Umma ambao umeshapita, wanayo yao waliyoyachuma, nanyi munayo yenu mliyoyachuma, na wala hamtaulizwa kwa yale waliyokuwa wakiyatenda."*

Hivi ndivyo ilivyo, inahuzunisha! majibu yetu yanavyokuwa ni kama unavyoona yanapotosha, akili haikubali na wala dini wala sheria haikubaliani nayo. Ewe Mwenyezi Mungu najitakasa kwako kutokana na maoni potofu na kuteleza kwa kufuata matamanio na najilinda kwako na upotofu wa shetani na najilinda kwako asinifikie."

Ni vipi akili iliyosalama itaamua kuwa jitihada ya Muawiyah itampa ujira mmoja kwa kumpiga vita Imam wa Waislamu, na kwa kuwauwa Waislamu wasiyokuwa na hatia na kwa maovu na machafu aliyoyafanya ambayo hakuna awezaye kudhibiti hesabu yake isipokuwa Mwenyezi Mungu.

Hapana shaka Muawiyah ni mashuhuri mbele ya wanahistoria kwa mauaji yake dhidi ya wapinzani wake, na jinsi wanavyomsifia kutokana na matumizi ya njia yake mashuhuri (katika kutekeleza mauaji) nayo ni kuwalisha (wapinzani wake) Asali iliyotiwa Sumu, - na alikuwa akisema, "Hakika Mwenyezi Mungu anao askari ndani ya asali."

Ni vipi wanachuoni wetu hawa wanaohukumu kuwa alifanya ijtihadi na kumpa ujira hali yakuwa hapana shaka kwamba Muawiyyah alikuwa ni Imamu wa kundi potofu? Kwani ndani ya hadithi mashuhuri ya Mtume ambayo imeandikikwa na wanachuoni wote wa hadithi wa Kisunni na Kishia na wengineo (Mtume kasema), "Nakuhurumia Ewe Ammar, litakuua kundi potofu." Hawajakhitilafiana Waislamu wawili kwamba aliyemuua Ammar na jamaa zake kuwa ni Muawiyah, basi vipi wanahukumu juu ya

ijtihadi yake naye ndiye aliyemuuwa Hujr ibn Adiyi na jamaa zake ndani ya kifungo na akawazika huko *Murju Adh-raa* katika jangwa la Shamu, kwa sababu tu wamekataa kumtukuana Ali ibn Abi Talib.

Ni vipi basi wanamtaka awe Sahaba muadilifu wakati ndiye aliyemtilia sumu Hasan ibn Ali Bwana wa vijana wa peponi na akamuua?

Ni vipi wanamtakasa hali yakuwa alichukua Baia kutoka kwa Umma wa Waislamu kwa nguvu, kwanza kwa nafsi yake kisha na mwanawe Yazid muovu, na akabadili utaratibu wa mashauriano na kufanya kuwa ufalme wa Kaisari?

*(Taz: Al-Khilafatu Wal-Mulk, cha Maudud na Yaumul-Islam cha Ahmad Amin.*

Namna gani wanahukumu juu ya ijtihad yake na kumpa ujira, hali yakuwa aliwalazimisha watu wamlaani Ali juu ya mimbari yeye na Watu wa nyumba ya Mtume ambao ni kizazi cha Mtume? Aliawaua Masahaba waliokataa kufanya hivyo, laana hiyo ikawa ni sunna inayofuatwa, watu huzeeka wakiifanya na watoto wadogo nao hukua hali yakuwa wanafanya hivyo. *"La haula Wala Quwwata Illah Billahil-aliyyil-Adhim".*

Swali siku zote lina rudi na kukaririka, Ewe Bwana ni nani kati ya makundi mawili aliye juu ya haki na ni yupi kati yao yuko kwenye upotufu?

Basi Imam Ali na wafuasi wake ni madhalimu na hawako kwenye haki, au Muawiyah na wafuasi wake ni madhalimu na hawako kwenye haki?

Kwa hakika Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) alikwishaweka wazi kila kitu.

Katika namna zote mbili bila shaka Masahaba wote kuwa waadilifu bila ya kumtoa hata mmoja ni jambo lisilowezekana wala halikubaliani na mantiki.

Maudhui zote hizi zina mifano mingi ambayo hawezi kudhibiti idadi yake isipokuwa Mwenyezi Mungu, na lau ningetaka kuingia kwa undani

na kuzitafiti kila upande ningehitajia vitabu vingi, lakini nilitaka kufanya mukhtasari, na nikachukua baadhi ya mifano tu kwa ajili ya utafiti huu. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba utafiti huu utakuwa ni wenye kutosheleza kubatilisha madai ya watu wangu ambao walizigandisha fikra zangu muda mrefu na wakanidumaza nisifahamu hadithi wala kuyachambua matukio ya kihistoria kwa kutumia mizani ya akili na vipimo vya kisheria ambavyo Qur'an na Sunna Tukufu ya Mtume vimetufunza.

Na kwa sababu hiyo basi nitaipinga nafsi yangu na kulipangusa vumbi la ung'ang'anizi walilonifunika, ili nijikomboe kutokana na vifungo na minyororo waliyonifunga nayo kwa zaidi ya miaka ishirini.

Kielelezo changu nawaambia kwamba, "Laiti watu wangu wangejua alivyonisamehe Mola wangu na akanifanya kuwa miongoni mwa waliokirimiwa. Oh! Laiti watu wangeuvumbua ulimwengu wasiyoujua na wanaoufanyia uadui bila ya kuufahamu!

# MWANZO WA KUBADILIKA

Nilibakia nimechanganyikiwa na kupigwa butwaa kwa muda wa miezi mitatu, hata usingizini nilikuwa navutana na fikra na mchanganyiko wa mawazo. Naihofia nafsi yangu kutokana na baadhi ya Masahaba niliokuwa nikihakiki historia yao, na kuchunguza baadhi ya mfarakano wa kutatanisha katika mienendo yao. Kwani mafunzo niliyokwishayapata muda wote wa maisha yangu yananitaka kuwaheshimu na kuwatukuza Mawalii wa Mwenyezi Mungu na wacha Mungu miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu ambao humdhuru yeyote awasemaye kwa ubaya au kuwakosea adabu hata kama hawapo au wamekufa.

Nilipata kusoma hapo zamani ndani ya kitabu kiitwacho, *"Hayatul-Hayawan Al-kubra"* cha Ad-Dumairi ya kwamba kuna mtu fulani alikuwa akimshutumu Umar ibn Al-Khatab, walikuwako jamaa zake ndani ya msafara huo wakimkataza, basi alipokwenda kujisaidia haja ndogo akaumwa na nyoka mweusi akafa pale pale. Wakachimba kaburi ili wamzike, humo kuburini wakamkuta nyoka mweusi, kisha wakachimba makaburi mengine na ndani ya kila kaburi walimkuta nyoka mweusi, basi mtu mmoja mwenye maarifa miongoni mwao akawaambia, "Mzikeni vyovyote mupendavyo, kwani hata kama mutaichimba ardhi yote basi mtamkuta nyoka mweusi, na hii ni kwakuwa Mwenyezi Mungu anataka amuadhibu duniani kabla ya huko Akhera kutokana na kosa lake la kumshutumu Sayyidna Umar."

Na kwa ajili hii utanikuta naitosa nafsi yangu ndani ya utafiti huu mzito, hali ya kuwa ni mwenye khofu ninababaika, khususan kwa kuwa mimi nimejifunza katika kitengo cha *"Az-Zaituni"* ya kwamba uhakika ulivyo, mbora wa Makhalifa ni Sayyidna Abubakris-Sidiq kisha baada yake ni Sayyidna Umar ibn al-Khatab Al-Farouq, ambaye kupitia kwake Mwenyezi Mungu huitenganisha haki na batili, kisha baada yake ni Sayyidina Uthman ibn Affan Dhun-Nurain ambaye Malaika wa Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma walimstahi na kisha baada yake ni Sayyidna

Ali ambaye ndiye mlango wa mji wa Elimu, kisha baada ya hawa wanne, waliobaki ni Masahaba sita miongoni mwa kumi waliobashiriwa pepo. Hao ni Tal-ha, Zubair, Saad, Said, Abdur-rahman na Abu Ubaidah. Na Baada ya hawa wanakuja Masahaba wote, na mara nyingi walipokuwa wakinifunza hutolea ushahidi wa aya ya Qur'an Tukufu isemayo: *"Hatutofautishi baina ya yeyote miongoni mwa Mitume wake,"* inayo wajibisha kuwaheshimu Masahaba waliobakia kwa aina ile ile ya heshima bila kumtia dosari yeyote kati yao.

Na kwa msingi huu nilichelea nafsi yangu, nikamuomba Mwenyezi Mungu mara nyingi anisamehe nikikusudia katika msamaha huo niache kuendelea na utafiti wa mambo kama haya ambayo yananifanya niwatilie mashaka Masahaba wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, zaidi ya hivyo yananifanya niitilie Mashaka dini yangu.

Lakini muda wote nilipokuwa nikizungumza na baadhi ya wanachuoni, nilikuta mambo yanayopingana ambayo hayakubaliki kiakili, walianza kunionya kwamba mimi ninafanya utafiti juu ya mazingira na hali za Masahaba, jambo hili ni hatari huenda Mwenyezi Mungu akanipokonya neema yake na kuniangamiza.

Kutokana na upinzani wao na kukanusha kwao kila nilisemalo utashi wangu wa kielimu na pupa yangu ili nifikie uhakika ilinilazimu kuitosa upya nafsi yangu ndani ya utafiti na nikapata nguvu ya ndani iliyonishinikiza sana.

# MAJADILIANO NA MWANACHUONI

Kuna mwanachuoni mmoja nilimwambia: "Ikiwa Muawiyah aliwauwa watu wasiokuwa na hatia na kuwavunjia heshima, nanyi mnasema kwamba alijitahidi akakosea na atapata ujira mmoja. Na iwapo Yazid ndiye aliyewaua Watoto wa Mtume na akaruhusu jeshi lake liukalie mji wa Madina, na (kwa tendo hili) ninyi mnasema kwamba alifanya ijtihadi akakosea na atapata ujira mmoja, kiasi kwamba baadhi yenu wamesema kuwa, *Husein (a.s.) aliuawa kwa upanga wa Babu yake* ili walitakase tendo la Yazid. Basi ni kwanini nami nisifanye jitihada katika utafiti, kitu ambacho kinanipa msukumo wa kuwatilia mashaka masahaba na kuwatoa baadhi yao miongoni mwao, na hili jambo (nilifanyalo mimi) huwezi kulilinganisha na mauaji aliyoyafanya Muawiyah na mwanawe Yazid kwa kizazi kitukufu cha Mtume. Basi nami iwapo nitapatia nitapata ujira mara mbili na nikikosea nitapata ujira mara moja, kwani ninapowakosoa baadhi ya Masahaba sikusudii kuwatukana wala kuwashutumu na kuwalaani, bali ninachokikusudia ni kufika kwenye ukweli ili nilitambue lile kundi lenye uokovu kutokana na makundi potofu. Huu ni wajibu wa kila Muislamu, na Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye ajuaye siri na kila kilichojificha moyoni."

Yule mwanachuoni alinijibu kwa kusema; "Ewe mwanangu hapana shaka kwamba mlango wa Ijtihadi umekwishafungwa siku nyingi."

Nikamwambia, "Ni nani aliufunga"? Akasema, "Maimamu wanne."

Nikasema kwa kujiamini, *"Al-Hamdulillahi!* ikiwa Mwenyezi Mungu na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu siyo walioufunga wala Makhalifa waongofu tulioamriwa kuwafuata, basi si makosa kwangu mimi nikijitahidi kama walivyojitahidi wao." Akasema: "Huwezi kufanya Ijtihadi mpaka uzifahamu fani kumi na saba, miongoni mwa hizo ni: Tafsiri, Lugha, Nahau, Sarfu, Balagha, Hadithi, Historia na nyinginezo."

Nilimkatiza kwa kusema, “Mimi sintafanya Ijtihadi ili niwabainishie watu hukmu za Qur’an na Sunnah, au ili nianzishe Madh-hebu katika Uislamu sivyo kabisa, lakini ili tu nifahamu nani yuko katika haki na nani yuko kwenye upotofu, na ili kufahamu kama Imam Ali yuko katika haki au Muawiyah kwa mfano. Jambo hili halihitajii kufuzu fani hizo kumi na saba, inatosha nisome maisha ya kila mmoja wao na mambo waliyoyafanya ili niutambue ukweli.”

Akasema: “Jambo gani la muhimu linakufanya utake kuyajuwa hayo? Hao ni watu waliopita wanayao waliyoyatenda nanyi munayenu muliyoyatenda na wala hamtaulizwa ni mambo gani walikuwa wakiyatenda.” Nikasema: “Je, unaisoma aya hii *Wala Tas-alūnna,* kwa kuitia fataha ‘Ta’ au kuitia *dhamma* (yaani) *Wala Tus-alūna:? Akasema, “Tus-salūna, kwa dhamma.”*

Mimi nikasema: “Al-Hamdulillah lau ingekuwa kwa fataha uchunguzi ungezuilika, maadam ni kwa *dhamma* basi maana yake ni kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu hatatuadhibu kwa yale waliyoyafanya, na hilo ni kama kauli yake Mwenyezi Mungu isemayo, *“Kila nafsi imefungika kwa yale iliyoyatenda” na “Mtu hatapata (malipo) ila kwa yale aliyoyatenda”.* Na Qur’an Tukufu imetuhimiza kuchunguza khabari za watu waliopita ili tupate mazingatio kutokana na kahabari hizo, na bila shaka Mwenyezi Mungu ametusimulia mambo juu ya Fir-aun, Hamāna, Namrūda, Qārūni na Mitume waliotangulia na mataifa yao siyo kwa lengo la kutuliwaza tu, bali kwa lengo la kutujulisha ukweli kutokana na upotofu.

Amma kauli yako uliposema ni jambo gani la muhimu linalokusukuma kutaka kufanya uchunguzi (wa hayo)? Mimi najibu kuwa, ninao umuhimu wa kuchunguza.

**Kwanza:** Ili nimfahamu Walii wa Mwenyezi Mungu nipate kumpenda, na nimjue adui wa Mwenyezi Mungu ili awe adui yangu. Na jambo hili ndilo ambalo Qur’an inanitaka kulifanya bali imenilazimisha.

**Pili:** Ni muhimu kwangu kufahamu ni jinsi gani nitamuabudu Mwenyezi Mungu na nitajikurubisha kwake kwa Faradhi alizozifaradhisha kama atakavyo yeye Mwenyezi Mungu na siyo kama atakavyo Malik au Abu

Hanifa, au wengineo miongoni mwa wanajitihada, kwani mimi nimemkuta Malik anasema kuwa ni karaha kusoma *Bismillahi Rahmani Rahiim* katika Sala, wakati ambapo Abu Hanifa anasema kuwa ni wajibu, na wengine nao wanasema kuwa Sala inabatilika kama haikusomwa *Bismillah*, na kwa kuwa Sala ni nguzo ya dini, inapokubaliwa basi mema mengine nayo hukubaliwa na ikikataliwa, na mengine nayo hukataliwa, basi mimi sitaki Sala yangu iwe batili.Vile vile Mashia wanasema kuwa, miguu ipakwe wakati wa (kutia) udhu, na Masunni wanasema ikoshwe na wakati huo huo tunasoma ndani ya Qur'an (kama ifuatavyo) *"Pakeni vichwa vyenu na miguu yenu"* na iko wazi kuwa ni kupaka, basi vipi bwana wangu unamtaka Muislamu mwenye akili akubali kauli ya huyo na aipinge ya yule bila kufanya uchunguzi na (kupata) dalili? Akasema: "Ni juu yako kuchukua kutoka kila Madh-hebu lile jambo linalokuathiri, kwani yote ni Madh-hebu ya Kiislamu na wote wanataraji kutoka kwa Mjumbe wa Mungu.

Nikasema, *"Naogopa kuwa miongoni mwa wale aliowasema Mwenyezi Mungu kuwa; Je, umemuona anayefanya matamanio yake kuwa ndiye Mungu wake, na Mwenyezi Mungu akamuacha apotee pamoja na kuwa ana ujuzi, na akapiga muhuri juu ya masikio yake na moyo wake na kumuwekea kifuniko juu ya macho yake, basi ni nani atakayemuongoza baada ya Mwenyezi Mungu, Je, hamzingatii?" (Qur. 45:23)*

Ewe Bwana wangu mimi siamini kwamba Madhehebu yote yako kwenye msingi wa haki maadam tu moja lina halalisha kitu hiki nia jingine linaharamisha kitu kile kile, haiwezekani kitu kimoja kuwa haramu na halali kwa wakati mmoja, na Mtume hakujipinga mwenyewe katika hukmu zake kwani huo ni Ufunuo utokao ndani ya Qur'an. *"Na lau ingekuwa (hii Qur'an) haikutoka kwa Mwenyezi Mungu basi wangekuta ndani muna hitilafu nyingi". (Qur. 4:82).*

Na kwa kuwa (hayo) madh-hebu manne ndani yake kuna hitilafu nyingi, basi (ujuwe) hayakutoka kwa Mwenyezi Mungu, wala kwa Mtume wake kwani Mtume hapingani na Qur'an".

Sheikh huyu alipoona maneno yangu yana mantiki na hoja yangu inakubalika alisema: "Nakusihi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu,

shaka yoyote itakayokupata usijaribu kuwashukia Makhalifa waongofu kwani wao ndiyo nguzo ya dini, na ukizibomoa nguzo jengo lote litaanguka.....”

Nikasema, *“Astaghfirul*lah! Ewe Bwana wangu, basi Mtume atakuwa na nafasi gani ikiwa wao ndiyo nguzo za Uislasmu?”

Akajibu: “Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ndiyo jengo lenyewe na yeye ndiyo Uislamu wote.”

Nilitabasamu kutokana na jawabu hili na nikasema, “Astaghafirullah!! kwa mara nyingine tena Sheikh unazungumza bila ya kufahamu, eti ya kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) hawezi kusimama isipokuwa kwa kuwategemea hawa (Makhalifa) wanne, (kinyume na kauli yako) Mwenyezi Mungu anasema: *“Ni yeye Mwenyezi Mungu aliyemtuma Mjumbe wake kwa uongofu na dini ya haki ili aipe ushindi juu ya dini zote, na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi.” (Qur. 48:28)*

Kwa hakika alimtuma Muhammad na ujumbe bila ya kumshirikisha yeyote miongoni mwa hawa, wala wasiokuwa hawa, na hapana shaka Mwenyezi Mungu amesema (kama ifuatavyo) kuhusu jambo hili: *“Kama tulivyomtuma kwenu Mjumbe anayetokana nanyi, akusomeeni aya zetu na akutakaseni na akufundisheni kitabu na hekima, na akufundisheni mambo ambayo mlikuwa hamyajui” (Qur. 2:151)*

Akasema: “(Majibu niliyokupa) hayo ndiyo tuliyojifunza kutoka kwa Masheikh wetu na Maimamu wetu, nasi katika zama zetu (tulipokuwa tukisoma) tulikuwa hatuwaulizi wala kujadiliana na Masheikh wetu kama ilivyo kwenu leo hii katika zama mpya, kwani mmekuwa na shaka katika kila jambo hata dini munaitilia mashaka na (kwa kweli) hizi ndizo dalili za Qiyama kwani Mtume (s.a.w.) amesema, “Hakitasimama Qiyama isipokuwa kwa viumbe waovu.”

Mimi nikamwambia “Ee! Bwana wangu vitisho hivi ni vya nini? Mimi najilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana na kuitilia shaka dini au kuingiza mashaka katika dini, bila shka namuamini Mwenyezi Mungu pekee asiyekuwa na mshirika, na Malaika wake na Mitume wake

(nawaamini) na ninaamini kwamba Bwana wetu Muhammad ni mja wake na ni Mjumbe wake, naye ndiye mbora wa Mitume na Manabii na ndiyo wa mwisho wao na mimi ni katika Waislamu, basi vipi wewe unanituhumu kwa tuhuma hiyo?"

Ninakutuhumu kwa mengi zaidi (kuliko haya niliyokuambia) na hii ni kwa sababu wewe unamshuku Bwana wetu Abubakr na Bwana wetu Umar, wakati Mtume (s.a.w.) amesema lau itapimwa imani ya umma wangu ikalinganishwa na imani ya Abubakr, basi imani ya Abubakar ingekuwa nzito".

Na amesema Mtume (s.a.w.) kuhusu haki ya Sayyidna Umar, "Nilioneshwa umma wangu hali umevaa kanzu isyofika kifuwani, na nilioneshwa Omar hali akiwa anaiburura kanzu yake, wakasema, umeitafsiri vipi ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu? Akasema: Hiyo ni dini." Leo unakuja wewe katika karne ya kumi na nne utie mashaka kuhusu uadilifu wa masahaba na hasa Abubakr na Omar?

Je wewe hujui kwamba watu wa Iraq ndiyo wavurugaji na ndiyo wenye kufru na unafiki?

Basi niseme nini kuhusu mwanachuoni huyu anayedai kuwa na elimu, mwanachuoni ambaye amechotwa na fahari mbaya, aliyeyabadilisha majadiliano yaliyokuwa kwa njia nzuri na kuyafanya kuwa zogo na uzushi na kueneza urongo mbele ya mkusanyiko wa watu walioathirika naye, ambao macho yao tayari yalikwishawiva na kufura kwa hasira na nikaona nyuso zao zina alama ya shari.

Basi hakuna nilichofanya isipokuwa niliondoka haraka na nikaenda nyumbani, nikawaletea kitabu cha *Muwatta* cha Imam Malik na Sahih Bukhari kisha nikasema, "Ewe Bwana wangu, hakika aliyenitia mashaka haya ni mwenyewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, halafu nikakifunguwa kitabu cha *Muwatta*, na ndani yake Malik anasimulia kwamba, "Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) amesema kuhusu haki ya mashahidi wa Uhud; "Hawa nashuhudia juu yao (kwa wema waliofanya)," Abubakr akasema, "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu sisi siyo miongoni mwa ndugu zao (nasi upate kushuhudia) tumesilimu kama walivyosilimu, na

tumepigana jihadi kama walivyopigana," Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema, yote uliyosema ni sawa, lakini mimi sijui ni yepi mutakayoyazua baada yangu!" Abubakr akalia, kisha akasema, Je, hivi ni kweli tutakuwa hivyo baada yako?" *Taz: Muwatta ya Imam Malik Juz. 1 uk. 307, Al-Maghazi ya Waqidi uk. 310.*

Kisha nikafungua Sahih Bukhari na ndani yake (tukakuta kama ifuatavyo), siku moja Umar ibn Khatab aliingia nyumbani kwa Hafsa na humo alikuwemo Asma binti Umeis. Umar alipomuona Asma akasema (kumuuliza Hafsa) ni nani huyu, akasema, ni Asma binti Umais, Umar akasema, huyu ni Mhabeshi au Mbahriyah, Asma akasema ndiyo, Umar akasema sisi tumekutangulieni kuhama (Maka) kwa hiyo sisi tunayo haki zaidi kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Asama binti Umeis akasema, Sivyo kabisa ulivyosema, ninyi mlikuwa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu yeye akiwalisha wenye njaa miongoni mwenu, na sisi tulikuwa ndani ya makazi au nchi ya mbali yenye kero (huko) Uhabeshi na yote hayo (yalitukuta) kwa ajili ya (kutaka) radhi ya Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake, namuapa Mwenyezi Mungu mimi sitokula chakula wala kunywa kinywaji mpaka nimwambie Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na tulipokuwa huko tulikerwa na kutishwa, na kutokana na maneno uliyoniambia sasa hivi nitamueleza Mtume nimuulize, Nani bora sisi au ninyi, naapa sitasema uongo wala kupotosha wala sitaongeza chochote juu ya haya uliyoyasema." Basi Asma alipokwenda kwa Mtume (s.a.w.) akasema, "Ewe Nabii wa Mungu Umar amesema, *Kadha wa kadha, mimi sikumwambia (kitu) isipokuwa (nilisema) Kadha wa kadha."*

Mtume (s.a.w.) akasema:- "Yeye hana haki zaidi kwangu mimi kuliko ninyi, na yeye na wenzake wanayo hijra moja tu wakati ninyi enyi watu wa Safina mnazo hijra mbili." Akasema; nilimuona Abu Musa na watu wa Safina (Wahajiri wa Uhabeshi) wakinijia mfululizo kuniuliza mazungumzo haya, basi hapana kitu chochote duniani walichokifurahia wala kilichobora ndani ya nafsi zao kuliko maneno aliyoyasema Mtume kwa ajili yao" *Taz: Sahih Bukhari Juz. 3 uk. 387 mlango unaohusu vita vya Khaibar.*

Baada ya yule Sheikh na watu waliohudhuria hapo kuzisoma hadithi hizi, nyuso zao ziliwabadilika wakawa wanatazamana wao kwa wao wakisubiri

jawabu la Sheikh aliyegongwa (na hadithi), basi hakuna kilichojitokeza kwake isipokuwa alinyanyua macho yake kama alama ya kustaajabu kisha akasema, *“Waambie, Ewe Mola wangu nizidishie Elimu.”*

Mimi nikasema, “Ikiwa kama Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) ndiye wa kwanza kumtilia mashaka Abubakr na hakukubali kumshuhudia (wema wake) kwa sababu tu hajui ni jambo gani atakalolizusha baada yake, na iwapo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hakukubali kumboresha Umar ibn Al-Khatab juu ya Asma bint Umais, bali Mtume alimboresha Asma juu ya Umar, mimi pia ninayo haki ya kuwa na mashaka na kutokumboresha yeye mpaka kwanza nibaini na kuufahamu uhakika, na ni wazi kabisa kwamba hadithi hizi mbili zinapingana na zile hadithi zilizokuja kuhusu Abubakr na Umar isitoshe zinazibatilisha, kwani na hizi mbili zinaingia akilini kuliko zile zinazodaiwa kuwa ni zenye kuwapa ubora.

Basi jamaa waliokuwepo hapo wakauliza kwa kusema, “Jambo hilo linakuja vipi?” Mimi nikasema “Hakika Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hakumshuhudia Abubakr na alichomwambia ni kwamba, hakika mimi sijui ni mambo gani mutayazua baada yangu! Jambo hili linaingia akilini sana, na Qur’an Tukufu imelikariri (mara nyingi) na historia nayo ni shahidi kwamba wao walibadilisha mambo mengi baada ya Mtume, na ndiyo maana Abubakr alilia, kwani hapana shaka alibadili mambo mengi na akamkasirisha Bibi Fatmah binti ya Mtume (s.a.w.) kama tulivyoeleza hapo kabla na aliendelea kubadili mambo mpaka akajutia kabla ya kufa na akatamani laiti asingekuwa mtu.

Ama ile hadithi isemayo, “Lau itapimwa imani ya umma wangu kulinganishwa na imani ya Abubakr, basi imani ya Abubakr ingeshinda imani zingine.” Hadithi hii ni batili wala haingii akilini, na wala haiwezekani kwa mtu ambaye umri wake wa miaka arobaini aliutumia katika kumshirikisha Mwenyezi Mungu na akiabudia sanamu akawa na imani kubwa kuliko umma wote wa Muhammad, wakati ndani ya umma huu wamo Mawalii wema wa Mwenyezi Mungu, Mashahidi na Maimamu ambao walitumia muda wao wote wakipigania dini ya Mwenyezi Mungu, basi anayo nafasi gani Abubakr kutokana na hadithi hii? Na lau kama itasihi ni kwanini mwishoini mwa uhai wake alikuwa akitamani asingekuwa mtu? Na lau pia imani yake ingeshinda imani za umma wote basi Bibi Fatmah

binti ya Mtume ambaye ni mwanamke bora kuliko wote asingemkasirikia na kuomba dua kwa Mwenyezi Mungu dhidi ya Abubakr katika kila sala aliyokuwa akisali.

Mwanachuoni yule hakurudisha jawabu lolote, lakini baadhi ya wanakikao walisema, "Bila shaka Wallahi hadithi hii imezua mashaka ndani ya nyoyo zetu." Pale pale yule Sheikh akasema kuniambia "Hivi ndivyo unavyotaka, hakika tayari umekwishawatia mashaka watu hawa katika dini yao." Kwa bahati nzuri mmoja wao alinitoshelezea jawabu kumjibu yule Sheikh akasema, "Siyo hivyo Sheikh, haki iko pamoja naye, maishani mwetu sisi hatujasoma kitabu chochote kwa ukamilifu, tumekufuateni na kuambatana nanyi katika imani ya upofu bila kujiuliza, na sasa imetubainikia kuwa ayasemayo Al-Haj ni Sahihi, wajibu wetu ni kusoma na kuchunguza." Baadhi ya waliokuwepo hapo waliafikiana naye katika maoni yake haya, na kwa kweli hali hii ilikuwa ni ushindi kwa upande wa haki, na wala haukuwa ni ushindi wa kutumia nguvu na shinikizo, lakini ni ushindi wa kiakili, hoja na dalili; *"Waambie leteni hoja zenu kama ninyi ni wasema kweli."*

Mazingira haya yalinipa msukumo na kunipa nguvu ya kuingia kwa undani katika uchunguzi, yalinifungulia milango yote nikaingia Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, kwa kumtegemea Mwenyezi Mungu na katika mila ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hali ya kuwa nikitarajia kutoka kwa Mola Mtukufu anipe mafanikio na uongofu, kwani ni yeye ndiye aliyeahidi kumuongoa kila anayefanya utafiti kuitafuta haki, na yeye Mwenyezi Mungu haendi kinyume na ahadi yake.

Utafiti uliendelea kwa makini miaka mitatu, kwa sababu nilikuwa nakariri niliyokuwa nimeyasoma baadhi ya wakati, kwa kukisoma kitabu mwanzo wa ukurasa hadi ukurasa wa mwisho wa kitabu.

Nilisoma kitabu kiitwacho *Al-Murajaat* cha Imam Sharafud-Din, nikakirudia mara nyingi, na kwa hakika kilifungua mbele yangu mwangaza uliosababisha niongoke nikakifungua kifua changu kwa kuwapenda watu wa nyumba ya Mtume.

Pia nilisoma kitabu kiitwacho *"Al-Ghadir"* nikakirudia mara tatu kutokana na yaliyomo miongoni mwa mambo ya haki iliyowazi mno,

nikasoma kitabu cha *Fidak* cha Sayyid Muhammad Baqir As-Sadri, pia kitabu cha *Saqifah* kilichoandikwa na Sheikh Muhammad Ridha Al-Mudhafar, na kutokana na vitabu hivi viwili nilifahamu siri nyingi za ndani na zikawa wazi. Vile vile nilisoma kitabu kiitwacho *An-Nas Wal-Ij-tihadi* basi hapa ndipo yakini ikaongezeka, hatimaye nikasoma kitabu kiitwacho *Abuhurairah* cha Sharafud-din, na kingine kiitwacho *Shaikhul-Muzirah* kilichotungwa na Sheikh Mahmud Abur-Rayyah wa Misri na nikafahamu ya kwamba Masahaba waliobadili mambo baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wamegawika mafungu mawili, kuna fungu moja walibadilisha hukmu kutokana na nguvu za utawala walizokuwa nazo, na wengine walibadili hukmu kwa kuweka hadithi za uongo kumzushia Mtume (s.a.w.).

Baada ya vitabu hivyo nilisoma kitabu kiitwacho *Al-Imam As-Sadiq Wal-Madhahibul-Arbah* kilichoandikwa Asad Haidar, na humo nilifahamu tofauti baina ya elimu ya kipawa na elimu ya kutafuta, nilifahamu tofauti iliyopo baina ya hekima ya Mwenyezi Mungu ambayo humpa amtakaye na kulelewa katika mazingira ya elimu na kujitahidi kwa njia ya maoni kitu ambacho kimeutenga umma wa Kiislamu na ile roho halisi ya Uislamu.

Nilisoma vitabu vingine vingi vya Sayyid Jaafar Murtaza Al-Amili na Sayyid Murtaza Al-Askari, Sayyid Tabatabai Sheikh Muhammad Zainud-Din, Fairuz Abad, Ibn Abil-Hadid Al-Muu'tazili katika Sherhe yake ya *Nahjul-Balagha* na *Fitnatul Kubra* cha mwandishi Taha Husain. Na miongoni mwa vitabu vya historia nilisoma *Tarikh At-Tabari, Tarikh ibn Al-Athir, Tarikh Al-Masoud* na *Tarikh Al-Yaaqubi,* nilisoma vitabu vingi nikakinaika kwamba Shia Imamiyyah wako kwenye haki. Kwa hiyo nikawa Shia na nikaipanda Safina ya Watu wa nyumba ya Mtume (s.a.w.) kwa baraka za Mwenyezi Mungu, nikashikamana na kamba ya kuwatawalisha, kwani namshukuru Mwenyezi Mungu, nilipata (viongozi) badala ya baadhi ya Masahaba ambao kwangu mimi ilikwishathibiti kwamba wao walirudi kinyume nyume kwa visigino vya miguu yao na hapana aliyeokoka miongoni mwao isipokuwa wachache. Nikawabadilisha hawa na mahala pao nikawaweka Maimamu wa nyumba ya Mtume, Maimamu ambao Mwenyezi Mungu amewatakasa kikamilifu, na akafaradhisha kuwapenda kuliko watu wote.

Walivyo Mashia, sivyo kama wanavyodai baadhi ya Wanachuoni wetu eti kuwa wao ni Wafursi (Waajemi) ambao Sayyidina Umar alivunja jeuri yao na utukufu wao na heshima yao katika vita ya Qadisiya, ndiyo maana wanamchukia na kumbughudhi!

Watu hawa wasiyojua nimepata kuwajibu kwamba, Kuwa mfuasi wa Watu wa nyumba ya Mtume siyo jambo linalowahusu Wafursi bali Mashia wapo Iraq, Hijaz, Syria na Lebanon na kote huko ni Waarabu, kama ambavyo Mashia wapo Pakistani, India, Afrika na Amerika na wote hawa siyo Waarabu wala si Wafursi.

Na lau tutatosheka na Mashia wa Iran basi hoja (yangu) itakuwa bora zaidi, kwani nimewakuta hawa Wafursi wanasema kuwa, Maimamu (wao) ni kumi na wawili na wote ni Waarabu tena Maquraishi katika Bani Hashim na ni kizazi cha Mtume (s.a.w.). Kwa hiyo lau Wafursi wangekuwa na chuki ya kuwachukia Waarabu kama wanavyodai baadhi ya watu, basi wangelimfanya Salman Al-Farisi kuwa ndiyo Imam wao kwa kuwa anatokana nao, tena ni Sahaba Mtukufu ambaye cheo chake kinafahamika kwa wote sawa sawa Mashia na Masunni.

Kwa upande mwingine nimekuta kwamba Ahlus-Sunna Wal-Jamaa, Maimamu wao ni Wafursi. Hii ni kwa sababu idadi kubwa ya Maimam wao ni Wafursi kama vile Abu Hanifa, Imamun- Nasai, Tirmidhi, Bukhari, Muslim, Ibn Majah, Razi, Imam Ghazali, Ibn Sina na Al-Faarabi na wengineo wengi ambao nafasi haitoshi kuwataja wote. Sasa basi ikiwa Mashia Wafursi wanampinga Umar ibn Khatab eti kwa sababu aliwabomoa wakubwa wao, ni kwa nini basi Mashia Waarabu na wengine wasiokuwa Wafursi nao wanampinga Umar? Madai haya hayana msingi, bali kilichopo ni kwamba upinzani wa Mashia kwa Umar unatokana na jinsi Umar mwenyewe alivyoshiriki kumtenga mbali Amirul-Muuminina na Bwana wa Mawasii Ali ibn Abi Talib kutoka kwenye nafasi ya Ukhalifa baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu jambo ambalo lilisababisha fitina na mitihani na kulegalega na hatimaye kuporomoka kwaUmma huu. Inatosha kabisa kwa yeyote yule anayefanya utafiti kwa uhuru kumuondoshea utata na kumfunulia ukweli wa mambo kiasi kwamba atakuwa mpinzani wa Umar bila ya kuwepo uadui hapo kabla baina yake na Umar.

Na ukweli ni kuwa, Mashia wakiwa ni Wafursi au Waarabu au wasiokuwa mataifa haya mawili, bila shaka ni wanyenyekevu na wenye kufuata maandiko ya Qur'an na maandiko ya hadithi za Mtume. Wamemfuata kiongozi wa uongofu na wanawe ambao ni taa zinazoondosha giza, na hawakumridhia mwingine asiyekuwa hawa, licha ya ile siasa ya Banu Umayyah iliyoambatana vivutio na vitisho, (siasa ambayo pia) ilifuatwa na watawala wa kibani Abbas kwa muda wa karne saba, na ndani ya kipindi hiki chote (watawala) hawa waliwafuatilia Mashia katika kila kona na kila mji wakawauwa na kuwatawanya, wakawanyima haki yao na kufuta athari zao. Kisha wakaeneza kila upande uzushi na madai ya uongo (dhidi ya Mashia) ambayo yatawafanya watu wawatenge na hali hii imeendelea kubaki hadi leo.

Lakini Mashia wamekuwa madhubuti na imara kabisa, na wenye subira, wameshikamana na haki, haiwaogopeshi lawama ya mwenye kulaumu (kwa kila walitendalo) kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na mpaka leo hii wanatetea msimamo huu. Nami kwa upande wangu natoa changamoto kwa Mwanachuoni yeyote miongoni mwa wanachuoni wetu kwamba afanye kikao na mwanachuoni wa Mashia ajadiliane naye, basi kamwe hatatoka kwenye kikao hicho isipokuwa atauona uongofu walionao Mashia.

Naam nimepata badala (ya kile nilichokuwa nacho), namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ameniongoza kwenye uongofu huu, kwani nisingeongoka lau yeye Mwenyezi Mungu asingeniongoa.

Sifa njema ni zake Mwenyezi Mungu na ninamshukuru kwa kunionesha lile kundi lenye kuokoka ambalo nilikuwa nalitafuta kwa hamu kubwa, na hapakubakia shaka yoyote kwangu kwamba, yeyote mwenye kushikamana na Imam Ali na Watu wa nyumba ya Mtume, huwa ameshika kishiko chenye nguvu kisichovunjika, na maneno ya Mtume juu ya hilo (la kushikamana na Watu wa nyumba yake) ni mengi, ambapo Waislamu wote wamekubaliana, na akili peke yake ni dalili iliyobora kwa mwenye kutega sikio na akawa makini. Ali alikuwa ni mjuzi mno kuliko Masahaba wote na alikuwa shujaa wao bila kupingwa, na hili nalo ni kwa makubaliano ya Umma (wa Kiislamu), na hili peke yake linatosha kuwa dalili ya kustahiki kwake Ukhalifa kuliko mtu mwingine.

Mwenyezi Mungu amesema: *"Nabii wao akawaambia, Hakika Mwenyezi Mungu amekuleteeni Talut awe Mfalme (wenu) wao wakasema, Itakuwaje awe mfalme wetu wakati sisi ni wenye haki mno kwa ufalme kuliko yeye na hakupewa wasaa wa mali. (Yule Nabii) akasema, bila shaka Mwenyezi Mungu amemchagua juu yenu na akamzidishia wasaa wa elimu na mwili, naye Mwenyezi Mungu humpa ufalme wake yule amtakaye na Mwenyezi Mungu ni mwenye wasaa na ni mjuzi". (Qur. 2:247)*

Naye Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amesema "Hapana shaka Ali anatokana nami, na mimi natokana naye, na yeye ndiye msimamizi wa mambo ya kila Muumini baada yangu".

*Taz: (1) Sahih Tirmidh Juz. 5 uk. 296*
*(2) Khasaisun-Nasai uk. 87*
*(3) Mustad-rak Al-Hakim Juz. 3 uk. 110*

Naye Imam Zamakhshari amesema ndani ya beti zake:- Mashaka na khitilafu vimezidi, na kila mmoja anadai yeye ndiye njia ya sawa, basi mimi (nilipoona hivyo) nikashikamana na *Lailaha Illallah,* napendo langu nikampa Ahmad na Ali. Mbwa alifuzu kwa kuwapenda watu wa pangoni *(As-habu-lkahfi)* vipi nitakuwa muovu kwa kuwapenda watu wa (kizazi cha) Mtume?

Naam, nimekwishapata badala (ya kile nilichokiamini zamani), namshukuru Mwenyezi Mungu na sasa baada ya Mtume ninamfuata Amirul-Muuminina na Bwana wa Mawasii na kiongozi wa Watu wateule, Simba wa Mwenyezi Mungu aliyemshindi Imam Ali ibn Abi Talib, na kitulizo cha nafsi ya Mtume katika Umma huu Imam Abu Muhammad Hasan Az-Zaki na Imam Abu Abdillah Husein na sehemu ya mwili wa Mustapha ambaye Mola Mtukufu hughadhibika pindi anapoghadhibika (naye) ni mwanamke bora kuliko wote Fatmah Az-Zahra.

Nimembadilisha Imam Malik; na sasa niko pamoja na Mwalimu wa Ummah Imam Jaafar As-Sadiq.

Na nikashikamana na Maimamu tisa wenye Isma wanaotokana na kizazi cha Husein (a.s.), hao ni Maimamu wa Waislamu na ni Mawalii wema wa Mwenyezi Mungu.

Nikabadili Masahaba (kutoka kwa wale) waliorudi nyuma kwa visigino vyao kama vile Muawiyah, Amr ibn Al-As, Abuhurairah, Ikrimah na Kaab Al-Ahbar na wengineo, (nimewabadili hawa nikashikamana na) Masahaba wenye shukurani ambao hawakutengua ahadi waliyomuahidi Mtume (Masahaba hao ni) kama Ammar ibn Yasir, Sal-man Al-Farisi, Abud-Dhari Al-Ghifari, Miqdad ibn Al-As-wad, Khuzaimah ibn Thabit Dhus-Shahadatain, Ubay ibn Kaa'b na wengineo. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuzindukana huku.

Nimebadilisha wanachuoni wa watu wangu ambao walizigandisha akili zetu, na wengi wao wamekuwa wafuasi wa masultani na watawala wakati wote, (nimewabadilisha hawa) kwa (kushikamana na) wanachuoni wa Kishia waliowema ambao hawakuufunga mlango wa *Ij-Tihadi* na wala hawakudhalilika na kuwa wanyonge kwa watawala madhalimu.

Naam, nimebadilisha fikra zilizogandamana zenye upinzani usiyo na hoja madhubuti, fikra zinazoamini mambo yanayopingana (nimebadilisha fikra hizi) kwa fikra zenye nuru na uhuru, zilizo wazi na zenye kuamini dalili na hoja.

Kama isemwavyo katika zama zetu hizi kwamba: "Nimeukosha ubongo wangu kutokana na uchafu ulioufunika kwa kipindi cha miaka thelathini na (nimeukosha ubongo wangu kutokana) upotovu wa kibanu Umayyah, nikautakasa kwa itikadi ya Watu wenye Ismah ambao Mwenyezi Mungu amewatakasa kwa tahara iliyokamilika na (nitabakia katika itikadi hii) katika uhai wangu uliobakia.

Ewe Mwenyezi Mungu tuweke hai ndani ya mila yao na utufishe katika Sunna yao, na utufufue pamoja nao, bila shaka Mtume wako (s.a.w.) amesema, "Mtu atafufuliwa pamoja na ampendaye."

Kwa yote haya ninakuwa nimerejea kwenye asili yangu, kwani baba yangu na ami zangu walikuwa wakitusimulia juu ya asili yao wanayoifahamu ya kuwa wanatokana na ukoo wa Masharifu waliokimbia kutoka Iraq chini ya ukandamizaji wa utawala wa Banu Abbas na wakakimbilia Afrika ya Kaskazini wakaja hadi Tunis na athari zao zimebakia hadi leo.

Na huko Afrika ya Kaskazini wako watu wengi mfano wetu ambao wanaitwa Masharifu kwa kuwa wanatokana na kizazi kitukufu (cha Mtume), lakini wamepotea ndani ya upotovu wa Banu Umayyah na Banu Abbas, hakuna uhakika wowote waliobakia nao isipokuwa hiyo heshima na cheo wanachovishwa na watu. Mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uongofu wake (alionipa), namshukuru Mwenyezi Mungu kwa utambuzi (nilioutambua) na kunifungua macho yangu na kuiona haki.

# SABABU ZA UTAMBUZI

Ama sababu zilizonifanya kuubaini ukweli, ni nyingi mno wala haiwezekani katika muda huu mfupi isipokuwa kutaja baadhi tu ya mifano miongoni mwake.

**i. Maandiko yanayohusu Ukhalifa.**

Bila shaka niliapa, wakati naingia ndani ya utafiti huu kwamba sitategemea isipokuwa kile kitu ambacho kimethibitishwa katika pande mbili na kukitupa kile ambacho upande mmoja umepwekeka. Na kwa msingi huu nitatafiti ile fikra ya ubora uliopo baina ya Abubakr na Ali ibn Abi Talib na kwamba Ukhalifa lilikuwa ni tamko (la Mtume) lililomuashiria Ali kama wanavyodai Mashia, au (Ukhalifa) ulikuwa ni kwa misingi ya uchaguzi na mashauriano kama wanavyodai Ahlus-Sunnah Wal-Jamaa.

Mtu yeyote anayefanya uchunguzi kuhusu maudhui hii, atakapoweka juhudi zake kwa lengo la kupata ukweli, basi bila shaka atakuta maandiko yaliyowazi juu ya (Ukhalifa wa) Ali ibn Abi Talib, kama vile kauli ya Mtume (s.a.w.)semayo, "Yeyote ambaye mimi nilikuwa mtawala wa mambo yake, basi huyu hapa Ali ni mtawala wa mambo yake." Maneno haya aliyasema baada ya kutoka katika hija ya kuaga hadi yakafanywa maandamano ya watu kwenda kumpongeza Ali ibn Abi Talib na mpaka Abubakr mwenyewe na Umar walikuwa miongoni mwa watu waliompongeza Imam Ali wakasema, "Hongera ewe mwana wa Abu Talib leo umekuwa mtawalia mambo kwa kila muumini wa kike na wa kiume". *Taz: Musnad Imam Ahmad Ibn Hambal J. 4 uk. 281, Sirul-Alamimina cha Imam Ghazal uk. 12, Tadh-Kiratul-Khawas cha Ibn Al-Jauzi, Ar-Riyaz-Un-Nazrah cha Tabari J. 2 uk. 169, Kanzul-Ummal J. 6 uk. 397, Al-Bidayah Wan-Nihayah cha Ibn Kathir J. 5 uk. 212, Tarikh Ibn Asakir J. 2 uk. 50, Tafsir Ar-Razi J. 3 uk. 63, Al-Hawi Lil-Fatawi cha Suyut J. 1 uk. 112.*

Tamko hili wamekubaliana Mashia na Masunni, nami sikuandika rejea yoyote ile kuhusu utafiti huu isipokuwa ni za Kisunni. Pamoja na hayo sikuzitaja rejea zote kwani ni nyingi mno kuliko idadi niliyoitaja, lakini ili kuchunguza kwa undani zaidi na kwa ufafanuzi namuomba msomaji asome kitabu kiitwacho Al-Ghadir cha Mwanachuoni mkubwa aitwaye Al-Amini na kimechapishwa mijaladi kumi na tatu, ambapo mwandishi amekusanya ndani yake wapokezi wa hadithi hii kwa njia za Kisunni.

Amma ile *Ijmai* (makubaliano) yanayodaiwa (kufanyika na) kumchagua Abubakar siku ile ya *Saqifah*, kisha kumpa baia Msikitini, bila shaka madai hayo hayana dalili kwani itakuwaje iwe *Ijmai* wakati ambapo baia yake ilipingwa na Ali, Abbas na Banu Hashim wengine? Kama ambavyo Usamah ibn Zaid, Zubair, Sal-man Al-Farisi, Abudhari Al-Ghifari, Miqdad ibn Al-As-wad, Ammar ibn Yasir, Hudhaifah ibn Yaman, Khuzaimah ibn Thabit, Abu Buraidah Al-Aslam, Al-Barraa ibn Azib, Ubay ibn Kaab, Sahl ibn Hunaif, Saad ibn Ubadah, Qays ibn Saad, Abu Ayyub Al-Ansari, Jabir ibn Abdillah, Khalid ibn Said, na wengineo, (wote hawa) waliipinga baia hiyo. T*az: Tarikh Tabari, Tarikh ibn Al-Athir, Tarikh Al-Khulafa, Tarikh Al-Khamis, Al-Istiiabu na kila Aliyeitaja baia ya Abubakar.*

Basi iko wapi hayo makubaliano yasemwayo enyi waja wa Mwenyezi Mungu? Kwani lau Ali ibn Abi Talib peke yake angekuwa ndiye aliyepinga baia hiyo, ingetosha kabisa kuyatuhumu hayo makubaliano, kwani ni yeye pekee ndiye aliyekuwa ameandaliwa na Mtume (s.a.w.) ili awe Khalifa hata kama tukikadiria kutokuwepo kwa tamko linalomgusa moja kwa moja (lakini yapo matamko wazi ya mwenyewe Mtume s.a.w.).

Kilichotokea ni kwamba baia ya Abubakar ilipatikana bila ya mashauriano, bali ilipatikana bila kutegemewa kwani wahusika na wakata shauri kama wanavyoitwa na wanachuoni wa Kiislamu hawakuwepo, bali walikuwa wameshughulika kumuandaa Mtume kwa mazishi. Nao watu wa Madina waliokuwa wamegubikwa na kifo cha Mtume wao walishitukizwa na kulazimishwa kufanya baia kwa nguvu baada ya tukio hilo kama ambavyo onyo lao (hao walioandaa baia hii) kwamba wangeiunguza nyumba ya Fatmah iwapo wapinzani wa baia hawatatoka nje. Basi ni vipi itafaa kwetu sisi baada ya (mambo kama) haya tuseme (eti) baia (ya Abubakr) ilipatikana kwa mashauriano na *Ijmai? Taz: Tarikh Al-Khulafa.*

Hapana shaka Umar ibn Al-Khatab mwenyewe alishuhudia ya kwamba baia ile ilikuwa (ni jambo la) ghafla, Mwenyezi Mungu aliwakinga Waislamu na shari yake, na akaendelea kusema, "Yeyote atakayerudia kufanya baia kama hiyo muuweni, au alisema, "Yeyote mwenye kufanya kampeni kama hiyo asipewe baia wala yule aliyembai." *Taz: Sahih Bukhar, J. 4 uk. 127.*

Naye Imam Ali anasema juu ya baia hiyo: "Ama namuapa Mwenyezi Mungu, hapana shaka mwana wa Abu Quhafah (Abubakr) alijivalisha Ukhalifa, hali ya kuwa anajua kwamba daraja yangu na Ukhalifa ni sawa na mhimili na jiwe la kusagia, kwangu mimi mafuriko huporomoka na wala ndege hafiki juu yangu.

Naye Saad ibn Ubbadah, Bwana wa Maansari ambaye aliwahujumu Abubakr na Umar siku ile ya Saqifah na alijaribu juhudi zake zote kuwazuwia na kuwaweka mbali na Ukhalifa, lakini akashindwa kwa sababu alikuwa mgonjwa asiyeweza hata kusimama, na baada ya Ansari kumpa baia Abubakr yeye alisema:- "*Wallahi* kamwe sitakupeni baia mpaka nimalize mishale yangu kukurushieni kutoka kwenye ala yangu ya mishale, na niuloweshe damu mkuki wangu nikupigeni kwa upanga wangu kadiri mkono wangu utakavyoweza kuumiliki, na nitakupigeni pamoja na watu nilionao miongoni mwa watu wangu na jamaa zangu. Hapana kabisa (siwaungi mkono) lau hata kama majini na watu wote wangekusanyika kwa ajili yenu nisingewapeni baia hadi nifike kwa Mola wangu."

Saad ibn Ubbadah alikuwa hasali pamoja nao au nyuma yao wala hasali nao sala ya Ijumaa na wala haendi nao kwenye Arafah.

Lau kuna mtu angemuunga mkono Saad kuwapiga vita angeliwapiga vita. Alibakia hivyo mpaka alipokufa huko Shamu katika kipindi cha Ukhalifa wa Umar. *Taz: Tarikhul-Khulafa J. 1 uk. 17*

Basi iwapo baia hii ilikuwa ya ghafla, ambayo Mwenyezi Mungu aliikinga shari yake kama alivyoeleza Umar ambaye ndiye aliyeimarisha nguzo zake, nawe unafahamu matokeo ya mambo ya Waislamu yaliyosababishwa na baia hiyo. Na iwapo Ukhalifa huu ulikuwa ni wa kujivalisha (kama kanzu) na Abubakr kama alivyoueleza Imam Ali kwani

yeye (Imam Ali) ndiye mstahiki wake kisheria. Na iwapo baia hii ilikuwa ni dhulma kama alivyoizingatia Saad ibn Ubbadah, Bwana wa Maansari ambaye alijitenga na jamaa kwa sababu ya baia hiyo. Na kama baia hii siyo ya kisheria kwa sababu ya kupingwa na Masahaba wakubwa pamoja na Abbas ambaye ni ammi yake Mtume. Ni ipi hoja (inayohalalisha) kusihi Ukhalifa wa Abubakar? Jawabu ni kwamba, hapana hoja yoyote waliyonayo Masunni.

Kwa hiyo kauli ya Mashia ndiyo sahihi ndani ya maudhui hii, kwani imethibiti kupatikana kwa maandiko juu ya Ukhalifa wa Ali kwa Masunni wenyewe, na wameyafanyia taawili (tafsiri) ili kulinda heshima ya Masahaba, lakini kwa mtu muadilifu hana njia ya kukwepa, isipokuwa kukubali maandiko hayo, na khasa pindi atakapofahamu utata uliyomo ndani ya jambo hili. Taz: Saqifah Wal-Khilafah cha Abdul-Fatah Abdul-Maqsood na As-Saqifa cha Sheikh Muhammad Ridhaa Mudhafar.

**ii. Kuhitilafiana kwa Fatmah na Abubakr**

Maudhui hii pia wamekubaliana Masunni na Mashia kuwa ni sahihi, haimpi nafasi mtu muadilifu isipokuwa kutoa maamuzi ya kwamba Abubakr alikosea, hata kama hakukiri juu ya dhulma aliyoifanya dhidi ya (Fatmah ambaye) ni mwanamke bora kuliko wote, kwani yeyote mwenye kufuatilia tukio hili la huzuni na kulichunguza kila upande atafahamu kwa yakini kabisa kwamba, Abubakr alikusudia kumuudhi Fatmah na kumkanusha ili asijetoa hoja dhidi yake kuhusu yale maagizo ya Mtume katika siku ya Ghadir na mengineyo yanayohusu Ukhalifa wa mumewe na Ibn Ammi yake Ali (a.s.), na tunakuta (dalili) nyingi kuhusu jambo hilo.

Miongoni mwake ziko zile ambazo wanahistoria wameziandika ya kwamba, Bibi Fatmah (a.s.) alitoka akiuzunguka (mji wa Madina) kwenye vikao vya Maansari akiwataka msaada wa kumpa baia Iibn Ammi yake basi wao husema “Ewe binti wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kwa hakika baia yetu tumekwisha mpa bwana huyu, na lau mumeo na Ibn Ammi yako angelitangulia kwetu kabla ya Abubakr kamwe tusingemkiuka”. Basi Imam Ali (ambaye) Mwenyezi Mungu ameutukuza uso wake husema: “Hivi kweli ilikuwa Busara nimuache Mjumbe wa Mwenyezi Mungu nyumbani mwake bila kumzika ili tu nitoke kuja kugombana na watu juu

ya cheo chake"? Hivyo basi Fatmah naye husema, "Alichofanya Abul-Hasan ndicho kilichompasa kukifanya, na wao wamefanya jambo ambalo Mwenyezi Mungu atawauliza na atawalipa (kwa tendo hilo)." *Taz: Tarikh Al-Khulafaa cha ibn Qutaibah Juz.1 uk. 19, Sharh Nahjul-Balagha cha ibn Abil-Hadid (Baiatu Abubakar.)*

Na lau Abubakr angelikuwa kakosea akiwa na nia njema, au kwa misingi ya Ish-tibahi basi Fatmah (a.s.) angelimkinaisha (kwa kumfahamisha) lakini sivyo bali (Fatmah) alimkasirikia (Abubakr) na hakumsemesha hadi kifo chake, kwa kuwa yeye Abubakr aliyakanusha madai yake na hakuukubali ushahidi wake na ushahidi wa mumewe na kwa yote haya ghadhabu yake dhidi ya Abubakar ilizidi kiasi kwamba hakumruhusu kuhudhuria mazishi yake kwa mujibu wa usia wake kwa mumewe ambaye alimzika usiku tena kwa siri. *Taz: Sahih Bukhar Juz. 3 uk. 36, Sahih Muslim Juz. 2 uk. 72 mlango usemao La-nurath ma Taraknahu Sadaqah.*

Na katika kueleza mazishi yake Bibi Fatmah kwamba yalikuwa usiku tena kwa siri, mimi wakati wa utafiti wangu huu nilisafiri kwenda Madina yenye nuru ili nipate kuchunguza mwenyewe binafsi juu ya baadhi ya uhakika (wa mambo) na nimegundua ya kwamba:-

**Kwanza:** Kaburi la Bibi Fatmah halijulikani lilipo, hapana ajuwaye, wako wasemao kwamba limo ndani ya chumba cha Mtume, na wengine wanasema kwamba limo ndani ya nyumba yake muqabala na chumba cha Mtume, na kauli ya tatu ni kwamba limo ndani ya (uwanja wa) *Jannatul-Baqii* katikati ya makaburi ya watu wa nyumba ya Mtume, bila ya kuwepo ufafanuzi.

Huu ni uhakika wa mwanzo niliougundua ya kwamba Bibi Fatmah alitaka hapo baadaye Waislamu wajiulize ni sababu zipi zilizomfanya amtake mumewe amzike kwa siri tena usiku na asiwepo miongoni mwao yeyote aliyehudhuria mazishi yake!!! Na kwa ajili hiyo itawezekana kwa kila Muislamu kupata baadhi ya ukweli wa mambo yanayozindua (fikra), wakati wa kuirejea historia.

**Pili:** Nimegundua kwamba yeyote anayetaka kuzuru kaburi la Uthman ibn Affan atatembea masafa marefu mpaka afike mwisho wa Baqii, atamkuta

chini ya ukuta wakati wengi wa Masahaba atawakuta wamezikwa mwanzoni tu mwa Baqii karibu na mlangoni Hata Malik ibn Anas muasisi wa madh-hebu ya Malik, ambaye ni Tabiit-Tabiina (siyo Sahaba) amezikwa karibu na wakeze Mtume (s.a.w.), na imenithibitikia kwamba, Uthman amezikwa *Hash Kaukab* ambalo lilikuwa eneo la Mayahudi. Ni kweli kwani Waislamu walizuwia kumzika *Baqii* ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na Muawiyah ibn Abi Sufiyan alipotawalia Ukhalifa aliinunua ardhi hiyo na kuingiza ndani ya eneo la *Baqii* ili apate kuliingiza ndani yake kaburi la ibn ammi yake Uthman. Na yeyote atakayezuru Baqii hata leo hii atauona ukweli huu wazi wazi.

Mimi nastaajabu sana ninapofahamu kwamba, Fatmah Zahra (a.s.) ndiye mtu wa kwanza kumfuatia Baba yake (kwa kufariki) kwani kuna miezi sita tu kwa makadirio makubwa baina ya kifo cha Mtume na Bibi Fatmah, kisha ni kwanini hakuzikwa pembezoni mwa baba yake?

Sasa iwapo Fatmah Zahra mwenyewe ndiye aliyeusia kuwa azikwe siri na hakuzikwa karibu na kaburi la baba yake kama nilivyoeleza, basi nini kilichotokea kwenye mwili wa mwanawe Hasan ambaye naye hakuzikwa karibu na kaburi la Babu yake? Jambo hili alilizuwia Ummul-Muuminina Aisha na alifanya jambo hilo pindi Husein (a.s.) alipouleta mwili wa nduguye Hasan ili auzike pembeni mwa Babu yake Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

Mama Aisha alipanda nyumbu akatoka akinadi na kusema “Msimzike nyumbani mwangu mtu nisiyempenda.”

Banu Umayyah na Banu Hashim wakajipanga kwa ajili ya vita, lakini Imam Husein (a.s.) akamwambia mama Aisha kwamba, “Yeye atatufu kaburi ya Babu yake akiwa na mwili wa nduguye kisha amzike Baqii kwa sababu Imam Hasan alimuusia ya kuwa wasije mwaga damu japo kidogo kwa ajili yake.”

Na kwa sababu hii Ibn Abbas alimwambia Bibi Aisha katika beti mashuhuri kama ifuatavyo:-

*Ulipanda ngamia ukapanda nyumbu, lau utaishi zaidi utapanda tembo, wewe unayo sehemu moja katika tisa lakini thumni yote umeitumia.*

Na huu ni ukweli mwingine miongoni mwa mambo yanayotisha. Itakuwaje kwa Bibi Aisha (peke yake) miongoni mwa wakeze Mtume wengi ambao ni tisa airithi nyumba yote kama alivyosema Ibn Abbas?

Na ikiwa Mtume harithiwi kama alivyodai Abubakr mwenyewe na kwa sababu hiyo akazuwia urithi wa Fatmah kwa Baba yake, basi ni vipi Bibi Aisha alirithi? Je, hivi ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu iko aya inayompa mke haki ya kurithi na kumnyima haki hiyo Binti? Au tuseme hizo ni siasa ambazo ndizo zilizobadilisha kila kitu zikamnyima Binti kila kitu na kumpa mke kila kitu?

Na kwa mnasaba huu naeleza kisa cha ajabu ambacho baadhi ya wanahistoria wamekieleza, na kinauhusiano na maudhui hii ya urithi.

Amesema Ibn Abil-Hadid Al-Muu'tazili ndani ya Sharhi Nahjil-Balagha:-

Mabibi Aisha na Hafsa walimwendea Uthman katika zama za Ukhalifa wake, wakamtaka awagawie urithi wao kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.). Uthman alikuwa kajiegemeza akakaa sawa na kumwambia Bibi Aisha: "Wewe na huyu mwanamke aliyeketi mlimleta bedui ambaye hujitahirisha kwa mkojo wake na hali ya kuwa ninyi mnashuhudia kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kasema, "Sisi Mitume haturithiwi", ikiwa kweli Mtume harithiwi, basi ninyi mnataka nini baada ya hayo? Na iwapo Mtume anarithiwa ni kwanini basi mlimnyima Fatmah haki yake"? Bibi Aisha akaondoka mbele ya Uthman hali ya kuwa amekasirika na akasema; "Muuweni Naa'thal hakika amekufuru." *Taz: Sharh Nahjil-Balagha cha ibn Abil-Hadid Juz. 16 uk. 220-223.*

**iii. Ali ndiye anayestahiki kufuatwa**

Miongoni mwa mambo yaliyonifanya nizindukane na kuacha mwenendo wa wazazi na mababu ni kipimo cha kiakili na maandiko yanayowahusu, Ali ibn Abi Talib na Abubakr.

Kama nilivyoeleza ndani ya milango iliyotangulia katika uchunguzi huu, kwa hakika mimi nategemea makubaliano wanayo afikiana Masunni

na Mashia Hapana shaka nimechunguza ndani ya vitabu vya makundi haya mawili kuhusu maelezo yaliyokuja miongoni mwa maandiko yaliyothibitishwa na rejea za pande mbili sijakuta isipokuwa makubaliano yaliyopo ni kwa Ali ibn Abi Talib, kwani wamekubaliana kuhusu Uimamu wake Mashia na Masunni, ndani ya maandiko yaliyokuja na kuthibitishwa na rejea za pande mbili. Wakati huo huo hakuna anayedai Uimamu wa Abubakr isipokuwa kundi moja miongoni mwa Waislamu, na hapo kabla tumeeleza maneno aliyoyasema Umar kuhusu baia ya Abubakr. Vile vile ubora na sifa wanazozieleza Mashia juu ya Ali ibn Abi Talib zinazo sanadi zinazopatikana na kuthibitishwa ndani ya vitabu vya Ahlus-Sunnah wanavyovitegemea, tena zimekuja kwa njia nyingi ambazo hazina shaka.

Idadi kubwa ya Masahaba wamesimulia hadithi juu ya ubora wa Imam Ali kiasi cha kumfanya Imam Ahmad ibn Hambal aseme:-

"Hapakuja hadithi nyingi kwa Sahaba yeyote miongoni mwa Masahaba wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kuhusu ubora kama zilivyokuja kwa Ali ibn Abi Talib. *Taz: Mustad-rak As-Sahihain cha Al-Hakim Juz. 3 uk. 107, Al-Manaqib cha Khawar-Zami uk. 3 na 19, Tarikh Al-Khulafa cha Suyut uk. 168, As-Sawaiqu Al-Muh-riqah cha ibn Hajar Al-Haithami uk. 72, Tarikh ibn Asakir Juz. 3 uk. 63, Shawahidut-Tanzil cha Al-Haskani Al-Hanafi Juz. 1 uk. 19.*

Naye Qadhi Ismail na An-Nasai na Abu Ali Nishapuri wamesema:- "Hapakuja kuhusu haki ya yeyote miongoni mwa Masahaba kwa Sanad njema kama ilivyokuja kwa Ali.

Kwa hiyo, pamoja na kutupia jicho hali ya Banu Umayyah ambao waliwalazimisha watu mashariki na magharibi ya ulimwengu wamtukane Imam Ali na wasitaje ubora wake, mpaka walizuwia mtu yoyte asiitwe kwa jina la Ali, lakini pamoja na yote haya sifa zake na fadhila zake zilichomoza licha ya upinzani huo. Anasema Imam Shafii kuhusu jambo hili:- "Nastaajabu, mtu ambaye maadui zake wameficha fadhila zake kwa sababu ya husuda, na wampendao wakazificha kwa sababu ya khofu, lakini sifa zake zimechomoza baina ya wawili hawa na kuenea ulimwengu mzima."

Ama kuhusu Abubakr, pia nimechunguza ndani ya vitabu vya pande hizi mbili sijakuta ndani ya vitabu vya *Ah-lus-Sunna Wal-Jamaa* walioandika sifa za Abubakr kwamba ana sifa ambazo zinaweza kulinganishwa au kuzidi zile fadhila za Imam Ali, kwa msingi kwamba ubora wa Abubakr unaotajwa ndani ya vitabu vya historia imma utakuwa umesimuliwa na Binti yake Aisha ambaye tumekwishafahamu msimamo wake dhidi ya Imam Ali, kwani Bibi Aisha amejaribu kwa juhudi zake zote kumjenga baba yake japokuwa kwa kutumia hadithi za kubuni, au zilizopokelewa toka kwa Abdallah ibn Umar ambaye naye ni miongoni mwa watu waliokuwa wamejitenga mbali na Imam Ali, na alikataa kumpa baia Imam Ali pindi watu walipokubaliana juu ya hilo na alikuwa akisimulia kwamba, "Mtu bora baada ya Mtume ni Abubakr kisha Umar kisha Uthman kisha haboreshwi mtu mwingine na baada ya hao, basi watu wengine ni sawa sawa." Hadithi hii ina maana kwamba, Abdallah ibn Umar, alimfanya Imam Ali kuwa ni miongoni mwa watu wakuongozwa kama walivyo watu wa kawaida hana aina yoyote ya daraja ya ubora. Yu wapi basi Abdallah ibn Umar na ule ukweli walioutaja wanachuoni wa umma (wa Kiislamu) ya kwamba hapakuja kwa Sahaba yeyote sanadi (za hadithi) zenye daraja njema kama zile zilizokuja (kutaja ubora wa) Ali ibn Abi Talib. Je hivi ni kweli Abdallah ibn Umar hakupata kusikia kutoka kwa Mtume japokuwa fadhila moja ya Ali?

Hapana kabisa, Wallahi amesikia na kuzidhibiti (fadhila za Ali), lakini siasa ilimzuga na kipi kitakacho kujulisha hiyo siasa ni kitu gani, hapana shaka hiyo siasa (iliyopita) ilikuwa ni kuugeuza ukweli na kufanya maajabu.

Hali kadhalika yataka ufahamu ya kwamba, watu kama Amri ibn Al-as, Abuhurairah, Ur-wa na Ikhrimah wamesimulia fadhila za Abubakr na wote hawa walikuwa dhidi ya Imam Ali na walimpiga vita ima kwa silaha au kwa kumsingizia na kuunda fadhila nyingi za maadui wa Imam Ali (a.s.).

Imam Ahmad ibn Hambal amesema: "Hapana shaka kwamba Imam Ali (a.s.) alikuwa na maadui wengi, maadui zake hao walitafuta jambo ambalo lingemuaibisha lakini hawakupata, hivyo basi wakamuendea mtu ambaye alikuwa akimpiga vita Imamu Ali (a.s.) wakamsifu sana kwa nia ya kumfanyia vitimbi Imam Ali."

Lakini Mwenyezi Mungu anasema, *"Bila shaka wao wanafanya hila, nami nazipindulia mbali hila zao, basi wape muda makafiri wape muda kidogo." (Qur.86:15-17)*

Kwa hakika ni miongoni mwa miujiza ya Mwenyezi Mungu tu kutokeza na kutambulikana kwa fadhila na ubora wa Imam Ali (a.s.) baada ya kupita karne sita za utawala dhalimu na wa mabavu dhidi ya Imam Ali na watu wa nyumba yake, kwani watawala wa Banu Abbas hawakupunguza kero, chuki, vitimbi na kuwanyanyasa Watu wa nyumba ya Mtume kama walivyofanya watawala waliowatangulia wa Kibanu Umayyah.

Pamoja na kwamba Abubakr ndiye aliyekuwa Khalifa wa kwanza na alikuwa na madaraka kama tulivyokwishakufahamu, na kwamba dola ya Banu Umayya ilikuwa ikitoa zawadi maalum na rushwa kwa kila mwenye kusimulia (hadithi) zinazowahusu Abubakar, Umar na Uthman pia zilitengenezwa hadithi nyingi zinazohusu ubora na sifa za Abubakr ambazo zimejaa ndani ya vitabu. Basi pamoja na yote haya, hazikuweza kufikia sehemu moja ya kumi ya daraja za Imam Ali na fadhila zake. Zaidi ya hayo ni kwamba iwapo wewe utazichambua hadithi zilizosimuliwa juu ya fadhila za Abubakr utazikuta haziafikiani na jinsi historia ilivyoyasajili baadhi ya matendo yake yanavyopingana na yaliyosemwa kumuhusu Abubakr, na wala akili haiwezi kuyakubali wala sheria. Hapo kabla umetangulia ufafanuzi wa ile hadithi isemayo; "Lau itapimwa imani ya Abubakr na imani ya umati wangu basi imani ya Abubakr itakuwa nzito." Na lau Mjumbe wa Mwenyezi Mungu angelifahamu ya kwamba Abubakr anayo daraja (kubwa) kama hii, basi asingemfanya Usamah ibn Zaid kuwa amiri na wala asingekataa kumshuhudia wema na mafanikio kama alivyowashuhudia mashahidi wa Uhdi, na isitoshe Mtume alimwambia (Abubakr); "Hakika mimi sijui ni mambo gani mutayazua baada yangu." Hali hiyo iliyomfanya Abubakr alie. *Taz: Muwata ya Imam Malik juz. 1 uk. 307, Maghazi ya Al-Waqidi uk. 310.*

Pia Mtume asingemtuma Ali ibn Abi Talib kumfuata Abubakar ili aichukue kutoka kwake Sura ya Baraa na kumzuwia kuifikisha. *Taz: Sahih Tirmidhi Juz. 4 uk. 339 Musnad Ahmad ibn Hambal Juz. 2 uk. 319, Mustadrak Al-Hakim Juz. 3 uk. 51*

Na wala Mtume alipokabidhi bendera siku ya Khaibar asingesema kuwa; "Kesho nitampa bendera yangu mtu ambaye anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanampenda mtu huyo, ni madhubuti kwenye mapambano harudi nyuma, Mwenyezi Mungu ameufanyia mtihani moyo wake kwa imani." Baada ya usemi huo akampa bendera Ali (a.s.) na hakumpa Abubakr. *Taz: Sahih Muslim, Babu Fadhail Ali Ibn Abi Talib.*

Na lau Mwenyezi Mungu angelitambua ya kwamba Abubakri anayo daraja hii ya imani na kwamba imani yake inashinda imani ya ummati Muhammad wote, basi Mwenyezi Mungu asingelimuonya kuwa mema yake yataporomoka pale aliponyanyua sauti yake juu ya sauti ya Mtume. *Taz: Sahih Bukhari Juz. 4 uk. 184.*

Na lau Ali ibn Abi Talib na Masahaba waliomfuata wangelifahamu ya kwamba Abubakr anayo daraja hii ya imani, basi isingejuzu kwao kuikhalifu *Baia* yake. Na lau Fatmah Az-Zahra angelifahamu ya kwamba Abubakr anayo daraja hii ya imani basi asingemkasirikia na kujizuwia kumsemesha na kujibu salamu yake na asingeomba dua dhidi yake katika kila sala. *Taz: Al-Imamah Was-Siyasah Juz. 1 uk. 14, Rasailul-Jahidh uk. 301, Aalaamun-Nisaa Juz. 3 uk. 1215.*

Kisha Bibi Fatmah asingelimzuia Abubakr kuhudhuria mazishi yake - kama ilivyokuja ndani ya usia wake. Na lau Abubakar angelifahamu kuwa yeye anayo daraja hii ya imani, basi asingetamani wakati wa mauti yake ya kwamba lau asingekuwa ameikashifu nyumba ya Bibi Fatmah (a.s.), na kwamba siku ya Saqifa angeliuacha Ukhalifa shingoni kwa mmoja kati ya watu wawili, yaani Umar au Abu Ubaidah. *Taz: Tarikh Tabari Juz. 4 uk. 52 Al-Imamah Was-Siyasah Juz. 1 uk. 18, Tarikh Al-Masoudi Juz. 1 uk. 414.*

Kwa hiyo basi mtu ambaye yuko katika daraja kama hii ya imani na hiyo imani yake inashinda imani ya umma wote, hawezi kujuta mwishoni mwa uhai wake kwa yale aliyomfanyia Fatmah na kujuta alipomuunguza Al-Faja-a Assalmi na kwa kutawalia Ukhalifa, kama ambavyo hawezi kutamani asiwe mtu na awe kapi au kinyesi cha mnyama.

Hivi kweli imani ya mtu kama huyu ni sawa na imani ya umma wa Kiislamu bali iko juu zaidi ya imani ya umma wa Kiislamu?

Na tutakapoichukua ile hadithi isemayo: "Lau ningekuwa mwenye kujifanyia mwandani, basi ningelimfanya Abubakr kuwa mwandani wangu."

Hadithi hii ni kama ile iliyotangulia, (tunajiuliza) kwani alikuwa wapi Abubakr siku ya *Muakhatus-Sughra* huko Makka kabla ya Hijra na siku ya *Muakhatul-Kubra* huko Madina baada ya Hijra na katika zote mbili, na mara mbili zote Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimfanya Ali kuwa ni nduguye na akasema, "Wewe ni ndugu yangu duniani na akhera"

Mtume hakumshughulikia Abubakr alimnyima udugu wa akhera kama vile alivyomnyima *kuwa mwandani wake.*

Na mimi sitaki kuirefusha maudhui hii ninatosheka na mifano hii miwili ambayo nimeileta kutoka ndani ya vitabu vya Kisunni. Ama kwa Mashia wao hawazikubali hadithi hizo moja kwa moja na wanazo dalili zilizo wazi ya kwamba ziliwekwa katika zama zilizokuja baada ya Abubakr.

Kwa hiyo basi ikiwa tutaacha (kutaja) fadhila na ubora wao na tukachunguza maovu (yaliyotendwa), bila shaka hatuwezi kupata ovu hata moja lililotendwa na Ali ibn Abi Talib wakati ambapo kwa wasiokuwa yeye tutakuta maovu mengi yaliyoandikwa ndani ya vitabu vya Kisunni kama vile sihahi (sita) na vitabu vya sira na historia.

Na kwa msingi huu inapatikana Ijmai ya pande zote mbili inayomuhusu Ali peke yake kama inavyotia nguvu jambo hilo historia na kwamba *Baia* sahihi haikuwa kwa mwingine isipokuwa kwa Ali peke yake.

Imam Ali aliikataa baia (yao baada ya kifo cha Athuman), lakini Muhajirina na Ansari wakamlazimisha na kuna watu fulani hawakufanya baia kwa Imam Ali lakini hakuwalazimisha wambai. Wakati huo huo baia ya Abubakr ilikuwa ni (tukio la) ghafla, Mwenyezi Mungu aliwakinga Waislamu kutokana na shari yake, kama asemavyo Umar ibn Khatab - na Ukhalifa wa Umar ulipatikana kwa usia wa Abubakr, nao Ukhalifa

wa Uthman (ulikuwa ni tukio la) unyonge kihistoria, na hiyo ni kwa kuwa Umar alipendekeza kamati ya watu sita (kujadili) suala la Ukhalifa (baada yake), na akawalazimisha wamchague mmoja wao na akasema, "Watakapoafikiana watu wanne na wawili wakapinga basi wawili hawa wauawe, na kama watu hawa sita watagawayika makundi mawili kila upande ukawa na watu watatu, basi chukueni maoni ya watu watatu ambao Abdurahman ibn Auf atakuwa pamoja nao, na iwapo muda utamalizika na watu hawa sita wakawa bado hawajaafikiana, basi wote hawa muwaue." Kisa hiki ni kirefu na ni cha kustaajabisha, lakini cha muhimu ni kwamba Abdur-rahman ibn Auf alimchagua Ali na kisha kumuwekea masharti kwamba awaongoze kwa mujibu wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mjumbe wake na sunna ya Masheikh wawili (yaani) Abubakr na Umar. Imam Ali aliikataa sharti hii na Uthman akaikubali na yeye akawa Khalifa kisha Ali alitoka katika Baia hiyo hali ya kuwa tangu mwanzo alifahamu matokeo yake yatakuwaje, na hapana shaka alilizungumzia jambo hilo ndani ya khutba yake ijulikanayo kama *"Khut-batus-Shaqshaqyah."*

Na baada ya Imam Ali (a.s.) Muawiya aliukalia Ukhalifa na akaubadilisha ukawa ni Ufalme wa Kaizari. Banu Umayyah wakawa wanapokezana, na baada yao wakaushika Banu Abbas mwana kumrithi baba, basi hakuja Khalifa isipokuwa kwa maagizo ya Khalifa aliyetangulia kwa yule ajaye au kwa nguvu ya upanga na silaha na hapakuwa na baia iliyo sahihi katika historia ya Uislamu kuanzia zama za Makhalifa (wa mwanzo) mpaka zama za Kamal Ataturki aliyemalizia Ukhalifa wa Kiislamu. Baia sahihi ilikuwa ni ya Amirul-Muuminina Ali ibn Abi Talib.

**iv). Hadithi zilizokuja kuhusiana na Imam Ali zinawajibisha kumfuata.**

Miongoni mwa hadithi nilizozichukuwa na zikanilazimisha nimfuate Imam Ali ni zile zilizoandikwa ndani ya sihahi za Kisunni na vikatilia nguvu usahihi wa hadithi hizo. Ama Mashia wao wanazo nyingi mno lakini - kama ilivyo ada, mimi sitatoa dalili wala kutegemea hadithi isipokuwa zile ambazo pande zote mbili wameafikiana na miongoni mwa hadithi hizo ni hizi zifuatazo:-

**a:** Hadithi isemayo “Mimi ndiyo mji wa elimu na Ali ndiyo mlango wake”.

Hadithi hii peke yake inatosha kubainisha kiigizo kinachopasa kukifuata baada ya Mtume (s.a.w.) kwani mwenye elimu ndiye anayefaa kufuatwa yaani yeye anastahiki mno kuwa kiigizo kuliko mjinga.

Mwenyezi Mungu amesema: *“Waambie, hivi wanalingana wale wanaofahamu na wale wasiyofahamu.” (Qur. 39:9)*

Na amesema vile vile kwamba:- “*Je aongozaye kwenye haki ndiye mwenye haki ya kufuatwa au yule asiyeongoka (mwenyewe) isipokuwa kwa kuongozwa (ndiye anayestahiki)? (Qur. 10:35)*

Hapana shaka mwenye maarifa ndiye anayeongoza na asiye na maarifa anastahiki kuongozwa na anahitajia mno uongofu kuliko mwingine yeyote.

Na kuhusu maelezo haya, historia imetuandikia ya kwamba Imam Ali yeye ni mwenye maarifa zaidi kuliko Sahaba yeyote kwa jumla, na wao Masahaba walikuwa wakimrejea Imam juu ya mas-ala yote mazito, nasi kamwe hatukupata kufahamu ya kwamba yeye Imam Ali aliwahi kuuliza kwa Sahaba yeyote, bali Abubakr anasema:- “Mwenyezi Mungu asinibakishe kwenye tatizo ambalo Abul-Hassan hayupo.”

Umar naye anasema:- “Lau asingelikuwa Ali basi Umar angeliangamia.” *Taz: Al-Istiabu Juz. 3 uk. 39, Manaqib Al-Khawarzami uk. 48, Ar-Riyadhun-Nadhrah Juz. 2 uk. 194.*

Ibn Abbas naye anasema:- “Elimu yangu na elimu ya Masahaba wa Mtume ukilinganisha na elimu ya Ali ni kama tone moja ndani ya bahari saba.” Imam Ali mwenyewe anasema:- “Niulizeni kabla hamjanikosa, namuapa Mwenyezi Mungu hamtaniuliza jambo lolote litakalokuwa mpaka siku ya kiyama isipokuwa nitakuelezeni, na niulizeni juu ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu, basi namuapa Mwenyezi Mungu, hapana aya yoyote isipokuwa mimi nafahamu kuwa ilishuka usiku au mchana, katika ardhi tambarare au mlimani.” *Taz: Ar-Riyadh An-Nadhrah Juz. 2 uk. 198,*

*Tarikh Al-Khulafa cha Suyut Al-Itqan Juz. 2 uk. 319, Fat-h Al-Bari Juz. 8 uk. 485, Tah-Dhibut-Tahdhib Juz. 7 uk. 338.*

Wakati huo huo Abubakr alipoulizwa maana *"Al-Abb"* iliyoko ndani ya kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo; *Wafakihatan wa Abban Mataan Lakum Walian-Amikum* Akasema, "Ni mbingu gani itakayonifunika na ardhi ipi itakayonibeba iwapo nitasema kitu nisichokijua ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu?"

Na Umar ibn Al-Khatab naye anasema:- "Watu wote wana elimu isipokuwa Umar, mpaka wanawake wenye bangili miguuni."

Sihahi za Kisunni na vitabu vyao vimeafikiana juu ya ubora wa Ali (a.s.) na kutangulia kwake katika elimu kuliko Masahaba wote, kwa mfano tu rejea maelezo yaliyomo ndani ya *Al-Istiabu Juz. 3 uk. 38-45* utakuta kauli za Masahaba wenyewe wakimtanguliza Imam Ali juu yao.

Umar ibn Al-Khataab aliulizwa (afafanue) aya fulani iliyomo ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu, matokeo yake akamkemea muulizaji na akampiga kwa mjeledi mpaka akamtoa damu kisha akasema, "Musiulize mambo, mkidhihirishiwa yatawakera." Na aliulizwa juu ya *Kalalah* hakuweza kufahamu.

Tabari ameandika ndani ya tafsiri yake kuhusu Umar kwamba amesema:- "Kwangu mimi kuifahamu maana ya *Kalalah* ni bora mno kuliko kupata majumba ya Shamu."

Vile vile Ibn Majah ameandika ndani ya Sunan yake kutoka kwa Umar ibn Al-Khatab amesema:- "Mambo matatu lau Mtume angeliyabainisha kwangu ingekuwa bora mno kuliko dunia na vilivyomo; Kalalah, Riba na Ukhalifa".

*Sub-hanallah,!* haiwezekani kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kuwa aliyanyamazia mambo haya akakosa kuyabainisha.

**b:** Hadithi isemayo:- "Ewe Ali wewe kwangu mimi unayo daraja kama ya Harun kwa Musa isipokuwa hapana Nabii baada yangu". *Taz: Sunan*

*Ad-Darami Juz. 1 uk. 54, Tafsiri ibn Kathir Juz. 4 uk. 232 Ad-Durul-Manthoor J. 6 uk. 111.*

Hadithi hii ambayo iko wazi kwa wenye akili, ndani yake kuna kuhusishwa Amirul-Muuminina Ali na Uwaziri, Uwasii na Ukhalifa.

Kwa hiyo kama alivyokuwa Haroon ni Waziri, Wasii, na Khalifa wa Musa alipoghibu na kwenda kwenye Miqat ya Mola wake, basi ni hivyo hivyo daraja ya Imam Ali naye ni kama Haroon amani imshukie yeye na Mtume wetu. Kwa hiyo Imam Ali (a.s.) ni mfano halisi wa Harun isipokuwa Utume ambao hadithi yenyewe imeuvua, na ndani yake pia ni kwamba Imam Ali ni Sahaba bora mno kuliko Masahaba wengine wote, na inavyofahamika ni kwamba hadithi hii inakubalika kwa Waislamu wote.

**c:** Hadithi isemayo:- "Yeyote ambaye mimi nilikuwa mtawalia mambo yake, basi huyu Ali ni mtawalia mambo yake, ewe Mwenyezi Mungu mpende atakayemtawalisha Ali, na umpinge atakaye mpinga, na umsaidie atakayemsaidia, na umdhalilishe atakayemdhalilisha na uizungushe haki pamoja naye popote atakakozungukia".

Hadithi hii peke yake inatosha kuyapinga madai ya kuwatanguliza Abubakr na Umar na Uthman kwa msingi wa kwamba (Ali) alisimikwa na mwenyewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu awe ni mtawalia mambo ya waumini baada ya Mtume, na hapana mazingatio yoyote kwa yule anayefasiri hadithi hii kwa maana ya mpenzi na msaidizi kwa kuitoa kutoka kwenye maana ya asili aliyoikusudia Mtume na yote hayo (yanafanyika) ili kulinda heshima ya Masahaba, kwani Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliposema kuhutubia siku hiyo kukiwa na joto kali alisema: "Je hamshuhudii kwamba mimi ni bora zaidi kwa Waumini kuliko nafsi zao?" Wakasema, "Bila shaka wewe ni bora ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu." Hapo ndipo aliposema:- "Basi yeyote, ambaye mimi nilikuwa mtawala wa mambo yake, huyu Ali ni mtawala wa mambo yake..." Hii ni Nassi (maagizo) yaliyowazi katika kumrithisha Ali Ukhalifa juu ya umma wake, na wala haiwezekani kwa mtu mwenye akili adilifu isipokuwa ni kuikubali maana hii na kuipinga ile tafsiri ya baadhi ya watu iliyolazimishwa, ili ili kwa kufanya hivi iwe ni kulinda heshima na utukufu wa Mtume kabla ya kulinda utukufu wa Masahaba. Kwani tafsiri yao hii ni

kudharau na kupuuza hekima ya Mtume ambaye alikusanya kundi kubwa la watu katika joto kali na jua utosini eti awambie kuwa Ali ni kipenzi cha Waumini na ni msaidizi wao. Je watu hawa wanaogeuza maandiko kwa lengo la kuhifadhi heshima ya wakubwa zao na mabwana zao, wataufasiri namna gani ule mkusanyiko wa watu waliompongeza Imam Ali jambo ambalo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliamuru (lifanyake)?

Mtume alianza na wakeze ambao ndiyo mama wa Waumini, na kisha wakaja Abubakr na Umar wakasema, "Hongera ewe mwana wa Abu Talib, leo kumekupambazukia na kukuchwea hali ya kuwa umtawalia mambo ya kila muumini mwanamume na mwanamke." Na ukweli historia inashuhudia kwamba, wale wanaogeuza (maana halisi iliyokusudiwa) ni waongo, na ole wao kwa yale wayaandikayo, amesema Mwenyezi Mungu: *"Bila shaka kuna kundi miongoni mwao wanauficha ukweli hali ya kuwa wanafahamu" (Qur. 2:146)*

**d:** Hadithi isemayo:- "Ali anatokana na mimi na mimi natokana na Ali, na wala hawezi mtu kutekeleza (jambo) kwa niaba yangu isipokuwa mimi mwenyewe au Ali." *Taz: Sunan Ibn Majah, Juz. 1 uk. 44, Khasaisun-Nasai uk. 20, Sahih Tirmidhi Juz. 5 uk. 300, Ar-Riyadhu An-Nadhrah J. 2 uk. 229.*

Hii ni hadithi nyingine tukufu iliyowazi ikieleza kwamba Imam Ali ni mtu pekee ambaye Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimpa ustahiki (wa kutenda) kwa niaba yake, na hadithi hii Mtume aliisema wakati alipomtuma Imam Ali akawasomee watu sura Al-Baraa siku ya Hija badala ya Abubakr, na Abubakr alirudi hali ya kuwa analia huku akisema, "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kuna kitu kimeshuka kwa ajili yangu?"Mtume (s.a.w.) akasema, "Mwenyezi Mungu ameniamuru hivyo kwamba, hawezi kutekeleza (jambo) kwa niaba yangu isipokuwa mimi mwenyewe au Ali."

Na hadithi hii inaitia nguvu ile (hadithi) nyingine aliyoisema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kumwambia Ali katika munasaba mwingine pale aliposema: "Wewe Ali utaubainishia Umma wangu yale mambo ambayo watahitilafiana ndani yake baada yangu." *Taz: Tarikh Damishq ya ibn Asakir Juz. 2 uk. 488, Kunuzul-Haqaiq cha Al-Mawi uk. 203, Kanzul-Ummal Juz. 5 uk. 33.*

Basi ikiwa (mtu mwingine) hawezi kutekeleza jambo kwa niaba ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu isipokuwa Ali, na ni yeye ndiye atakayeubainishia Umma (wa Kiislamu) mambo watakayohitilafiana ndani yake baada ya Mtume, basi itakuwaje amtangulie mtu ambaye hafahamu maana ya "Al-Abb" na yule asiyefahamu maana ya "Al-Kalalah", kwa hiyo naapa ya kwamba huu ni miongoni mwa misiba iliyoukumba Umma wa Kiislamu na kuuzuia usiweze kutimiza jambo muhimu ambalo Mwenyezi Mungu aliuchagulia Umma huu. Na hii haitakuwa ni hoja dhidi ya Mwenyezi Mungu wala dhidi ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wala Amirul-Muuminin Ali ibn Abi Talib, bali hoja iliyowazi itakuwa dhidi ya wale walioasi na kubadilisha.

Mwenyezi Mungu amesema:-

*"Na wanapoambiwa njooni kwenye yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, na (mje) kwa Mtume, wao husema, yanatutosha yale tuliyowakuta nayo baba zetu, je hata kama baba zao walikuwa hawajui kitu wala hawakuongoka.?" (Qur. 5:104)*

**e:** Hadithi ya Ad-Dar Yaumul-Indhar.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amesema hali ya kuwa akimuashiria Ali: "Hakika huyu ni ndugu yangu, wasii wangu na Khalifa wangu baada yangu, basi msikilizeni na mumtii."

*Taz: Tarikh Tabari Juz. 2 uk. 319, Tarikh Ibn Athir Juz. 2 uk. 62, Siratu Al-Halabiyah Juz. 1 uk. 311 Shawahidut-Tanzil cha Al-Haskani Juz. 1 uk. 371 Kanzul-Ummal Juz. 15 uk. 15. Tarikh ibn Asakir Juz. 1 uk. 85 Tafsir Al-Khazin ya Alaud-Dini Shafii Juz. 3 uk. 371, Hayatu Muhammad cha Husain Haikal, chapa ya kwanza mlango wa Waandhir Ashira Takal-Aqrabina.*

Hadithi hii pia ni miongoni mwa hadithi sahihi walizozinakili wanahistoria mwanzoni tu mwa kutumwa kwa Mtume na wakaiweka kuwa ni miongoni mwa miujiza ya Mtume (s.a.w.), lakini siasa ndiyo iliyobadili na kupotosha ukweli na hali halisi, na siyo ajabu hali hii kutokea kwani yaliyotokea katika zama hizo zenye giza yanajirudia leo katika zama zenye mwanga. Huyu Muhammad Husain Haikal ameiandika hadithi hii kwa ukamilifu ndani ya kitabu chake kiitwacho "Hayatu Muhammad"

(yaani maisha ya Muhammad) ndani ya ukurasa wa 104 chapa ya kwanza ya mwaka 1354 A.H. na katika chapa ya pili na zilizofuatia, katika hadithi hiyo hiyo kumeondolewa ile kauli ya Mtume isemayo (wasii wangu na Khalifa wangu baada yangu); vile vile ndani ya Tafsiri ya Tabar Juz. ya 19 ukurasa 121 wameondosha ile kauli ya Mtume isemayo (wasii wangu na Khalifa wangu) na wakabadilisha kwa kauli isemayo: ***"Hakika huyu ni ndugu yangu na hivi na hivi."*** wakasahau kwamba Tabari ameitaja hadithi hii kwa ukamilifu ndani ya kitabu chake cha historia juzuu ya pili ukurasa wa 319.

Angalia ni vipi wanavyopotosha maneno kutoka mahala yanapostahiki na wanayageuza mambo, wao wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao na Mwenyezi Mungu ataitimiza nuru yake...

Na wakati nilipokuwa nikifanya utafiti, nilitaka nisimame juu ya msingi uliowazi, basi niliitafuta ile chapa ya kwanza ya kitabu kiitwacho *"Hayatu Muhammad"* na nilikipata, namshukuru Mwenyezi Mungu, lakini baada ya tabu na mashaka na ili nigharimu kiasi kikubwa lakini la muhimu ni kwamba niliuona ule upotoshaji, na kilinizidishia yakini kwamba watu waovu wanajaribu kwa juhudi zao kuufuta ukweli uliothibiti kwa sababu tu ni hoja yenye nguvu inayowaunga mkono makhasimu wao!

Lakini mtafiti mwenye uadilifu pindi anapoona kitu miongoni mwa upotoshaji na udanganyifu kama huu huzidi kujitenga na watu kama hao na bila shaka huwa anafahamu kwamba hawana hoja isipokuwa kupotosha na kutia uongo na kugeuza ukweli kwa gharama yoyote ile.

Hapana shaka kwamba wameajiri waandishi wengi na kuwamiminia mali nyingi, kama ambavyo wamewamiminia sifa kemkem na shahada za vyuo vikuu za uongo ili wawaandikie yale wayatakayo miongoni mwa vitabu na makala zinazowashutumu Mashia na kuwakufurisha. Yote haya yanafanyika ili waitetee kwa juhudi zao zote heshima ya baadhi ya Masahaba waliogeuka kinyume nyume kwa visigino vyao hata kama sifa hiyo ni batili, na (Masahaba hao) ndiyo waliobadilisha haki kuwa batili baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. *"Vivyo hivyo walisema wale waliokuwa kabla yao mfano wa kauli yao hii, nyoyo zao zimefanana, bila shaka tumezibainisha hoja zetu zote kwa watu wenye kuyakinisha mambo". (Qur. 2:118)*

# HADITHI SAHIHI ZINAZOLAZIMISHA KUWAFUATA AHLUL-BAIT

**i). Hadithi ya Vizito Viwili:**

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amesema: "Enyi watu nimeacha kwenu vitu ambavyo mkivichukua kamwe hamtapotea, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Kizazi changu watu wa nyumba yangu." Na pia amesema: "Inakaribia kuwa atanijia Mjumbe wa Mola wangu nami nitaitika, na kwa hakika mimi ninaacha kwenu vizito viwili cha kwanza ni kitabu cha Mwenyezi Mungu, ndani yake muna uongofu na nuru, na Watu wa nyumba yangu, nakukumbusheni Mwenyezi Mungu juu ya Watu wa nyumba yangu, nakukumbusheni Mwenyezi Mungu juu ya watu wa nyumba yangu."

*Taz: Sahih Muslim, Babu Fadhail Ali Juz. 5 uk. 122, Sahih Tirmidh Juz. 5 uk. 328, Mustadrak Al-Hakim Juz. 3 uk. 148, Musnad Imam Ahmad Ibn Hambal Juz. 3 uk. 17.*

Tukiangalia kwa makini ndani ya hadithi hii tukufu ambayo sihah za Ahlus-Sunnah zimeiandika, tunakuta ni Mashia peke yao tu ndiyo waliovifuata vizito viwili hivyo, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi kitukufu cha Mtume, ambapo Ahlus-Sunnah Wal-Jamaa wamefuata kauli ya Umar isemayo; "Kinatutosha kitabu cha Mwenyezi Mungu".

Laiti wao wangekifuata Kitabu cha Mwenyezi Mungu bila ya kukifasiri kufuatana na matamanio yao. Ikiwa Umar mwenyewe hafahamu maana ya *Alkalala* iliyomo ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu wala hakuifahamu aya ya kutayammamu na hukmu nyinginezo, basi itakuwaje hali ya mtu aliyekuja baada yake na kamfuata bila ya kufanya ijtihadi kwa mujibu wa maoni yake kuhusu maandiko ya Qur'an? Na kwa namna hali ilivyo

huenda watanijibu kwa kutumia hadithi iliyopokelewa kwao (Masunni) nayo ni ile isemayo, "Nimekuachieni Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna zangu."

Hadithi hii kama itasihi, na ni sahihi kwa mujibu wa maana yake kwani maana ya kizazi kufuatia kauli yake Mtume ndani ya hadithi ya vizito viwili iliyotangulia ni kuwarejea Ahlul-Bait wangu ili wakufundisheni:

**Kwanza**: Sunna zangu au wakunukulieni hadithi sahihi kwani wao wametakasika kutokana na uongo na kwamba Mwenyezi Mungu amewahifadhi kwa aya ya utakaso.

**Pili:** Ili wawafasirieni maana zake na makusudio yake, kwani Kitabu cha Mwenyezi Mungu peke yake (kama kilivyo) hakitoshelezi kuwapeni uongofu, ni mara ngapi baadhi ya vikundi vinatoa hoja kwa kutumia Kitabu cha Mwenyezi Mungu hali ya kuwa vimo ndani ya upotovu, kama yalivyokuja maelezo ya mwenyewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliposema, "Ni mara ngapi msomaji wa Qur'an (husoma) Qur'an nayo ikawa inamlaani?" Kitabu cha Mwenyezi Mungu kimenyamaa kimya na kimebeba namna nyingi, na ndani yake kuna (aya) Muhkam na Mutashabih na hapana budi zifahamike kwa kuwarejea wale waliobobea katika elimu kama isemavyo Qur'an, na kuwarejea Ahlul-Bait kwa mujibu wa tafsiri ya Mtume.

Mashia wao katika kila kitu wanawarejea Maimamu Maasum wanaotokana na Ahlul-Bait wa Mtume, na wala hawafanyi ijtihadi isipokuwa katika jambo ambalo halina Nassi ndani yake. Ama sisi tunarejea kwa Masahaba katika kila kitu, sawa sawa katika tafsiri ya Qur'an au katika kuthibitisha Sunna na tafsiri yake, na hapo kabla tumekwishakufahamu hali za Masahaba na yale waliyoyatenda na waliyoyaeleza na kujitahidi ndani yake kwa mtazamo wao dhidi ya maandiko yaliyowazi. Mambo hayo ni mengi kwa mamia na haiwezekani kuwategemea watu mfano wao baada ya kupatikana mengi kutokana nao.

Na tutakapowauliza wanachuoni wetu, "Ni Sunna gani mnayoifuata"? Moja kwa moja watatujibu kuwa, "Ni Sunna ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.)." Ukweli wa historia haukubaliani na hilo, kwani ni wao hao hao waliopokea mapokezi yasemayo kwamba mwenyewe Mtume amesema, "Shikamaneni na Sunna zangu na Sunna za Makhalifa

wangu viongozi baada yangu, ziumeni kwa magego." Kwa hiyo Sunna wanayoifuata kwa kiwango kikubwa ni Sunna ya Makhalifa, na hata hiyo Sunna ya Mtume waisemayo ni ile iliyopokelewa kupitia watu hawa.

(Cha ajabu) ni kwamba sisi ndani ya vitabu vyetu tumeandika ya kuwa Mtume aliwazuwia (Masahaba) wasiandike Sunna zake ili zisije zikachanganyika na Qur'an, na ndivyo alivyofanya Abubakar na Umar wakati wa Ukhalifa wao. Kwa hiyo baada ya maelezo haya haitabakia hoja yoyote ndani ya kauli yetu kwamba, "Nimekuachieni Sunna zangu"

Mifano michache nimeitaja ndani ya uchunguzi huu lakini hii inatosha kuirudi hadithi hii kwani miongoni mwa Sunna za Abubakr na Umar na Uthman zinaipinga Sunna ya Mtume na kuibatilisha kitu ambacho kiko wazi.

Iwapo tukio la kwanza lililotokea baada tu ya kifo cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na likasajiliwa na Ahlus-Sunnah Wal-Jamaa pamoja na wanahistoria ni lile la Bibi Fatma Zahra kumkasirikia Abubakr ambaye (alizuwia mirathi ya Bibi Fatmah) kwa kutolea ushahidi wa hadithi isemayo "Sisi Mitume haturithiwi tunachokiacha ni sadaka."

Bibi Fatmah (a.s.) aliipinga hadithi hii na akaibatilisha kwa mujibu wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu, akatoa hoja kwa kusema kuwa baba yake (yaani) Mtume (s.a.w.) hawezi kupingana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu ambacho kiliteremshwa kwake kwani Mwenyezi Mungu anasema:

*"Mwenyezi Mungu anakuusieni juu ya watoto wenu, mwanaume apate sawa na sehemu ya wanawake wawili." (Qur. 4:11)*

Na hii aya inawakusanya Manabii na wasiokuwa Manabii, pia akampa hoja ya kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

*"Na Suleiman akamrithi Daudi." (Qur. 27:16) Na wote hawa wawili ni Manabii.*

Na pia kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

*"Basi nipe mrithi kutoka kwako, atakayenirithi na kuwarithi kizazi*

*cha Yaqub na umfanye mwenye kukuridhisha ewe Mola wangu" (Qur. 19:5-6).*

Tukio la pili ni lile lililotokea kwa Abubakr katika zama za Ukhalifa wake, na likasajiliwa na wanahistoria miongoni mwa Masunni, pale Abubakr alipohitilafiana na mtu wa karibu yake ambaye ni Umar ibn Khatab. Tukio hilo ni lile ambalo kwa muhtasari ni ule uamuzi wake wa kuwapiga vita wanaozuwia kutoa zaka na kuwauwa, kwani Umar alikuwa akimpinga na kumwambia, "Mimi nimesikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) anasema, Nimeamuriwa niwapige vita watu mpaka waseme *Lailaha Illallah Muhammadur-Rasulullah* basi, mwenye kusema hivyo mali yake na damu yake imehifadhika tokana nami na hesabu yake iko kwa Mwenyezi Mungu.

Hii ni Nassi aliyoiandika Muslim ndani ya Sahih yake ya kwamba, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimpa Ali bendera siku ya Khaibar kisha Ali akasema, "Ni juu ya msingi wa jambo gani nikawapige vita"? Mtume (s.a.w.) akasema.,"Wapige mpaka washuhudie ya kwamba hapana Mola apasiwaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wakifanya hivyo basi watakuwa wameizuwia damu yao na mali zao kutokana nawe isipokuwa kwa haki inayostahiki na hesabu yao ni juu ya Mwenyezi Mungu." *Taz: Sahih Muslim Juz. 8 uk. 51 Kitabul-Iman.*

Lakini Abubakr hakukinaishwa na hadithi hii yeye akasema: "Wallahi nitawapiga vita wanaotenganisha baina ya sala na zaka kwani zaka ni haki ya mali." Au alisema, "Wallahi lau watanizuwilia sadaka waliyokuwa wakiitowa kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu basi ningewapiga kwa sababu ya kuizuia."

Umar ibn Khatab baadaye aliridhika na hali hiyo na akasema, "Nilimuona, Abubakr ameng'ang'ania jambo hilo mpaka nami Mwenyezi Mungu akakifungua kifua changu."

Mimi sielewi ni vipi Mwenyezi Mungu hufungua vifua vya watu kwa kuikhalifu Sunna ya Mtume wao?

Hii ni tafsiri itokanayo na wao wenyewe ili tu wajihalalishe kuwapiga vita Waislamu ambao Mwenyezi Mungu ameharamisha kuwauwa pale aliposema ndani ya kitabu chake kitukufu: *"Enyi mlioamini! mtakaposafiri katika njia ya Mwenyezi Mungu basi hakikisheni wala musimwambie anayekutoleeni salamu: Wewe si Muumini. Je, mnataka mafao ya dunia hii hali ya kuwa kwa Mwenyezi Mungu kuna mafao mengi zaidi. Hivyo ndivyo mlivyokuwa ninyi zamani na Mwenyezi Mungu, akakuneemesheni. Basi chunguzeni sawa sawa. Hakika Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda. (Qur. 4:94)*

Watu hawa waliomkatalia kumpa zaka Abubakr zaka zao, hawakupinga msingi wa wajibu wa kutoa zaka, lakini walichelewa kufanya hivyo ili wachunguze mambo yalivyo. Mashia wao wanasema, "Bila shaka watu hawa walishitushwa na Ukhalifa wa Abubakr kwani wako miongoni mwao ambao walikuwa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika Hija yake ya mwisho na wakasikia toka kwa Mtume lile tangazo la juu ya Ali ibn Abi Talib kuhusu Ukhalifa. Walifanya uzito wakingojea uhakika lakini Abubakr alitaka tu wanyamaze wasifuatilie ukweli. Na kwa kuwa mimi sitoi ushahidi wala hoja kwa maneno wasemayo Mashia basi naliacha jambo hili kwa yoyote anayeona umuhimu wake ili aifuatilie.

Kwa msingi huu sitaacha kukieleza kisa cha Thaalabah, ya kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika zama za uhai wake kilimtokea kisa cha huyu Thaalabah ambaye alimuomba Mtume amuombee dua ya utajiri na akang'ang'ania mno kuombewa dua hiyo, isitoshe kamuahidi Mwenyezi Mungu kwamba atatoa sadaka. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akamuombea na Mwenyezi Mungu akamtajirisha kutokana na fadhila zake. Hatimaye mji wa Madina na viunga vyake ukawa ni mdogo kwake kwa wingi wa ngamia na mbuzi, ikamlazimu awe mbali (na mji) na hakuweza kuhudhuria sala ya Ijumaa. Na pindi Mtume alipowatuma watumishi wa idara ya zaka (yule Thaalabah) alikataa kuwapa chochote katika zaka akasema:- "Hii sasa ni kodi au mfano wa kodi." Lakini pamoja na hali hii Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hakumpiga vita bali ilishuka Qur'an juu ya mtu huyu ikasema: *"Na miongoni mwao (hao wanafiki) wako waliomuahidi Mwenyezi Mungu kuwa akitupa katika fadhila zake tutatoa sadaka na tutakuwa miongoni mwa watendao mema, lakini alipowapa hizo fadhila walizifanyia ubakhili na wakageuka na huku wakipuuza". (Qur. 9:75-76)*

Baada ya kushuka aya hii, Thaalabah alikuja akamtaka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aikubali zaka yake (lakini) Mtume alikataa kama riwaya inavyoeleza.

Sasa ikiwa Abubakar na Umar wanafuata Sunna ya Mtume, upinzani huu ni wa nini na (mbona) wanahalalisha kumwaga damu ya Waislamu wasio na hatia (isipokuwa) kwa kuzuwia kutoa zaka? Ama wale wanaomtakia udhuru Abubakr (kwa tendo lake la kuwapiga vita waliozuwia zaka) na wale wanaotaka kulihalalisha kosa lake kwa kulipa tafsiri ya kwamba zaka ni haki ya mali, basi hawatabakia wao wala yeye na udhuru wowote baada ya kisa cha Thaalabah ambaye aliipinga zaka na kuona kuwa ni kodi (lakini Mtume hakumfanya kitu). Lakini nani ajuaye, kwani huenda Abubakr alimkinaisha sahibu yake Umar kwamba ni wajibu kuwauawa wanaozuwia kutoa zaka ili usienee wito wao katika nchi za Kiislamu kwani wito wao ungeweka hai lile tamko la Ghadir Khum ambalo lilimweka Ali kwenye kiti cha Ukhalifa.

Na kwa ajili hiyo Mwenyezi Mungu akakikunjua kifua cha Umar ibn Khatab kama anavyodai mwenyewe ili akubaliane kuwapiga vita wanaozuwia zaka na yeye huyu Umar ndiye ambaye alionya kuwa angewaua wale wapinzani wa *baia* waliokuwa ndani ya nyumba ya Fatmah na kwamba angewachoma kwa moto. Yote hayo ni kwa ajili ya kutaka achukue toka kwao *baia* kwa ajili ya sahibu yake.

Ama tukio la tatu ambalo lilimtokea Abubakr mwanzoni mwa Ukhalifa wake na katika tukio hilo Umar alimkhalifu (Abubakr) na aliyabadilisha maandiko ya Qur'an na Sunna ya Mtume ni lile tukio la Khalid ibn Walid ambaye alimuuwa Malik ibn Nuwairah na akamtendea uchafu mkewe ndani ya usiku ule ule (aliomuuwa mume).

Umar alikuwa akimwambia Khalid, "Ewe adui wa Mwenyezi Mungu, umemuua mtu Muislamu kisha umemtendea uchafu mkewe, Wallahi nitakupiga kwa mawe." Taz: Tarikh Tabari J. 3 uk. 280, Tarikh Abul-Fida Juz. 1 uk. 158, Tarikh Yaqubi Juz. 2 uk. 110, Al-Isabah Fimaarifatis-Sahaba Juz. 3 uk. 336.

Lakini Abubakr alimtetea (Khalid) na akasema: "Ewe Umar mwachie

amefasiri na amekosea, wacha kumsema sema Khalid."

Hii ni fedheha nyingine iliyotendwa na sahaba mkubwa ambayo imesajiliwa na historia, na tumtajapo (sahaba huyu) humtaja kwa heshima na utukufu, bali tumempa *laqabu ya Saifullahil-Mas-lul* yaani upanga wa Mwenyezi Mungu ulio nje ya ala.

Niseme nini juu ya sahaba anayefanya matendo kama haya, anamuua Malik ibn Nuwairah ambaye ni Sahaba Mtukufu Bwana wa ukoo wa Bani Tamim na Bani Yar'buu na ni mtu wa kupigiwa mfano kwa murua (wake), ukarimu na ushujaa.

Hapana shaka, wanahistoria wamesimulia ya kwamba, Khalid ibn Walid alimfanyia khiana Malik na watu wake baada ya kuwa wameweka silaha chini na wakasali jamaa akawatia kamba. Na miongoni mwao akiwemo Layla binti Min-Hal mke wa Malik ambaye alikuwa mwanamke mashuhuri kwa uzuri miongoni mwa wanawake wa Kiarabu, na inasemekana ya kwamba hakupata kuonekanwa mwanamke mzuri kuliko yeye, kwa hiyo Khalid akafitinika kwa uzuri wake. Malik akamwambia Khalid, "Ewe Khalid ungetupeleka kwa Abubakr yeye ndiye awe mwenye kutuhukumu." Abdallah ibn Umar na Abu Qatadah Al-Ansari waliingilia kati wakamsisitiza Khalid awapeleke kwa Abubakr, lakini Khalid akapinga akasema: "Mungu hatonisamehe iwapo sintakuua." Basi Malik alimgeukia mkewe Layla na akamwambia Khalid, "Anayenuia ni huyu hapa" yaani mkewe. Basi Khalid akaamuru shingo ya Malik ikatwe kisha akamkamata Layla mke wa Malik na akamuingilia usiku ule ule. *Taz: Tarikh Abul-Fida Juz. 1 uk. 158, Tarikh Al-Yaqubi Juz. 2 uk. 110, Tarikh ibn Shahnah Hamish ya Al-Kamil Juz. 11 uk. 114, Wafiyatul-Aayan Juz. 6 uk 14.*

Niseme nini juu ya Masahaba hawa ambao wanahalalisha aliyoyaharamisha Mwenyezi Mungu na wanaua nafsi za Waislamu kwa ajili ya matamanio ya nafsi na wanahalalisha tupu alizoziharamisha Mwenyezi Mungu, kwani ndani ya Uislamu haolewi mwanamke aliyefiwa na mumewe isipokuwa baada ya eda ambayo ameieleza Mwenyezi Mungu ndani ya kitabu chake kitukufu. Lakini Khalid matamanio yake aliyafanya kuwa ndiyo mungu wake akaangamia. Je, kwa Khalid eda ina kiwango gani (cha kuheshimiwa) baada ya kumuua mume wake (Layla) hali ya kuwa kamtia kifungoni na kwa dhulma? Pia akawaua watu wake

hali ya kuwa ni Waislamu (na alifanya yote haya) mbele ya ushuhuda wa Abdallah ibn Umar na Abu Qatadah ambaye alikasirika mno kutokana na matendo ya Khalid, na aliondoka akarudi Madina na akaapa kwamba (kamwe) hatokuwa ndani ya uongozi uliopo (chini ya) Khalid ibn Walid. *Taz: Tarikh Tabari Juz. 3 uk. 280, Tarikh Yaqubi Juz. 2 uk. 110, Tarikh Abul-Fida, Al-Isabah Juz. 3 uk. 336.*

Yatutosha kuhusu Qadhia hii mashuhuri kukiri kwa Ustadh Haikal ndani ya kitabu chake kiitwacho *As-Sidiq Abubakar* chini ya anuani isemayo, "Maoni ya Umar na hoja yake." Amesema:- "Ama Umar alikuwa ni mfano wa uadilifu thabiti, yeye alikuwa akimuona Khalid kwamba alimfanyia uadui Muislamu na kumtenda tendo chafu mkewe kabla ya kumalizika eda yake, basi haifai kwa mtu kama huyo kubakia ndani ya uongozi wa jeshi ili asije rudia kosa kama hili na hatimaye kuharibu mambo ya Waislamu na kuichafua heshima yao mbele ya Waarabu." (Ustadh Haikal anaendelea) anasema, "Haifai kabisa kuachwa bila ya kuadhibiwa kutokana na yale aliyoyafanya kwa Layla."

Basi lau itasihi kwamba yeye alijitahidi akakosea kuhusu jambo la Malik - kitu ambacho Umar hakukikubali- basi yatosha kuadhibiwa kwa yale aliyoyatenda kwa mkewe (Malik), basi hawezi kuleta udhuru kwamba yeye ni upanga wa Mwenyezi Mungu na kwa ajili hiyo asiadhibiwe kwa mujibu wa sheria. Na ungekuwa ni mfano mbaya wa kupigiwa Waislamu katika kuheshimu kitabu cha Mwenyezi Mungu, ndiyo maana Umar hakuacha kumrudia Abubakr na kumsisitiza mpaka akamwita Khalid na akamlaumu ....." *Taz: Kitabu Siddiq Abubakr cha Ustadh Haikal uk. 151.*

Hebu tumuulize Ustadh Haikal na walio kama yeye miongoni mwa wanachuoni wetu ambao wanapotosha (mambo) kwa msingi wa kulinda heshima ya Masahaba, hebu tuwaulize "Ni kwanini Abubakr hakumuadhibu Khalid"? Ikiwa Umar - kama alivyosema Ustadh Haikal ya kwamba alikuwa ni mfano wa uadilifu madhubuti, basi ni kwanini (Umar) alitosheka tu na (adhabu) ya kuondolewa kwenye uongozi wa jeshi na wala haikusimamishwa adhabu ya kisheria dhidi ya Khalid kulingana na kosa alilotenda? Kwa kufanya hivyo ili isijekuwa ni mfano mbaya unaopigiwa Waislamu katika kuheshimu Kitabu cha Mwenyezi Mungu kama alivyoeleza? Je, wao walikiheshimu Kitabu cha Mwenyezi Mungu

na wakasimamisha adhabu (alizoziweka) Mwenyezi Mungu? Sivyo kabisa hiyo ni siasa, na ni kipi kitachokujulisha hiyo siasa ni kitu gani? Ni kule kufanywa maajabu na hakika ya mambo kugeuzwa na maandiko ya Qur'an kupigwa ukutani.

Hebu tuwaulize baadhi ya wanachuoni wetu ambao wanasimulia ndani ya vitabu vyao kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) alikasirika mno pale Usamah alipomjia na kumuombea msamaha yule mwanamke mwenye mheshimiwa aliyeiba.

Mtume (s.a.w) alisema, "Ole wako, wamuombea tumsamehe adhabu miongoni mwa adhabu za Mwenyezi Mungu, Wallahi lau Fatimah binti Muhammad angekuwa ndiye aliyeiba ningemkata mkono wake, bila shaka waliangamizwa waliokuwa kabla yenu, pindi anapoiba mtu mwenye mheshimiwa humuacha na anapoiba mnyonge humuadhibu kwa mujibu wa sheria."

Ni vipi wanachuoni hawa wananyamazia mauaji ya Waislamu wasio na hatia, na wake zao kuingiliwa katika usiku ule ule hali ya kuwa wameghubikwa na huzuni za vifo vya waume zao? Ni bora lau wangenyamaza lakini wao wanajaribu kulitakasa tendo la Khalid kwa kuunda uzushi na kumtengenezea sifa na mambo mema mpaka wakampa Laqabu ya kuwa ni upanga wa Mwenyezi Mungu ulio nje ya ala (tayari kumshambulia adui).

Mmoja kati ya rafiki zangu ambaye alikuwa akipendelea utani na kugeuza maana alinishangaza nilipokuwa namuelezea sifa za Khalid ibn Walid katika siku za ujinga wangu nikamwambia "Bila shaka yeye ni upanga wa Mwenyezi Mungu ulio nje ya ala." Yeye akanijibu akasema: "Yeye ni upanga wa shetani uliopooza." Nilimshangaa siku hiyo, lakini baada ya uchunguzi Mwenyezi Mungu amenifungulia macho yangu na kunitambulisha daraja ya watu hawa ambao waliukalia Ukhalifa na wakazibadilisha hukmu za Mwenyezi Mungu na wakachupa mipaka ya Mwenyezi Mungu na kuivunja.

Na huyu Khalid ibn Walid anacho kisa (alichokifanya) katika zama za uhai wa Mtume (s.a.w.), pindi Mtume alipomtuma kwenda kwa Bani

Judhaimah ili awalinganie Uislamu, na wala hakumuamuru kuwapiga vita. (Watu hawa) hawakuweza kutamka vema neno *Aslamnaa* yaani tumesilimu, badala yake wakasema *Sabaana Sabaana,* basi Khalid akaanza kuwauwa na kuwashika mateka na hao mateka akawatoa kwa wenzake na akawaamuru wawauwe, baadhi yao walikataa kuwaua pale ilipowabainikia kwamba wamesilimu, na waliporudi (Madina) walimueleza Mtume (s.a.w.) juu ya jambo hilo.

Mtume (s.a.w.) alisema: "Ewe Mwenyezi Mungu najitakasa kwako kutokana na yale aliyoyafanya Khalid ibn Walid." Alisema hivi mara mbili. Taz: Sahih Bukhari Juz. 4 uk 171 mlango usemao: Idhaa Qadhal-Hakim Bijaurin Fahuwa Raddun.

Na hatimaye Mtume alimtuma Ali ibn Abi Talib aende kwa Bani Judhaimah akiwa na mali akafidia damu na mali zao zilizoharibiwa, mpaka akafidia vyombo vya mbwa, na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alielekea kibla hali ya kuwa amesimama amenyoosha mikono yake mbinguni hadi ikaonekana sehemu ya kwapani kwake akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi najitakasa kwako kutokana na yale aliyoyatenda Khalid ibn Walid." Mara tatu. *Taz: Siratu Ibn Hisham Juz. 4 uk. 53 Tabaqat ibn Saad, Usudul-Ghabah Juz. 3 uk. 102.*

Tunauliza, uko wapi basi uadilifu wa Masahaba usemwao? Ikiwa Khalid ibn Walid naye kwetu sisi ni miongoni mwa watukufu wetu mpaka tumempa Laqabu ya Upanga wa Mwenyezi Mungu. Hivi kweli Mola wetu alikuwa akiunyoosha upanga wake na kuuwezesha kufanya kazi dhidi ya Waislamu na watu wasiokuwa na hatia na pia kuvunja heshima ya vitu vitakatifu? Katika jambo hilo kuna utata kwani Mwenyezi Mungu anakataza kuuwa nafsi na anakataza maovu na machafu na ujeuri, lakini yeye (Khalid) katika wakati huo huo ananyoosha panga la ujeuri ili kuwafanyia khiyana Waislamu, kumwaga damu yao, kuharibu mali zao, kuwateka wanawake zao na watoto wao. Kwa hakika huu ni uzushi na uongo ulio wazi (kumwita Khalid kuwa ni upanga wa Mwenyezi Mungu na kuwa ni muadilifu). Umetakasika ewe Mola wetu na sifa njema ni zako, umetukuka na kutakasika mno kutokana na hayo, utakatifu ni wako, hukuumba mbingu na nchi na vilivyomo kwa mchezo, hiyo ni fikra ya wale ambao wamekufuru, basi ole wao waliokufuru kutokana na moto.

Vipi ilifaa kwa Abubakr hali ya kuwa ni Khalifa wa Waislamu kusikia madhambi hayo yanayoangamiza kisha akayanyamazia bali akamtaka Umar asimsemeseme Khalid na akamkasirikia Abu Qatadah kwa sababu ya upinzani wake kwa tendo la Khalid? Hivi kweli alikuwa ameyakinisha kwamba Khalid alikuwa amefanya Taawili na akakosea? Basi kutakuwa na jibu gani kwa waovu baada ya tukio kama hili watendapo yaliyoharamishwa kisha wadai kuwa wameyatenda kwa kuyapa tafsiri?

Ama mimi siamini kwamba Abubakar alikuwa ni mwenye kuawili (kujitahidi) kuhusu jambo la Khalid ambaye Umar alimuita kuwa ni adui wa Mwenyezi Mungu, na maoni ya Umar ilikuwa ni kwamba (Abubakar) amuuwe Khalid kwa sababu amemuua mtu Muislamu na ampige kwa mawe kwa sababu amemzini mke wa Malik. Lakini hapakuwa chochote dhidi ya muuaji huyu muovu bali alitoka akiwa ni mshindi dhidi ya Umar ibn Khatab kwani Abubakr alisimama upande wake hali ya kuwa anamfahamu vilivyo Khalid kuliko mwingine yeyote.

Wanahistoria wameandika kwamba, Abubakar alimtuma tena Khalid baada ya tukio hili baya aende Yamamah mji ambao alitoka akiwa mshindi na alifuatishia kumuoa msichana kama vile alivyomfanyia Layla kabla damu za Waislamu hazijakauka wala damu za wafuasi wa Musailamah nazo hazijakauka. Abubakr alimkemea mno kwa tendo lake hili kuliko alivyomkemea juu ya tendo lake alilomfanyia Layla. *Taz: As-Siddiqu Abubakr cha Ustadh Haikal uk. 151 na kuendelea.*

Hapana shaka kwamba binti huyu mwingine, naye alikuwa na mume, Khalid akamuuwa na kumtenda binti tendo chafu kama alivyomfanya Layla mke wa Malik, vinginevyo asingestahiki kukemewa mno na Abubakr kuliko alivyomkemea kuhusu tendo lake la mwanzo, kwani wanahistoria wanaitaja barua ambayo Abubakr alimpelekea Khalid ibn Walid na ndani yake iliandikwa kama ifuatavyo:-

"Naapa ewe Khalid bila shaka wewe huna maana, unaoa wanawake hali ya kuwa kwenye uwanja wa nyumba yako kuna damu ya watu mia mbili miongoni mwa Waislamu haijakauka. *Taz: Tarikh Tabari Juz. 3 uk. 254, Tarikh Al-Khamis uk. 343.*

Khalid alipoisoma barua hii akasema, “Hii ni kazi ya Al-Asar akiwa na maana ya Umar ibn Khatab.

Hizi ni sababu muhimu zilizonifanya niwaepuke Masahaba kama hawa na wafuasi wao wanaobadilisha maagizo na kuunda simulizi za kubuni ili tu wayatakase matendo ya Abubakr, Umar, Uthman, Khalid ibn Walid, Muawiya, Amru ibn Al-Aas na ndugu zao.

Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba msamaha na ninatubia kwako, Ewe Mwenyezi Mungu mimi najitakasa kwako kutokana na matendo ya watu hawa na maneno yao ambayo yamekwenda kinyume na hukumu zako, yakavunja heshima ya vitu vyako vitakatifu na yakavuka mipaka yako. Unisamehe makosa yaliyotangulia ikiwa ni pamoja na kuwatawalisha wao kwani nilikuwa miongoni mwa watu wajinga, na kwa hakika Mjumbe wako amesema, “Haombewi udhuru mjinga kwa ujinga wake.” Ewe Mwenyezi Mungu hakika viongozi wetu na wakubwa wetu wametupoteza njia na wakatuzuwilia (kuuona) ukweli, wakatuonesha Masahaba waliogeuka kinyume, ya kwamba hao ndiyo viumbe bora baada ya Mjumbe wako. Hapana shaka kwamba baba zetu na babu zetu walikuwa ni wahanga wa uzushi na udanganyifu uliokusudiwa na Banu Umayyah na Banu Abbas waliokuja baada ya Banu Umayyah. Ewe Mwenyezi Mungu wasamehe wazee wetu wewe ndiwe ujuwaye mambo ya siri na yaliyofichikana vifuani, kwani heshima yao na kuwatukuza kwao masahaba haikuwa isipokuwa ni kwa nia njema kwamba (masahaba hao) ni watetezi na wapenzi wa Mjumbe wako Muhammad (s.a.w.) ... nawe ewe Bwana wangu, unalijua penzi lao na penzi letu (namna lilivyo) kwa kizazi kitukufu che Mtume (chenye) Maimamu ambao umewaondoshea uchafu na umewatakasa mno wakiongozwa na Bwana wa Waislamu na Amir jeshi wa Waumini ambaye ni kiongozi wa watu mashuhuri wateule, na ni kiongozi wa wachamungu Bwana wetu Ali ibn Abi Talib.

Unijaalie ewe Mwenyezi Mungu niwe miongoni mwa wafuasi wake wenye kushikamana na kamba ya kuwatawalisha, na wenye kufuata njia yao, na wenye kupanda ndani ya Safina yao. (Na unijaalie) miongoni mwa wenye kushikamana na kishiko chao imara, na unijaalie miongoni mwa wenye kuingia katika milango yao na wenye kudumu ndani ya mapenzi yao, wenye kuzitumia kauli zao na matendo yao na unijaalie miongoni mwa wenye kushukuru kwa fadhila zao na upaji wao.

Ewe Mwenyezi Mungu (nakuomba) unifufue ndani ya kundi lao, hakika Mjumbe wako (s.a.w.) amesema: "Mtu atafufuliwa pamoja na yule aliyekuwa akimpenda".

**ii). Hadithi ya Safinah.**

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.), amesema:-

"Bila shaka mfano wa Watu wa nyumba yangu kwenu ninyi ni mfano wa Safina ya Nuh kwa watu wake, yeyote mwenye kuipanda ataokoka na mwenye kuipa mgongo atazama" *Taz: Mustadrak Al-Hakim Juz. 3 uk. 151, Tal-Khis Adhahabi, Yanabiul-Mawaddah, As-sawaiqul-Muhriqah cha ibn Hajar uk. 184 na 234, Tarikh Al-Khulafaa cha Suyuti, na Aljamius-Saghir, Is-aafur-Raghibin.*

"Bila shaka mfano wa watu wa nyumba yangu kwenu ni mfano wa mlango wa msamaha kwa Banu Israil, yeyote mwenye kuingia mlango huo atasamehewa". *Taz: Majmauz-Zawaid cha Haithami Juz. 9 uk 168.*

Ibn Hajar ndani ya kitabu chake kiitwacho As-Sawaiqul-Muhriqas ameiandika hadithi hii kisha akasema, "Na kufananishwa kwao na Safina ya Nuhu ni kwamba, mwenye kuwapenda na kuwatukuza kwa kushukuru neema ya ubora wao na kuchukua uongofu wa wanachuoni wao ataokoka kutokana na kiza cha khitilafu mbali mbali, na mwenye kulipa mgongo jambo hili atazama ndani ya bahari ya kukufuru na ataangamia ndani ya jangwa la upotofu. Na kufananishwa kwao na mlango wa msamaha ni kwamba , hapana shaka Mwenyezi Mungu Mtukufu amejaalia kuingia ndani ya mlango huo ambao ni mlango wa Arihaa au kuingia Baitul-Muqaddas kwa unyenyekevu, na kuomba msamaha ndiyo sababu ya kusamehewa, na ameujaalia Umma huu mapenzi ya (kuwapenda) Watu wa nyumba ya Mtume kuwa ni sababu ya msamaha na kuokoka."

Aah, laiti mimi (ningepata nafasi ya) kumuuliza Ibn Hajar hivi yeye alikuwa miongoni mwa wale waliopanda Safina hii au walioingia ndani ya mlango huu na wakachukua uongofu wa wanachuoni (wao), au yeye ni miongoni mwa wale wasemao wasiyoyatenda na wanakwenda kinyume na kile wanachokiamini? Watu wengi wasiojua kitu pindi ninapowauliza

kuhusu (Ahlul Bait) na kutoa hoja dhidi yao, wao husema, “Sisi ni wa mwanzo mno kwa (kuwapenda) Ahlul Bait na Imam Ali kuliko mwingine asiyekuwa sisi kwani sisi, tunawaheshimu Ahlul-Bait na tunawatukuza na hakuna (miongoni mwetu) anayepinga ubora wao na heshima yao!

Naam wanasema kwa ndimi zao mambo yasiyokuwemo ndani ya nyoyo zao au wanawaheshimu na kuwatukuza lakini hapo hapo wanawafuata maadui zao na wanafanya Taqlid ya hao na wale waliowaua na kuwakhalifu.

Au wao mara nyingi wanakuwa hawafahamu Ahlul Bait ni kina nani. Ukiwauliza, ni nani Ahlul Bait? Kwa haraka sana watajibu: “Ni wakeze Mtume ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na amewatakasa mno.”

Kuna mmoja wao aliniondolea mushkeli huu pale nilipomuuliza na akanijibu huku akisema:- “Ahlus-Sunna wote wanawafuata Ahlul-Bait.” Nilistaajabu na kisha nikasema, “Munawafuata vipi.”? Akasema: “Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amesema: “Chukuweni nusu ya (maarifa ya) dini yenu kutoka kwa hiki kijanajike chekundu.” Yaani Aisha. Basi sisi tumechukua nusu ya dini yetu kutoka kwa Ahlul-Bait.

Na kwa msingi huu yanaeleweka maneno yao juu kuwaheshimu na kuwatukuza Ahlul-Bait. Ama pindi utakapowauliza kuhusu Maimamu kumi na wawili hakuna wamjuaye isipokuwa Ali, Hasan na Husein, pamoja na kwamba hawakiri Uimamu wa Hasan na Husein, na wakati huo huo wao wanamtukuza Muawiyah ibn Abi Sufiyan ambaye alimtilia sumu Hasan na akamuua. Na (huyu Muawiyah) wanamuita kuwa ni “Mwandishi wa Wahyi.” Pia amri ibn Al-as (wote hawa wanawatukuza) kama wanavyomtukuza Imam Ali.

Hakika hali kama hii ni yenye kupingana na kuchanganya mambo, kuchanganya haki na batili na ni kuufunika mwangaza kwa kiza, vinginevyo, itawezekanaje ndani ya moyo wa muumini lichanganyike pendo la kumpenda Mwenyezi Mungu na shetani kwa pamoja?

Mwenyezi Mungu amesema ndani ya kitabu chake kitukufu:- *“Hutawakuta watu wanaomuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho*

*wanawapenda wale wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake hata wakiwa ni baba zao au watoto wao au ndugu zao au jamaa zao, hao ndiyo ambao (Mwenyezi Mungu) ameandika nyoyoni mwao imani na akawatia nguvu kwa roho itokayo kwake na atawaingiza katika mabustani yapitayo mito ndani yake watakaa humo daima, Mwenyezi Mungu amewaridhia na wao wamekuwa radhi naye hao ndiyo kundi la Mwenyezi Mungu, fahamuni (ya kwamba) bila shaka kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kufaulu" (Qur. 58:22)*

Kadhalika amesema: Mwenyezi Mungu mtukufu:- *"Enyi mlioamini, msiwafanye adui zangu na adui zenu kuwa ni marafiki, munawapa upendo kwa ajili ya urafiki hali ya kuwa wao wamekwishaipinga haki iliyokujieni" (Qur. 60:1)*

**iii). Hadithi isemayo:**
**Atakayefurahishwa kuishi maisha niliyoishi mimi.**

Amesema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.):- "Yeyote atakayefurahishwa kuishi maisha (niliyoishi) mimi na kufa kama kifo changu na kuishi ndani ya pepo ya milele, basi na amtawalishe Ali baada yangu mimi, na (pia) amtawalishe aliyetawalishwa naye, na afuate nyayo za Ahlul-Bait wangu baada yangu kwani wao ni kizazi changu. Wameumbwa kwa udongo nilioumbiwa mimi, na wamepewa fahamu yangu na elimu yangu. Ole wao wenye kupinga ubora wao katika umati wangu, wenye kukata maungamano yao kwangu, basi Mwenyezi Mungu asiwape Shafaa yangu." *Taz: Mustadrak Al-Hakim Juz. 3 uk. 128, At-Tabrani fil-Jamil-Kabir, Al-Isabah cha Ibn Hajar Al-asqalani, Kanzul-Ummal Juz. 6 uk. 155, Al-Manaqib cha Khawar-zami uk. 34, Yanabiul-Mawaddah uk. 149 Hil-Yatul-Auliyaa Juz. 1 uk. 86, Tarikh Ibn Asakir Juz. 2 uk. 95.*

Hadithi hii kama tunavyoiona, ni miongoni mwa hadithi zilizowazi ambayo haikubali Taawili na wala haimuachii Muislamu namna yoyote ya hiyari bali inakata kila hoja dhidi yake. Na ikiwa Muislamu hakumtawalisha Ali na hakufuata nyayo za Ahlul-Bait ambao ni kizazi cha Mtume, basi atakuwa ameharamishiwa Shafaa uombezi wa Babu yao ambaye ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.).

Na inafaa kuashiria hapa ya kwamba, wakati wa uchunguzi niliokuwa nikiufanya, kwanza niliingiwa na mashaka juu ya kusihi kwa hadithi hii na nilishtushwa na maonyo na makemeo yaliyomo kwa yeyote mwenye kwenda kinyume cha Ali na Ahlul-Bait na khususan kwa kuwa hadithi hii haikubali Taawili. Mashaka yaliniondoka pindi niliposoma ndani ya kitabu kiitwacho *Al-Isabah* kilichoandikwa na Ibn Hajar Al-as-Qalani, baada ya kuiandikika hadithi hii amesema:-

"Mimi nasema kuwa ndani ya sanad ya hadithi hii yumo Yahya ibn Yaala al-Muharibi naye ni dhaifu." Basi kwa kauli hii Ibn Hajar akawa ameniondolea baadhi ya mishkeli iliyokuwa akilini mwangu kwani nilikuwa nadhani kwamba Yahya ibn Yaala al-Muharibi ni mzushi wa hadithi na wala siyo muaminifu, lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu alitaka kuniweka kwenye ukweli uliokamilika, kwani siku moja nilisoma kitabu kiitwacho, *"Munaqashatu Aqaadiyah fi Maqalati Ibrahima Al-Jab-han" uk. 26.* Kitabu hiki kikaniweka kwenye hali iliyo bayana, pindi kilipobainisha kwamba Yahya ibn Yaala Al-Muharibi ni miongoni mwa watu waaminifu ambao Masheikh wawili wa hadithi Bukhari na Muslim wamewategemea. Binafsi yangu nilifuatilia nikakuta Bukhari ameandika hadithi zake ndani ya mlango wa *Ghaz-watul-Hudaibiyyah* ndani ya juzuu ya tatu ukurasa wa 31.

Vile vile Muslim ndani ya sahihi yake ameandika hadithi ya Yahya katika mlango wa Hudud ndani ya Juzuu ya 5 ukurasa 119, na Dhahabi mwenyewe - pamoja na ugumu wake amemueleza kuwa ni mkweli, yaani ameeleza hadithi zake ni mur'sali zinazokubalika na Maimamu wa Jarhi na Taadil wamemuhesabu kuwa yu miongoni mwa watu waaminifu na Masheikh wawili wamemtolea hoja. Basi ni wa nini uzushi huu na kumpaka matope na kugeuza ukweli kisha kumtuhumu mtu muaminifu ambaye waandishi wa Sihah wametoa hoja kupitia kwake?

Alaa! ni kwa kuwa ameeleza ukweli halisi juu ya kufuata nyayo za Ahlul-Bait, hivyo basi malipo yake toka kwa Ibn Hajar yakawa ni kumdhalilisha na kumfanya kuwa ni dhaifu. Lakini Ibn Hajar hakujua kama baada yake wako wanachuoni mabingwa wanaompa changamoto juu ya kila jambo dogo na kubwa na wataiumbua chuki yake na ujinga wake kwani wao wanang'ara kwa nuru ya Utume na wanafuata uongofu wa Ahlubait.

Na baada ya hayo nimefahamu ya kwamba baadhi ya wanachuoni wetu wanajaribu kwa juhudi zao kuufunika ukweli ili mambo ya Masahaba na Makhalifa yasije yakaumbuka, Masahaba ambao walikuwa ndiyo maamiri wao na vigezo vyao. Kuna wakati utawakuta wanageuza maana ya *Maula* katika hadithi ya *Mankuntu Maulahu* badala ya kuwa *Aula* (yaani mstahiki) wanafanya kuwa mpenzi, mtetezi. Wanachuoni wa Kisunni wanasema kuwa hadithi hii ni sahihi, lakini ni wajibu kuiawili (kuipa tafsiri) imaanishe maana ya mpenzi na mtetezi na wanafanya hivi ili kuupasisha Ukhalifa wa Abubakr, Umar na Uthman, vinginevyo itakuwa ni wajibu Ali (a.s.) awe ni mwenye kustahiki Ukhalifa kuliko wote. Kwa hiyo utaona ndani yake kuna mambo, ikiwemo kupotoka Masahaba wengi waliompa baia Abubakr, na kusema hivi kwao ni kauli isiyofaa.

Hii ndiyo kauli ya wanachuoni wa Kisunni kama walivyonieleza wengi wa wanachuoni wetu wa Tunis. Nilipowaambia kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) kabla ya (kuisema) hadithi hii alipokuwa akiwahutubia aliwauliza “Je mimi siyo bora kwenu kuliko nafsi zenu?” Wakasema “Bila shaka (wewe ni bora kwetu kuliko nafsi zetu) hapo ndipo Mtume aliposema, “Basi yeyote ambaye mimi nilikuwa mtawalia mambo yake basi huyu hapa Ali ni mtawalia mambo yake.” Baadhi yao walinijibu wakisema, “Hiyo ni miongoni mwa ziyada zilizozidishwa na Mashia.” Na nilipowauliza, “Hivi kweli inaingia akilini, kwamba Mtume (s.a.w.) awakusanye mamia ya watu miongoni mwa Mahujaji katika joto kali linalounguza eti tu kwa ajili ya kuwaambia kwamba Ali (a.s.) ni mpenzi na msaidizi wa Waislamu? Hivi kweli inaingia akilini?” Walinyamaza hawakujibu kitu.

Kuna wakati mwingine wanazipinga na kuzikanusha zile hadithi ambazo zinapingana na madh-hebu yao hata kama zimeandikwa ndani ya vitabu vyao Sahihi na Musnad zao. Mfano wa hilo ni ile hadithi isemayo, “Makhalifa baada yangu ni kumi na wawili wote wanatokana na Maquraish”, na katika riwaya nyingine “Wote wanatokana na Bani Hashim”. Hadithi hii wameiandika wote Bukhari na Muslim na pia Sihahi zote za Kisunni. Lakini pamoja na hali hii wao wanakanusha kuwa kwamba wote hawa ndiyo wale Maimamu kumi na wawili wanaotokana na Ahlubait ambao Mashia Ithnaasharia ndiyo wanaosema kuwa ni Maimamu na watawalia mambo ni wao.

Masunni kwa upande wao huwahesabu wale Makhalifa wanne na humuongeza juu ya hawa Khalifa Umar ibn Abdul-Aziz na inakuwa idadi yao ni watano na hapo wanasimama kwa sababu wao hawamuhesabu Muawiyah wala mwanawe Yazid wala Mar-wan ibn Al-Hakam na wanawe kuwa nao ni miongoni mwa *Khulafaur-Rashiduna,* na kwa kutowahesabu hao kuwa miongoni mwa *Khulafaur-Rashiduna*, idadi ya Makhalifa kumi na wawili kwa Masunni inabakia ni utata usiokuwa na ufumbuzi labda wakubaliane na kauli ya Mashia!

Na kuna wakati mwingine huwa wanafuta nusu ya hadithi au theluthi mbili ili waibadili kwa kuweka *Kadha wa kadha!!* Mfano wa hilo ni ile hadithi isemayo, "Hakika huyu ni ndugu yangu na ni wasii wangu na ni Khalifa wangu baada yangu, msikilizeni na mumtii." Hii ni ile hadithi aliyoisema Mtume hali ya kuwa ameshika shingo ya Ali, na ni hadithi ambayo imeandikwa na Tabari ndani ya Tarikh yake na Ibn Al-Athir ndani ya Kamil yake, vile vile Kanzul Ummal, Musnad Imam Ahmad, na Siratul-Halabiyah na Ibn Asakir, lakini mchapishaji aliyechapisha kitabu cha tafsiri ya *Tabari Juz. 19 uk. 121* hakuiacha hadithi hii kamilifu kama alivyoitamka mwenyewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, bali ameondosha maana yake yote na akaibadili ikabakia "Hakika huyu ndugu yangu na *kadha wa kadha."* Akasahau kwamba Tabari ameiandika hadithi hii kwa ukamilifu ndani ya kitabu chake cha historia *Juz. 2 uk. 319-321* hakika huo ndiyo uaminifu wa elimu.

Huenda mwanachuoni huyu hakuwa na ujanja wa kuikanusha hadithi hii, na aliona kuwa ndani yake kuna maagizo ya Mtume yaliyowazi kuhusu Ukhalifa wa Imam Ali baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.), kwa hiyo akakusudia kuyafunika maagizo haya na kuyabadilisha kwa kuandika *kadha wa kadha.* Masikini (mtu) huyu alidhani kwamba anaweza kufunika nuru ya jua wakati yeye atakapofumba macho yake, au anaweza kuwatosheleza wasomaji na wanataaluma kwa kusema kwake *kadha wa kadha.* Sivyo kabisa, hayo ni maneno ayasemayo yeye.

Wakati mwingine Masunni huwa wanawatilia mashaka wapokezi wa kuaminika kwa sababu tu wamesimulia mambo ambayo nafsi zao haziyapendi. Mfano wa hilo ni pale wanapomtuhumu Yahya ibn Yaala Al-Muharib, ambaye ni miongoni mwa wapokezi (wa hadithi) wanaoaminika

ambao Bukhari na Muslim wametoa hoja kupitia hadithi zake. Lakini Ibn Hajar Al-Asqalani amemtuhumu na kumwita kuwa ni dhaifu, si kwa sababu yoyote ila tu ni kwa kuwa amesimulia hadithi ya *Wilayah* ambayo ndani yake Mtume (s.a.w.) aliwaamuru Masahaba wake wamtawalishe Ali na Ahlul Bait.

Na kwa mujibu wa Hadithi (ilivyo) siyo ajabu kwa Ibn Hajar na walio kama yeye ambao wanajaribu kwa bidii zao kuufuta ukweli ambao Muawiyah ibn Abi Sufiyan alitoa kila anachokimiliki katika dhahabu na fedha kwa lengo la kuufuta ukweli lakini hakufaulu, basi ni vipi itawezekana kwa Ibn Hajar kuufuta ukweli kwa njia ya kuwatuhumu wasimulizi wanaoaminika? Bila shaka Muawiya alikuwa na mali nyingi, hila, nguvu, madaraka na kitisho, lakini pamoja na yote hayo alishindwa vibaya na alifedheheka kisha zama zikamfunika akawa hajulikani, wakati ambapo nuru ya Imam Ali inasambaa siku zote. Basi ni vipi inawezekana kwa Ibn Hajar na walio kama yeye kutia mashaka kuhusu ukweli wa Ahlu-Bait kwa kiasi cha kufanya tuhuma dhidi ya wapokezi (wa hadithi) ambao ni waaminifu tena wanaotegemewa?

Katu haitawezekana kabisa nuru ya Mwenyezi Mungu kuzimwa kwa vinywa.

Wakati mwingine watu hawa huiandika hadithi ndani ya chapa ya mwanzo kwa ukamilifu na katika chapa zingine huiondoa bila ya kuashiria sababu za kuiondoa, licha ya kwamba wasomi hufahamu sababu za kufanya hivyo. Mfano wa hilo ni kitendo alichokitenda Muhammad Husein Haikal ndani ya kitabu chake kiitwacho *Hayatu Muhammad*, kwani ndani ya chapa ya kwanza uk. 104 amesema: “Iliposhuka kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo *“Waandhir Ashiratakal-Aqrabina”* yaani -*Waonye jamaa zako wa karibu*-kisha akakieleza kile kisa kama walivyokieleza wanahistoria, na mwishoni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) alisema: “Hakika huyu ni ndugu yangu na ni wasii wangu na ni Khalifa wangu kwenu ...” Lakini yeye (Muhammad Haikal) katika chapa ya pili akaiondosha riwaya hii, pia ndani ya chapa zilizofuatia bila ya maelezo wala ufafanuzi mambo ambayo yanaashiria kwa ukaribu au umbali uliosababisha kuondosha sehemu ya hadithi hii ya Mtume (s.a.w.). Japokuwa Sheikh Muhammad Jawad Mughniyyah - ukweli halisi anao mwenyewe - amenakili tukio hili

ndani ya kitabu chake kiitwacho *As-Shiatu fil-Mizan* amesema kwamba, "Muhammad Husein Haikal aliondosha sehemu hii (ya hadithi) kwa kupokea maelfu ya pauni." Na kwa kuwa Haikal hakuikanusha habari hii na wala hakutoa sababu za kuondosha sehemu hiyo iliyotajwa, basi bila shaka unabainika ukweli wa Sheikh Muhammad Jawad Mughuniyyah na pia ufuatiliaji wake juu ya mambo yanayotendeka!

Kwa msingi huu sisi tunasema kuwaambia watu hawa na wengine kama hawa ambao wanaziuza aya za Mwenyezi Mungu kwa thamani ndogo ya dunia, "Muogopeni Mwenyezi Mungu na mseme kauli zilizo sawa sawa na kumbukeni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema:-

*Hakika wale wanaoficha yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu miongoni mwa ubainifu na uongofu, baada ya kuwa tumewabainishia watu ndani ya Kitabu, watu hao Mwenyezi Mungu anawalaani na kinawalaani kila (kiumbe) chenye kulaani" (Qur. 2:159)*

Na pia kauli nyingine ya Mwenyezi Mungu isemayo:-

*"Hakika wale wanaoyaficha yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu katika kitabu na wanayauza kwa thamani ndogo ya dunia watu hao hawali matumboni mwao isipokuwa moto, na wala Mwenyezi Mungu hatawasemesha siku ya Qiyama na wala hatawatakasa, na watapata adhabu kali." (Qur. 2:174)*

Basi je si inawapasa watu hawa watubie kwa Mwenyezi Mungu na waukubali ukweli ili Mwenyezi Mungu akubali toba yao kabla wakati haujawapita?

Kwa hakika yote haya kwangu mimi yalithibitika baada ya utafiti na uchunguzi, nikiwa na dalili zisizo na shaka kwa haya niyasemayo. Wao wamejaribu bila mafanikio kuyatakasa matendo ya Masahaba ambao walirudi kinyume nyume kwa visigino vyao, basi kauli zao zimekuja zikipingana zenyewe kwa zenyewe na zinapingana na historia.

Laiti wao wangeliifuata haki japo kuwa ni chungu, hakika wangestarehe na hiyo ingekuwa ni sababu ya kuwa na umoja katika Umma huu, umoja

ambao umeparaganyika na kusababisha ugomvi si kwa lolote isipokuwa kwa kutaka kuunga mkono kauli zao au kuzikanusha.

Sasa basi, ikiwa baadhi ya Masahaba wa mwanzo siyo waaminifu katika kunakili hadithi tukufu za Mtume, wakawa huzibatilisha zile zisizokubaliana na matakwa yao khususan hadithi hizo zikiwa ni miongoni mwa usia aliousia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) wakati wa kufariki kwake, kwani Bukhari na Muslim wameandika ya kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ameusia mambo matatu wakati wa kifo chake.

"Waondoweni washirikina katika bara Arabu, wapeni wajumbe kama nilivyokuwa nawapa, kisha msimulizi wa hadithi hii anasema: Jambo la tatu nimelisahau.

*Taz: Sahih Bukhari Juz. 1 uk. 121 Babu Jawazil-wafai Minkitabil-Jihad, Sahih Muslim Juz. 5 uk. 75 Kitabul-Wasiyyah.*

Basi je katika hali kama hii inaingia akilini ya kwamba Masahaba waliokuwepo ambao waliusikia usia wa Mtume juu ya mambo matatu wakati wa kufa kwake, wanaweza kusahau usia wa jambo la tatu, hali ya kuwa ndiyo wao hao hao waliokuwa wakihifadhi kasida za mashairi marefu baada tu ya kuyasikia mara moja? Haiwezekani, lakini kilichopo ni kwamba siasa ndiyo iliyowalazimisha wasahau wasikumbuke. Hakika huu ni unyonge mwingine miongoni mwa unyonge waliokuwa nao masahaba hawa.

Na kwa kuwa wasia muhimu wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, bila shaka ulikuwa ni kumpa Ukhalifa Ali ibn Abi Talib ndiyo maana msimulizi wa hadithi hakuutaja.

Pamoja na yote hayo mchunguzi yeyote juu ya mas-ala haya ataikuta harufu ya wasia juu ya Ali inanukia licha ya kufichwa na kutotajwa, kwani Bukhari ameandika ndani ya sahihi yake, Kitabul-Wasaya, kama ambavyo Muslim pia ameandika ndani ya sahihi yake kwamba, "Palizungumzwa mbele ya mama Aisha ya kwamba Mtume aliusia juu ya Ali."

*Taz: Sahih Bukhari Juz. 3 uk. 68 Babu maradhi Nnabi wa Wafatih, Sahih Muslim Kitabul-Wasiyyah.*

Angalia ni jinsi gani Mwenyezi Mungu anavyoidhihirisha Nuru yake japokuwa madhalimu wataifunika.

Narudia kusema, "Ikiwa Masahaba hawa siyo waaminifu katika kunukuu wasia wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, basi baada ya hapo hakuna lawama kwa wale waliowafuatia (Masahaba) wala wale waliowafuatia hawa."

Na ikiwa mama Aisha ambaye ni mama wa waumini hawezi hata kulitaja jina la Ali, na wala nafsi yake haifurahii kheri yoyote kwa Ali kama alivyoyaeleza haya Ibn Saad ndani ya Tabaqat yake, naye Bukhari ndani ya Sahihi yake, Babu Maradhi Nnabi wa Wafatih, na iwapo mama Aisha anasujudu kumshukuru Mwenyezi Mungu pindi aliposikia kuwa Ali amefariki basi ni vipi itatarajiwa kutoka kwake utajo wa usia juu ya Ali hali ya kuwa mama Aisha anatambulika kwa wote juu ya uadui wake na kero yake dhidi ya Ali na wanawe na Watu wa nyumba ya Mtume?

*Lahaula wala Quwata Illa Billahi l-Aliyil-Adhim.*

# MSIBA ULIOTUFIKA UMETOKANA NA KUFANYA IJTIHADI DHIDI YA NNASI

Ndani ya uchunguzi (niliofanya) nimegundua ya kwamba msiba ulioufika Umma wa Kiislamu umetokana na jitihada ambayo waliifanya Masahaba dhidi ya Nnasi (maagizo ya Qur'an au Mtume) yaliyo bayana, na kwa sababu hiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu ikabomoka na Sunna za Mtume zikapotea, na hatimaye wanachuoni na Maimamu wakawa wanakisia kwa kutumia ijtihadi zilizofanywa na Masahaba na wakati mwingine wakafikia hatua ya kuyapinga maagizo ya Mtume pindi yanapopingana na tendo la mmoja wa Masahaba. Na sintakuwa ninatia chumvi kwa kusema kwamba hata andiko la Qur'an walilipinga kwani hapo kabla nimetangulia kueleza namna gani walivyofanya licha ya kuwepo maelekezo juu ya kutayamam ndani ya kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume iliyothibiti, lakini licha ya yote hayo kuwepo wao walifanya jitihada zao wakasema kuwa, "Sala itaachwa kusaliwa ikiwa patakuwa hapana maji kwa ajili ya udhu." Abdallah ibn Umar alitoa sababu zake za kufanya ijtihadi yake kama tulivyoonesha pahala pengine ndani ya uchunguzi wetu.

Na miongoni mwa Masahaba waliofungua hii milango (ya ijtihadi) ni Khalifa wa pili ambaye alitumia maoni yake dhidi ya andiko la Qur'an baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.), akazuwia fungu la wale wenye kutiwa nguvu katika imani zao, fungu ambalo Mwenyezi Mungu amelifaradhisha kwao kutoka ndani ya zaka, na yeye akasema kuwaambia, "Sisi hatuna haja nanyi."

Ama ijtihadi zake kuhusu maagizo ya Mtume ni nyingi mno hazina idadi, kwani yeye alifanya ijtihadi yake hata katika zama za uhai wa Mtume mwenyewe na alimpinga mara nyingi.

Hapo kabla tumeashiria upinzani wake alioufanya katika siku ya sulhu

ya *Hudaibiyyah*, na pale alipozuwia yasiandikwe maagizo ya Mtume na akasema, "Kinatutosha kitabu cha Mwenyezi Mungu." Kadhalika lipo tukio jingine lililotokea baina yake na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.), bila shaka litatupa picha iliyowazi jinsi alivyo Umar ambaye alijihalalishia kumjadili na kumpinga Mtume. Tukio hilo ni lile la Mtume kubashiria pepo, pale Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipomtuma Abuhurairah akamwambia, "Utakayekutana naye hali ya kuwa anashuhudia kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, moyo wake ni wenye kuyakinisha jambo hilo, basi mbashirie pepo." Abuhurairah akatoka ili akambashirie huyo atayekutana naye, Umar akamfuata na kumzuia kufanya hivyo na akampiga mpaka akaanguka chini. Abuhurairah akarudi mpaka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hali ya kuwa analia na akamweleza Mtume tendo alolitenda Umar. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akamwambia Umar, "Ni kitu gani kilichokufanya utende hivyo."? Umar akasema, "Je wewe ndiye uliyemtuma ambashirie pepo yule atakayesema *Lailaha Illallah* hali yakuwa moyo wake ni wenye kuyakinisha hivyo." Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema "Ndiyo." Umar akasema, "Usifanye hivyo, kwani mimi hakika nachelea watu watategemea *Lailaha Illallah!*

Na huyu mwanawe Abdallah ibn Umar anachelea watu watategemea kutayammamu, basi yeye akawaamuru waache sala, laiti wangeliyaacha maagizo hayo kama yalivyo na wasiyabadilishe kulingana na ijtihadi zao zisizo na faida ambazo zinapelekea kufuta sheria na kuvunja heshima ya mambo matukufu ya Mwenyezi Mungu na kuugawa umma katika madhhebu mbali mbali mengi na maoni yenye kutofautiana na farka zenye uhasama.

Na miongoni mwa mitazamo mbali mbali ya Umar kumuhusu Mtume na Sunna yake, tunafahamu ya kwamba yeye alikuwa haamini hata siku moja kwamba Mtume anayo Ismah , bali alikuwa akimuona kwamba ni mtu tu anayekosea na kupatia.

Na kutokana na msingi huu, ndiyo ile fikra ya wanachuoni wa Kisunni ilipokuja nayo ni kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ana Ismah katika kubalighisha Qur'an tu, na yasiyokuwa Qur'an anakosea na wanatolea ushahidi juu ya jambo hilo kwamba Umar aliyasahihisha maoni ya Mtume mara nyingi katika matukio kadhaa!

Basi iwapo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) - kama waonavyo baadhi ya watu wasiojua kitu - anayakubali mazumari ya shetani ndani ya nyumba yake hali ya kuwa kalala chali na wanawake wanapiga madufu, shetani naye anacheza na kufurahia pembeni yake mpaka alipoingia Umar ibn Khatab shetani yule akakimbia na wanawake wale nao wakayaficha madufu chini ya makalio yao, kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akamwambia Umar, "Hatakuona shetani ukipita njia fulani isipokuwa atapita njia nyingine isiyokuwa yako."

Kutokana na hali hiyo siyo ajabu kwa Umar ibn Khatab kuwa na nafasi ndani ya dini au kuipa nafasi nafsi yake ya kumpinga Mtume katika mambo ya kisiasa na hata katika mambo ya dini kama ilivyotangulia hapo kabla juu ya lile tukio la kuwabashiria pepo waumini.

Na kutokana na fikra ya ijtihadi na kutumia rai dhidi ya Nnasi, kilianza au kilitengenezeka kikundi cha Masahaba wakiongozwa na Umar ibn Khatab. Na bila shaka tumekwishawaona ni jinsi gani siku ile ya msiba ule wa siku ya Alkhamisi walivyokinga mkono na kuitia nguvu rai ya Umar dhidi ya maagizo bayana ya Mtume.

Na kwa ajili hiyo pia tunaona kwamba watu hawa hata siku moja hawakuikubali Nnasi (maagizo) ya Ghadir ambayo Mtume (s.a.w.) alimsimika Ali kuwa ndiyo Khalifa wake kwa Waislamu, na wao wakaitumia nafasi ya kufanya ijtihadi zao kuyapinga maagizo ya Mtume wakati wa kifo chake, kwani mkutano wa Saqifah ukawa ni wa kumchagua Abubakr yakiwa ni matokeo ya ijtihadi hii.

Na baada ya mambo kuwakalia vizuri na watu kuyasahau maagizo ya Mtume kuhusu Ukhalifa, hapo ndipo walipoanza kufanya ijtihadi katika kila jambo mpaka wakathubutu kukilemaza Kitabu cha Mwenyezi Mungu, wakaipuuza mipaka ya Mwenyezi Mungu, wakazibadilisha hukmu za Mwenyezi Mungu. Hivyo basi madhila yaliyomfika Fatmah Zahra yalikuja baada ya madhila yaliyomfika mumewe kwa kunyang'anywa Ukhalifa, kisha ukafuatia msiba wa kuuawa watu waliokataa kutoa zaka, na yote hayo ni matokeo ya kufanya ijtihadi dhidi ya maandiko au maagizo ya Mwenyezi Mungu na Mtume. Hatimaye Ukhalifa wa Umar ibn Khatab ulikuja ukiwa ni matokeo halisi ya ijtihadi hiyo, kwani

Abubakr alijitahidi kwa maoni yake akayapuuza mashauriano ambayo hapo kabla alikuwa akiyatolea ushahidi wa kusihi kwa Ukhalifa wake, na Umar naye akaongeza maji ndani ya unga pale alipotawalia mambo ya Waislamu, akahalalisha mambo aliyoyaharamisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na akaharamisha mambo aliyohalalisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Alipokuja Uthman baada ya Umar yeye alikwenda mbali zaidi katika kufanya ijtihadi, akazidisha kuliko waliomtangulia mpaka ijtihadi yake ikayaathiri maisha ya kisiasa na dini kwa jumla, yakafanyika mapinduzi matokeo yake akatoa uhai wake kwa thamani ya ijtihadi yake.

Na pindi Imam Ali (a.s.) alipotawalia mambo ya Waislamu alikuta kuna kazi ngumu ya kuwarejesha watu kwenye Sunna tukufu ya Mtume na kwenye uzio wa Qur'an. Alijaribu kwa juhudi zake kuondosha bid'a ambazo ziliingizwa ndani ya dini, lakini baadhi ya watu walipiga kelele wakasema, "Iko wapi Sunna ya Umar?"

Mimi nakurubia kuamini na kuamua kwamba, wale waliompiga vita Imam Ali na wakamkhalifu, hapana shaka walifanya hivyo kwa kuwa yeye Imam Ali (a.s.) aliwalazimisha kufuata njia ya sawa na aliwarejesha kwenye maagizo sahihi. Kwa ajili hiyo akaziua bid'a zote na ijtihadi zote ambazo zilikuwa zimeambatanishwa na dini kwa muda wote wa robo karne, na watu walikwisha zizowea hasa wale wenye tamaa ya dunia ambao mali ya Mwenyezi Mungu waliifanya kuwa ni ya kupeana wao kwa wao, na waja wa Mwenyezi Mungu wakawafanya kuwa ni watumwa. Walijilimbikizia dhahabu na fedha, na wakawanyima wanyonge haki zao za msingi hata zile ndogo mno ambazo Uislamu umeziweka.

Bila shaka katika kila zama tunawakuta Wastakbari wanaopendelea kufanya ijtihadi na kuzitilia mkazo kwa sababu huwapa nafasi ya kuyafikia malengo yao kwa kila njia. Amma maandiko ya Mwenyezi Mungu na Mtume huwa yanazuwia njama zao na kuweka kizuizi baina yao na kile wanachokikusudia.

Kisha ijtihadi imepata watu wa kuitetea katika kila zama na kila mahali, hata hao wanyonge wenyewe, kutokana na kuwepo wepesi wa utekelezaji

wa mambo na kukosa kuwa na *Iltizam*. Na kwa kuwa maagizo ya Mwenyezi Mungu na Mtume yanayo *Iltizam* na yanaondoa uhuru wa kujiamulia na hii kwa watu wa siasa huwa wanaiita kuwa ni hukmu au utawala wa siasa kali -*kwa lugha kileo*- ya kidini wakimaanisha - hukmu za Mwenyezi Mungu. Ama ijtihadi kwa kuwa ndani yake kuna uhuru unaovuka mipaka na hakuna *Iltizam* ya mipaka ya sheria basi wao huita kuwa ni hukmu au utawala wa kidemokrasia yaani maamuzi ya wananchi.

Kwa hiyo basi, wale waliokusanyika ndani ya Saqifah baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.) walipuuza serikali yenye hukmu za Mwenyezi Mungu alizoziasisi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu juu ya msingi wa maandiko ya Qur'an, na wakabadilisha kwa kuweka serikali ya kidemokrasia ambayo wananchi ndiyo watakaomchagua wamuonaye kuwa anafaa kuwaongoza. Masahaba hao hawakuwa wakifahamu neno Demokrasia kwa kuwa neno hilo siyo la kiarabu, lakini walichokuwa wakikifahamu wao ni nidhamu ya Shuraa.

Kwa hiyo wale ambao hawaikubali Nassi ya Ukhalifa (leo hii) wao ni watetezi wa demokrasia, na wanajifakharisha kwa jambo hilo wakidai kwamba Uislamu ndiyo wa mwanzo kuiona nidhamu hii, na wao pia ndio watetezi wa ijtihadi na kufanya mabadiliko ndani ya dini hali ya kuwa leo hii ndiyo wao walio karibu mno na tawala za kimagharibi. Kwa ajili hiyo leo hii tunazisikia serikali za kimagharibi zinawasifia watu hawa na kuwaita kuwa ni Waislamu walioendelea tena wenye msimamo wastani.

Amma Mashia wao ni watetezi wa Theocracy au hukumu ya Mwenyezi Mungu, na ambao wanaipinga ijtihadi dhidi ya Nnassi na wanatofautisha baina ya hukmu ya Mwenyezi Mungu na Shuraa, kwani Shuraa kwao wao haina uhusiano na Nnassi, bali shuraa na ijtihadi hupatikana katika mambo ambayo hakuna Nnassi ndani yake. Je, huoni kwamba Mwenyezi Mungu ndiye aliyemchagua Mtume wake Muhammad, lakini pamoja na hayo amemwambia: Washauri katika mambo. (Qur. 3:159)

Ama yale mambo yanayohusiana na kuchagua viongozi ambao watawaongoza viumbe Mwenyezi Mungu amesema: *"Na Mola wako ndiye anayeumba akitakacho na ndiye anayemchagua amtakaye wao hawana hiyari." (Qur. 28:68)*

Kwa hiyo pale Mashia wanapozungumzia kuwa Ukhalifa ni wa Imam Ali baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hapana kingine isipokuwa huwa wanashikamana na maagizo ya Mwenyezi Mungu na Mtume. Hali kadhalika wanapowashutumu baadhi ya Masahaba, si jinginelo bali huwatuhumu wale waliobadilisha maagizo na kuweka ijtihadi, na kwa ajili hiyo wameipoteza hukmu ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wakawa wamefungua mwanya katika Uislamu ambao haujafungika hadi leo.

Na kwa ajili hii vile vile tunazikuta serikali za kimagharibi na wanafikra wao wanawakejeli Mashia na kuwaita kuwa ni wenye chuki za kidini, na pia wanawaita kuwa wasio na maendeleo kwa sababu tu ya wao kuirejea Qur'an ambayo inakata mkono wa mwizi na kumpiga mawe mzinifu, na inaamrisha kufanya jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu. Yote hayo kwao wao ni hukumu za kiimla na kishenzi. Na kwa kupitia uchunguzi huu nimefahamu kwamba, ni kwa nini baadhi ya wanachuoni wa Kisunni waliufunga mlango wa ijtihadi tangu karne ya tatu hijiriya. Basi huenda ilitokea hivyo kutokana na hii ijtihadi kuuvutia umma huu maangamizi na masaibu, mambo ya kuchukiza na vita vya kumwaga damu ambavyo viliunguza vibichi na vikavu, na pia ijtihadi hiyo iliubadilisha umma bora uliotolewa kwa watu na kuwa umma wenye kugombana wao kwa wao na kuuana. Umma unoongozwa na mambo ya vurugu na kutawaliwa na ukabila unaogeuka kutoka kwenye Uislamu na kurudi kwenye *Jahiliyyah.* Kuhusu Mashia ambao walibakia na mlango wa ijtihadi ulio wazi muda wote ambapo maandiko na maagizo ya Mwenyezi Mungu na Mtume yakiwa yapo na thabiti, na haiwezekani kwa yeyote yule kuyabadilisha na juu ya msingi huo pia wamesaidiwa kwa kuwepo Maimamu kumi na wawili ambao wamerithi elimu ya babu yao Mtume s.a.w. na wamekuwa wakisema kwamba, "Hapana lolote isipokuwa linayo hukmu ya Mwenyezi Mungu na hapana shaka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) amelibainisha."

Pia tunafahamu ya kwamba Masunni walipokuwa wamefuata uongozi wa Masahaba wenye kufanya ijtihadi ambao walizuwia kuandikwa Sunna ya Mtume, walijikuta wenyewe wakilazimika kufanya ijtihadi pale inapokosekana Nnassi kwa kutumia maoni na kiasi na kufunga mlango wa mianya na sababu nyingine zisizokuwa hizo.

Kadhalika tunafahamu kutokana na yote hayo kwamba Mashia walishikamana na Imam Ali ambaye ndiye mlango wa mji wa elimu, na ni yeye ambaye alikuwa akiwaambia “Niulizeni jambo lolote lile, kwa hakika Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amenifundisha milango elfu moja ya elimu, ambayo kila mlango unafunguliwa milango (mingine) elfu moja.”

*Taz: (1) Tarikh Dimishq ya Ibn Asakir Juz. 2 uk. 484 Tarjuma ya Imam Ali Ibn Abi Talib. (2) Maqtalul-Husein cha Al-Khawarzami juz. 1 uk. 38, (3) Al-Ghadir cha Al-Amini Juz. 3 uk. 120.*

Wakati huo huo wasiokuwa Mashia walishikamana na Muawiyah ibn Abi Sufiyan ambaye alikuwa haijuwi Sunna ya Mtume isipokuwa kidogo, na alikuwa ndiye Imamu wa kundi potofu, lakini wakamfanya kuwa amiri jeshi wa waumini baada ya kifo cha Imam Ali, na ndipo alipofanya mambo ndani ya dini ya Mwenyezi Mungu kwa namna aonavyo zaidi kuliko waliomtangulia.

Masunni wao wanasema kuwa alikuwa ni mwandishi wa wahyi na kwamba yeye alikuwa miongoni mwa wanachuoni na Mujtahidina, lakini ni vipi wanahukumu juu ya ijtihadi yake hali ya kuwa ndiye mtu aliyemtilia sumu na kumuua Imam Hasan ibn Ali Bwana wa vijana wa peponi? Lakini huenda wao watasema kuwa tendo hili pia ni miongoni mwa ijtihadi yake kwani alijitahidi akakosea!

Ni vipi wanamhukumu kuwa ni mwenye kufanya ijtihadi hali ya kuwa alichukua Baia yake mwenyewe binafsi kwa nguvu toka kwa umma kisha akafanya hivyo hivyo kwa mwanawe Yazid, na akaigeuza nidhamu ya shuraa na kuwa ni Ufalme wa Kaizari?

Ni vipi basi wanamzingatia kuwa mwenye kufanya ijtihadi na kumpa malipo hali ya kuwa hapana shaka kwamba ni yeye ndiye aliyewalazimisha watu wamlaani Imam Ali pamoja na Watu wa kizazi cha nyumba ya Mtume juu ya mimbari kwa muda wote wa miaka sitini na tendo hili likawa ni Sunna inayofuatwa katika kipindi hicho chote?

Bali inakuwaje wanamuita kuwa ni mwandishi wa wahyi ... hali ya kuwa katika muda wa miaka ishirini na tatu ya kushuka kwa Wahyi juu

ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) yeye Muawiya alikuwa ni mwenye kumshirikisha Mwenyezi Mungu katika kipindi cha miaka kumi na moja miongoni mwa miaka hiyo ishirini na tatu? Na aliposilimu baada ya ushindi Makka hatujaipata hadithi isemayo kuwa aliishi Madinah, hali yajulikana pia kuwa Mtume Mtukufu hakurudi kuishi Makah baada ya ushindi, huo basi ilikuwaje Muawiya apate fursa ya kuwa mwandishi wa wahyi? *Lahaula wala quwata illa Billah L-Aliyyil-Adhim!*

Siku zote suali linarudi kuwa, "Ni lipi kati ya makundi mawili ndilo lililo kwenye haki, na ni lipi kati ya makundi hayo liko kwenye batili? Basi imma watakuwa Mashia ndiyo madhalimu na hawako kwenye haki na imma Muawiya na wafuasi wake ndiyo madhalimu na hawako kwenye haki.

Hapana shaka kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amebainisha kila kitu isipokuwa baadhi ya wanaodai kuwa ni wafuasi wa Sunna ya Mtume wanaitafutia dosari. Hapana shaka kwamba imenibainikia wakati nikifanya utafiti na kupitia kumtetea Muawiyah kuwa, kwa hakika wale wanaomtetea ni wale wafuasi wake na wafuasi wa Banu Umayyah na siyo kama wanavyodai kwamba wao ni wafuasi wa Sunna ya Mtume, na khususan iwapo utafuatilia misimamo yao, kwani wao wanawachukia wafuasi wa Ali na huwa wanasherehekea siku ya Ashura kuwa ni sikukuu kadhalika wanawatetea Masahaba waliomuudhi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika uhai wake na baada ya kufa kwake na pia makosa ya Masahaba hao wao hujaribu kuyatakasa na kuyafanya kuwa ni matendo sahihi.

Ewe Bwana, waona ni jinsi gani mnadai kwamba mnampenda Ali na Watu wa nyumba ya Mtume na wakati huo huo mnawaombea radhi kwa Mwenyezi Mungu maadui zao na waliowaua? Vipi mnampenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kisha mnawatetea waliobadilisha hukmu za Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakafanya jitihada zao na kuawili kwa kufuata maoni yao ndani ya hukmu za Mwenyezi Mungu?

Ni vipi basi mwampa heshima mtu ambaye hukumpa heshima Mjumbe wa Mwenyezi Mungu bali alimsingizia Mtume kuwa anaweweseka na aliutuhumu uongozi wake?

Ni jinsi gani mnawafuata wasimamizi waliosimikwa na dola ya Banu Umayyah au dola ya Banu Abbas kwa ajili ya mambo ya kisiasa, na

mnawaacha Maimamu waliotamkwa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa idadi yao na majina yao.

Ni vipi basi mnamfuata mtu ambaye hakumfahamu ipasavyo Mtume na mnamuacha ambaye ndiye mlango wa mji wa elimu na ndiye ambaye kwa Mtume (s.a.w.) daraja yake ni kama ile ya Harun kwa Musa?

***Ni nani aliyeanzisha Istilahi ya Ahlus-Sunnah Wal-Jamaa?!**

Hapana shaka, nimefanya uchunguzi ndani ya historia, lakini sijakuta isipokuwa ni kwamba, wao waliafikiana kuuita ule mwaka ambao Muawiyah alitwaa madaraka kuwa, Ni mwaka wa umoja na hiyo ilikuja kutokana na umma kugawanyika makundi mawili baada ya mauaji ya Uthman, kundi moja la Mashia wa Ali na jingine wafuasi wa Muawiyah. Na pindi Imam Ali (a.s.) alipouawa, Muawiyah akatawala baada ya sulhu aliyoipitisha yeye pamoja na Imam Hasan ndipo Muawiyah akawa Amirul-Muuminin, na hapo ndipo mwaka huo ulipoitwa, "Mwaka wa Umoja" *(Aamul-Jamaah)*. Kwa hiyo basi kuitwa *"Ahlus-Sunnah Wal-Jamaah"* kunajulisha juu ya kuwa mfuasi wa sunna ya Muawiyah na kushikamana juu ya misingi yake, na wala haimaanishi kuwa ni kufuata Sunna ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kwani Maimamu wanaotokana na kizazi chake (Mtume) ndiyo wanaoifahamu na ni wajuzi mno wa Sunnah ya Babu yao kuliko Maimamu wanaotokana na waachwa huru.

Na ilivyo ndivyo ni kwamba, wenye nyumba ndiyo wajuao kilichomo nyumbani mwao, na watu wa Makkah ndio wajuao vichochoro vya Makkah, lakini sisi tumewakhalifu Maimamu kumi na wawili ambao Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) aliagiza tuwafuate na badala yao tumewafuata maadui zao.

Licha ya sisi kukiri kuwepo na kusihi kwa hadithi ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amewataja ndani ya hadithi hiyo Makhalifa kumi na wawili na wote ni Maquraishi, lakini siku zote sisi tunakomea kwa Makhalifa wanne. Labda Muawiyah aliyetupatia jina la *"Ahlus-Sunna Wal-Jamaa"* alikuwa akikusudia tujumuike kwenye sunna aliyoianzisha ya kumtukana Ali na Watu wa nyumba ya Mtume, sunna ambayo iliendelea kwa miaka sitini na hakuna aliyeweza kuiondosha isipokuwa Umar

ibn Abdil-Aziz Mwenyezi Mungu ampe radhi yake. Na hapana shaka kwamba baadhi ya wanahistoria wanatusimulia kwamba Banu Umayyah walikula njama ya kumuuwa Umar ibn Abail-Aziz hali ya kuwa yeye ni miongoni mwa Banu Umayyah kwa ajili tu ya kuiua hiyo sunna ambayo ni ya kumlaani Ali ibn Abi Talib.

Enyi watu wangu na jamaa zangu, kwa kufuata misingi ya muongozo wa Mwenyezi Mungu, hebu tuelekee kwenye uchunguzi wa kuitafuta haki, tuiweke chuki pembeni, kwani sisi ni kafara ya Banu Umayyah na Banu Abbas, na ni kafara ya historia yenye kiza na pia sisi ni wahanga wa fikra iliyoganda, fikra ambayo wametupandikizia hao waliotangulia. Hapana shaka sisi ni wahanga wa hila na vitimbi vya Muawiyah ambavyo alisifika kuwa navyo, pia Amr ibn Al-Aas na Mughirah ibn Shu'bah na watu kama hawa.

Kwa hiyo basi chunguzeni undani wa historia yetu ya Kiislamu ili muweze kuupata ukweli halisi. Naye Mwenyezi Mungu atakupeni malipo yenu mara mbili, kwani huenda Mwenyezi Mungu akaunga umoja wa umma huu kupitia kwenu ambao ulipotoka baada ya kifo cha Mtume wake na ukatawanyika na kuwa makundi sabini na tatu, basi njooni muunganishe chini ya bendera ya *Lailaha Illallah Muhammadun Rasulullah* na kuwafuata Watu wa nyumba ya Mtume ambao yeye Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ametuamuru kuwafuata akasema, "Musiwatangulie mutaangamia, wala musiwape mgongo mutaangamia, na wala musiwafundishe, bila shaka wao ni wajuzi mno kuliko ninyi."

*Taz: Addurul-Manthoor cha Suyuti Juz. 2 uk. 60, Usudul-Ghabah Juz. 3 uk. 137, As-Sawaiqul-Muhriqa cha ibn Hajar uk. 148, Yanabiul-Mawaddah uk. 41 na 355, Kanzul-Ummal Juz. 1 uk. 168, Maj-Mauz-Zawaid Juz. 9 uk. 163.*

Lau tutafanya hivyo, basi hapana shaka Mwenyezi Mungu ataondosha hasira yake na ghadhabu yake kwetu, na atatubadilishia amani baada ya khofu yetu na atatumakinisha katika ardhi na kutupatia urithi ndani yake na angetudhihirishia walii wake Imam Mahdi (a.s.) ambaye kupitia kwake Mtume wa Mwenyezi Mungu ametuahidi kuwa ataijaza ardhi yetu usawa wa uadilifu kama ambavyo imejazwa dhulma na ujeuri na hapana shaka Mwenyezi angeitimiza nuru yake ulimwenguni kote.

# MWITO KWA MARAFIKI KUJA KUFANYA UTAFITI

Mabadiliko yalikuwa ndiyo mwanzo wa mafanikio ya kiroho, kwani nilihisi raha ya nafsi na ukunjufu wa moyo kuyaendea madh-hebu ya haki niliyoyagundua au unaweza kusema kuwa ***"Uislamu halisi ambao hauna shaka ndani yake."*** Furaha kubwa na fahari vilinifunika kutokana na neema aliyonineemesha Mwenyezi Mungu kwa uongofu na mwongozo. Sikuweza kunyamaza na kuficha yale yote yaliyokuwa yakinipeketa kifuani mwangu na nikajiambia mwenyewe, "Inanibidi niudhihirishe ukweli huu kwa watu kwani neema ya Mola wako isimulie." Nayo ni miongoni mwa neema kubwa, au ni neema kubwa mno duniani na akhera na yeyote anayenyamazia haki ni shetani bubu. Na hakuna kingine baada ya haki isipokuwa ni upotofu.

Kilichonizidishia yakini ndani ya hisia zangu ili kuwajibika kuueneza ukweli huu, ni kule kutokuwa na dhambi kwa Massuni ambao wanampenda Mtume (s.a.w.) na Ahli Bayt wake, na yatosha kuwaondolea tandabui iliyofumwa na historia mbele yao ili waifuate haki. Jambo hili ndilo lililonifika mimi binafsi.

Mwenyezi Mungu anasema: *"Namna hiyo ndivyo mlivyokuwa hapo kabla, basi Mwenyezi Mungu akakuneemesheni" (Qur. 4:94)*

Basi, niliwaita marafiki wanne miongoni mwa Waalimu ninaofanya kazi pamoja nao chuoni, wawili kati yao walikuwa wakifundisha mafunzo ya dini na watatu akifundisha Kiarabu, na huyu wa nne alikuwa mtaalamu wa falsafa ya Kiislamu. Wote hawa wanne hawakuwa wakitoka Qafsah bali walikuwa ni kutoka Tunis, na Jammal na Sausah.

Niliwaita wawe pamoja nami katika utafiti wa maudhui hii ya hatari, na niliwaonesha kuwa mimi nashindwa kufahamu baadhi ya maana za

mambo fulani na nimechanganyikiwa, pia ninayo mashaka ndani ya baadhi ya mambo. Walikubali kuja nyumbani kwangu baada ya kazi, nami nikawaacha wanasoma kitabu kiitwacho *"Al-Murajaat"* kwa msingi kuwa, mtunzi wa kitabu hicho anadai vitu vya ajabu na ni vigeni katika dini. Watatu miongoni mwao walikipenda sana kitabu hicho, ama yule wa nne ambaye husomesha Kiarabu yeye alituacha baada ya vikao vinne au vitano na alisema: "Sasa hivi wazungu wanakwenda mwezini ninyi bado munatafiti mambo ya Ukhalifa wa Kiislamu."

Hatukuwahi kukimaliza kitabu hicho ndani ya kipindi cha mwezi mmoja isipokuwa hao watatu walikuwa tayari wamekwisha kuuona ukweli, na kwa hakika niliwasaidia mno kuufikia ukweli huu kwa njia fupi kulingana na upana wa ufahamu uliojengeka kwangu katika kipindi cha uchunguzi. Nilionja utamu wa uongofu na niliufurahia mustaqbali (wangu) nikaanza kuwaita mara kwa mara baadhi ya marafiki wa Qafsah ambao vipindi vya masomo vilikuwa vikiniunganisha nao Msikitini au mahusiano yaliyokuwa kwa njia ya Twariqah za Kisufi, na baadhi ya wanafunzi wangu ambao walikuwa wakiambatana nami.

Haukupita mwaka ila tulikuwa tumefikia idadi kubwa (ya watu) tunaowatawalisha Ahlul-Bait, tunamtawalisha mwenye kuwatawalisha wao na tunamfanya kuwa adui mwenye kuwafanyia uadui, tunafurahi katika sikukuu zao na tunahuzunika katika *Ashura* na kufanya vikao vya maombolezo, yote haya ni kwa msaada wa Mwenyezi Mungu.

Barua yangu ya mwanzo ambayo inabeba khabari za kuuona kwangu ukweli, niliiandika kwa Sayyid Al-Khui na Sayyid Muhammad Baqir As-Sadr na ilikuwa katika munasaba wa Idi ya Ghadir kwani kwa mara ya kwanza tuliisherehekea katika mji wa Qafsah.

Mambo yangu yakatangaa kwa watu maalum na wengine wote ya kwamba mimi nimekuwa Shia na kwamba mimi nalingania watu kwenye Ushia, yaani kuwafuata Watu wa nyumba ya Mtume (s.a.w.). Na hapo zikaanza tuhuma mbali mbali na uvumi ukavuma nchini ya kwamba mimi ni jasusi la Israel ninafanya kazi ya kuwatia mashaka watu katika dini yao, na kwamba mimi na watukana Masahaba, pia mimi ni mtu wa fitna na mengineyo. Katika mji mkuu wa Tunis, niliwasiliana na marafiki wawili,

Rashid Al-Ghannushi na Abdul-Fattah Moro. Upinzani wao dhidi yangu ulikuwa mbaya mno, na katika mazungumzo yaliyofanyika baina yetu ndani ya nyumba ya Abdul-Fattah, mimi nilisema, “Ni wajibu wetu kama Waislamu kuvirejea vitabu vyetu na historia yetu.” Nilitoa mfano wa Sahih Bukhari ambayo ndani yake mna mambo ambayo akili haiyakubali wala dini haikubaliani nayo.

Walifura kwa hasira zao na wakaniambia: “Wewe ni nani hata umkosoe Bukhari”? Mimi nilitoa juhudi zangu zote niwatosheleze ili tupate kuingia ndani ya utafiti wa maudhui za kielimu. Wote wawili walilikataa jambo hilo wakasema: “Ikiwa wewe umekuwa ***Shia*** usitufanye sisi kuwa Mashia! Sisi tuna jambo muhimu mno kuliko hilo la ***Ushia***, nalo ni kuipinga serikali ambayo haihukumu kwa mujibu wa sheria za Kiislamu.” Nilisema ni faida gani mtapata mtakapofika kwenye ngazi ya uongozi wa serikali, mtafanya vibaya zaidi ya waliopo leo hii maadamu hamjui hakika ya Uislamu. Mawasiliano yetu yaliishia hapo.

Hali hii ilifuatiwa na uvumi mwingi dhidi yetu kutoka kwa baadhi ya watu na wakaeneza uvumi wa ajabu kwa watu wa kawaida kwa lengo la kuwaweka mbali na mimi na pia kunisingizia kwa namna zote ili watu wanitenge - Mwenyezi Mungu Mtukufu awasamehe.

Hatimaye tulianza kutengwa na baadhi ya vijana na Masheikh ambao ni wafuasi wa Tariqa za kisufi, na tuliishi ndani ya kipindi kigumu tukajiona kama wageni miongoni mwa ndugu zetu na jamaa zetu ndani ya nchi yetu. Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu alitubadilishia watu bora kuliko wao, kwani baadhi ya vijana walikuwa wakija kutoka miji mingine wakiutafuta ukweli, nami nilikuwa nikitoa upeo wa nafasi niliyonayo kuwatosheleza juu ya ukweli wa njia ya Ahlul-Bait (a.s.) na pia uhakika wa kihistoria. Basi vijana wengi waliiona haki kutoka mji mkuu wa Tunis, na pia miji ya Qairawan, Susah na Sayidi Buzaid. Nilipokuwa katika safari yangu ya kwenda Iraqi wakati wa kipupwe nilipitia Ulaya na nikakutana na baadhi ya marafiki zangu huko Ufaransa na Holland. Nilizungumza nao juu ya maudhui hii ya Ukhalifa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba nao waliona haki na kuifuata.

Hakika furaha yangu ilikuwa ni ya hali ya juu mno pindi nilipokutana

na Sayyid Muhammad Baqir As-Sadri katika mji Mtukufu wa Najaf nyumbani mwake na palikuwa na kikundi cha wanachuoni na ndipo Sayyid alipoanza kunitambulisha kwao ya kwamba mimi ni mbegu ya wafuasi wa Ahlul-Bait wa Mtume (s.a.w.) katika nchi ya Tunisia, kama ambavyo aliwatambulisha pia kwamba yeye alilia kwa furaha pindi ilipomfikia barua yangu iliyobeba bishara ya kufanyika kwa mahfali yetu kwa mara ya kwanza kuadhimisha sikukuu ya Ghadir njema. Nilimfahamisha pia juu ya mambo yanayotusibu ikiwemo upinzani na uzushi dhidi yetu na kutengwa. Sayyid alisema katika utangulizi wa maneno yake "Ni lazima mstahamili mashaka kwa sababu njia ya Ahlul-Bait ni ngumu na ina matatizo, kuna mtu alikuja kwa Mtume (s.a.w.) akamwambia, Hakika mimi nakupenda ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Mtume akamwambia yule mtu, Basi jibashirie balaa nyingi. Akasema (tena yule mtu) Pia nampenda Ibn Ami yako Ali, Mtume akasema; Jibashirie kuwa na maadui wengi. Yule mtu akasema, Na ninawapenda Hasan na Husein. Mtume akamwambia jiandae kwa umaskini na balaa nyingi. Sasa je sisi tumetanguliza nini katika (kutetea) njia ya haki ambayo Abu Abdillah Husein (a.s.) alijitolea nafsi yake, watu wake, watoto wake na wafuasi wake kwa thamani ya njia hiyo? Kama ambavyo kipindi chote cha historia Mashia wamejitolea kwa thamani ya kuwatawalisha kwao watu wa nyumba ya Mtume (s.a.w.), ni lazima ewe ndugu yangu kustahmili baadhi ya taabu na kujitolea katika njia ya haki, kwani Mwenyezi Mungu akimuongoa mtu mmoja kupitia kwako ni bora kwako kuliko dunia na vilivyomo."

Vile vile Sayyid Sadri alinipa nasaha nisijitenge, bali aliniamuru nijikurubishe zaidi kwa ndugu zangu *Ahlus-Sunnah Wal-Jamaa* kila wanapojaribu kunitenga. Kadhalika aliniamuru nisali nyuma yao ili mawasiliano yasikatike, na niwaone kuwa wao hawahusiki na lolote katika mambo yaliyotokea, kwani wao ni wahanga wa habari za propaganda za uzushi na historia iliyopotoshwa, na kwamba watu ni maadui wa kitu wasichokijua.

Kwa hakika Sayyid Al-Khui naye alinipa nasaha kama hiyo hiyo kama ambavyo Sayyid Muhammad Ali Tabatabai Al-Hakim naye siku zote alikuwa akitumia nasaha zake ndani ya barua zake nyingi ambazo zilikuwa na athari kubwa ndani ya mwenendo wa ndugu ambao tayari walikwishauona uongofu.

Kwa hiyo basi ziyara zangu kuutembelea mji mtukufu wa Najaf na wanachuoni wa Najaf katika minasaba mingi ziliongezeka, kisha niliapa kuwa kila mwaka nitaitumia likizo yangu ya kipindi cha kipupwe ndani ya uwanja wa Haram ya Imam Ali ili nipate kuhudhuria mafunzo ya Sayyid Muhammad Baqir As-Sadri, mafunzo ambayo nilifaidika nayo sana na yalininufaisha mno, vile vile niliapa kuyazuru maeneo (ya kumbukumbu) za Maimamu kumi na wawili.

Kwa hakika Mwenyezi Mungu aliyatimiza makusudio yangu kwa kuniwafikisha hata kumzuru Imam Ridha ambaye kaburi lake liko Mashhad ambao ni mji ulioko karibu na mpaka wa Urusi huko Iran, na huko nilijitambulisha kwa wanachuoni mashuhuri na nilifaidika nao sana.

Sayyid Al-Khui ambaye sisi tulikuwa tukifuata fatwa zake alinipa ruhusa ya kuwa muwakilishi wake katika matumizi ya Khumsi na Zaka na kuwapa wale walioiona haki huku kwetu kile wanachokihitajia miongoni mwa vitabu na misaada na mengineyo.

Nilitengeneza maktaba inayojitosheleza kwa rejea muhimu ambazo zinahusika katika uchunguzi, na ilikuwa imekusanya vitabu vya pande zote mbili na ilikuwa inaitwa *Maktabatu Ahlil-Bait (a.s.)* na kwa hakika inanufaisha wengi.

Mwenyezi Mungu aliiongezea furaha yetu kuwa furaha mbili na mafanikio yetu kuwa mafanikio ya namna mbili, kwani kabla ya miaka kumi na tano, Mwenyezi Mungu aliturahisishia mambo kwa kumfanya Meya wa mji wa Qafsah aafiki kuupa jina la Imam Ali ibn Abi Talib (a.s.) mtaa niliokuwa nikikaa. Sitaacha kumshukuru kwa uoni huu mtukufu, kwani yeye ni miongoni mwa Waislamu wenye juhudi na anayo mapenzi makubwa kwa Imam Ali, na kwa hakika nilimzawadia kitabu cha Muraja'ati naye anawasiliana nasi kwa mapenzi na heshima kubwa, Mwenyezi Mungu amlipe wema na ampe yale anayoyakusudia.

Wako baadhi ya watu wenye chuki ambao walijaribu kuuondoa ule ubao unaoonesha jina la mtaa wetu lakini njama zao hazikufaulu, kwani Mwenyezi Mungu alikwisha taka kuudumisha. Hatimaye barua nyingi zikawa zinatufikia kutoka kila pembe ya ulimwengu na juu yake liko

jina la Mtaa wa Imam Ali ibn Abi Talib (a.s.) ambaye jina lake tukufu liliubarikia mji wetu mzuri.

Kwa kutumia nasaha za Maimamu wa Ahlul-Bait na vile vile nasaha za wanachuoni wa Najaf tukufu, tulikusudia hasa kujikurubisha kwa ndugu zetu wa madh-hebu mengineyo na tukaulazimu umoja na tukawa tunasali kwa pamoja, na kwa sababu hii basi chuki ilipungua na tukaweza kuwakinaisha baadhi ya vijana kupitia masuali yao kwetu jinsi tunavyosali, tunavyotawadha na itikadi yetu.

# UONGOFU WA HAKI

Katika moja ya miji iliyoko kusini mwa Tunisia, kulikuwa na hafla ya harusi, hivyo wanawake fulani walikuwa wakizungumza juu ya mwanamke mmoja ambaye ni mke wa mwanaume fulani. Bibi Kizee mmoja aliyekuwa kakaa katikati yao akisikiliza mazungumzo yao, alishangazwa kuwa mwanamke yule ni mke wa Bwana yule, na walipomuuliza sababu ya kushangazwa kwake, alisema kwamba yeye amewanyonyesha mume yule na mke yule kwa hiyo wao ni ndugu wa kunyonya.

Wanawake hawa walizichukua habari hizi za kutisha hadi kwa waume zao na wakazifanyia kazi, matokeo yake mzazi wa yule mwanamke alikiri kuwa Binti yake alinyonyeshwa na Bibi kizee yule ambaye ni maarufu kwa wote kuwa ni mnyonyeshaji, kama ambavyo mzazi wa yule mwanaume naye alikiri kwamba mwanawe alinyonyeshwa na Bibi yule yule.

Basi hapo palizuka kutokuelewana baina ya familia hizi mbili, wakapigana kwa fimbo, kila mmoja wao akiutuhumu upande mwingine kuwa umesababisha msiba ambao huenda utawaingiza ndani ya ghadhabu na adhabu ya Mwenyezi Mungu, na khasa kwa kuwa ndoa hii imeshafikisha miaka kumi na huyu mwanamke amekwisha zaa watoto watatu. Mwanamke huyu aliposikia habari hizi alirudi nyumbani kwa baba yake na alisusa kula na kunywa na akataka kujinyonga kwa sababu hakuweza kuvumilia pigo hili na ni jinsi gani yeye aliolewa na nduguye hali ya kuwa hajuwi. Kuna idadi kadhaa ya watu walijeruhiwa kati ya koo mbili hizi, lakini mmoja kati ya wazee wakubwa aliingilia kati akasimamisha vita hii na akawanasihi waende kwa wanachuoni ili kuomba fatwa ya jambo hili huenda wakapata ufumbuzi.

Basi wakawa wanazunguka katika miji mikubwa ya jirani wakiwauliza wanachuoni wa miji hiyo juu ya ufumbuzi wa tatizo hili, na kila walipowasiliana na mwanachuoni fulani na kumueleza jambo hili, aliwaambia kuwa ndoa hiyo ni haramu na ni lazima Bibi na Bwana

watenganishwe moja kwa moja na pia waachie huru mtumwa au kufunga miezi miwili, na Fat-wa nyinginezo.

Walifika pia Qafsah na wakawauliza wanachuoni wa hapo lakini jawabu likawa ni lile lile kwani, wafuasi wa madh-hebu ya Malik wote wanaharamisha kunyonyeshwa japo tone moja wakifuata maoni ya Malik ambaye aliyafanyia kiasi maziwa kwa pombe kwani kinacholewesha ni haramu ikiwa ni kingi au kidogo kwa hiyo kunyonyesha kunaharamisha japo kwa tone moja la maziwa.

Kilichotokea hapo Qafsa ni kwamba mmoja wa watu waliohudhuria kikao cha fatwa hiyo aliwachukua pembeni akawaonesha nyumba yangu huku akiwaambia, "Muulize Tijani Qadhia kama hizi kwani yeye anayafahamu madh-hebu yote nimekwishamuona anajadiliana na wanachuoni hawa mara nyingi na anawashinda kwa hoja madhubuti."

Hivi ndivyo alivyonieleza mume wa mwanamke yule neno kwa neno pindi nilipomuingiza ndani ya maktaba yangu, na akanisimulia tukio lote kwa urefu mwanzo hadi mwisho, na akasema, "Ewe Bwana wangu! hakika mke wangu anataka kujinyonga na wanangu wametelekezwa nasi hatujui ufumbuzi wa tatizo hili, na wametuelekeza tuje kwako, na kwa hakika nimebashiria kuwa itakuwa kheri pindi nilipoona unavitabu hivi vingi ambavyo sijapata kuviona maishani mwangu mfano wake, basi huenda kwako kutakuwa na ufumbuzi."

Nilimletea kahawa kisha nikatafakari kidogo halafu nikamuuliza, kuhusu ni mara ngapi alinyonya kwa huyo mama, akasema, "Sifahamu, lakini mke wangu alinyonya mara mbili au mara tatu kwa huyo mwanamke na Baba yake mke wangu alishuhudia kwamba alimchukua bintiye mara mbili tu au mara tatu kumpeleka kwa Bibi huyo mwenye kunyonyesha." Mimi nikamwambia, "Ikiwa hivi usemavyo ni sahihi hapana kitu juu yenu na ndoa yenu ni sahihi na ni halali."

Bwana yule masikini alijitosa kwangu akawa anakibusu kichwa changu na mikono yangu huku akisema, "Mwenyezi Mungu akupe kheri kwa hakika umefungua mlango wa utulivu mbele yangu." Hapo hapo akanyanyuka kwa haraka na wala hakuimaliza kahawa yake wala hakutaka

nimfafanulie na wala hakutaka dalili isipokuwa aliniomba ruhusa atoke ili akamfahamishe mkewe, wanawe, watu wake na jamaa zake.

Katika siku iliyofuata alirudi akiwa na watu saba na akawatambulisha kwangu huku akisema, “Huyu ni mzazi wangu, na huyu ni mzazi wa mke wangu, na huyu wa tatu ni chifu wa kijiji, wanne ni Imam wa Sala ya Ijumaa na jamaa na huyu wa tano ni kiongozi wa Dini wa sita ni Mzee wa Jumuiya, na huyu wa saba ni Mkuu wa shule, na tumekuja ili utufafanulie kuhusu tatizo lile la kunyonya na ni vipi umelihalalisha?”

Wote niliwaingiza maktaba na nikawa nayasubiri majadiliano yao, nikawaletea kahawa kisha nikawakaribisha. Wakasema, “Sisi tumekujia ili tukujadili kuhusu kuhalalisha kwako Qadhiya ya kunyonya wakati Mwenyezi Mungu ameiharamisha ndani ya Qur’an, naye Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ameiharamisha kwa kauli yake aliposema, “Inakuwa haramu kwa kunyonya kama ambavyo inakuwa haramu kwa sababu ya nasaba. Kadhalika Imam Malik ameharamisha.”

Mimi nilisema, “Enyi mabwana zangu, ninyi *Mashaallah* ni watu wanane na mimi ni mtu mmoja, iwapo nitazungumza basi huenda nisikukinaisheni na majadiliano yetu yatapotea hewani, ila mimi napendekeza kwenu mumchague mmoja wenu ili nijadiliane naye nanyi mutakuwa mahakimu baina yangu na yeye.”

Fikra hii iliwafurahisha na wakaiona kuwa ni nzuri, na mambo yao wakamkabidhi yule kiongozi wa Dini hali ya kuwa wanasema kwamba, “Yeye ni mjuzi mno kuliko wao na ni mwenye uwezo.” Yule bwana alianza kwa kuniuliza, “Ni vipi ninahalalisha jambo alililoliharamisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Maimamu.”

Nikasema, “Najilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana na kufanya hivyo! lakini Mwenyezi Mungu ameharamisha kwa aya ambayo ni Mujmal na hakubainisha ufafanuzi wa jambo hilo, bali ufafanuzi wake umewakilishwa kwa Mtume wake ambaye ameweka wazi makusudio ya aya, (kwamba) ni unyonyeshaji upi na mara ngapi.”

Akasema, “Imam Malik ameharamisha kunyonya japokuwa tone moja.”

Mimi nikasema “Hilo nalijua, lakini Imam Malik yeye siyo hoja juu ya Waislamu, isipokuwa unasemaje juu ya Maimamu wengine?”

Alijibu akasema: “Mwenyezi Mungu awawie radhi, kwani wote wanataraji kutoka kwa Mtume (s.a.w.).” Nikasema; “Kwa hiyo nini hoja yako mbele ya Mwenyezi Mungu kutokana na wewe kumfuata Imam Malik ambaye maoni yake yanakwenda kinyume na maagizo ya Mtume (s.a.w.)?”

Akasema, hali ya kuwa amechanganyikiwa, “Subhanallah, mimi sijui kwamba Imam Malik ambaye ni Imam wa Darul-Hijra, anakhalifu maagizo ya Mtume.” Wote waliokuwepo hapo walichanganyikiwa kutokana na kauli hii, na walinishangaa kwa ujasiri huu dhidi ya Imam Malik, kitu ambacho hapo kabla hawakupata kukifahamu kwa mtu asiyekuwa mimi. Pale pale niliwahi nikasema, “Hivi Imam Malik alikuwa miongoni mwa Masahaba”? Akasema: “Hapana.” Nikasema “Je, alikuwa katika Tabiina?” Akasema “Hapana bali alikuwa miongoni mwa waliowafuatia Tabiina.”

Nikasema, “Basi ni yupi aliyekaribu zaidi na Mtume ni yeye au Imam Ali ibn Abi Talib?”

Akasema, “Imam Ali yuko karibu zaidi kwani yeye ni miongoni mwa Khulafaur-Rashidina.”

Mmoja wa watu waliokuwa wamehudhuria hapo akasema, *“Sayyidna Ali Karramallahu Waj-Hahu yeye ndiye mlango wa mji wa elimu.”*

Basi mimi nikasema, “Ni kwa nini basi mmeuacha mlango wa mji wa elimu na mmemfuata mtu ambaye hayuko miongoni mwa Masahaba wala Tabiina, bali amezaliwa baada ya fitna na baada ya mji wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kukaliwa na jeshi la Yazid na wakafanya mjini humo waliyoyafanya, wakawauwa Masahaba wema, na wakavunja heshima ya mambo Matakatifu, wakaibadilisha Sunna ya Mtume kwa bidaa walizozua basi ni vipi baada ya yote haya mtu atakuwa na utulivu wa moyo kwa Maimamu hawa ambao waliridhia watawala waliokuwa wakitawala kwa sababu tu ya wao kutoa Fat-wa zinazoafikiana na matamanio ya watawala hao?”

Mmoja wao akazungumza akasema, “Sisi tumesikia kwamba wewe ni Shia na unamuabudu Imam Ali.” Basi mwenzake aliyekuwa pembeni yake akampiga kwa ngumi iliyomuumiza na akamwambia, “Nyamaza, huoni aibu kusema maneno kama haya kwa mtu mheshimiwa kama huyu, kwa hakika mimi nimewafahamu wanachuoni siku nyingi lakini mpaka sasa jicho langu halijawahi kuona maktaba mfano wa maktaba hii, na huyu mtu anazungumza kwa kutumia maarifa na ukweli kwa yale ayasemayo.”

Mimi nilimjibu kwa kusema; “Mimi ni Shia na hii ni sawa, lakini Mashia hawamuabudu Imam Ali bali badala ya kumfuata Imam Malik wao wanamfuata Imam Ali kwa kuwa yeye ni mlango wa mji wa elimu kwa mujibu wa ushahidi wenu mlioutoa sasa hivi.”

Yule kiongozi wa Dini akasema, “Watu walionyonya ziwa moja Imamu Ali amehalalisha waowane?”

Nikasema: “Hapana, lakini yeye anaharamisha ikiwa kunyonya kutakapofikia mara kumi na tano mfululizo tena kunyonya kunakoshibisha au kama kutakuza nyama na mfupa.”

Uso wa yule mzazi wa mke ukachanua (kwa furaha) na akasema, “Namshukuru Mwenyezi Mungu, basi Binti yangu hakunyonya isipokuwa mara mbili au tatu tu, na bila shaka ndani ya kauli hii ya Imam Ali ndimo ilimo salama yetu kutokana na maangamivu haya, na hii ni huruma ya Mwenyezi Mungu kwetu baada ya kuwa tulikata tamaa.”

Yule kiongozi wa Dini akasema, “Tupe dalili juu ya kauli hii ili tutosheke.”

Nikawapa kitabu cha *Min-Hajus-Salihina* cha Sayyid Alkhui, na akawasomea yeye mwenyewe mlango wa kunyonyesha, wakafurahia mno khasa mume ambaye alikuwa akikhofu kwamba (huenda) nisiwe na ushahidi unaotosheleza. Kisha wakanitaka niwaazime kitabu hicho ili wapate kutolea hoja kijijini kwao, nikawapa na wakatoka hali ya kuwa wakiniaga na kuniombea huku wakitaka radhi.

Kiasi tu cha wao kutoka, walikutana na mmoja wa maadui (zetu)

akawachukua hadi kwa baadhi ya wanachuoni waovu, wakawatisha na kuwahadharisha kwamba mimi ni kibaraka wa Israel na kwamba kitabu cha *Minhajus-Salihina* ambacho niliwapa chote ni upotofu mtupu, na kwamba watu wa Iraqi ni watu wa kufru na unafiki, na kuwa Mashia ni majusi (wanaoabudu moto) wanahahalalisha kuoa madada kwa hiyo siyo ajabu kwa mimi kuhalalisha ndoa ya dada wa kunyonya, na mengineyo miongoni mwa tuhuma na fitna. Bwana huyo aliwashika akiwahadharisha mpaka wakabadili msimamo baada ya kuwa walikinaika na maelezo yangu, wakamlazimisha mume yule apeleke madai ya talaka kwenye Mahakama ya mwanzo mjini Qafsah, na huyo rais wa Mahakama hiyo aliwataka waende mji mkuu wa Tunis na wawasiliane na Mufti wa Jamhuri ili aweze kutoa ufumbuzi wa tatizo hili.

Bwana yule alikwenda na akabakia huko kwa muda wa mwezi mmoja kamili mpaka ikawezekana kumuona Mufti na akamsimulia kisa chake mwanzo mpaka mwisho.

Yule Mufti alimuuliza kuhusu wanachuoni waliomwambia kuwa ndoa ile ni halali na sahihi. Yule Bwana alijibu kwamba, “Hakuna aliyesema kuwa ndoa hiyo ni halali isipokuwa mtu mmoja tu naye Tijani Samawi.”

Mufti aliliandika jina langu kisha akamwambia yule Bwana, “Wewe rudi, nami nitatuma barua kwa rais wa Mahakama ya Qafsah” Na kweli barua ilikuja toka kwa Mufti wa Jamhuri na wakili wa mume akaisoma na kumjulisha mume huyu kuwa “Mufti wa Jamhuri ameiharamisha ndoa hii”

Hivi ndivyo alivyonisimulia mume wa mke yule ambaye unyonge na kuchanganyikiwa vilionekana (wazi) juu yake kutokana na taabu nyingi, hali ya kuwa akiomba msamaha kwa kero na usumbufu alionisababishia. Mimi nilimshukuru kwa wema wake huku nikistaajabu ni vipi Mufti wa Jamhuri anaibatilisha ndoa sahihi katika Qadhiya kama hii.

Nilimtaka aniletee barua yake aliyoipeleka Mahakamani ili niitangaze ndani ya magazeti ya Tunisia na nibainishe kwamba Mufti wa Jamhuri hayafahamu madhehebu ya Kiislamu na wala hajui tofauti zake za Kifiqhi kuhusu mas-ala ya kunyonyesha.

Yule mume akasema kuwa, hawezi kuyaona mafaili ya Qadhiya yake licha ya kuniletea barua toka kwake, basi hapo tukaachana.

Baada ya siku kadhaa ulinijia mwito toka kwa rais wa Mahakama akiniamuru nilete kitabu na dalili juu ya kutokubatilika ndoa baina ya watu wawili walionyonya ziwa moja. Mimi nilikwenda hali ya kuwa nimebeba rejea kadhaa nilizokuwa nimezichagua toka hapo mwanzo, na ndani ya kila kitabu niliweka kipande cha karatasi katika mlango wa kunyonyesha ili iwe rahisi kuufungua ukurasa huo mara moja.

Nilikwenda katika siku na saa iliyotajwa, na Katibu wa Mahakama akanipokea na kuniingiza ndani ya ofisi ya rais wa Mahakama, nikawakuta humo rais wa Mahakama ya mwanzo, rais wa Mahakama ya kanda na wakili wa Jamhuri na wajumbe watatu wote wamevalia mavazi maalum ya kutolea hukumu kana kwamba wako ndani ya kikao rasmi. Vile vile nilimuona mume wa mke amekaa mkabala wao mwishoni mwa ukumbi, nikawasalimia wote na wote walikuwa wakiniangalia kwa chuki na dharau.

Nilipoketi, yule rais alinisemesha kwa lugha kavu akasema, “Wewe ndiyo Tijani Samawi?” Nikasema; “Ndiyo.” Akasema, “Wewe ndiye uliyetoa fatwa kwamba ndoa iliyoko katika shauri hili ni sahihi?”

Nikasema, “Hapana, mimi siyo mufti, lakini Maimamu na wanachuoni wa Kiislamu ndiyo waliotoa fatwa ya uhalali na kusihi kwake.”

Akasema, “Kwa ajili hiyo ndiyo tumekuita, na wewe sasa umo ndani ya mzingo wa tuhuma, iwapo hutathibitisha madai yako kwa kutumia dalili basi tutakuhukumu kifungo na hutatoka hapa isipokuwa ni gerezani moja kwa moja.” Na hapo kweli nilitambua kwamba nimo ndani ya mzingo wa tuhuma, siyo kwa kuwa mimi nimetoa fat-wa katika shauri hili, lakini ni kwa kuwa baadhi ya wanachuoni waovu wamewaambia Mahakimu hawa kuwa mimi ni mtu wa fitna, na kwamba mimi ninawatukana Masahaba na ninaeneza *Ushia* kuwafuata Ahlu-Bait wa Mtume, na huyu rais wa Mahakama alikwisha mwambia kwamba iwapo utaniletea mashahidi wawili basi nitamtupa gerezani.”

Zaidi ya hapo ni kwamba, jamaa miongoni mwa ndugu Waislamu waliipotosha fatwa hiyo na kuifanya isieleweke kwa watu makhsusi na watu wa kawaida na badala yake ikaeleweka kwamba, mimi nahalalisha kuoa madada na hiyo (eti) ndiyo kauli ya Mashia - kwa mujibu wa madai yao.

Yote hayo niliyafahamu kabla na niliyakinisha wakati rais wa mahakama alipokuwa akinionya kuwa atanitia gerezani. Basi hapana kilichokuwa kimebakia mbele yangu isipokuwa ni kuwapa changamoto na kujitetea nafsi yangu kwa ushujaa wote, ndipo nilipomwambia yule rais: "Je, naweza kuzungumza wazi wazi bila ya khofu?"

Akasema, "Ndiyo, wewe huna wa kukutetea." "Mimi nikasema "Kabla ya yote, mimi sijajipa cheo cha umufti, lakini huyu hapa mbele yenu mume wa huyo mke muulizeni, ni yeye ndiye aliyenijia nyumbani kwangu akagonga mlango wangu na akaniuliza, basi ulikuwa ni wajibu wangu kumjibu kwa kile ninachokifahamu na nilimuuliza kuhusu idadi ya kunyonya (kulikonyonywa), na aliponijulisha ya kwamba mkewe hakunyonya isipokuwa mara mbili basi pale pale nilimpa hukmu ya Kiislamu kuhusu shauri hilo, mimi siyo miongoni mwa wanajitihadi wala wanaoweka sheria.

Yule rais akasema, "Ni ajabu, sasa hivi wewe unadai kwamba unaujuwa Uislamu na sisi eti hatuujui"?

Mimi nikasema, "Mwenyezi Mungu anisamehe, mimi sikukusudia hivyo, lakini watu wote hapa wanayafahamu madh-hebu ya Imam Malik na wametosheka naye, na mimi (kwa upande wangu) nimeyafanyia utafiti kila madh-hebu na nikaupata ufumbuzi wa shauri hili." Rais akasema, "Ni wapi uliopoupata ufumbuzi?" Nikasema, "Kabla ya kufanya jambo lolote je naweza kuuliza swali moja ewe Bwana rais?"

Akasema, "Uliza ukitakacho." Nikasema, "Nini kauli yenu kuhusu madh-hebu (mengine) ya Kiislamu"?

Akasema, "Yote ni sahihi, kwani wote wanataraji kutoka kwa Mtume, na ndani ya khitilafu zao kuna rehma."

Mimi nikasema, “Kama ni hivyo, basi muhurumieni huyu masikini, hali ya kuwa ninamuashiria yule mume wa mwanamke yule, ambaye sasa hivi amemaliza muda wa zaidi ya miezi miwili hali ya kuwa kajitenga na mkewe na wanawe, wakati ambapo kuna wanachuoni wa madh-hebu ya Kiislamu ambao wamekwisha litatua tatizo lake.”

Akasema hali ya kuwa na ghadhabu, “Lete dalili ya kutosha usifanye mchezo, sisi tumekupa nafasi ujitetee nafsi yako na sasa umekuwa mtetezi wa mtu mwingine.”

Nikamtolea kitabu cha *Minhajus-Salihina* cha Sayyid Khui kutoka mkobani mwangu na nikasema, “Haya ni madh-hebu ya Ahlul-Bait na ndani yake imo dalili.”

Basi alinikatisha kwa kusema, “Achana na madh-hebu ya Ahlu-Bait, sisi hatuyajui na wala hatuyaamini.”

Toka mwanzo nilikuwa nikingojea kutokea kitu kama hiki, kwa hiyo baada ya utafiti na uchunguzi siku hiyo nilikuwa nimeleta rejea nyingi za Kisunni ambazo nilizipanga vema, kwa namna nijuavyo. Niliiweka sahih Bukhari katika daraja la kwanza, kisha sahih Muslim, na baada yake nikaweka kitabu cha fatwa cha Mahmud Shaltut, kitabu cha Bidayatul-Muj-Tahid na kitabu kiitwacho *Nihatul-Muqtasid* cha Ibn Rushd, kitabu kiitwacho *Zaadul-Masir fi Ilmit-*Tafsir cha Ibn Al-Jauzi na rejea nyinginezo miongoni mwa vitabu vya Kisunni.

Hivyo basi, wakati rais alipokataa kuangalia ndani ya kitabu cha Sayyid Alkhui nilimuuliza ni kitabu gani ambacho yeye anakiamini. Alisema, *“Bukhari na Muslim.”*

Nikatoa Sahih Bukhari na nikaufungua ule ukurasa unaohusika kisha nikasema, “Tafadhali ewe Bwana hebu soma.” Akasema, “Soma wewe.”?

Mimi nikasoma, “Ametusimulia fulani naye kutoka kwa fulani, toka kwa (mama) Aisha Mama wa Waumini, amesema, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) alifishwa na wala hakuharamisha kutokana na kunyonya isipokuwa mara tano na kuendelea.”

Basi yule rais akakichukua kitabu toka kwangu, na akasoma yeye binafsi kisha akampa Wakili wa Jamhuri aliyekuwa pembeni mwake, naye akasoma na akampa anayefuatia. Wakati huo mimi nilitoa Sahih Muslim na nikamuonesha hadithi zile zile kisha nilifungua kitabu cha fatwa cha Sheikh Shal-tut wa Az-Har, naye hapana shaka kabisa, ameeleza ikhitilafu za Maimamu kuhusu mas-ala ya kunyonyesha, kwani wako ambao wamesema kuwa, kunyonyesha kunakoharamisha ni kule kunakofikia mara kumi na tano na wengi wamesema mara saba, na miongoni mwao wameharamisha kama ni zaidi ya mara tano, isipokuwa Malik ambaye ameikhalifu *Nnasi* (maandiko) na akaharamisha japo kwa tone moja.

Kisha Shaltut amesema, "Mimi ninaungana na maoni ya kati kwa kati ninasema mara saba na zaidi."

Baada ya rais wa Mahakama kuona yote hayo akasema, "Inatosha." Kisha akamgeukia yule mume wa mke na kumwambia, "Nenda kaniitie baba wa mkeo ili aje ashuhudie mbele yangu kwamba mkeo alinyonyeshwa mara mbili au tatu na ikithibiti hivyo utamchukua mkeo leo hii."

Masikini yule aliruka kwa furaha, ndipo Wakili wa Jamhuri alipoomba ruhusa yeye na wajumbe waliohudhuria ili wakaendelee na kazi zao, naye rais akawaruhusu.

Pindi kikao kilipokuwa kimebakia kwetu tu, rais alinigeukia hali ya kunitaka radhi akasema: "Nisamehe ewe Ustadh, hakika watu wamenipotosha kuhusiana nawe, wamesema mengi ya ajabu juu yako, nami hivi sasa nimefahamu kwamba wao ni mahasidi na wana malengo maovu dhidi yako, wanakutakia wewe shari."

Moyo wangu ulifurahia mno mabadiliko haya ya haraka na nikasema, "Kila sifa njema anastahiki Mwenyezi Mungu ambaye amejaalia nusra yangu kupitia mikononi mwako ewe Bwana wangu rais."

Yeye akasema, "Nimesikia kwamba wewe unayo maktaba kubwa, je katika maktaba hiyo kimo kitabu kiitwacho; *"Hayatul-Hayawanilkubra* cha Ad-Dumair?"

Nikasema, “Ndiyo.” Akasema, “Je, unaweza kuniazima kitabu hicho kwani imepita miaka miwili ninakitafuta.” Nikasema “Umekipata ewe bwana wangu wakati wowote ukitaka.”

Akasema, “Je, unao wakati unaokuruhusu uje kwenye maktaba yangu ili tuzungumze na niweze kufaidika kutoka kwako?” Nikasema, “Mwenyezi Mungu anisamehe, mimi ndiyo nifaidike kutokana nawe kwani wewe ni mkubwa kuliko mimi kwa umri na cheo, nami ninazo siku nne za mapumziko katika wiki nitakuwa rehami wa maelekezo yako.”

Basi tuliafikiana siku ya Jumamosi katika kila wiki, kwa kuwa siku hiyo hakuna vikao vya Mahakama.

Na baada ya kuniomba nimuachie kitabu changu cha Bukhari na Muslim na kitabu cha Fatawa cha Mahmud Shaltut ili aihariri ile Nnassi, alisimama na kunitoa ofisini akanisindikiza mwenyewe.

Nilitoka kwa furaha nikimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ushindi huu, kwani niliingia hali ya kuwa ni mwenye khofu nikitishiwa kufungwa gerezani, na sasa ninatoka hali ya kuwa rais wa mahakama akiwa amebadilika na kuwa rafiki mpenzi anayeniheshimu, na akinitaka tuketi naye ili afaidike kutoka kwangu. Kwa hakika hizo ni miongoni mwa baraka za (kufuata) njia ya watu wa nyumba ya Mtume ambao mwenye kushikamana nao hapati hasara, na hupata amani mwenye kuwategemea.

Yule mume akaizungumza khabari hii kijijini kwake na ikaenea katika kila kijiji kilicho jirani baada ya mke kurejea nyumbani kwa mumewe na shauri lile kumalizika kwa ndoa ile kuwa halali. Basi watu wakawa wanasema kwamba mimi ni mjuzi mno kuliko wote na ni mjuzi mno kuliko hata Mufti wa Jamhuri. Yule mume alikuja nyumbani akiwa na gari kubwa, akaniita niende kijijini mimi na familia yangu yote na akaniambia kwamba watu wote wanasubiri kufika kwangu na watachinja kondoo watatu ili kufanya sherehe ya faraja.

Nilimtaka radhi kutokana na shughuli zangu mjini Qafsah na nikamwambia, “Nitawatembeleeni wakati mwingine pindi apendapo Mwenyezi Mungu.”

Naye rais wa Mahakama akawazungumza marafiki zake na shauri hili likawa mashuhuri, Mwenyezi Mungu akavishinda vitimbi vya wakaidi, na baadhi yao walikuja niomba radhi.

Kwa hakika Mwenyezi Mungu alizifungua nyoyo za baadhi yao wakaongoka na wakawa miongoni mwa watu wenye utakaso wa moyo.

*Hiyo ni fadhila ya Mwenyezi Mungu humpa amtakaye, naye Mwenyezi Mungu ni mwingi wa fadhila.*

*Na maombi yetu ya mwisho ni kuwa kila sifa njema anastahiki Mwenyezi Mungu, kisha Rehma za Mwenyezi Mungu zimshukie Bwana wetu Muhammad na ziwashukie kizazi chake walio wema waliotakasika.*

*****

# Rejea Zilizotumika:


**Vitabu vya Tafsir:**

1. Qur'an Tukufu
2. Tafsiri ya al-Tabari
3. Al-Durr al-Manthur fi al-Tafsiri bi al-Ma'thur ya al-Suyuti.
4. Tafsir al-Mizan ya al-Tabatabai.
5. Al-Tafsir al-Kabir ya al-Fakhr al-Razi.
6. Tafsir Ibn Kathir.
7. Zad al-Maseer fi Ilm al-Tafsir ya Ibn al-Jawzi
8. Tafsir al-Qurtubi.
9. Shawahid al-Tanzil ya al-Haskani.
10. Al-Hawi Lil Fatawi ya al-Suyuti.
11. Al-Itqan fi Ulum al-Qur'an.

**Vitabu vya Hadithi:**

1. Sahih Bukhari.
2. Sahih Muslim.
3. Sahih Tirmidhi.
4. Sahih Ibn Majah.
5. Mustadrak al-Hakim.
6. Musnad al-Imam Ahmad ibn Hanbal.
7. Sunan Abi Dawood.
8. Kanz al-Ummal.
9. Muwatta'al-Imam Malik.
10. Jami' al-Usul cha Ibn al-Athir.
11. Al-Jami' al-Saghir na al-Jami' al-Kabir vya al-Suyuti.
12. Minhaj al-Sunnah cha Ibn Taymiyah.
13. Majma al-Zawa'id cha al-Haythami.
14. Kunuz al-Haqa'iq cha al-Manawi.
15. Fath al-Bari fi Sharh al-Bukhari.

**Vitabu vya Historia:**

1. Tarikh al-Umam wa al-Muluk cha al-Tabari.
2. Tarikh al-Khulafa cha al-Suyuti
3. Tarikh al-Kamil cha Ibn al-Athir.
4. Tarikh Dimashq cha Ibn Asakir.
5. Tarikh al-Masudi [Muruj al-Dhahab]
6. Tarikh al-Ya'qubi.
7. Tarikh al-Khulafa cha Ibn Qutaybah.
   Kinachojulikana kama Imamah wa al-Siyasah.
8. Tarikh Abi al-Fida'.
9. Tarikh Ibn al-Shuhnah.
10. Tarikh Baghdad.
11. Al-Tabaqat al-Kubra cha Ibn Sa'd.
13. Sharh Nahj al-Balagha cha Ibn Abi al-Hadid.

**Vitabu vya Sirah:**

1. Sirat Ibn Hisham.
2. Al-Sirah al-Halabiyah.
3. Al-Isti'ab.
4. Al-Isabah fi Tamyeez al-Sahabah.
6. Hilyat al-Awlia cha Abi Nu'aym.
7. Al-Ghadir fi al-Kitab wa al-Sunnah cha al-Amini.
8. Al-Ta'rif cha Ibn Tawus.
9. Al-Fitnah al-Kubra cha Taha Husayn.
10. Maisha ya Muhammad cha Muhammad Hasanain Haykal.
11. Al-Riyadh al-Nadirah cha al-Tabari.
12. Al-Khilafah wa al-Mulk cha Abu al-Aala al-Mawdudi.

**Vitabu Mbalimbali:**

1. Is'af al-Raghibeen.
2. Tahdhibut-Tahdhib.
3. Tadhkirat al-Khawass cha Ibn al-Jawzi.
4. Al-Bidayah wa al-Nihayah cha Ibn Kathir.
5. Sirr al-Alamin cha al-Ghazali.

6. Al-Swaaiqal-Muhriqah Ibn Hajar al-Haythami.
7. Al-Manaqib al-Khawarizmi.
8. Yanabi'al-Mawaddah cha al-Qanduzi al-Hanafi.
9. Al-Nass wa al-Ijtihad cha Sharaf al-Din al-Musawi.
10. Al-Muraja'at cha Sharaf al-Din al-Musawi.
11. Al-Saqifah cha Shaykh al-Muzaffar.
12. Fadak cha al-Sayyid Muhammad Baqir al-Sadr.
13. Al-Siddiq Abu Bakar cha Husain Haykal.
14. Munaqashah' Aqaidiyyah fi Maqalat Ibrahim al-Jabhan.
14. Lisan al-Arab cha Ibn Manzur.
16. Sharh Nahj al-Balaghah cha Muhammad Abduh.
17. Abu Hurayrah cha Sharaf al-Din al-Musawi.
18. Al-Saqifah wa al-Khilafah cha Abdul Fattah Abdul Maqsud.
19. Shaykh al-Mudirah cha Mahmud Abu Rayyah.